Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 4 Agosti, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri natangaza tu kwamba, kama kawaida wageni tutawatambulisha mara baada ya kipindi cha maswali.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA (K. n. y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):**

Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 345

**Wilaya Mpya ya Kilolo**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI (K. n. y. MHE. HAZARA P. CHANA)** Mheshimiwa Spika, naomba swali hilo liondolewe. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa, una ridhaa yake?

**MHE. PROF. MWALYOSI:** Ndiyo, tuna ridhaa yake.

**SPIKA:** Una ridhaa yake.

**MHE. PROF. MWALYOSI:** Ndiyo.

Na. 346

**Mlundikano Mkubwa wa Kesi Mahakamani**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD** aliuliza: -

Kwa kuwa Mahakama nyingi zina mlundikano mkubwa wa kesi zenye makosa madogo madogo zinazochukua muda marefu kupata ufumbuzi: -

Je, Serikali haioni kuwa sasa kuna haja ya kuandaa utaratibu wa kutoza faini kwa washtakiwa bila ya kuwapandisha mahakamani?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kufuata utaratibu wa kisheria uliopo hivi sasa, mashauri yote yanapaswa yasikilizwe na kuamuliwa na Mahakama au Mabaraza ya Usuluhishi.

Mheshimiwa Spika, inapobainika kwamba upo umuhimu wa kuweka utaratibu wa kutoza faini kwa aina fulani ya makosa, Serikali haisiti kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria na kuliomba Bunge kutunga sheria husika. Sheria zilizopo zinazoweka masharti ya kutoza faini bila mtuhumiwa kufikishwa mahakamani ni pamoja na Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 na kadhalika.

Hata hivyo, sheria hizo zinaelekeza kwamba sharti mtuhumiwa akubali kosa. Sheria hizo pia zimezingatia haki ya mtuhumiwa kupewa haki ya kusikilizwa kwa ukamilifu na haki ya kukata rufani au kupata nafuu nyingine ya kisheria. Endapo mtuhumiwa atakataa kosa, basi lazima apelekwe mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, tunawaomba Wabunge, wadau mbalimbali na wananchi kwa ujumla kutoa mapendekezo na kuishauri Serikali kuhusu utaratibu mbadala au unaofaa zaidi katika kushughulikia makosa mengine yanayoonekana ni madogo madogo.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tuna upungufu mkubwa nchini wa Mahakimu. Je, Waziri haoni sasa iko haja kutafuta utaratibu huo kwa haraka zaidi ili wale wenye matatizo madogo madogo waweze kuhukumiwa na kupata haki yao?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu nchini na Serikali inajitahidi kwa namna itakavyoweza kuongeza Mahakimu kila inapokuwa na uwezo huo na ni kweli ili kuweza kuharakisha kesi ambazo zipo au kupunguza mlundikano wa kesi ni vyema basi tukatafuta utaratibu mbadala. Kama tunavyoomba asubuhi kwa kuongoza maombi hapa Bungeni tunasema kwamba: "Watu watendewe haki kwa mujibu wa sheria" na ndiyo maana basi inabidi kama mtu hayuko tayari kuwa na hiyo njia mbadala aende mahakamani. Lakini nakubaliana naye kwa kweli, kwa wale ambao watakuwa tayari kuwe na utaratibu mbadala ili kusiwe na mlundikano wa kesi na wale ambao wana haki ya kusikilizwa na Mahakimu waweze kupata hiyo haki. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kuna mlundikano mkubwa wa kesi mbalimbali na kwa sababu huchukua muda mrefu sana. Je, Serikali haioni kuwa kuna urahisi wa kutatua matatizo haya kwa kukubaliana na mambo ambayo yanafanywa na wenzetu katika suala la *sentencing bargaining? (Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ni kweli kama kuna mlundikano wa kesi za jinai na kwamba lazima Serikali ichukue hatua ya kuona kwamba mlundikano huo unapungua. Ninakubaliana naye na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Wabunge na wadau wengine pamoja na wananchi watupe mapendekezo na kwa hivyo nimechukua pendekezo lake kutoka hapa Bungeni.

Na. 347

**Upatikanaji wa Haki ya Msingi**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza: -

Kwa kuwa upatikanaji wa haki kwa wakati ni haki ya msingi kwa wananchi: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, Mahakama zote nchini hasa za Mwanzo zinapatiwa Mahakimu wa kutosha?
(b) Je, Chuo cha Lushoto *(IJA)* kinatoa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wangapi kwa kila mwaka?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mbunge wa Lushoto, lenye kipengele (a) na (b), naomba kutoa maelezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna Mahakama za Mwanzo 1,105 nchini na kuna upungufu wa wastani wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 392.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Mshangama kama ifuatavyo: -

(a) Ili kuhakikisha Mahakama za Mwanzo zinapatiwa Mahakimu wa kutosha, Serikali imechukua hatua zifuatazo: -

(i)Kuajiri Watanzania wenye sifa (Stashahada ya Sheria) kutoka katika vyuo mbalimbali vinavyotambuliwa na Serikali.

(ii)Kupanua Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na chuo hicho kutoka 247 kwa sasa na kuwa 500.

(iii) Kuajiri kwa mkataba, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wastaafu wenye sifa ya uadilifu na tabia njema.

(iv) Kuboresha maslahi na mazingira ya kazi ya Mahakimu ili Mahakimu wawe wanavutiwa na kazi hiyo.

(b) Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kilianza kutoa mafunzo mwezi Septemba mwaka 2000. Hadi kufikia mwezi Julai 2006, chuo kimekwishatoa wahitimu 279. Kati ya wahitimu hao waliodhaminiwa na Mahakama ni 182 na katika idadi hiyo ni wahitimu 73 tu ndiyo walioajiriwa kuwa Mahakimu. Wengine hawakuajiriwa ama kwa sababu waliamua kuendelea na masomo ya Chuo Kikuu au hawakuwa na sifa na maadili ya kufanya kazi ya Uhakimu au waliajiriwa sehemu nyingine.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nami napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mahakama za Mwanzo zilizoko katika Mikoa ya Pembezoni na Wilaya za Mipakani mara nyingi zinakaa muda mrefu bila kutembelewa na Viongozi wao, hali inayosababisha maamuzi yao mengine yawe ama ni ya kuzirejea kesi zilizokwishaamuliwa Mahakama za Juu, ama kuamua maamuzi ambayo hayawatendei haki wale ambao wamewahukumu na kwa kuwa Mahakama hizo zikiishaamua wananchi wanashindwa kuendelea na kesi zao ngazi za juu badala yake wanakubali ile hukumu hata kama ni ya kuwaonea: -

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo walio katika Mikoa na Wilaya za Mipakani wanakaguliwa mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba wanatenda haki?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nimepokea malalamiko ya Mheshimiwa Ruth Msafiri ambaye anatoka katika moja ya Wilaya za Pembezoni. Nakubaliana naye kwamba tutaongeza juhudi au jitihada za ngazi za juu kutembelea Mahakama za Mwanzo ili kuona kwamba Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanafanya kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, wakati nikiwasilisha hotuba ya Bajeti yetu hapa Bungeni nilieleza kwamba sasa kila Wilaya imepewa gari ili ukaguzi uwe rahisi kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo. Lakini napenda niwaeleze kwamba, kuna upungufu mkubwa sana wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na vile vile vitendea kazi ni duni sana katika Mahakama za Mwanzo na mazingira ya kazi si mazuri sana. Kwa hiyo, inaweza ikaonekana kwamba pengine Mahakimu hawafanyi kazi inavyotakiwa kwa ajili ya maadili, lakini ikawa ni kwa sababu ya mazingira hayo magumu ya kufanyia kazi.

Naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, kupitia Bajeti ya Serikali na fedha za wafadhili ambazo zinatusaidia kufanya maboresho ndani ya Mahakama, tutajitahidi sana kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi katika Mahakama za Mwanzo ili tuweze kuwapambanua wale ambao hawatendi kazi zao kutokana na maadili yao mabovu na kwamba tutaongeza ukaguzi kwenye Mahakama zetu za Mwanzo kwa sababu kule ndiko kwenye watu ili haki iweze kutendeka zaidi.

**SPIKA**: Nimekuona Mheshimiwa Benson Mpesya, siku nyingi sana hujauliza swali la nyongeza.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwanza wewe kwa jicho lako la huruma. Naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ufanisi wa Mahakama za Mwanzo hutegemea sana kuwepo kwa Wazee wa Mabaraza na hawa wazee kwa muda mrefu wamekuwa wakidai posho za malimbikizo nyingi hasa kwa Mahakama ya Mwanzo ya Mwanjelwa na ninaamini katika nchi nzima. Je, Serikali ina mpango gani wa kuliondoa tatizo hili la Wazee wa Baraza kukaa kudai pesa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mahakama za Mwanzo zinategemea sana ufanisi wa Wazee wa Mahakama na kwa hivyo kama kuna hitilafu yoyote ile ni wazi kwamba haki haitatendeka. Moja ya matatizo ambayo ameyasema ni kwamba kuna mlundikano au posho zao hazijalipwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa utaratibu wa Mahakama, Wazee wa Mahakama wanalipwa baada ya kesi moja kwisha. Hilo nalo lenyewe linaweza likawa ni tatizo kama kesi hiyo inachukua muda mrefu. Lakini ni kweli vile vile, wakati mwingine pengine kwa ajili ya ufinyu wa Bajeti ya Mahakama, inawezekana kuna wengine ambao hawajalipwa. Kwa hiyo, Wizara yetu itaangalia kwamba wale wazee ambao hawajalipwa kwa sababu palikuwa hakuna fedha, tutajitahidi kuwalipa na vile vile tutaangalia huu utaratibu ili tuone ni namna gani tunaweza tukaongeza ufanisi katika kutoa haki kwenye Mahakama zetu za Mwanzo.

Na. 348

**Tatizo la Maji Msewe, Changanyikeni na Makongo**

**MHE. HALIMA J. MDEE (K.n.y. MHE. SUSAN A. J. LYIMO)** aliuliza: -

Kwa kuwa mbali na hali ya ukame uliojitokeza nchini mwetu kuna baadhi ya maeneo Jijini Dar es Salaam ambayo hayana maji kwa mfano Msewe, Changanyikeni na Makongo: -

(a) Je, ni nini hasa sababu ya tatizo hilo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo ili wananchi wapate maji kama ilivyo kwa jirani zao za Chuo Kikuu Dar es Salaam ambao awali walikuwa na tatizo hilo na sasa ni historia?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maeneo ya Msewe na Changanyikeni hupata maji ya bomba kutoka Mfumo wa Maji wa Mtambo wa Ruvu Juu. Aidha, eneo la Makongo hupata maji kutoka Mtambo wa Ruvu Chini. Tatizo la maji katika maeneo mengi ya Dares Salaam yenye mtandao wa mabomba yakiwemo maeneo ya Msewe, Changanyikeni na Makongo linatokana na uchakavu wa mitambo ya kusukuma maji iliyoko Ruvu Juu na Ruvu Chini, uchakavu wa mtandao wa mabomba pamoja na uwezo wa mitambo hiyo ukilinganisha na mahitaji halisi. Kwa mfano, Mtambo wa Ruvu Juu huzalisha lita milioni 73 dhidi ya mahitaji halisi ya lita milioni 135 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, baada ya kununua pampu 2 na kuzifunga mwanzoni mwa mwezi Mei 2006, katika Mtambo wa Ruvu Juu, Shirika la *DAWASCO* ambalo linasimamia utoaji wa huduma ya maji Jijini Dar es Salaam; limeweka utaratibu wa mgao wa maji ili kila eneo lipate maji angalau mara mbili kwa wiki. Maeneo ya Msewe, Changanyikeni na Makongo yanapata maji kwa mgao kama ifuatavyo: -

(i) Msewe wanapata maji siku za Jumatatu na Alhamisi kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 8 mchana.

(ii) Changanyikeni wanapata maji siku za Jumanne na Alhamisi mara baada ya maji kufunguliwa kwenye matanki ya Kimara kati ya saa 12 asubuhi hadi saa 8 mchana. Hata hivyo, eneo la Mbuyuni na Chuo cha Takwimu maji hupatikana kwa muda mfupi, kutokana na uwezo mdogo wa mabomba na matumizi makubwa yaliyomo njiani kabla ya kufika Mbuyuni na Chuo cha Takwimu.

(iii) Makongo Juu hupata maji siku za Jumatatu na Alhamisi kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa nane mchana.

(iv) Makongo Kati hupata maji siku za Jumanne na Jumamosi kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa nane mchana.

(v) Makongo Chini hupata maji siku za Jumatano, Ijumaa na Jumapili kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa nane mchana.

Aidha, katika jitihada za kuboresha huduma ya maji, pampu nne zaidi zimeagizwa na zinatarajiwa kuwasili na kufungwa mwezi huu. Hatua hizi zitaboresha ufanisi wa mitambo na uhakika wa upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam.

(b) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam *(DAWASA)* inatekeleza mradi wa kukarabati na kuboresha mabomba makuu yanayosafirisha maji kutoka Mtambo wa Ruvu Juu hadi Kimara ili kupunguza uvujaji njiani.

Aidha, *DAWASA* inatayarisha mkakati kabambe wa kupanua na kuboresha mifumo ya mabomba ya usambazaji majisafi na majitaka katika maeneo mbalimbali Jijini kwa mahitaji ya Jiji la Dar es Salaam hadi mwaka 2025. Maeneo ya Msewe, Changanyikeni na Makongo yatahusika katika mradi huo kabambe. Kazi hii itaanza katika mwaka wa fedha 2006/2007. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake yenye ufafanuzi mzuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba *program* inaishia 2025. Sasa Makongo na Msewe wasubiri mwaka 2025 au *at least* hiyo sehemu yao anajua ni muda gani ambapo wanaweza wakawa wamepata maji? Sijui kama amenielewa swali langu.

**SPIKA:** Mheshimiwa, hebu rudia swali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, *program* yake ya Dar es Salaam inaishia mwaka 2025 kwa mapana yake. Hili swali la Mheshimiwa Susan Lyimo *specifically* lilikuwa ni kwa Makongo, Msewe na Changanyikeni.

Sasa ningependa kujua kama ana taarifa Msewe na Makongo wanaweza wakapata maji lini yaani kuanzia kipindi cha sasa mpaka mwaka 2025, au wategemee hapo *in between* siku yoyote ile?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa Mtambo wa Ruvu Juu ambao ndiyo unatoa maji kwa Changanyikeni na Msewe, sasa hivi tuna mitambo mingine ambayo itafungwa mwezi huu na baada ya mitambo hiyo kufungwa maji ya Msewe na Changanyikeni yataongezeka kwa kiasi kikubwa ambacho yatakuwa sawa.

Aidha, Makongo ambao wanapata maji kutoka Ruvu Chini, maji hayo yanaongezeka na pia kuna juhudi mbalimbali ambazo Wizara yangu inafanya ikiwemo kuchimba visima virefu katika Mto Mpiji kwa ajili ya kuongeza maji Dar es Salaam na Makongo ikiwemo ndani yake.

Kwa hiyo, maji yataongezeka siku hadi siku mpaka itakapofika mwaka 2025 ndiyo tutatimiza lile lengo ambalo tulikuwa tumekadiria. Ahsante.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Mimi ninaishi Makongo kwa sehemu fulani, ndiyo nyumbani kwa mzee Mongella.

Ninakubaliana na Waziri kwamba kuna mgao wa maji. Jambo la kusikitisha ni kwamba, kila tunapopata mgao kwa sababu mabomba ni chakavu maji yote humwagika:

-

Je, kwa nini kabla ya kufanya mpango huo kabambe, suala hili la kuzuia maji kumwagika na kuhakikisha kwamba maji haya yanafika mwisho kwa Mongella kule lisifanyike kama suala la dharura? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mongella pamoja na kupongeza majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri kama ifuatavyo: -

Kama ni tatizo kwamba mabomba yanatoa maji kabla hayajafika nyumbani kwa Mheshimiwa Mongella, tutalishughulikia hivi leo ili kuhakikisha kwamba yanafika siku ya mgao. Ninachotaka kuongeza hapa ni kwamba maji ya Jiji la Dar es Salaam na hatua tunazozichukua kama ilivyo kwa miradi ya maji huchukua muda. Lakini ziko jitihada kubwa za makusudi ambazo zinaboresha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na kuna sehemu ambazo zilikuwa hazipati maji kabisa sasa zimeanza kupata na ushahidi ni huo anaoutoa Mheshimiwa Mongella. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, tunafanya kila jitihada na Dar es Salaam tunaipa umuhimu wa kwanza kutokana na idadi kubwa ya watu wanaoishi katika Mji huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kuzingatia muda … Aah, basi yuko *Senior Citizen*, Mheshimiwa John Cheyo. *(Kicheko)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi naishi Masaki na ni mojawapo ya Dar es Salaam. Mheshimiwa Spika na wewe uko huko huko pamoja na Waziri Mkuu. Tumengojea maji kwa muda wa miaka 31 na tunapata maji ya *appointment*. Sasa kama Mheshimiwa Waziri anaweza kupeleka hayo maji kwa Mheshimiwa Mongella kesho, ni lini atahakikisha kwamba kuna maji yanayokwenda kwa Waziri Mkuu na kwangu pia pale Masaki? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Na kabla Mheshimiwa Waziri hujajibu, Spika naye anakaa huko huko *Chole Road,* Masaki. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anayosema Mheshimiwa Cheyo kwamba katika enoo la Masaki kumekuwepo na matatizo makubwa ya maji. Lakini ni kweli vile vile kwamba ziko hatua ambazo zinaonekana dhahiri zinachukuliwa kupeleka maji Masaki. Bomba linalopeleka maji Masaki ambalo linaunganisha bomba kuu linalotoka mlimani *University* pale mahali panaitwa Morocco, pakiunganisha hivi sasa ndiyo jitihada inayofanyika maji yatafika Masaki na bomba la kutoka hapo mpaka Masaki limekwishafika Masaki isipokuwa kuunganisha pale Morocco ndiyo kazi inaendelea hivi sasa.

Lakini hata hilo bomba likishafika itabidi yawepo mabomba madogo madogo ambayo yanasaidia kufikisha maji nyumbani kwa watu. Kwa hiyo, tuvute subira kidogo

jitihada za kufikisha maji Masaki kwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Spika, Waziri wa Afya na kwa Mheshimiwa Cheyo ziko njiani. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 349

**Barabara ya Tunduma – Sumbawanga**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 kuna uwezekano mkubwa wa ujenzi wa barabara ya lami kutoka Tunduma hadi Sumbawanga kama agizo la Ilani ya Uchaguzi 2005 inavyoanisha:-

(a) Je, isingekuwa vizuri Serikali ikawapa makandarasi wawili au watatu kwa pamoja ili kazi hii isichukue muda mrefu na kusababisha gharama kubwa hapo baadaye?

(b) Kwa kuwa barabara kuu hii itapita katikati ya Mji wa Sumbawanga, isingekuwa bora kuanza kuandaa michoro ya barabara za wapite kwa miguu ili kuepusha hatari ya ajali kutokea hapa Mjini?

(c) Je, nini hatma ya barabara hiyo kuunganisha Sumbawanga hadi Kasanga na pia Sumbawanga hadi Mpanda ili iwe kiungo cha Ziwa Tanganyika na reli huko Mpanda?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Tunduma – Sumbawanga ipo katika Mikoa ya Mbeya na Rukwa na sehemu kubwa ya barabara hii inapitika wakati wote wa mwaka kwa vile inafanyiwa matengenezo ya mara kwa mara. Wizara yangu kwa kupitia Wakala wa barabara (*TANROADS*) imeshamteua Mhandisi mshauri anayefanya kazi ya usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni. Wizara pia itatumia ushauri utakaotolewa na Mhandisi Mshauri huyo kutoa uamuzi wa sehemu ngapi barabara hii igawanywe ili kurahisisha ujenzi wake.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu kwa barabara hii ilifanywa na kampuni ya kihandisi ya *GIBB Africa Ltd* ya Nairobi, Kenya na ilikamilika mwezi Januari 2004 ambapo michoro ya eneo la Sumbawanga Mjini, ilizingatia vigezo vichache kama vile, mfumo wa maji machafu, njia ya waendesha baiskeli na wasukuma mikokoteni. Aidha kazi za usanifu wa kina na uandaaji wa michoro na nyaraka za zabuni kwa sehemu ya Tunduma hadi Laela zilianza mwezi Januari 2006 na sehemu ya Laela

hadi Sumbawanga zimeanza mwezi Julai 2006 chini ya usimamizi wa *TANROADS*. Wizara yangu imeelekeza wahakikishe kwamba michoro itakayoandaliwa na Mhandisi Mshauri inajumuisha barabara za wapita kwa miguu na miundombinu nyingine ambayo itasaidia kupunguza ajali kutokea katika eneo la Mji wa Sumbawanga.

(c) Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kutatua matatizo ya usafiri kwa Mkoa wa Rukwa ili kurahisisha usafirishaji wa mazao mbalimbali yanayolimwa Mkoani humo nia hiyo ipo. Ili kufanikisha lengo hilo, Wizara yangu itaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa barabara zitakazounganisha Mji ya Sumbawanga na Kasanga na pia Sumbawanga hadi Mpanda ili kuunganisha barabara hiyo na reli na pia Mkoa wa Kigoma.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ndugu yetu Basil Mramba ukurasa wa 22 alioanisha barabara karibu 10 ambazo zitajengwa kwa kiwango cha lami kwa mwaka huu wa fedha, Sumbawanga ikiwa mojawapo kutoka Tunduma. Lakini katika Bajeti yake aliyokuwa ameiweka ameweka shilingi milioni 867 tu ambayo ni sawa na km 2 au 3 kama hiyo ni kweli;

(a) Je, Serikali ina nia nzuri ya kujenga barabara ya Tunduma hadi Sumbawanga wakati barabara nyingine zimepata mabilioni ya fedha? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amekubali ya kwamba kutakuwa na mpango wa kugawa sehemu mbalimbali ili barabara hiyo kwa vile ni ndefu kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga Makandarasi walau watatu/wanne wapatikane. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami ya kwamba ili wananchi wa Mkoa wa Rukwa waamini kwamba kweli wanajengewa barabara basi upande mmoja wa upande wa Rukwa barabara ianzie Sumbawanga na nyingine ianzie Tunduma. Wakati huo huo makandarasi wale ambao wanaonekana wameshindwa kutekeleza wajibu wao wasiruhusiwe tena kujenga barabara hii kama walivyofanya katika Mikoa mingine? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Kimiti kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia barabara hii pamoja na Wabunge wengine wa Mkoa wa Rukwa. Kuhusu maswali yake, swali la kwanza kwamba fedha zilizotengwa ni kidogo shilingi milioni 867 kama nilivyosema kwa kweli fedha hizi ni za kukamilisha usanifu wa kina, lakini fedha za ujenzi hazikuwa kwenye Bajeti ya mwaka huu. Lakini nilitaka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Kimiti kwamba barabara hii ina mategemeo makubwa ya kuanza kujengwa mwakani kwa sababu imewekwa katika kipaumbele ya kupata (*MCC*) *Millennium Challenge Cooperation.* Kwa hiyo, nina hakika kwamba tukishamaliza shughuli hizi za usanifu barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kutokana na fedha hizo ambazo zinatoka nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ushauri kama nilivyosema katika jibu la msingi baada ya mshauri kukamilisha kazi yake tutaangalia kwamba barabara ile tuigawe katika sehemu ngapi za ukandarasi kama ni sehemu mbili au tatu itategemea na ushauri utakaokuwa umetolewa. Wazo lake mkandarasi mmoja aanzie Sumbawanga mwingine

aanzie Tunduma ni suala ambalo ni jema tutaliangalia kutegemea na utaalam utakaokuwa umetushauri. Kwa hiyo, mimi nadhani hili suala ambalo linaweza likaangaliwa. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Rukwa, pamoja na wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Mikoa ya jirani kwamba nia ya Serikali kujenga barabara hii iko juu sana kwa sababu barabara hii iko katika *priority* namba moja. (*Makofi*)

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, swali langu linahusu sehemu ya (c) ambapo Bandari ya Kisanga inatajwa. Kutokana na uchambuzi wa kiuchumi inaonekana kwamba wenzetu wa upande wa Kusini wameamua kuunganisha Mpulungu na Kasama ili waelekeze bidhaa zote na mizigo yote upande wa Kusini na hivyo kudhoofisha *TAZARA*. Je, isingekuwa vizuri wakati wanafikiria wazo hili wakawa wanafikiria uwezekano wa kujenga barabara ya moja kwa moja kutoka Tunduma hadi Kasanga na ikiwezekana hata reli kusudi kufufua kutumia bidhaa za Congo na vile vile kutumia vizuri reli ya *TAZARA*? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, wazo lake kwa kweli ni zuri linaweza kuangaliwa kwa maana ya mipango ya muda mrefu. Lakini kwa sasa mpango wa Serikali baada ya barabara hii niliyoielezea katika jibu langu la msingi tunaendelea kuboresha barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Kasanga ambayo tayari na Sumbawanga kwenda Kasese kupitia Matai. Uboreshaji huu unafanyika na wakala wa *TANROADS* ili kuhakikisha barabara hizi za kwenda Kasese pamoja na Kasanga zinapitika wakati wote ili kuwezesha kufika katika *Port* ya Kasanga. Lakini vile vile katika mipango ya Wizara Bandari ya Kasanga iko katika utaratibu wa kukarabatiwa ili iweze kuwezesha usafirishaji wa mizigo katika Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, fedha zimetengwa kwa ajili ya *berth* ile ya Kasanga na iko katika Bajeti ya mwaka huu. Kwa hiyo, nia ya Serikali ni kuweza kuibua uchumi wa maeneo haya na kuwezesha usafirishaji wa mazao pamoja na watu kuweza kufanikisha. (*Makofi*)

Na. 350

**Ujenzi wa Barabara ya Kisesa – Fella hadi Usagara (Mwanza)**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. JACOB D. SHIBILITI)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Kisesa – Fella hadi Usagara (Mwanza) ilishafanyiwa upembuzi yakinifu tayari kwa ujenzi:-

(a) Je, ujenzi wa barabara hiyo utaanza lini?

(b) Je, gharama za ujenzi huo zitagharamiwa na nani kwa kiwango gani kwa fedha za Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, barabara ya Usagara – Fella – Kisesa inayojulikana pia kama *Kisesa Bypass* ni sehemu ya barabara zilizopo kwenye Ukanda wa Ziwa *(lake circuit corridor)*. Barabara hii inaunganisha barabara ya Mwanza – Nyangunge – Musoma katika eneo la Kisesa na barabara kuu ya Mwanza – Shinyanga katika eneo la Usagara. Barabara hii ina urefu wa kilometa 17 na hivyo inafupisha safari kwa kilometa 22 ukilinganisha na ile ya kupitia Mjini Mwanza na pia kukwepesha magari makubwa kutoka au kuelekea Musoma yasipite Mwanza Mjini. Barabara hii ilifanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2005. Matokeo ya upembuzi huu yalionyesha kuwa barabara hii ina faida (*economically feasible*) kama ikijengwa kwa kiwango cha lami. Hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kuitisha zabuni za kumpata Mhandisi Mshauri (*consultant*) atakayefanya kazi ya usanifu wa kina.

(b) Mheshimiwa Spika, usanifu pamoja na ujenzi wa barabara hii utagharamiwa kwa pamoja kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*) na Serikali ya Tanzania. Gharama za usanifu zimekisiwa kugharimu jumla ya shilingi milioni 705 na gharama za ujenzi kwa kiwango cha lami ni shilingi bilioni 10.2. Gharama halisi zitajulikana baada ya zabuni kuwasilishwa na kuchambuliwa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ninashukuru Serikali kwamba imekiri kwamba hii ya Kisesa – Fella mpaka Usagara ni muhimu sana katika magari ambayo yanaweza kuinua uchumi wetu. Kumekuwa kunafanyika upembezi wa barabara kama hizi lakini utekelezaji wake umekuwa si wa karibu sana. Kwa kuwa upembezi umeshafanyika wa Kisesa – Fella Usagara na barabara ya Kisesa Fulo, Sumve mpaka Nyambite umeshakamilika na haya ni hizi ni barabara ambazo zinafungua Wilaya ya Kwimba, Wilaya ya Magu na Misungwi. Je, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa kutengeneza barabara hizi muhimu kwa kiwango cha lami? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** katika jibu langu la msingi nimezungumzia utengenezaji wa barabara hiyo ya Kisesa *Bypass* kwa kiwango cha lami. Kusema kwamba utekelezaji wa barabara hizi unachelewa ni kutokana ni ukosefu wa fedha na kama unavyoona kwa mfano hata barabara hii fedha zinatafutwa kutoka nje ya nchi na pale ambapo fedha zinatafutwa kwa wafadhili inabidi usubiri kwa kweli. Lakini hata uwezo wetu wa ndani haupo wa kuweza kujenga barabara zote kwa mara moja kwa kiwango cha lami na ndiyo maana tunajaribu kupanga tu vipaumbele ili hatimaye katika kufikia mwaka 2015 kama ambavyo tumeweka angalau *trunk roads* zote ziwe zimejengwa kwa lami. Sasa amezungumzie barabara nyingine, hiyo tutaendelea kuiboresha kwa sasa kwa kiwango ambacho tunafanya cha changarawe lakini kwamba na yenyewe ijengwe kwa lami katika kipindi hiki bado uwezo wa fedha hakuna.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Fella hadi Usagara ni mwendelezo wa barabara ya Usagala kwenda Geita na barabara ya Usagara kwenda Geita ndiyo inapokea magari makubwa yote yanatokea maeneo hayo. Kwa kuwa Serikali ilishatangaza tarehe 1 mwezi 7 kupata mzabuni wa kutafuta mkandarasi wa kutengeneza barabara ya kutoka Usagara kwenda Geita. Je, hatua hii imefikia wapi tunasubiri kuona kazi inafanyika? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo yeye mwenyewe amekubali au ameliona tumeshatangaza tenda kwa ajili ya kufanyia usanifu wa kina barabara hiyo na kuanza ujenzi kwa mpango wa *design* mbili. Kwamba umefikia wapi, ni kwamba taratibu zinaendelea kama kawaida na hakuna kilichorudi nyuma kwa sababu katika taratibu za *procurement* ziko taratibu unangoja unapokea unafungua. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba ile ratiba ambayo tulitoa kwa Wabunge husika inaendelea kuzingatiwa na hakika barabara hii itaanza kujengwa kama tulivyoahidi hapa Bungeni.

Na. 351

**Ujenzi wa Maabara Katika Shule Nchini**

**MHE. SAID AMOUR ARFI - (K.n.y. MHE. CHACHA ZAKAYO WANGWE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 1999 Serikali ilitoa fedha kwa wakandarasi mbalimbali kujenga maabara za kwenye shule za sekondari hapa nchini na maabara 5 kati ya 7 zilizotakiwa kujengwa Mkoa wa Mara zimekamilika na kukabidhiwa lakini maabara mbili (2) za shule za Mogabiri na Manga – Tarime hazikujengwa na Mkandarasi *Wesons (T) Ltd* ambaye alishapewa fedha za kazi hiyo kutoka Serikali:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa mkandarasi huyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikamilisha maabara hizo kwani wanafunzi wa Manga na Mogabiri wanaendelea kupata shida na kusababisha wanafunzi hao kutofanya vizuri katika masomo ya Sayansi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali dhidi ya Mkandarasi aitwaye M*/S Weason (T) Ltd* aliyeshindwa kuendelea na ujenzi wa maabara za Shule za Sekondari ya Manga na Mogabiri zilizoko Wilaya ya Tarime ni kama ifuatavyo:-

- Kumsimamisha Mkandarasi huyo kulingana na mkataba wa ujenzi.

- Kumwandikia Msajili wa Bodi ya Wakandarasi (*CRB*) juu ya uzembe wa Mkandarasi huyo, ambapo naye alimwandikia barua ya kumwonya na kuchukua hatua kwa mujibu wa taratibu zao.

- Wizara imezuia gharama ya *performance Bond* ambayo anaweka Mkandarasi dhidi ya mwajiri wake pindi akishindwa kumaliza kazi kulinga na mkataba. Dhamana hii hufidia asilimia kumi (10%) ya gharama za ujenzi. Vile vile Wizara imezuia *Retention Fund* ambayo asilimia 10 yake hukatwa kama tahadhari iwapo kazi iliyofanyiwa na mkandarasi itakuwa na kasoro au inatakiwa ifanyiwe marekebisho.

(b)Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kukamilisha ujenzi wa maabara hizo ni kujenga kwa utaratibu wa *force account* kwa kuwatumia wahandisi wa Wizara. Makubaliano yamefikiwa kati ya Serikali na benki ya *ADB* juu ya kumalizia ujenzi wa utaratibu huo. Fedha za kumalizia kazi iliyobakia zitatokana na:-

-Fedha zilizotengwa kwenye mkataba kwa kazi ambayo haijafanyika.

-Fedha zilizotokana na zuio la dhamana *(perfomance bond)* na *(retention fund)* ya asilimia 10 ya gharama za ujenzi na makato ya malipo ya mkandarasi kwa kazi aliyofanya ambayo hakuikamilika.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tunapongeza kwanza jitihada za kukamilisha majengo, lakini kujenga na kukamilisha majengo ya maabara ni moja. Vifaa vya maabara ni muhimu zaidi ili maabara hizo zinazojengwa ziweze kutumika ipasavyo. Je, Serikali iko tayari kupeleka vifaa vya maabara katika majengo ya maabara iliyojengwa katika shule ya sekondari ya Inyonga? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba kwa kuwa Serikali imeonyesha nia ya kuzikamilisha ni dhahiri kwamba haitaitwa maabara mpaka iwe na vifaa ndani yake. Lengo hilo tunalo na hata katika Bajeti yetu tumeonyesha kwamba kuna nia madhubuti ya kuziboresha maabara kwa kuzipatia vifaa. (*Makofi*)

Na. 352

***CD4 Count Machine* na Elimu Juu ya ARVs kwa Wananchi.**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. ELIETTA SWITI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imejitahidi kupeleka *CD4 Count Machine* kila hospitali ya Mkoa ili kuwapa fursa waathirika wa Virusi vya UKIMWI kupima na kujiandaa kutumia *ARVs*, na kwa kuwa Wananchi wengi wanashindwa kwenda kupima japo hawagharamii vipimo vyenyewe.

(a) Je, upo uwezekano wa Serikali kupeleka *CD4 Count Machines* kwenye Hospitali za Wilaya kusaidia wasiojiweza kiuchumi?

(b) Pamoja na kupeleka *CD4 Count Machines* Mikoani, je, upo uwezekano wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya *ARVs* na matumizi yake?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu Swali la Mheshimiwa Elietta Switti, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Ni azma ya Serikali kupeleka mashine za *CD4 Count* katika hospitali za Wilaya kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha za kununua mashine hizo. Hii inakwenda sambamba na sera ya Wizara ya kupeleka huduma karibu na wananchi. Hivi sasa Wizara inaendesha mafunzo kwa wataalam wa kuziendesha mashine hizo katika ngazi hiyo. Hadi sasa Wilaya tatu zimepatiwa mashine hizo, zikiwemo Rombo, Same na Makete.

(b)Zoezi la kutoa elimu kwa wananchi kuhusu dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI yaani *ARVs* tayari limeanza katika vituo vyetu vya kutolea huduma, machapisho mbalimbali na vipindi vya radio na televisheni. Wananchi wote wanaopata fursa ya kupata ushauri nasaha wanaelezwa kuwapo kwa dawa hizi hapa nchini, kwamba zinatolewa bure kwa wale wanaostahili kupata, umuhimu wa kutokatisha matumiz pindi wakianza kutumia na *side effects* zinazoweza kutokea. Kampeni ambayo itahitimishwa tarehe 5 Agosti, 2006 inalenga kuwapa wananchi uelewa wa masuala ya UKIMWI pamoja na kuwahimiza waungane na Serikali yao katika mikakati ya kuongeza kazi ya kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Naomba anitumie Bunge lako Tukufu kuwaeleza wananchi kuwa *ARVs* hazitolewi kwa kila mtu anayegundulika kuwa na Virusi vya Ukimwi bali wanapewa wale ambao kinga yao kwa mujibu wa vipimo imepungua sana. Aidha, silaha ya kuaminika kama tunataka kushinda mapambano dhidi ya UKIMWI na tumedhamiria kuushinda, ni kuzuia maambukizi. Hivyo kampeni na elimu vinaendelea kusisitizwa.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akijibu suala hili alisema mpaka sasa hivi ni Wilaya tatu ambazo zimepata dawa za *CD4*, je, ni kigezo gani kinachotumika katika kuchangia kuwapelekea hizi mashines katika hizi Wilaya? Ni idadi ya wagonjwa au ni vigezo gani vinavyotumika? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, hakuna kigezo muhimu ambacho kimewekwa kuwapelekea mashine za *CD4 count* Wilaya lakini kuna masuala mengine lazima tuangalie kwa mfano Wilaya ya Makete ambao wamepata *CD4 count mashine* hivi sasa ni mojawapo ya Wilaya ambazo zimeathirika sana. Kwa hiyo, tumeona kwamba ni vizuri waweze kupata hizi kwa sababu wagonjwa ni wengi sana ukiangalia katika takwimu ili waweze kupatiwa huduma. Lakini hakuna kusema kwamba ni labda iliyo na wagonjwa wengi au vipi hatuna *criteria* ya kutoa. (*Makofi*)

Na. 353

**Hospitali ya Kibondo Kupatiwa Jokofu na Umeme**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hospitali ya Wilaya ya Kibondo haijawahi kupata jokofu na pindi wagonjwa wanapofariki kama ndugu zao wako mbali hulazimika kuzikwa siku hiyo hiyo kuepuka athari za miili kuoza:-

Je, lini Serikali itapeleka jokofu na jenereta ya umeme katika hospitali ya Wilaya ya Kibondo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo:-

Katika kuendesha na kuboresha huduma za afya kwa Serikali imeziwezesha Halmashauri za Wilaya kuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo:-

1. Fedha za Mishahara.
2. Fedha za Maendeleo.
3. Fedha za Mfuko wa Pamoja (*Basket Fund).*
4. *O.C.* (*Other Charges).*
5. 5% toka Halmashauri.
6. Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa.
7. Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*).

Mheshimiw Spika, katika utamaduni wetu, mwili wa marehemu unastahili kupewa heshima zote na wakati mwingine kuzidi heshima alizopewa hata akiwa hai. Ni wajibu wa jamii na Serikali kuhakikisha kuwa mwili wa Marehemu unatunza vizuri hadi wakati wa mapumziko Marehemu anapopumzishwa kwa mara ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali inatoa fedha na kuzipeleka Wilayani ambapo kila Wilaya inapanga mipango yake kabambe ya Afya Wilayani na kuainisha vyanzo vya fedha zitakazotumika kufuatana na uzito na matatizo na vipaumbele vilivyoainishwa. Wilaya zote hivi sasa zinaweza kununua vifaa vingi na dawa zinazohitajika kwa kutumia mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaishauri Wilaya ya Kibondo pamoja na wilaya nyingine zenye tatizo kama hili, kuweka mpango wa ununuzi wa jokofu la chumba cha maiti na jenereta ya umeme katika mipango kabambe ya afya ya Halmashauri ya Wilaya kwa kutumia fedha za maendeleo (*Development Budget*) pamoja na mifuko ya afya kama ilivyo kwa magari ya wagonjwa. (*Makofi*)

**MHE. FELIX N. KIJIKO**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na pia napenda kushukuru kwa majibu mazuri ambayo Naibu Waziri ametoa. Lakini kwa kuwa Wilaya ya Kibondo imekuwa na ongezeko la watu na hasa baada ya ujio wa wakimbizi na kwa kuwa suala la wakimbizi linafahamika Kiserikali pamoja na kwamba tunalipiga vita kwamba wakimbizi waondoke. Je, Serikali haioni kwamba ina haja ya kuongeza huduma kwa sababu ongezeko la watu katika Wilaya hiyo limesababishwa na wakimbizi siyo wale watu wa Kibondo kama ilivyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NDANI YA NCHI (k.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII)** Mheshimiwa Spika, katika zile Wilaya ambazo zina wakimbizi ikiwemo Wilaya ya Kibondo anakotoka muuliza swali, Serikali ikishirikiana na Shirika la Wakimbizi Duniani *UNHCR* na wafadhili mbalimbali wanajenga hospitali za nyongeza kwanza ndani ya makambi yenyewe na vijiji vinavyozunguka makambi wanapeleka madawa ya nyongeza katika zahanati zinazozunguka yale makambi.

Kwa hiyo, nilitaka kulihakikishia Bunge lako tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba kwa kweli maeneo ya wakimbizi wanapata huduma ya nyongeza kwa mzigo wa nyongeza walionao wa kuhifadhi wakimbizi. *(Makofi)*

Na. 354

**Mazao Mbadala kwa Wakulima wa Pamba Songwe**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1997 zao la pamba ambalo ndilo lililokuwa zao la biashara katika Tarafa ya Songwe lilisitishwa kutokana na kugundulika kwa funza wekundu na kwa kuwa, wananchi wa maeneo hayo wameitikia wito wa Serikali wa kulima mazao mengine ya ufuta, alizeti, mlonge badala ya pamba lakini hawana mbegu za mazao hayo:-

(a) Je, Serikali katika kuunga mkono juhudi za wananchi hao inaweza kuwatafutia mbegu za mazao hayo?

(b) Kwa kuwa wananchi hao sasa wamehamasika kuunda umoja wa kuweka na kukopa (*SACCOS*). Je, Serikali inaweza kutoa mikopo kwa wakulima ili waendeleze kilimo hicho kwa faida na maendeleo yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida, Serikali haitoi mbegu kwa wakulima ila inawashauri na kuwaelekeza mahali pa kuzipata. Serikali huwajibika kuwapatia mbegu wakulima wakati wa dharura tu ambapo wananchi hawana uwezo wa kupata mbegu hizo. Katika hali ya kawaida wananchi hawana budi kujitafutia mbegu bora kutoka katika vyanzo vilivyopo. Kwa upande wa zao la ufuta, zipo aina za mbegu zenye sifa nzuri zilizozalishwa katika Shamba la Utafiti la Serikali la Msimba, Arusha na Kituo cha Utafiti cha Naliendele, Mtwara.

Aina hizi za mbegu ambazo ni Lindi 02, Naliendele 92, Ziada 94 na Zawadi 94 zina sifa ya ukinzani dhidi ya magonjwa na wadudu, zinakomaa haraka na zinatoa mafuta mengi. Mbegu bora za Alizeti aina ya *record* zinapatikana katika Mashamba ya Mbegu ya Serikali ya Msimba, Dabaga, Arusha na Kituo cha Utafiti cha Ilonga, Kilosa. Zipo pia aina ya mbegu chotara za Alizeti kama vile *PAN 7369* na K Fedha ambazo zinatolewa na Kampuni binafsi za mbegu za *Kibo Seed Ltd* na *Pannar Seed Ltd*. za Mjini Arusha.

Hadi sasa, hakuna kampuni au taasisi inayozalisha mbegu za mlonge. Mbegu za zao hilo zilikuwa zinasambazwa na Kampuni ya *Optima Afrika Ltd.,* ambayo hivi sasa imesitisha ununuzi na usambazaji wa mbegu hizo baada ya kusimamisha shughuli zake nchini. Chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya ikiwemo Wilaya ya Chunya wakulima wanahimizwa kuzalisha aina za mbegu za ufuta na alizeti ambazo si chotara, katika madaraja ya kuazimiwa *(Quality Declared Seeds)* chini ya mpango wa uzalishaji mbegu vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo unao utaratibu wa kutoa mikopo kwa kupitia Shirikisho la Vyama vya Kuweka na Kukopa (*SCCULT*). Masharti ya mikopo ni pamoja na:-

Maombi ya mkopo kupitishwa na Afisa Kilimo na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, *SACCOS* kusajiliwa kisheria, *SACCOS* kuwa na akiba isiyopungua theluthi moja ya mkopo unaoombwa, muhtasari wa kikao kilichoridhia kukopa na *SACCOS* inayoomba mkopo kuwa mwanachama wa *SCCULT*.

Tangu utaratibu huo ulipoanza msimu wa 2003/2004, jumla ya *SACCOS 142* zilikwishakupewa mikopo ya pembejeo yenye thamani ya shilingi 3,081,074,000. Miongoni mwa *SACCOS* za Mkoa wa Mbeya zilizokopeshwa ni pamoja na tatu za Wilaya ya Chunya ambazo ni Chunya Kurugenzi *SACCOS,* Matwiga *SACCOS* na Lupatingatinga *SACCOS* zilizopewa mkopo wa jumla ya shilingi 19,000,000.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wananchi majimboni mwao wajiunge katika Vyama vya Ushirika vya

Akiba na Mikopo ili waweze kunufaika na fursa hii ya kukopa kutoka kwenye Mfuko wa Pembejeo.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake ambayo ni maelekezo ya matumaini. Nina swali moja dogo la nyongeza. Mwaka jana kulifanyika majaribio ya kujaribu kuangalia kama yule mdudu bado yupo. Na bahati mbaya ikaonekana kwamba yule mdudu yupo, anaendelea tena ndiyo ananenepa kweli kweli. Sasa swali je, huyo mdudu kwa sababu bado anaendelea na kwa sababu pamba hailimwi sasa hivi ambacho ndicho kilikuwa chakula chake. Hawezi kushambulia mazao mengine?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naamini yule mdudu anayemsema japo hakumtaja anamzungumzia mdudu funza, kama ndivyo Wizara yangu bado inaendelea kumdhibiti mdudu huyo, na kama tunavyojua tatizo kama hilo linapojitokeza wataalam wanalishughulikia na haliwezi likaisha kwa wakati huo huo kwa sababu mambo mengine ni masuala ya utafiti.

Mpaka sasa hivi sisi tunaendelea kiwizara kuhakikisha kwamba karantini tuliyoweka kudhibiti kueneza ugonjwa huo inaendelea. Na tatizo ambalo hivi sasa lililopo ni kwamba wakulima wangependa waruhusiwe walime pamba katika eneo hilo. Lakini sisi hatuwezi kuruhusu pamba iendelee kulimwa halafu mdudu yule azungushwe Tanzania nzima na kuharibu maeneo mengine ya pamba.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara inaendelea kuchukua hatua za kumdhibiti mdudu huyu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali hivi sasa kimekwisha. Ninayo matangazo. Mtaniwia radhi leo ni mengi kidogo. Kwanza kuhusu wageni, ningependa kutambulisha Bibi Kudra Maghembe, kwenye *Speaker's Gallery* ni mke wa Waziri wa Kazi, yupo na sisi. Yule pale, karibu sana!

Wapo Viongozi 12 wa Vyama vya Wafanyakazi nchini ambavyo ni TUKTA, RAU, CHODAU, TUICO, TUJ, TUGHE, CWT, DOWTA na TRAU wako kwenye *Speaker's Gallery.* Naomba msimame. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vijana wetu wa Solassian Seminary ya Mjini Dodoma kundi lingine wapo hapa leo pamoja na Walimu wao, nawaona upande wa kushoto pale. Naomba msimame. Karibuni sana. Pia tunao vijana 25 kutoka Taasisi ya *Tanzania Youth Aware (TAYOA)* wakiongozwa na Mkurugenzi Ndugu Peter Masika. *TAYOA* wale pale upande wa kulia. Karibuni sana. Miongoni mwenu tunaanza kubaini viongozi wa baadaye. Tunawatakia kheri katika yote mema mnayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bura, ameniomba niwatambue viongozi wa *TUICO* toka Matawi ya *CRDB* nchi nzima ambao pamoja nao yupo Katibu Mkuu Msaidizi wa *TUICO* Taifa, Ndugu Ngemela, wale pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri Miundombinu, leo amebahatika kupata mgeni wake ambaye ni mkewe Florence pamoja na Binti yao anaitwa Consolata, nadhani wako *Speaker's Gallery*. Hapana, loo*!* Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri mnapokuwa na wageni wenu ni kumwarifu Ofisini kwangu, Bwana Ndalu ili wakaye *Speaker's Gallery.* Inafaa zaidi. Tunawaenzi na mna kazi ngumu sana. Ahsante Mheshimiwa. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Godfrey Zambi, wanawe wawili wapo hapa, Samwel Zambi na Jackline Zambi. Wale pale. Karibuni sana Wajukuu zangu. Kutoka *Press Club Mbeya* Mheshimiwa Mpesya, ana wageni ambao ni Waandishi wa Habari, Bwana Said Benjamin, Bi. Janet Mwenda na Bi. Esther Macha kutoka *Mbeya Press Club.* Wale pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Kutoka Maswa, Mheshimiwa Shibunda, ameniomba niwatambulishe wageni Ndugu Emmanuel Mwandu, Katibu wa Baraza la Madiwani wa CCM Maswa, yule pale. Ndugu Daudi Malando, Katibu Kata wa CCM Shishiu. Yule pale na Ndugu Samwel Mwanga, Mwandishi wa Habari wa Jimbo la Maswa. Yule pale. Ahsante sana, karibuni sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, ametembelewa na mgeni ambaye anamwita mwanawe wa pekee wa kiume jina lake ni Abdulrahaman Mpakanjia, ana umri wa miaka mine, yule pale *Speaker's round.* Ahsante sana. Huyu mtoto anaonekana ni machachari kama mama yake huyu. Karibu sana mjukuu wangu. *(Kicheko/Makofi)*

Matangazo mengine, kutakuwa na semina kesho saa 5 asubuhi juu ya huduma za kifedha kwa wananchi wenye kipato cha chini, semina hii muhimu sana sana. Hii ni Jumapili kweli, samahani. Hii ni ya Jumapili tarehe 6. Hakuna semina kesho. Basi nikipata taarifa nyingine nitawatangazia. Lakini hii ni semina ya Jumapili saa 5 inahusu huduma za kifedha kwa wananchi wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Adam Malima, Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Fedha na Uchumi, ananiomba nitangaze kwamba kutakuwa na kikao na Uongozi wa *Standard Chartered* kwa hiyo Waheshimiwa wafutao wanaombwa wahudhurie leo Ijumaa tarehe 4 saa 5 asubuhi. Mheshimiwa Harisson Mwakyembe, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Gedion Cheyo, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Saa 5 ukumbi Na.133.

Pia Mheshimiwa huyo huyo Adam Malima, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ameniomba nitangaze kuwa kutakuwa na kikao saa hizo hizo kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Nadhani maana yake ni kwamba Wajumbe wa Kamati pamoja na hawa wa Kamati nyingine niliowasoma Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Gedion Cheyo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Anne Malecela, kumbi ni tofauti, basi nadhani mkikutana mtaweza kuelewana wapi muweze kwenda.

Waheshimiwa Wabunge sina matangazo mengine. Kwa hiyo sasa namwita Katibu ili tuendelee na shughuli zinazofuata. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
### Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inayohusu Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, na kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili mpango wa kazi na kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwa Wizara yangu hotuba hii ni ya kwanza baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana. Hivyo, naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura za kihistoria kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa Makamu wa Rais. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, na kupitishwa na Bunge lako tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue fursa hii kuwapa pongezi Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi katika uchaguzi uliopita na kwa wengine wote. Na, niwapongeza kwa dhati wabunge wote walioteuliwa na Rais kuwa Mawaziri na Manaibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu lilipokutana hapa Dodoma mwezi Januari 2006, lilikuchagua wewe kuwa Spika na Mheshimiwa Anne Semamba Makinda kuwa Naibu Spika. Niruhusu pia nikupongeze wewe pamoja na Mheshimiwa Job Ndungai na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Wananchi wa Mwanga kwa kunipa ushindi wa Kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na kuniwezesha niwe Mbunge wao. Nawaahidi kutumia uwezo wangu kwa kadri atakavyonijalia Mwenyezi Mungu, kuwatumikia na kushirikiana nao katika kuleta maendeleo ya Wilaya yetu. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua kuwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 24 na 25 Juni 2006 Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi ulimchagua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kauli moja kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Napenda kumpa pongezi zangu za dhati, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Yusuph Rajab Makamba kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi. Aidha nawapongeza Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mheshimiwa Rostam Aziz, Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mheshimiwa Salehe Ferouz, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro na Mheshimiwa Jaka Mwambi kwa kuteuliwa kwao katika nyadhifa nyeti ili waiongoze Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakhia Hamdani Meghji kwa hotuba zao nzuri zilizoelezea vema mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2006/2007. Malengo, maelekezo na vigezo vilivyomo kwenye Hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii pia kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Haroub Masoud Mbunge wa Koani, iliyojadili na kuyakubali makadirio ya matumizi ya Wizara yangu tarehe 5 Juni, 2006. Hotuba hii imezingatia ushauri uliotolewa na kamati ambao tunaamini utaiwezesha Wizara kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kutoa maelezo kuhusu majukumu ya Wizara yangu kwa ujumla:-

Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana inazo Idara tano ambazo ni, Idara ya Kazi, Idara ya Ajira, Idara ya Maendeleo ya Vijana, Idara ya Utawala na Utumishi na Idara ya Sera na Mipango.

Aidha, Wizara inavyo vitengo vya Fedha na Uhasibu, Ukaguzi wa Ndani na Kitengo cha Mawasiliano na Habari. Aidha, Wizara inasimamia shughuli za Ofisi, Mashirika na Taasisi zifuatazo:-Ofisi ya Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA)* Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* na Mahakama ya Kazi

Aidha, Wizara ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana; Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii; na Sera ya Taifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi. Ufuatayo ni muhtasari wa maelezo ya majukumu ya kila Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Kazi ina jukumu la kuratibu na kusimamia Sera na Sheria za kazi ili kuleta amani sehemu za kazi kwa kulinda haki na wajibu wa wafanyakazi na waajiri, kupunguza na kutatua migogoro ya kikazi, kukuza majadiliano kati ya wafanyakazi na waajiri kwa azma ya kuwezesha ukuaji wa uchumi, ajira, tija na kulinda kazi ya staha (*Decent Work*).

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ajira ina jukumu la kuratibu masuala ya ajira nchini pamoja na kuainisha na kupendekeza maeneo muhimu ya kukuza ajira kama nyenzo muhimu ya kuondoa umasikini.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maendeleo ya Vijana ina jukumu la kubuni na kusimamia Sera na Taratibu zinazojenga mazingira endelevu, yanayowawezesha vijana kujiimarisha kiuchumi na kijamii na kukua katika maadili mema.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Utumishi ina majukumu mbalimbali yakiwemo ya kuajiri, kusimamia utendaji kazi, kusimamia na kuendeleza masuala ya jinsia, kutoa mafunzo ya utendaji kazi, kupambana na rushwa na ugonjwa hatari wa UKIMWI Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri anasimamia na kuratibu shughuli za vyama vya wafanyakazi na waajiri nchini kwa mujibu wa sheria Na. 10 ya Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya Kazini *(OSHA)* uliozinduliwa mwaka 2001 chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997, una jukumu kubwa la kufanya ukaguzi katika viwanda na maeneo mengine ya uzalishaji, ili kuhakikisha kuwa mazingira, na nyenzo za kazi zinazotumiwa katika uzalishaji mali hazihatarishi usalama, afya na maisha ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii lina majukumu ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kulipa mafao kwa wanachama. Aidha ili kuboresha mafao ya wanachama Shirika litaendelea kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali kama vile dhamana za Serikali, mabenki, mikopo na hisa za makampuni yaliyosajiliwa kwenye soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE)* na katika ujenzi wa nyumba na ofisi za kupangisha na kuuza.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa lina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli za kuboresha Tija katika Taifa letu ili kuongeza pato la Taifa, kama kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya kazi ina majukumu ya kusikiliza na kuamua; na kukaza hukumu za migogoro ya kiajira na kusimamia utoaji haki, upatikanaji wa tija na udumishaji wa mahusiano mazuri na ya utulivu kati ya waajiri na wafanyakazi mahali pa kazi kama ilivyoainishwa katika Sheria Na. 41 ya mwaka 1967 na kufanyiwa marekebisho mbalimbali, Sura ya 60 toleo lililorejewa 2002,

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa majukumu na ahadi zilizoihusu Wizara yangu kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

Katika kutekeleza awamu ya kwanza ya marekebisho ya Sheria Na.6 ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria Na. 7 ya Taasisi za Kazi za mwaka 2004, Baraza la Kazi, Uchumi na masuala ya Kijamii *(LESCO)* limeundwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 7/9/2005.

Kwa msaada wa *DANIDA,* ukarabati wa ofisi za kazi katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam umeanza kufanyika.

Mafunzo yametolewa kwa maafisa kazi na wabia jamii juu ya sheria mpya za kazi. Jumla ya maafisa 90 wameshiriki katika mafunzo haya.

Madai 166 ya malipo ya fidia kwa watumishi walioumia kazini yalipokelewa na kiasi cha Shilingi milioni 17 zimelipwa.

Migogoro 117 ya kikazi ilipokelewa na kushughulikiwa. Kati ya hiyo migogoro 72 imefikishwa Mahakamani kwa rufaa.

Rufaa 265 zilizopokelewa kutoka kwa wafanyakazi na waajiri zilipelekwa kwa Waziri kwa maamuzi. Kati yake rufaa 155 zilishughulikiwa hadi hatua ya maamuzi.

Mikataba ya hiari 19 ilipokelewa na kushughulikiwa. Mikataba 26 ikiwemo malimbikizo ya mwaka uliopita ilipelekwa kusajiliwa katika Mahakama ya Kazi.

Uandaaji wa Rasimu ya mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii umekamilishwa.

Wizara kwa kushirikiana na wadau wakuu wa masuala ya kazi ikiwamo Wizara ya Kazi, Wanawake, Vijana na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Nchi Huru za Afrika, huko Cairo-Misri na Mkutano Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani huko Geneva Uswisi.

Maandalizi ya *Best Practices and Code of Conduct* kwa ajili ya kupambana na UKIMWI sehemu za kazi yamekamilishwa.

Mkakati wa kuzuia ajira ya mtoto umetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili kuufanya ueleweke kwa urahisi zaidi na kusambazwa kwa wadau.

Mkataba wa makubaliano na Shirika la Kazi la Dunia *(ILO)* ili kutekeleza awamu ya pili ya mpango wa kukomesha utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari ulisainiwa. Chini ya usimamizi wa Idara ya kazi mabaraza 20 ya ushirikishaji wafanyakazi sehemu za kazi katika mashirika, Taasisi za Umma na Taasisi za Serikali yaliundwa.

Mafunzo kwa watumishi mbalimbali 300 yaliendeshwa katika Taasisi za Umma na binafsi kuhusu Sheria mpya za Kazi, pamoja na kujulishwa wajibu na Majukumu yao kama wajumbe wa mabaraza ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 majukumu yafuatayo yalitekelezwa:-

Ukarabati wa jengo kwa ajili ya kufungua Kituo cha Ajira *(Labour Exchange Centre)* katika Jiji la Mwanza umeanza, ili kupanua wigo wa huduma za ajira kwa Umma. Kituo hicho kinatarajia kuanza kutoa huduma mara ukarabati huo utakapokamilika mapema mwaka huu. Uanzishaji wa kituo hicho ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa muda mrefu wa kuanzisha vituo vingine kwa kanda, ambapo tunatarajia kuweka vituo katika miji ya Mbeya, Arusha, Dodoma na Mtwara.

Kituo cha Ajira cha Dar es Salaam kimeandikisha watafuta kazi 1,150 katika kipindi cha Julai 2005 hadi Juni 2006. Kituo hicho kilipata nafasi 677 za kazi na kiliweza kuwaunganisha watafuta kazi 712 na waajiri kwa kipindi hicho.

Watafuta kazi 894 walipatiwa ushauri nasaha na mafunzo ya kujiandaa kwa usaili pamoja na mbinu za kujitafutia kazi. Mafunzo haya huwasaidia watafuta kazi kufanya vizuri katika usaili na hivyo kujiongezea uwezekano wa kuajiriwa, na pia kuwawezesha kujitafutia kazi wao wenyewe bila kusubiri kituo kiwatafutie.

Kituo cha Ajira kilishiriki kwa ufanisi katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Sabasaba Julai 2005 Jijini Dar es-Salaam. Kupitia maonyesho hayo waajiri, watafutakazi na wananchi kwa ujumla walielezwa juu ya huduma za kituo na wanaendelea kuzitumia ipasavyo.

Wizara ilishiriki maonyesho ya sita ya Sekta isiyo rasmi kwa nchi za Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Kampala, Uganda mwezi Novemba 2005. Kituo cha Huduma za Ajira kilishiriki katika maonyesho hayo na kuhakikisha kwamba huduma zake zinafahamika vizuri zaidi kwa waajiri na wanajumuia wa Afrika Mashariki, kama sehemu ya kujiandaa kutekeleza wajibu wa kituo hicho ipasavyo katika soko la ajira la jumuiya hiyo. Maonyesho hayo yalikuwa na malengo yafuatayo:-

Kuwa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi ndizo injini za uhakika katika kupanua na kukuza ajira, kuongeza mapato ya familia na kutokomeza umaskini.

Kubadilishana ujuzi na uzoefu katika utengenezaji wa bidhaa zenye ubora na mvuto kwa wateja.Kuimarisha na kupanua masoko katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kudumisha ushirikiano baina ya wananchi wa Tanzania, Kenya na Uganda.

Wizara iliongoza Tume ya pamoja ya kuchunguza ongezeko la ajira ya wageni katika Sekta ya Hoteli. Uchunguzi huo ulifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Taarifa ya uchunguzi huo inaonesha kuwa ingawa kwa wastani idadi ya wafanyakazi wageni haizidi asilimia 5, lakini wengi wao

wameshika nafasi ambazo hata watanzania wanaweza kuzishika, wanalipwa mishahara mikubwa kuliko watanzania, hakuna vyama vya wafanyakazi, hawana ujuzi mkubwa sana kuliko watanzania na taratibu za mafunzo kwa watanzania sio nzuri. Kufuatia hali hiyo Wizara inakamilisha taratibu za uthibiti zaidi na hivyo kupunguza ongezeko la wafanyakazi wa kigeni wasio wa lazima.

Maombi 1,407 ya vibali vya kuajiri wataalamu wa kigeni yalipokelewa. Kati ya maombi hayo, 817 yalikuwa ya mara ya kwanza, 475 yalikuwa ya kuongeza muda na maombi 115 hayakushughulikiwa kwa sababu ya kutokamilika kwa taarifa kutoka kwa wahusika. Kati ya maombi mapya 817, maombi 544 yalikubaliwa na 273 yalikataliwa, na kati ya maombi 475 ya kuongeza muda, 341 yalikubaliwa na maombi 134 yalikataliwa.

Wizara imeendelea kufanya ukaguzi katika viwanda na kampuni mbalimbali nchini. Kampuni au viwanda vilivyo kaguliwa ni pamoja na: *Nida Textile Mills. Namera Group of Industries, Sunfresh Company Ltd, SDV Transami, NBC (T) Ltd, Sea Cliff na Mohammed Interprises LTD.*

Katika kaguzi hizi ilibainika kuwa baadhi ya viongozi wa makampuni au viwanda hivyo huwanyanyasa wafanyakazi wazalendo, muda wa mafunzo kwa wazalendo ni mfupi ukilinganishwa na wageni, na mishahara inatofautiana sana kati ya wageni na wazalendo. Kufuatia taarifa hiyo, ushauri ulitolewa na hatua mbalimbali zilichukuliwa kwa wale waliovunja Sheria ikiwemo kufukuzwa nchini na wengine kuondoka wenyewe kutokana na kukiuka masharti ya vibali vyao vya kazi.

Wizara imekamilisha programu (*Automated System Database*) ambayo itaweza kutunza kumbukumbu za wataalam wa kigeni wanaoomba vibali vya kufanya kazi nchini, kuboresha taarifa au kumbukumbu za maombi ya vibali kwa wageni na kupunguza udanganyifu wa maombi ya vibali vya wageni kwenye taasisi mbalimbali. Pia mafunzo yametolewa kwa maafisa watakaotumia programu hiyo.

Utekelezaji wa Utafiti wa Nguvukazi wenye lengo la kupima kasi ya ukuaji wa ajira katika sekta mbalimbali, mwenendo wa ajira ya watoto na ongezeko la nguvukazi kwa jumla ulianza mwezi Januari 2006. Utafiti huu unafanyika nchi nzima kwa ushirikiano na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2006.

Rasimu ya pili ya Sheria ya kukuza ajira iliyoshirikisha wadau mbalimbali imeandaliwa na itakamilika mara tu baada ya Sera ya Taifa ya Ajira kupitishwa na Baraza la Mawaziri.

Wizara iliratibu mafunzo ya ujuzi wa watu kuweza kujiajiri na kuondoa umaskini *(Demand – Driven Skills Training Programme)* ili kutoa nafasi za ajira zaidi. Watu zaidi ya 400 waliweza kupata mafunzo hayo katika mwaka 2005/06.

Katika kuzingatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 – 2010 kuhusu ongezeko la ajira zaidi ya milioni moja ifikapo 2010, Wizara imekamilisha maandalizi ya rasimu ya kwanza ya Mkakati wa Kukuza Ajira nchini. Zoezi hili lilishirikisha Wizara zote za Serikali pamoja na Shirikisho la Wafanyakazi *(TUCTA),* Chama cha Waajiri *(ATE)* na Asasi zingine za kijamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu ilitekeleza kazi zifuatayo:-
Imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, na sasa rasimu hiyo ipo kwenye mchakato wa kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri.

Iliendelea na taratibu za kisheria za kuunda Baraza la Taifa la Vijana. Baraza hilo lipo katika hatua za kujadiliwa na wadau kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri.

Iliendelea kukusanya taarifa/takwimu za vijana ili kujua idadi yao, mahali walipo na wanafanya nini *(Youth Mapping).* Hadi sasa kazi hii imekwishafanyika katika Wilaya 76.

Aidha, zoezi la uandaaji wa orodha ya vikundi vya vijana na kazi wanazofanya *(Youth Directory)* liliendelea kufanyika.

Ilitoa mafunzo kwa vijana 105 katika nyanja za uwekezaji na ukuzaji wa biashara, masoko, ufundi, uongozi na utawala wa miradi ili kuimarisha uzalishaji katika vikundi vyao. Mafunzo haya yalitolewa katika chuo cha mafunzo ya vijana cha Ilonga.

Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani iliandaa mkutano ulioshirikisha vijana wa Dar es Salaam pamoja na wadau wengine katika zoezi la kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa kukuza ajira. Mikutano mingine itaendelea ili kuwahusisha vijana wengi zaidi nchini.

Kwa kushirikiana na Jumuiya ya Madola imewezesha kikundi cha Vijana cha Madale Wilaya ya Kinondoni kupata £1000 (zaidi ya shilingi milioni 2), baada ya kushinda mashindano ya vikundi vya uzalishaji katika Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika. Aidha, Ilishiriki katika mkutano wa Kanda ya Afrika wa Mpango wa Jumuiya ya Madola Nchini Lesotho na mkutano wa Mawaziri wa Vijana huko Bahamas na kujadili mkakati wa Maendeleo ya Vijana.

Mkutano huu ulihusisha Wizara yangu na Wizara ya Kazi, Wanawake, Vijana na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Iliendelea kuboresha mazingira ya utoaji mafunzo kwa vijana kwa kukarabati vyumba vya madarasa; mabweni, mfumo wa maji, ununuzi wa vifaa vya mafunzo na ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Chuo katika Chuo cha Vijana cha Marangu.

Wizara imeendelea kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa ambazo kilele chake kilikuwa tarehe 14/10/2005 Mkoani Singida. Kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka jana, jumla ya miradi ya maendeleo 1,547 yenye thamani ya shilingi 54,818,437,404/= ilizinduliwa au kuwekewa mawe ya msingi.

Vile vile wananchi walichanga fedha taslimu kiasi cha shilingi 500,210,889/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Aidha mwaka huu, Mbio za Mwenge wa Uhuru zimezinduliwa Mjini Morogoro tarehe 31/05/2006 na kilele chake kitakuwa Mjini Songea, Mkoani Ruvuma tarehe 14 Oktoba 2006, kikitanguliwa na wiki ya Vijana.

Mwenge wa Uhuru utaendelea kuthaminiwa kwa sababu:-

(a) Ni chombo pekee ambacho kimeweza kutumika kuhamasisha na kufikisha ujumbe katika pembe zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mwenge umeweza kukumbusha na kuweka msukumo kwa wananchi kuhusu kujitolea na kuchangia maendeleo.

(c) Ni nyenzo ya kukuza muungano kwa sababu Wizara zote za Vijana kutoka pande zote mbili zimeshirikiana kuratibu, vijana wa pande zote wanashiriki na Mwenge kukimbizwa Wilaya zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kuhakikisha kuwa shughuli za Mwenge zinaendelezwa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa, Wizara iliendesha mkutano wa siku tatu wa kutathmini Mbio za Mwenge mwaka 2005 kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali huko mkoani Mbeya.

Katika kukuza moyo wa kujitolea miongoni mwa vijana, Wizara iliandaa na kuendesha kambi ya kazi za kujitolea huko Kilosa Mkoani Morogoro na Marangu Mkoani Kilimanjaro, ambazo zilishirikisha jumla ya vijana 90 kutoka katika vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali na Taasisi za vijana. *(Makofi)*

Iliendelea kuratibu utoaji na urejeshaji wa mikopo ya mfuko wa maendeleo ya vijana kwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa. Hadi sasa Jumla ya Halmashauri za Wilaya 15 ambazo zilipatiwa Shilingi 92,674,536/= zimekamilisha marejesho ya mkopo na kupatiwa mgao mwingine.

Chini ya Mtandao wa Kitaifa wa kukuza Ajira kwa Vijana, Wizara iliandaa warsha kwa ajili ya mashirika na Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali kwa lengo la kuhamasisha ukuzaji wa ajira kwa wadau wa vijana kote nchini.

Katika jitihada za kukuza ajira kwa vijana Wizara imeendeleza juhudi za kuwahamasisha vijana kote nchini kujiunga katika vikundi na kuanzisha miradi ya kiuchumi katika sekta za Kilimo, Uvuvi, Ufugaji, Uchimbaji Madini na ufundi mbalimbali.

Iliboresha mitaala mitatu ya mafunzo ya vijana ambayo ni uongozi, uanzishaji na uendelezaji wa miradi pamoja utunzaji wa kumbukumbu za Fedha.

Kwa kushirikiana na Benki ya Dunia chini ya mradi wa *Tanzania Multisectoral Aid Project (TMAP*) Wizara ilitoa mafunzo ya stadi za maisha katika kupambana na UKIMWI na magonjwa mengine ya ngono kwa vijana 30 kutoka vikundi vya vijana Tanzania Bara yaliyofanyika jijini Arusha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara kupitia Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri imetekeleza yafuatayo:-

Jumla ya maombi 6 ya kuandikishwa vyama yamepokelewa kutoka kwa vyama vya wafanyakazi na waajiri. Katika orodha hii chama kimoja cha wafanyakazi kimesajiliwa baada ya kutimiza masharti yaliyowekwa kisheria, na hivyo kufanya idadi ya vyama vya wafanyakazi na waajiri vilivyosajiliwa kufikia 19.

Imeendelea kuratibu shughuli za vyama vya wafanyakazi na waajiri. Jumla ya vyama 14 vimewasilisha taarifa zake za mwaka zinazohusu idadi ya wanachama na kiasi cha michango yao kwa mwaka ulioishia tarehe 31/12/2005.

Kaguzi 54 za kumbukumbu za wanachama wa Vyama vya Wafanyakazi pamoja na vitabu vya mapato na matumizi zilifanyika katika Mikoa ya Shinyanga, Mtwara, Lindi, Arusha na Manyara.

Imeendesha semina kwa watendaji wakuu wa vyama vyote vya wafanyakazi na waajiri ili kujadili kwa pamoja maendeleo na matatizo ya vyama vya wafanyakazi na waajiri nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 majukumu yafuatayo yalitekelezwa:-

Ili kujaza nafasi zilizo wazi watumishi 34 waliajiriwa, 28 kuthibitishwa kazini na 11 kupandishwa vyeo.

Kamati ya maadili, nidhamu na kudhibiti rushwa katika Utumishi wa Umma imeanzishwa.

Watumishi 308 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya kitaaluma kama ifuatavyo:-

- Shahada/Stashahada ya uzamili - 7
- Stashahada ya uzamili (mafunzo maalum) - 70
- Shahada/Stashahada ya juu - 21
- Stashahada - 3
- Cheti (Ndani na Nje ya Nchi) - 207

Aidha, Mafunzo ya mabadiliko ya utendaji kazi *(OPRAS)* kwa Maafisa Kazi wa wilaya na mikoa na Maafisa Vijana wa vyuo na vituo vya maendeleo ya vijana wafawidhi wa ofisi zote Tanzania Bara yalifanyika. Semina ya kuboresha na kuingiza masuala ya jinsia katika mipango na bajeti ya Wizara ilifanyika Morogoro pia.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya mahali pa kazi *(OSHA),* katika mwaka wa fedha 2005/06 Ulitekeleza yafuatayo:-

Ilifanya jumla ya kaguzi 3,432 za kawaida *(General workplace inspections)* za afya na usalama kazini na kutoa ushauri kama ipasavyo.

Mitambo ya kuzalishia mvuke *(boilers)* ipatayo 239 ilifanyiwa ukaguzi wa kisheria wa kila mwaka kwa mujibu wa sheria.

Vyombo vya kutunzia upepo *(Compressors)* vipatavyo 780 vilifanyiwa ukaguzi.

Kaguzi za usalama wa umeme katika viwanda na sehemu nyingine za kazi 1,986 zilifanyika nchini kote.

Wafanyakazi 12,400 walichunguzwa afya zao katika sehemu mbalimbali za kazi nchini kote.

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali Wakala uliandaa na kuadhimisha kitaifa Siku ya Afya na Usalama mahala pa kazi Duniani (tarehe 28 Aprili 2006), hii ikiwa ni kampeni maalumu ya kimataifa ya kuwataka wadau wote na umma kwa ujumla kuboresha afya na usalama wa wafanyakazi.

Wakala umeendelea kutoa mafunzo ya namna ya kuunda na kuendesha kamati za afya na usalama mahali pa kazi.

Ukarabati wa jengo la ofisi la makao makuu uliendelea ambapo sehemu ya ofisi na chumba cha mafunzo vilikamilika.

Katika juhudi za kuongeza idadi na ubora wa huduma za *OSHA* wakaguzi wapya 10 wameajiriwa. Baadhi ya wakaguzi hao watapelekwa kuimarisha ofisi za *OSHA* za kanda.

Kwa kushirikiana na wadau wengine, rasimu ya mswada wa marekebisho ya Sheria ya Afya na Usalama kazini umeandaliwa. Tunatarajia kuwa mswada huo utawasilishwa Bungeni katika Mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mchakato wa kuanzisha mfumo maalum wa kuripoti na kutoa taarifa za ajali na magonjwa yatokanayo na kazi ulianza kwa kuendesha kikao cha wadau kutoa maoni na namna mfumo huo utakavyofanya kazi.

Vifaa mbalimbali vya kutolea huduma za afya na usalama kazini kama vile vifaa vya kupima mapigo ya moyo, mizani za kupima uzito, na vifaa vya kupima macho vilinunuliwa.

Uimarishwaji wa ofisi za kanda umeendelea kwa kuzipatia kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini nyenzo za usafiri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2005/2006 Shirika lilitekeleza yafuatayo:-

Lilikusanya kiasi cha shilingi milioni 198,906.7 kutoka kwenye vyanzo vyake mbalimbali. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 98.2 ya lengo la kukusanya shilingi milioni 202,552.8 katika kipindi hicho na kutumika kulipa mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali na gharama za uendeshaji.

Linatoa mafao saba likiwemo fao la matibabu kwa wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii lililoanza kutolewa mwezi Julai, 2005. Katika kipindi hiki, Shirika limetumia jumla ya shilingi milioni 36,449 kwa ajili ya mafao ya wanachama sawa na asilimia 130 ya lengo lililokusudiwa kwa kipindi hicho la shilingi milioni 28,000.0.

Limejenga vituo vya kuweka kumbukumbu katika Mikoa ya Iringa, Mtwara, Morogoro na Mwanza. Vile vile limeendeleza ujenzi wa ofisi katika jiji la Mwanza na Mkoa wa Kagera. Shirika limeendelea na ujenzi wa jengo Pensheni la Benjamin Mkapa (*Ex Mafuta House)* na pia limekamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba za *Ex-Tazara Hostel.*

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2005/2006, Shirika la Tija la Taifa liliendelea na majukumu yake ya kuboresha tija katika Taasisi za Umma, Mashirika yasiyo ya kiserikali na kampuni binafsi kwa kufanya yafuatayo:-

Liliendesha mafunzo 70 ya kuboresha ufanisi na Tija sehemu za kazi kwa Taasisi za Umma na Binafsi.

Watanzania 860 walipatiwa mafunzo ya kuongeza tija sehemu za kazi kati ya 1000 waliotegemewa.

Lilitoa huduma za ushauri elekezi kwa Taasisi za Umma na Binafsi 18, kati ya 12 zilizopangwa.

Lilifanya tafiti 4 za kuboresha Tija kati ya 5 zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Mahakama ya Kazi imetekeleza yafuatayo:-
Imefanikiwa kusikiliza, kumaliza na kutoa maamuzi 109 kutoka mashauri 323 yaliyokuwepo katika vikao vya kusikiliza migogoro ya kimwanzo, mikataba ya hiari na marejeo.

Imeweza kuendesha vikao vya kimwanzo katika Mikoa ya Mbeya, Mwanza, Morogoro, Tanga, Dodoma na Dar es Salaam na vya kimarejeo katika mikoa ya Arusha na Dar es Salaam.

Imeendelea kushiriki katika upitiaji wa Sheria mpya za kazi ambazo zimeanzisha Kamisheni ya Usuluhishi na Utatuzi wa migogoro ya kazi *(Commision for Mediation and Abritration (CMA)* na Mahakama ya Kazi itakayokuwa Idara ya Mahakama Kuu.

Iliendesha warsha mbili katika miji ya Tanga na Arusha kwa watumishi wake wote kuhusu maadili ya kazi, janga la UKIMWI na masuala ya jinsia. Pia iliwaelimisha wadau wake, kwa njia ya semina, vipeperushi, Radio na *TV* juu ya mabadiliko ya Sheria za kazi na Taasisi za Kazi kama ilivyopitishwa na Bunge.

Imefanikiwa kupata jengo kutoka kwa Wakala wa Majengo na litakuwa tayari kukarabatiwa na kuhamia mara taratibu nyingine zitakapokamilika. Ukarabati huu utagharamiwa na Serikali ya Denmark kupitia shirika lake la misaada la *DANIDA* kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nia ni kupata mahali pa kufanyia kazi panapokidhi mahitaji na penye mazingira mazuri.

Iliendelea na mpango wa kuwa na mahusiano ya kidada na Mahakama ya Kazi ya Denmark. Pia ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa Majaji na Wasajili wote wa Mahakama zote za Kazi za Afrika Mashariki na Ethiopia uliofanyika Arusha na kutembelewa na Mahakama ya Kazi ya Denmark, Kenya na Mahakama Kuu ya Malawi.

Mpango wa Mahakama ya Kazi wa Kusajili, kupanga na kusikiliza mashauri kwa njia ya mtandao wa kompyuta *(Computerised Case Management System)* unaendelea

Mheshimiwa Spika, Sasa napenda kutoa maelezo ya majukumu na kazi zitakazotekelezwa na Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Wizara kupitia Idara ya kazi itatekeleza yafuatayo:-

Kukamilisha awamu ya pili ya marekebisho ya Sheria za Kazi.

Kukamilisha maandalizi ya kuandaa Kanuni za Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria ya Taasisi za kazi zote za mwaka 2004, ili kuwezesha Sheria hizo kuanza kufanya kazi katika robo ya kwanza ya 2006/2007

Kuunda Tume ya Usuluhishi na Utatuzi wa Migogoro ya Kikazi *(Commission for Mediation and Arbitration)* na kuiwezesha kuanza kufanya kazi, katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2006/2007.

Kutoa elimu kwa umma juu ya dhana nzima ya masuala ya kazi na Hifadhi ya Jamii, mchango wa sekta hizi katika kuondoa umaskini na Sheria Mpya za Kazi katika mfumo wa utatu kwa lengo la kudumisha mahusiano mema kazini.

Kushirikiana na Idara ya Mahakama na kuanzisha Divisheni ya Mahakama ya Kazi katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

Uundaji wa Bodi za Kisekta za Vima vya Chini vya Mishahara, kwa kuzingatia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria ya Taasisi za Kazi zote za mwaka 2004.

Kuwapatia vitendea kazi muhimu Wakuu wa Ofisi za Kazi za Mikoa na Wilaya ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi na kutoa taarifa na takwimu kama inavyotakiwa.

Kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa Watumishi wa Idara ya Kazi kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija pamoja na kufanya ukarabati wa ofisi za kazi kwa awamu.

Kuendeleza juhudi za kutoa elimu juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI kwa Waajiri na Wafanyakazi katika maeneo ya kazi nchini.

Kuendelea kupokea na kushughulikia Rufaa, mikataba ya hiari na madai ya malipo ya fidia kwa wafanyakazi walioumia au kupata maradhi kazini.

Kuratibu ufanisi wa kazi za mabaraza ya usuluhishi.

Kuratibu na kusimamia Sheria na Sera zinazopambana na ajira mbaya ya mtoto.Kukamilisha taratibu za kutunga Sheria ya Hifadhi ya Jamii nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikari ya awamu ya nne imeahidi kutengeneza ajira milioni moja katika kipindi cha miaka mitano ijayo, yaani 2006 – 2010. Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inatambua kuwa sehemu kubwa ya jamii ya Watanzania ni vijana na kundi hilo ndilo linaloathilika zaidi na ukosefu wa ajira. Kwa hiyo, changamoto kubwa iliyopo mbele yetu ni kuweka mazingira mazuri ya kukuza ajira kwa makundi mbalimbali yanayoathirika ikiwa ni pamoja na vijana.

Lengo la Mpango wa Taifa wa Kukuza Ajira ni kuwa na Mkakati wa kitaifa unaohusisha sekta na wadau mbalimbali ili kupunguza tatizo la ajira nchini kwa kuhakikisha kwamba zaidi ya watanzania milioni moja wanapata ajira endelevu ifikapo mwaka 2010.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara kwa kupitia Idara ya Ajira itatekeleza yafuatayo:-

Kukamilisha na kuanza kutekeleza Mpango wa Taifa wa kukuza Ajira nchini. Aidha Wizara itaratibu na kusimamia shughuli za kukuza ajira katika sekta rasmi na sekta isiyo rasmi.

Kuendelea kukusanya mawazo na mbinu za kukuza ajira katika sekta mbalimbali na kupima kasi ya ukuaji wa ajira na Nguvu kazi nchini. Wizara itashirikiana na Ofisi ya Takwimu ya Taifa kufuatilia ukuaji wa Ajira na kutoa Takwimu sahihi za sekta ya Ajira.

- Kwa kuwa upatikanaji wa mitaji ni moja ya kichocheo kikubwa cha Ajira, Serikali inakamilisha taratibu za upatikanaji wa mitaji kupitia mabenki kutokana na fedha za wastani wa shilingi milioni 500 kwa kila mkoa zilizotolewa na Serikali kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, taratibu na kanuni za namna fedha hizo zitakavyowafikia walengwa wanaoandaliwa kwa ushirikiano wa Wizara yangu, Wizara ya Mipango Uchumi na Uwezeshaji, Benki Kuu na Benki za Biashara ambazo zitashiriki. Utaratibu huo unazingatia kuwa fedha hizo zitatumika kama dhamana ya mikopo ya masharti nafuu itakavyotolewa na mabenki na Taasisi nyingine za fedha kwa Wajasiriamali mbalimbali. Walengwa wakuu wa mpango huu ni wajasiriamali ambao kwa kupata mikopo hiyo watapanua shughuli zao za uzalishaji mali au biashara na hivyo kujiongezea uhakika wa ajira zao wenyewe na watu wengine. Mikopo hiyo inatarajiwa kuanza kutolewa mapema katika robo ya kwanza ya mwaka huu 2006/2007.

- Serikali inahimiza kuwa fedha za mikopo ya uwezeshaji zilenge vikundi vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS),* na inawahimiza viongozi wa Mikoa, Wilaya na Waheshimiwa Wabunge kuwaunganisha vijana, akina mama na wote wasio na Ajira katika vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ili kurahisisha zoezi la upatikanaji wa mitaji, usimamizi wa zoezi lenyewe na urejeshaji wa mikopo.

- Katika azma hii, ni lazima tufanikiwe. Hivyo Wizara yangu itatoa kila aina ya ushirikiano ili azma ya Taifa ya kuwapatia kazi zaidi ya watanzania milioni moja ifikiwe kabla ya mwaka 2010.

- Kamati ya kutoa vibali vya ajira kwa wageni imeundwa upya ili kuzingatia Sera ya nchi ya kukuza Ajira, kuongeza uwekezaji na udhibiti wa utoaji wa vibali hivyo ili uendane na malengo ya Taifa ya kukuza na kulinda Ajira za ndani ya nchi. Aidha, Idara itafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika makampuni mbalimbali ili kuhakiki ajira kwa wageni na kujiridhisha kuwa Sheria za nchi zinafuatwa.

- Itaanzisha kitengo cha *Cross border placement services* kwa ajili ya kuwatafutia Watanzania nafasi za kazi nje ya nchi na kusaidia Watanzania waishio nje ya nchi kupata nafasi za kazi za utaalamu adimu hapa nchini.
- Kuratibu maonesho ya biashara ya Sekta isiyo Rasmi (nguvu kazi) kwa nchi za Afrika Mashariki yatakayofanyika Jijini Dar es Salaam Novemba 2006 kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Taasisi za Sekta Isiyo Rasmi.

- Kutoa taarifa kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano ili kuwawezesha wananchi kujua namna ya kupata mitaji na mafunzo ya kujiajiri na kuondoa umaskini.

- Kujenga uwezo wa Idara ya Ajira na wa wafanyakazi wa Idara hiyo ili kuboresha tija na ufanisi katika utendaji kazi na utoaji huduma. Aidha, nia ni kuondokana na dhana ya *business as usual* na kwenda kwa Kasi mpya, Nguvu mpya na Ari Mpya katika kutekeleza jukumu hili kubwa la Taifa. (*Makofi*)

- Kuratibu na kuendeleza uanzishwaji wa wakala binafsi wa huduma za ajira nchini.

- Kukamilisha hatua ya pili ya marekebisho ya Sheria za Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 wizara kwa kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana itafanya yafuatayo:-

- Kuendelea kuratibu mpango wa kukuza Ajira kwa kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) vya vijana katika Wilaya zote nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Lengo ni kuwa na *SACCOS* moja ya vijana katika kila Kata au Tarafa kulingana na mazingira.

- Chini ya mtandao wa Kitaifa wa kukuza Ajira kwa vijana Duniani, warsha za wadau zitaandaliwa kwa ajili ya mashirika na Taasisi za Serikali na *NGO* zenye lengo la kuhamasisha ukuzaji wa ajira kwa vijana katika mikoa yote.

- Kuchapisha na kusambaza kwa vijana na wadau wengine Sera ya Maendeleo ya Vijana iliyofanyiwa mapitio baada ya kupitishwa na Baraza la Mawaziri. Aidha programu ya utekelezaji wa Sera hiyo itaandaliwa na kuanza kutekelezwa, ili kukuza ajira kwa vijana, kujenga uchumi na kupambana na umasikini.

- Wizara yangu baada ya kukamilisha zoezi la kuvitambua vikundi vya uzalishaji vya vijana katika Wilaya 76 za Tanzania Bara, itafanya juhudi kubwa ya kuwawezesha vijana hawa kuongeza uzalishaji mali, ubora wa bidhaa na upatikanaji wa masoko ya uhakika. Tunahimiza kila Mheshimiwa mbunge ajue na kuvisaidia vikundi hivi vya uzalishaji na "vijiwe" vya vijana ili vijiunge na kuanzisha ushirika wa akiba na mikopo ili kujihakikishia upatikanaji wa mitaji.

- Ili kuhakikisha kuwa vijana wanaomaliza vyuo vikuu na vyuo vya elimu ya ufundi wanaajiriwa au kujiajiri wenyewe Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

  - Kushirikiana na vyuo vikuu kuhakikisha kuwa vijana wote wanaomaliza vyuo vikuu wanaandikishwa katika vituo vya Ajira kama nguvu kazi iliyo tayari kwa ajira.
  - Kushirikiana na waajiri kuhakikisha kuwa kazi zilizo wazi zinarekodiwa katika vituo vya ajira ili kukutanisha watafuta kazi na nafasi za kazi/waajiri.
  - Kuwapa elimu ya ujasiriamali na stadi za kujiwasilisha na kushiriki kwenye usaili.
  - Kuwawezesha Vijana kujiunga na kuanzisha kampuni za kitaaluma ili wajiajiri wenyewe.

- Kwa kuwa Kampuni hizi zitakuwa katika nyanja na sekta mbalimbali, Wizara husika zitaratibu na kufuatilia kampuni hizi ili kuzisaidia kupata mikataba ya kazi na kutekeleza.

- Aidha, kampuni za vijana wetu wataalamu zitapewa mikopo nafuu na ya muda mrefu ili ziweze kujizatiti kikamilifu kikazi, kujenga uwezo wa kampuni na kuweza kulipa mikopo. Hatua hii itaziwezesha kampuni za wataalamu kuwekeza kwenye kilimo, mifugo, uvuvi, kurina asali pamoja na sekta za uhandisi, sheria, uhasibu, ushauri wakitaaluma na kadhalika.

- Kuimarisha uzalishaji katika vikundi vya vijana na "vijiwe" kwa kuwapatia mafunzo katika nyanja za ukuzaji biashara na masoko, ufundi, uongozi na utawala wa miradi. Aidha, juhudi kubwa zitafanywa kupitia kwa waheshimiwa wabunge na uongozi wa Wilaya zote, kuvigeuza vikundi vya uzalishaji-mali viwe vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo, kupitia mfuko wa uwezeshaji.
- Kuendelea kuratibu shughuli za mfuko wa maendeleo ya vijana kwa kuweka utaratibu mzuri zaidi utakaohakikisha fedha zinazotolewa zinawafikia walengwa. Aidha, wakopaji wanapatiwa mafunzo kabla ya kupewa mikopo na kuwajengea uwezo vijana ili waweze kurejesha mikopo kwa wakati.

- Kukusanya takwimu za vijana na shughuli zao katika Wilaya zilizobakia. Aidha zoezi la uandaaji wa orodha ya vikundi vya vijana (*Youth Directory*) litakamilishwa.

- Kuendeleza ukarabati wa vituo vya mafunzo kwa vijana vya Ilonga, Sasanda na Marangu na pia kuendelea kuimarisha kituo cha mtandao wa mawasiliano (Tovuti ya Vijana) kilichopo Ilonga na kuwahamasisha vijana wengi zaidi kukitumia.

- Kuandaa na kutekeleza mpango wa malezi utakaojumuisha vijana na viongozi wa *"NGOs"* za vijana katika kutoa ushauri nasaha, stadi za maisha, afya ya uzazi, na vita dhidi ya UKIMWI. Aidha mipango ya kudhibiti UKIMWI kwa vijana itaimarishwa na kuendelezwa zaidi.

- Kuendelea kuwahamasisha vijana kushiriki kwenye shughuli za kujitolea katika siku ya kujitolea Duniani, na kuendesha kambi za kujitolea za vijana kwa kushirikiana na *UNDP*, ikiwa ni utekelezaji wa kuinua moyo wa kujitolea kwa vijana nchi nzima.

- Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vituo vya maendeleo ya vijana katika ngazi ya Wilaya kote nchini *(Youth Development Centres).*

- Kuendelea kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana na kuhamasisha kila Halmashauri ya Wilaya kuadhimisha Wiki ya Vijana ambayo inafanyika kila mwaka 8 – 14 Oktoba.

- Kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ili kuajiri Maofisa Vijana katika Halmashauri ili kuwafikia vijana kwa urahisi na wengi zaidi.

- Kuendelea kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Vijana kisheria, pamoja na kuhamasisha kuanzishwa kwa vikundi vya vijana na kuvisajili katika ngazi ya Kata na Kijiji ikiwa pia ni maandalizi ya kuunda Baraza la Vijana kuanzia ngazi ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara kupitia Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri itatekeleza yafuatayo:-

- Itaendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri kwa mujibu wa Sheria mpya ya kazi.

- Itaendelea kufanya kaguzi za vyama pamoja na matawi yake yaliyopo nchini kote ili kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi.

- Itaendelea kutoa ushauri na kuelimisha vyama juu ya utekelezaji wa Sheria Mpya za Kazi pamoja na majukumu yake kwa mujibu wa kanuni na katiba za vyama hivyo ili kupunguza migogoro.

- Kwa kushirikiana na *ILO,* yatafanywa mafunzo ya kuboresha uwezo wa majadiliano kwa viongozi wa vyama vya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 majukumu yafuatayo yatatekelezwa:-

- Shughuli za kiutawala na kiutumishi zitaendelea ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi na vitendea kazi.

- Kukamilisha mchakato wa kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma kwa umma.

- Kuendeleza mkakati wa kuongeza idadi ya Watumishi kwa kuajiri watumishi wapya na kuboresha mazingira ya kazi ili kuleta ufanisi na ubora unaotakiwa.

- Kuzindua Mkataba wa Huduma kwa Wateja (*Clients Service Charter).*

- Kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za michezo kwa wafanyakazi na Wizara ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Wizara inashiriki michezo ya Mawizara na Idara za Serikali (SHIMIWI).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Shirika litafanya yafuatayo:-

- Litakusanya mapato yanayofikia shilingi bilioni 208.7 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato na kulipa mafao na kuwekeza katika vitega uchumi mbalimbali.

- Litaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuweka Kompyuta katika Ofisi zake za Mikoa na Wilayani na kuziunganisha katika mtandao wa Shirika.

- Litaendelea kuboresha uwekaji wa kumbukumbu mbalimbali za wanachama kwa kujenga vituo vitatu vya kuweka kumbukumbu katika Mikoa ya Mbeya, Shinyanga na Mara.

- Litaendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi katika Jiji la Mwanza, Mkoa wa Kagera na Ujenzi wa Ofisi Wilaya ya Mbozi.

- Litakamilisha mradi wa ujenzi wa Jengo la Pensheni la Benjamin Mkapa *(Ex Mafuta House).*

- Litaanza miradi ya ujenzi wa jengo la Ubalozi wa Tanzania Jijini Nairobi nchini Kenya, Ujenzi wa Nyumba za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Ujenzi wa Nyumba za Jeshi la Polisi, Ujenzi wa Nyumba za Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* uendelezaji wa kiwanja wa *EX-AISCO* Jijini Dar es Salaam na ujenzi wa sehemu za biashara ndogo ndogo (*Industrial Parks*) katika jiji la Dar es Salaam na kwa jiji la Mwanza pindi viwanja vitakapopatikana.

- Litakamilisha taratibu za maandalizi ya ujenzi wa daraja la Kigamboni, ambapo ujenzi wake utaanza katika mwaka wa fedha wa 2007/2008.

- Litaanza Ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Waalimu Chang'ombe *(DUCE)* Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 *OSHA* itatekeleza kazi zifuatazo:-

- Kufanya kaguzi 3,800 za kawaida za usalama na afya viwandani na sehemu zingine za kazi.
- Kufanya kaguzi 3,680 maalumu na za kisheria za usalama na afya mahali pa kazi.

- Kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi.

- Kuimarisha ofisi mbili za kanda ya Kaskazini na kanda ya Ziwa zinazohusiana na usalama na afya mahali pa kazi.

- Kuendelea kutoa mafunzo ya afya na usalama mahali pa kazi kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo redio, televisheni, magazeti na vipeperushi ili kuwafikia walengwa kwa wingi zaidi, hususan namna ya kuunda na kuendesha kamati za afya na usalama mahala pa kazi.

- Kuendelea kukamilisha ukarabati wa jengo la ofisi sehemu ya maabara na maktaba.

- Kuendelea kuboresha shindano la Afya na Usalama mahali pa kazi katika sehemu za kazi, na waajiri wanaofanya vizuri kupewa tuzo katika jitihada za kuboresha afya na usalama mahali pa kazi.

- Kuwahamasisha wafanyabiashara wadogowadogo na wa kati ili waweze kuboresha mazingira ya kazi kwa kuendesha warsha katika mikoa sita ya Tanzania Bara.

- Kuajiri wakaguzi zaidi ili kuimarisha kanda zote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Shirika litatekeleza yafuatayo:-

- Kuendesha mafunzo ya uongozi 80 yatakayo wanufaisha watanzania 1100 kutoka Taasisi za Umma na Binafsi.

- Kutoa huduma za uelekezi kwa wateja 30.

- Kufanya tafiti 8 katika maeneo yanayolenga kuboresha tija pamoja na kuchangia katika juhudi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Mahakama ya Kazi itakuwa sehemu ya Mahakama Kuu ya Tanzania na hivyo usimamizi wa shughuli zake utahamia Wizara ya Sheria na Katiba na itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuamua mashauri yatakayowasilishwa kwa mara ya kwanza mbele ya Mahakama pamoja na kukaza hukumu zake na kumalizia mashauri yaliyopo. Pia itapokea, itasikiliza na kuamua rufaa, marejeo na rejea kutoka Kamisheni ya usuluhishi na utatuzi wa migogoro *(CMA)*.

- Kukarabati Jengo la Mahakama na kuhamia.

- Kuboresha huduma za Mahakama kwa kuweka na kutumia vifaa vya kisasa vya Kimahakama, usajili, ukatibu na kiutawala.

- Kuboresha utendaji wa Mahakama kwa kuwaendeleza na kuwa na watumishi wenye sifa ili kuleta ufanisi zaidi.

- Kufikisha huduma za Mahakama kwa wahitaji kwa kufungua ofisi za kanda, kutumia *Circuit/Mobile Courts* na njia za kisasa za mawasiliano pamoja na kuwapatia watumishi wa Mahakama vitendea kazi.

- Semina na mafunzo mbalimbali yataendeshwa ili kuongeza uelewa kwa wafanyakazi na wadau juu ya janga la UKIMWI, uwajibikaji kazini, kuzuia na kuepusha rushwa na mazingira ya rushwa na kujenga maadili mema ya wafanyakazi na wadau.

- Kuwaelimisha wadau na kutoa taarifa mbalimbali kwenye vyombo vya habari juu ya haki za wadau katika Mahakama ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara itatekeleza shughuli zifuatazo za maendeleo:-

- Kufanya ukarabati wa ofisi za kazi za Morogoro, Dodoma, Mtwara, Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro na Kigoma, na kufanya maandalizi ya ukarabati kwa Ofisi za Kazi za Shinyanga, Mara, Kagera, Rukwa, Tabora, Singida na Lindi.

- Ukarabati wa vituo vitatu vya mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana vya Marangu, Ilonga na Sasanda.

- Uanzishaji wa vituo vya ajira katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Arusha.

- Ununuzi wa vitendea kazi, pamoja na uimarishaji wa mfumo wa taarifa, kumbumbu na takwimu ndani ya Wizara.

- Kuendelea na Mapambano dhidi ya UKIMWI kwa watumishi na wadau mbalimbali wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, huduma zinazotolewa na Wizara yangu zinawagusa wananchi wengi kwa njia moja au nyingine. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yao mbalimbali ya mawazo na ushauri walioutoa ndani na nje ya Bunge hili kwa Wizara yangu kwa nia ya kuboresha huduma tunazotoa. Wizara iko tayari kupokea na kuyafanyia kazi mapendekezo, ushauri na maoni watakayoendelea kuyatoa Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kusaidiana katika kuboresha huduma hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, majukumu yote niliyoyaeleza yametekelezwa kwa ushirikiano na mshikamano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana pamoja na Mashirika na Taasisi zake.

Viongozi wote na wafanyakazi wameonesha juhudi kubwa katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwanza kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano aliyetoa maelekezo na matarajio yake kuhusu Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana alipotembelea Wizara mapema baada ya kuundwa kwa Baraza la Mawaziri.

Nawashukuru sana Mheshimiwa Jeremia Solomon Sumari Mbunge wa Arumeru Mashariki, Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana (Kazi na Vijana) na Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko Mbunge wa Kasulu Mashariki Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana (Ajira) kwa msaada na ushauri wao wa karibu.

Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu Dr. Ladislaus Komba, Naibu Katibu Mkuu Bwana Edris Mavura, Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara yangu, watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara na Bodi zao ambao wameshirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuwashukuru washiriki wetu wote ambao kwa namna mbalimbali wametuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Na kwa njia ya pekee naomba niitaje Bodi ya Ushauri wa Kazi (Labour, *Economic & Social Council (LESCO*) Bodi ya Ushauri ya Wizara (*Ministerial Advisory Board*), Shirikisho la Waajiri Tanzania *(ATE)* na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)* kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Aidha, Katika kipindi cha miezi 7, nimekutana na viongozi wote wa Vyama Huru vya Wafanyakazi. Nawashukuru kwa kunielimisha kuhusu vyama vyao na hali ya mahusiano ya kazi kati ya vyama hivyo na waajiri wao. Nawaomba tuendelee kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, Mwisho katika mtiririko wa shukrani zangu lakini sio mwisho kwa umuhimu, naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Mwanga kwa ushirikiano wanaonipa na uchapakazi wao, sifa ambazo zinafanyakazi ya kuwatumikia iwe rahisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kutambua michango mbalimbali ya wahisani ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu yetu.

Kwa uchache naomba shukrani za dhati ziende kwa Serikali za nchi na Mashirika ya Kimataifa ya Denmark, Marekani, Ujerumani, *World Bank, Global Fund*, *ILO*, *UNDP*, *UNICEF*, *TACAIDS*, Kahama *Mining Ltd.* na *Kagera Sugar Ltd,* kwa misaada mbalimbali kwa Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwisho, Mahitaji ya Fedha, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2006/2007, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.11,457,655,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo chini ya Fungu 65. *(Makofi)*

Matumizi ya kawaida: Jumla ya Shilingi 8,057,655,000/= ikiwa ni mishahara *(PE)* na matumizi mengine *(OC).*

Matumizi ya Maendeleo: Jumla ya Shilingi 3,400,000,000/= fedha za ndani na nje kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi za Kazi, na Vituo vya Mafunzo kwa Vijana na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa watumishi na wadau mbalimbali wa Wizara.

Aidha, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 731,753,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 706,600,000 kwa ajili ya maendeleo ya Mahakama ya kazi chini ya Fungu 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIPANGO UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni Na. 81(1) ya Mwaka 2004**,** naomba sasa nitumie nafasi hii kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka uliopita 2005/2006 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2006/2007 wa Wizara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku hii ya leo, pia nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati mbele ya bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika**,** Kwa kuwa hii ni taarifa ya kwanza ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa Wizara hii katika awamu hii, kwa niaba ya kamati napenda kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Tawala. Aidha naungana na wasemaji waliotangulia kuwapongeza wale wote walioteuliwa na kuchaguliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Luteni Mstaafu Yusuph Makamba. (*Makofi*)

Napenda pia nitumie fursa hii kukupongeza kwa dhati wewe Mheshimiwa Spika (Bwana Viwango) kwa kuchaguliwa kwako na kuanza kuendesha Bunge hili kwa Kasi na Viwango vya hali ya juu. Aidha, nampongeza sana Naibu Spika na Wenyeviti wetu kwa umakini wao wakati wa kuliongoza Bunge letu kupitia Kamati zao. (*Makofi*)

Naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge kwa kuteuliwa na kuthibitishwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya, nawapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kazi zao nzuri.

Niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi wao na jinsi walivyoanza kazi zao vizuri. Nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama na wajumbe wote wa kamati kwa jinsi tunavyoshirikiana vizuri.

Mheshimiwa Spika, na sasa kwa namna ya pekee kabisa namshukuru sana mume wangu mpenzi Mohamed Othman Mpakanjia, namshukuru pia mtoto wangu Abdulrahman Mpakanjia ambaye yuko hapa siku ya leo, wazazi wangu na Watanzania wote kwa ujumla walioniwezesha kwa namna moja au nyingine kufika hapa nilipo leo na kwa jinsi wanavyonipa moyo katika kazi zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii tena kuwashukuru kwa dhati kabisa ya moyo wangu wapiga kura wangu ambao ni wajumbe wa Baraza kuu la Umoja wa Vijana wa CCM Taifa, wakiongozwa na Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi ambaye sasa ni Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Nawashukuru sana kwa heshima kubwa waliyonipa na ninawaahidi kwamba sitawaangusha.

Aidha,natoa shukrani kwa Umoja wa Wanawake Tanzania(UWT) chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mama Anna M. Abdallah kwa kukubali kuongeza nafasi za Ubunge kwa vijana wanawake kutoka nafasi moja mwaka 2000 hadi nafasi mbili, mwaka 2005, ni matumaini yetu kuwa mwaka 2010 nafasi hizo zitaongezeka zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Kamati ilizingatia mambo yafuatayo:-

1. Dira ya Wizara
2. Muundo na majukumu ya Wizara
3. Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Kipindi cha Mwaka 2005/2006.
4. Mapato na Matumizi kwa kipindi cha 2005/2006
5. Mafanikio na Matatizo yaliyojitokeza wakati wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka 2005/2006
6. Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa Fedha 2006/2007.
7. Mahakama ya Kazi na
8. Maombi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007.

Dira ya Wizara, ni kuwa na Wizara inayowezesha kwa uhakika kuwako kwa mahusiano mazuri yenye kuleta tija na usawa mahali pa kazi, upatikanaji nafasi za ajira na maendeleo ya vijana kwa ajili ya maisha bora kwa kila Mtanzania. (*Makofi*)

Muundo na Majukumu ya Wizara Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana inazo Idara tano ambazo ni Idara ya Kazi, Idara ya Ajira, Idara ya Maendeleo ya Vijana, Idara ya Utawala na Utumishi na Idara ya Sera na Mipango. Aidha,Wizara inavyo vitengo vitatu, Kitengo cha Fedha na Uhasibu, kitengo cha Ukaguzi wa ndani na kitengo cha Mawasiliano na Habari.Wizara pia inasimamia Shughuli za Ofisi,Taasisi na Mashirika manne yafuatayo:-

1. Ofisi ya Msajili wa vyama vya Wafanyakazi
2. Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA)*

3. Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*)
4. Shirika la Tija la Taifa (*NIP*)
5. Mahakama ya Kazi. (*Makofi*)

Wizara ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa sera Zifuatazo:-

1. Sera ya Taifa ya Ajira.
2. Sera ya Maendeleo ya Vijana.
3. Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii.
4. Sera ya Usalama na Afya mahali pa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Kipindi Kilichopita 2005/2006, Kamati imeridhika kwa kiasi kikubwa na Utekelezaji uliofanywa na Wizara kuhusu maagizo yaliyotolewa kwa kipindi kilichopita cha 2005/2006. Hata hivyo, Kamati inasisitiza katika mambo yafuatayo:-

(i) Shirika la Tija la Taifa Kamati ilitambua umuhimu wa Shirika la Tija la Taifa kwa mafunzo mbalimbali yanayotolewa na Shirika hilo kwa Wafanyakazi. Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Shirika hilo na Mashirika mengine mbalimbali ili wafanyakazi wafaidike na mafunzo yanayotolewa na Shirika hilo.

(ii)

(ii) Kiwanja cha Shirika la Tija. Kamati inasikitishwa na Serikali kutotekeleza ushauri wa Kamati wa kulirudishia Shirika gharama kiasi cha TSh.213,900,000/= zilizotumika kuendeleza kiwanja hicho ambacho kwa sasa Serikali imekigawa kwa Kampuni nyingine ya nje.

(iii) Mradi wa Kuendeleza Usawa Mradi umepata mafanikio katika Mkoa wa Dar-es-Salaam, Kamati inashauri mradi huo usiishie Dar-es-Salaam bali uendelee na mikoa mingine na ikiwezekana kuanzia mwaka huu wa Bajeti.

(iv) Mahakama ya Kazi: Mahakama ya kazi ni chombo cha kitaifa cha sheria kilichoanzishwa kwa lengo la kusimamia uzalishaji kwa kusimamia haki, tija na uhusiano kati ya waajiri na wafanyakazi mahali pa kazi. Kwa kipindi cha 2005/2006, mahakama ya kazi imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

1.Mahakama ya kazi imetoa maamuzi 160 kutoka kesi 292 zilizokuwepo.

2.Mahakama imeendelea kushiriki katika kupitia sheria mpya za kazi ambazo zitaanzisha kamisheni ya usuluhishi na uamuzi *(CMA)* na Mahakama ya Kazi.

3. Mahakama imeweza kuendesha warsha mbili kwa watumishi wake kuhusu maadili ya kazi, janga la ukimwi na mambo ya Jinsia. Pia iliwaelimisha wadau wake juu ya mabadiliko ya sheria za kazi na taasisi za kazi kama ilivyopitishwa na Bunge.

4. Mahakama imeweza kuendesha vikao Mwanza, Mbeya, Morogoro, Tanga, Dodoma pamoja na Dar es Salaam.

5. Mahakama ya Kazi pia imefanikiwa kupewa jengo la kukarabati kutoka wakala wa majengo na litakuwa tayari kukarabatiwa mara taratibu nyingine zitakapokamilika. Ukarabati huu utafanywa na Serikali ya Denmark kwa kushirikina na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matarajio ya Kamati kuwa majukumu hayo yatatekelezwa kikamilifu. (*Makofi*)

(iv) Idara ya Maendeleo ya Vijana.Kwa kipindi cha 2005/2006 idara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, na sasa rasimu hiyo ipo kwenye mchakato wa kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri.Shughuli nyingine zilizofanywa na Idara ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(a) Idara iliendelea na taratibu za kisheria za kuunda Baraza la Taifa la Vijana, Baraza hilo nalo liko katika hatua za kujadiliwa.

(b) Idara iliendelea na kazi ya kukusanya taarifa/takwimu za Vijana ili kujua idadi yao, mahali walipo na wanafanya nini. Hadi sasa kazi hii imefanyika katika wilaya 78. Aidha, zoezi la uandaaji wa orodha ya vikundi vya Vijana linaendelea.

(c) Idara iliendelea kuwapatia Vijana mafunzo katika nyanja za ukuzaji wa biashara, masoko, ufundi, uongozi na utawala wa miradi ili kuimarisha uzalishaji katika vikundi vyao vya uzalishaji mali.

(d) Idara imeendelea kuratibu mbio za mwenge wa Uhuru na wiki ya Vijana kitaifa ambazo kilele chake kilifanyika tarehe 14/10/2005 Mkoani Singida. Aidha mwaka huu Mwenge wa Uhuru uliwashwa Mjini Morogoro tarehe 31/5/2006 na kilele kitakuwa Mkoa wa Ruvuma mwezi Oktoba mwaka huu wa 2006. Ni matarajio ya kamati kuwa Idara itatekeleza majukumu hayo kwa wakati na kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2006/2007, Kamati ilipitia na kuchambua maombi ya Makadirio ya fedha kwa mwaka 2006/2007 ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na kiasi cha Tsh. 11,457,655,000/- kiliombwa kwa ajili ya matumizi ya Fungu Na. 65 na kiasi cha Tsh.1,438,353,0000/= kwa ajili ya matumizi ya fungu namba 60, kama ifuatavyo:-

**Fungu 65**

Matumizi ya Kawaida 8,057,655,000/=
Miradi ya Maendeleo 3,400,000,000/=

**Fungu 60**

Matumizi ya Kawaida 731,753,000/=
Miradi ya Maendeleo 706,600,000/=

Mheshimiwa Spika, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati, baada ya Kamati kupitia na kupata maelezo ya kina kutoka kwa Waziri, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ajira, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha Kituo cha Ajira jijini Dar es Salaam na kukipongeza kituo hiki kwa kazi nzuri inayofanywa na kituo ya kuwaunganisha watafuta kazi na Waajiri. Aidha Kamati inatoa ushauri kwa Kituo cha Ajira juu ya haya yafuatayo:-

(i) Kufanya utafiti na kutambua ni fani gani zinazohitaji ujuzi wa Watanzania na zile zinazohitaji wageni. Kamati inashauri kuwa ajira zote zinazohitaji ujuzi ambao unapatikana hapa nchini, ajira hizo wapewe Watanzania.

(ii) Kuwatambua wahitaji na watoaji wa ajira waliopo hapa nchini.

(iii) Kuweka uhusiano kati ya Mashirika yanayotoa ajira, elimu na Kituo cha Ajira.

Hata hivyo Kamati kupitia Taarifa ya Wizara imeelezwa kuwa ni watafuta kazi 551 tu kati ya 950 wameweza kuunganishwa na Waajiri katika kipindi cha Julai 2005 hadi Machi 2006 Mheshimiwa Spika kiasi hiki ni kidogo sana ukilinganisha na Watanzania wengi wanaotafuta kazi kwa wakati huu. Kamati inashauri Kituo hiki cha Ajira kijitangaze zaidi kwani ni Watanzania wachache tu wanaokifahamu kuwa kipo. Kamati ilitembelea kituo hicho na kugundua kuwa kina matatizo makubwa ya vitendea kazi ikiwemo usafiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kuona umuhimu wa Kituo cha Ajira cha Dar es Salaam na kuamua kufungua Kituo kingine Jijini Mwanza na hivyo kufanya Vituo vya Ajira kuwa viwili sasa. Hata hivyo Kamati inashauri Serikali kuanzisha vituo hivi vya Ajira angalau kimoja katika kila Mkoa kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa ajira kwa kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa spika, Ilani ya Uchaguzi 2005 inazungumzia kuhusu ongezeko la ajira milioni moja (1,000,000) ifikapo 2010. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza ajira kwa kiasi hiki. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na hasa Kituo cha Ajira, kuweka mikakati madhubuti kwa ajili ya utekelezaji wa Ilani hii, kwani idadi hii ya ajira siyo ndogo inahitaji mikakati maalum. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutenga kiasi cha Shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa kupitia benki zilizopo kwa ajili ya uwezeshaji wa Wananchi na kuongeza ajira kupitia mikopo yenye masharti nafuu, Kamati inasisitiza kuwa wadau wote wa mpango huo wafuate kanuni na taratibu zitakazowezesha wananchi wote na hususani vijana kunufaika na mpango huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na ongezeko kubwa la ajira kwa wageni, hata katika nafasi ambazo zingeweza kuajiri Watanzania. Kamati imebaini maeneo yafuatayo yanayoashiria ukubwa wa tatizo hili:

Eneo la kwanza ni Biashara ndogondogo mitaani (Machinga), kwa mfano katika soko la Kariakoo na maeneo mengine ya masoko, Eneo la pili, ni Mahoteli na migahawa ya Kitalii, Eneo la tatu Mikataba ya Tenda mbalimbali k.m. Machimbo, Ujenzi na barabara. Eneo la nne, Ofisi za Mashirika yasiyo ya Kiserikali, kwenye mabenki, sekta ya ulinzi binafsi, na kadhalika.

Kamati hailewi ni kwa vipi hawa wageni wamepata kibali cha kuingia nchini na kufanya kazi hiyo ya Umachinga. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika utoaji wa vibali vya Wageni wanaoingia nchini ili kufanya kazi. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Kazi Ajira na Maendeleo ya Vijana kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na Wizara nyingine zinazohusiana na tatizo hili katika utoaji wa vibali kwa wageni wanaokuja kufanya kazi nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Idara ya Vijana, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuanza kukusanya takwimu za vijana ili kujua idadi yao, mahali walipo na shughuli wanazofanya, mpaka sasa ni Wilaya 78 tu zilizokwishafanyiwa ukusanyaji wa taarifa. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha zoezi hili la ukusanyaji wa takwimu za Vijana ili Wilaya zote zifikiwe. Aidha, Kamati inashauri uandaaji wa orodha ya vikundi vya vijana uharakishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Idara iliendelea na kuratibu utoaji na urejeshaji wa mikopo ya mfuko wa vijana kwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa ili kuvijengea uwezo vikundi vya vijana. Kwa mwaka 2005/2006 Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi 400,000,000/= kwa ajili ya mfuko huo. Hadi sasa Jumla ya Halmashauri za Wilaya 14 zimekwishakamilisha marejesho ya mkopo na kupatiwa mgao mwingine. Aidha, Kamati inasisitiza juu ya mambo yafuatayo:-

(i)Kuwa na utaratibu mzuri wa kutoa mikopo ili iwafikie walengwa.

(ii)Kuanzishwa *SACCOS* sehemu mbalimbali nchini ili vijana wafaidike na mikopo ya *SACCOS* hizo.

(iii)Kamati inasikitika kuwa Wizara haijatoa taarifa juu ya ongezeko au punguzo la mikopo kwa vijana.

Kamati inaishauri Serikali kufuatilia utoaji wa mikopo hii katika Halmashauri na kuona kuwa mikopo hii inazifikia Halmashauri zote. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ishirikiane kwa karibu na Wizara nyingine kufuatilia urejeshwaji wa mikopo ya vijana Kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* Kamati inaipongeza *OSHA* kwa kazi nzuri inayofanya ya ukaguzi wa afya na usalama

mahali pa kazi.  Kamati ilibaini kwamba utendaji wa Shirika hilo hauridhishi kutokana na sababu zifuatazo:-

(i)Idadi ndogo ya wafanyakazi.

(ii)Shirika bado halijajulikana na watanzania walio wengi.

(iii)Fungu dogo la Idara hii, hivyo Kamati inashauri fungu liongezwe ili kutatua matatizo ya uchache wa wafanyakazi, usafiri, na  kadhalika.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kukamilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, ili Sheria hiyo iletwe Bungeni na kufanyiwa Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), Kamati inalipongeza Shirika la *NSSF* kwa kazi nzuri inayofanywa na shirika hilo katika kuwekeza, kuwahudumia wanachama wake na kumaliza mgogoro wa *NSSF* na *TPDC*, hivyo kuleta tija kwa wananchi.  Hata hivyo Kamati inaishauri Wizara kuweka msisitizo juu ya mambo yafuatayo:-

(i)  Mikopo kwa wanachama wa kawaida.

(ii)  Mafao ya Wanachama.

(iii)  Mradi wa nyumba za bei nafuu uendelezwe hadi maeneo mengine na;

(iv)  Wizara kukamilisha rasimu ya Sera ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo yaliyojitokeza katika utoaji wa mikopo Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya Mikataba ya Mikopo ya *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mpango wa *NSSF* kujenga Daraja la Kigamboni yapata miaka mitatu mpaka sasa na mpango huo umetajwa katika Ilani ya Uchaguzi 2005 ya Chama cha Mapinduzi.  Hata hivyo utekelezaji wa ujenzi wa daraja hilo umebaki ukisuasua kwa muda mrefu.  Kamati imekutana na Wizara ya Miundombinu na kuacha maagizo ambayo yanafanyiwa kazi juu ya ujenzi wa daraja hilo, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia suala hili ili ujenzi wa daraja hili uweze kuanza mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika**,** kutokana na Sheria za Mashirika ya Akiba, Wafanyakazi wa *NSSF* hawaruhusiwi kuwa wanachama wa mfuko huo na hivyo kulazimika kuwa Wanachama wa *PPF*.  Katika kipindi hiki cha ushindani kibiashara, inakuwa vigumu kwa *NSSF* kuwashawishi watu kuhusu ubora wa Shirika lao kwa kuwa wao wenyewe hawawezi kuwa wanachama katika mfuko wao.  Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa Wafanyakazi wa *NSSF* kujiunga uanachama na Shirika lao badala ya kuwa wanachama wa Mfuko mwingine wa (*PPF*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa *(NIP),* Kamati inalipongeza Shirika la Tija la Taifa kwa kazi nzuri inayoifanya ya kutoa mafunzo ya kuboresha ufanisi na Tija sehemu za kazi kwa Taasisi za Umma na Binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika**,** kumekuwepo na tatizo la Shirika hili kunyang'anywa kiwanja chake ambacho kilikuwa kimeendelezwa kwa gharama ya Tsh.213,900,000/= na kupewa mtu mwingine wa nje.

Hali hii Mheshimiwa Spika inarudisha nyuma maendeleo ya Mashirika yetu ya Umma na mwisho kuishia kufa kwa mashirika. Kamati inapenda kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi kuwapatia *NIP* eneo lingine la Ardhi litakaloweza kukidhi mahitaji yake ikiwa ni pamoja na kurejesha gharama zote zilizotumika katika kuendeleza eneo hilo. Lililogawiwa kwa mtu mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kuulinda Muziki kama chanzo cha Ajira, Muziki una nafasi kubwa sana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu, muziki unatumika kama burudani, kwenye Harusi, kampeni, vilioni, kanisani, kwenye elimu, na kadhalika. Hivi sasa muziki umekuwa ni mojawapo ya Ajira kwa vijana wengi. Hivyo ni vyema tuuchukulie Muziki kuwa ni ajira inayochangia katika pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa mitaani kuna vijana katika mitaa mbalimbali nchini wanaouza kanda za muziki na wanategemea biashara hiyo kuendesha maisha yao. Lakini imegundulika kuwa kanda nyingi zinazouzwa mitaani zinatengenezwa pasipo mikataba maalum kati ya mtunzi wa muziki huo, hivyo faida kubwa huenda kwa watengenezaji na wauzaji kuliko mwanamuziki mwenyewe. Mwaka 1997 Serikali ilileta sera ya utamaduni na mwaka 1979 ililetwa sheria ya haki miliki, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko nayo iliandaa kanuni na kupitishwa mwaka 2003 ili zitumike katika kulinda haki za utunzi.

Mheshimiwa Spika,hali iliyopo sasa ni kuwa ajira katika Muziki inakatisha tamaa kwa kuwa watengenezaji wa muziki wanaendelea kuneemeka bila kulipa kodi yoyote, Kamati inaishauri Serikali iangalie upya sheria ya haki miliki ya muziki ili hatimaye muziki uweze kuwa ajira nzuri kwa vijana wetu na pia uchangie katika pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Mahakama ya Kazi kuamua mashauri yatakayowasilishwa mbele yake kwa muda muafaka, kukarabati jengo la Mahakama na kuhamia, kuboresha huduma za mahakama kwa kuweka na kutumia vifaa vya kisasa.

Lakini pia kamati ilijadili kuhusu na masuala mbalimbali ya vyama vya wafanyakazi na kamati inavipongeza sana vyama vya wafanyakazi kwa kazi nzuri sana ya kushughulikia mambo mbalimbali ya wafanyakazi. Pia kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza mishahara kwa wafanyakazi. (*Makofi*)

Hata hivyo bado japo matatizo na migogoro mbalimbali mahali pa kazi ipo basi kamati inashauri Wizara iendelee kufanyakazi karibu na vyama hivyo ili kuleta utendaji wenye tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na majukumu mengi iliyo nayo Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kiasi cha Tsh.12, 896,008,000/= kilichotengwa kwa ajili ya Fungu Na.65 na Fungu Na.60 ni kidogo. Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kuiongezea Wizara bajeti kwa Mwaka wa Fedha ujao 2007/2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mbunge, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa maelezo yake ya kina wakati wa kuwasilisha bajeti yake mbele ya Kamati hii. Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mbunge, Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, Mbunge hawa ni Manaibu Waziri, Katibu Mkuu Dk. Radislaus Komba na Maafisa wote wa Wizara kwa Ushirikiano waliotoa mbele ya Kamati wakati wa kupitia bajeti ya Wizara.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii tena kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa michango yao wakati wa kujadili Mapendekezo ya Bajeti hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wajumbe hao Mheshimiwa Jenista J. Mhagama ambaye ni Mwenyekiti na Mheshimiwa Haroub S.Masoud, Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wengine ni Mheshimiwa M Mheshimiwa Maulidah A. Komu, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji,Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan,Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Fatma Othmani Ali, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Anna R. Lupemba, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Philip Bujiku Sakila, Mheshimiwa Dorah H. Mushi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii, kukushukuru sana wewe binafsi na Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mbunge kwa Uongozi wenu hodari na makini katika kuliendesha Bunge letu tukufu. (*Makofi*)

Aidha, namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila kukwama. Vile vile niwashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Angelina L. Sanga na Ndugu Joshua Chamwela kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuandaa taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa Kamati yangu inaunga Mkono Mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Naomba Bunge lako tukufu likubali kuijadili na hatimaye kuipitisha bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake ya uzima kwetu sote. Naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha maoni juu ya hotuba ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu na nakupongeza kwa uongozi wako mahiri wa Bunge hili unaoongozwa na falsafa yako ya Kasi kali lakini inayozingatia viwango.

Aidha, nawashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Tumbe, kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwawakilisha kwenye Bunge hili Tukufu na naushukuru Uongozi mzima wa Chama cha Wananchi *(CUF)*, kwa kunifanya nistahili kugombea nafasi hii. Pia, naushukuru uongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa kuniamini kuiwakilisha na kuwa Msemaji Mkuu katika Wizara muhimu ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine jukumu la Idara ya Kazi ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za kazi, lakini/ama kutokana na uzembe au kutowajibika kwa Watendaji wa Wizara husika jukumu hili linaonekana kuwa gumu kwao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria mbili muhimu za kazi. Sheria hizo ni *Employment and Labour Ralations Act, Act No.6 of 2004* na *Labour Institutions Act, Act No.7 of 2004.*

Mheshimiwa Spika, dhumuni la Sheria husika pamoja na mambo mengine lilikuwa ni kutengeneza Sheria zitakazoendana na hali ya soko la ajira kitaifa na Kimataifa, vilevile kuwa na Sheria ambazo zitafanikisha utatuzi ya migogoro ya kazi haraka, hivyo kupunguza ama kuondoa kabisa kero iliyokuwepo ambapo mashauri yalikuwa yakichukua muda mrefu sana kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, tunaelekea mwaka wa tatu sasa Sheria haijaanza kutumika, mashauri mapya ya kazi yanayoongezeka kila uchao, hali inayolazimisha kuendelea kutumika kwa Sheria za zamani ambazo Sheria mpya ilizibadilisha. Hii ni kutokana na

ukweli kwamba miundombinu itakayopelekea matumizi ya Sheria mpya mpaka sasa bado haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufafanuzi juu ya mambo yafuatayo:-

(i) Ni lini hasa Sheria husika zitaanza kutumika?

(ii) Hatua za kutengeneza miongozo *(Regulations)* zitakazopelekea kuanza kutumika kwa Sheria hiyo imefikia wapi?

(iii) Hatua ya kutafuta majengo ya zitakazokuwa Ofisi za *CMA (Commission of Mediation and Arbitration)* imefikia wapi?

(iv) Wizara imejiaandaje kuweza kukabiliana na changamoto ya upungufu wa wataalam wa *CMA* kwa kuzingatia kwamba kati ya watu 90 waliopata mafunzo ya *CMA*, watumishi wa Idara walikuwa 60 tu (wengine walitoka Vyama vya Wafanyakazi na wengine walitoka Vyama vya Waajiri) na kati ya hao 60 idadi imepungua kutokana na wahusika kupata ajira sehemu nyingine kutokana na kukatishwa tamaa na hali ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Kazi ni mhimili mkuu wa uchumi wa Tanzania japo Serikali inaonekana bado kutoitilia mkazo. Umuhimu wake unatokana na kwamba ni kitengo nyeti kinachohusika moja kwa moja na kuzuia au kutatua migogoro sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, ninyi nyote ni mashahidi mgomo sehemu za kazi kasi yake imekuwa ikishamiri kwa kasi ya ajabu katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Hii inatokana na ukweli kwamba kutokana na kuwa na fungu dogo la Bajeti, Idara imeshindwa kutekeleza jukumu lake la kufanya kazi ukaguzi sehemu za kazi (*Inspection*) ili kuhakikisha kwamba waajiri na waajiriwa wanazingatia Sheria na taratibu za ajira. Matokeo yake Idara imekuwa ikisubiri mgogoro ufukute ndio wakimbilie kuutatua.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, kutokana na Wizara kutokuwa na vitendea kazi vya kutosheleza, watatuzi wa migogoro hiyo hujikuta wakipanda daladala kwenda kukutana na waajiri na wafanyakazi kwa madhumuni ya kutatua migogoro husika.

Mheshimiwa Spika, unyonge huu unawafanya Maafisa Kazi kudharauliwa na wakati mwingine kutokusikiliwa kabisa na waajiri, kwani kwa mwonekano wa nje tu wanaonekana ni watu wasiothaminiwa hata huko wanakotoka.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali katika Bajeti ijayo, iangalie Wizara hii kwa unyeti zaidi, kwani kufanikiwa kwake ndiko kutakakoonyesha dira ya soko la ajira na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mahusiano mema baina ya wadau wakuu wa ajira, yaani Serikali Waajiri na Waajiriwa kupitia Vyama vyao ni hitaji muhimu katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Uzalishaji makini na tija hutegemea sana uhusiano huu.

Mheshimiwa Spika, uhuru halisi wa Vyama vya Wafanyakazi ni nguzo muhimu siyo tu ya utawala bora, ila pia ni mhimili wa demokrasi iliyo ya kweli. Kauli na sauti ya wafanyakazi huwa ni kauli ya wazalishaji, ambayo pia ni kauli na sauti ya walipa kodi. Vyama vya Wafanyakazi vilivyo huru na makini ni sehemu ya jamii huru ya kiraia au *Civil Society.* Watendaji Serikalini ni lazima waijue kwa kina dhana nzima ya Vyama vya Wafanyakazi (*trade unionism*), ndani ya ukweli na mazingira ya soko huria.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* ni kitengo muhimu sana, hasa linapokuja suala la mustakabali wa afya za wafanyakazi makazini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanzishwa kwa Wakala wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi *(OSHA)* bado haijawa na meno na nguvu ya kusimamia kwa ukamilifu Sheria ya Bunge iliyoanzisha *OSHA*.

Mheshimiwa Spika, huduma za ukaguzi wa kuwepo kwa tahadhari za kiusalama na kuwepo kwa vifaa vya kuhakikisha afya na maisha ya wafanyakazi wakiwa kazini ni salama, zimezorota mno katika Tanzania huru. Yawezekana ukaguzi huo, kama wanavyodai wengine, ulikuwa makini zaidi kabla ya uhuru kuliko sasa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya maeneo mengi ya kiviwanda na hata maofisi kuungua moto, ni matokeo ya kukosekana ukaguzi wa mara kwa mara na wa uhakika katika maeneo ya kazi. Kumalizana katika mazingira yanayoashiria rushwa kati ya Wakaguzi wa Wizara na waajiri au wenye viwanda, yawezekana ni jambo lililojichimbia kwa miongo kadhaa sasa.

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wanaoumia na hata kupata ulemavu wakiwa kazini, bado sio ya kutia moyo na upo urasimu mkubwa wa kufukuzana na hata hivyo vijisenti visivyotia moyo. Sheria za kazi, ikiwa ni pamoja na zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu ili zianze kutumikia katika mwaka huu wa fedha, yaani Sheria za Ajira na Mahusiano kazini Na.6 na Na. 7 za mwaka 2004, zimejikita zaidi katika kuwalinda wamiliki wa mitaji (waajiri) ndani ya uchumi wa soko huria, ambao ni ubepari wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Tanzania ni lazima lijielekeze katika kutunga Sheria zinazotambua haki za msingi za wavuja jasho, walalahoi na wapinda mgongo wa nchi yetu. Mfanyakazi akiumia au hata kupoteza kiungo au viungo akiwa kazini, ni lazima fidia anayoipata imhakikishie maisha ya uhakika yeye na familia yake mpaka mwisho wa maisha yake. Sheria zote zinazohusika na masuala ya ajira ni munimu ziwe na lengo la kulinda haki za kimsingi za wafanyakazi, lakini bila ya kuzikandamiza haki za waajiri na hata Serikali.

Mheshimiwa Spika, licha ya umuhimu wa kitengo hiki, kimekuwa kama hakipo, Kambi ya Upinzani ingependa kupewa taarifa kuhusiana na:-

(i) Utendaji wa kazi wa Kitengo husika na mipango yake katika kuhakikisha kwamba usalama wa afya sehemu za kazi inazingatiwa;

(ii) Mikakati ya Wizara kuhakikisha kwamba fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali wakiwa sehemu za kazi zinaongezwa ikizingatiwa kwamba zilizokuwepo sasa ni ndogo mno na zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, licha ya Tanzania kuwa moja ya nchi zilizoridhia Mikataba ya Kimataifa ya Kuzuia Ajira kwa Watoto, hali bado ni mbaya sana. Ripoti ya MKUKUTA, Juni 2005 inaonesha kwamba, ajira kwa watoto, achilia mbali watoto wanaofanya kazi majumbani, inakua kwa kasi ya kutisha na hali ni mbaya zaidi Vijijini. Utafiti wa ajira ya watoto (*child labour Survey 2000/2001*) inaonyesha kwamba watoto walioko kwenye ajira ni milioni 1.2. Kwa mujibu wa ripoti husika maeneo manne maarufu katika kutumikisha watoto ni:-

1. Kilimo cha biashara *(Commercial Agriculture);*
2. Migodini;
3. Watumishi wa Majumbani; na
4. Biashara ya Ukahaba *(Commercial Sex).* Kipengele hiki waathirika wakuu ni watoto wa kike ambao husafirishwa kwa kudanganywa kwamba wanakwenda kutafutiwa ajira Mijini, hatimaye wanaishia kupelekwa kwenye madanguro.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara iliambie Bunge hili Tukufu, ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba tatizo hili linalokua kwa kasi ya ajabu linapatiwa ufumbuzi endelevu. Tunalisema hili tukielewa kwamba utatuzi wa kero hii unakwenda sambamba na kupunguza umaskini kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, majukumu makubwa ya *NSSF*, ni pamoja na kuandikisha wananchama kujiunga na Mfuko wa Hifadhi, kukusanya michango ya wanachama na kulipa mafao kwa wanachama, kuwekeza mafao ya wanachama kwenye vitega uchumi mbalimbali ili kuboresha mafao ya wanachama.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi za dhati kwa Shirika la *NSSF* kwa kazi nzuri inayofanya, mojawapo ikiwa ni uwekezaji katika jengo hili la Bunge la aina yake katika Afrika, ujenzi wa *hostel* za wanafunzi Chuo Kikuu Dar es Salaam. Hata hivyo, pamoja na mafanikiohayo makubwa na kazi nzuri inayofanywa na *NSSF*, Kambi ya Upinzani inapenda kusisitiza kuwa wadau wakuu wa *NSSF,* yaani waajiri na waajiriwa, washirikishwe kikamilifu katika kufanya maamuzi ya uwekezaji hasa wanapofanya hivyo na makampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika, uwazi katika shughuli zao ndio msingi wa kuondoa mashaka katika uwekezaji wao. Aidha, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iihamasishe *NSSF* na mifuko mingine ya hifadhi za jamii kujenga *hostel* za wanafunzi hasa wasichana ili kukabiliana na tatizo la malazi kwa wasichana katika Shule mbalimbali za Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi ya Upinzani inaipongeza *NSSF* kwa kujenga nyumba za bei nafuu zilizopo Kinyerezi Dar es Salaam. Hata hivyo, tunapenda kuishauri Serikali kuwa mradi huu wa nyumba za bei nafuu usiishie Dar es Salaam peke yake. Shirika lifanye jitihada za makusudi ili kuendeleza mradi huu mzuri katika Mikoa mingine ya Tanzania Bara na Visiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine duniani zimetumia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kuleta maendeleo ya nchi zao. Tunapenda kuishauri Serikali iitumie Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini ikiwa ni pamoja na *NSSF* kwa kukusanya nguvu zao kwa pamoja na kutekeleza miradi mikubwa mikubwa ambayo ina manufaa kwa nchi yetu kama kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji na miradi hiyo kukodishwa kwa wakulima. Pia, inaweza kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya maeneo ambayo yana raslimali kubwa ya kilimo na hivyo kurahisisha mzunguko mzima wa biashara ya kilimo kwenye maeneo hayo, kitu kitakachoongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania wanaishi na kutegemea kilimo. Kwa kuwa nchi yetu hadi sasa haina Benki ya Kilimo, yaani *(Agricultural Bank),* tunaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kutumia mfuko au Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama *NSSF* kwa ajili ya kutoa mikopo ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa biashara, tunaishauri Serikali ihamasishe Mifuko ya Hifadhi ya jamii nchini ili kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo na hasa wanachama wa mifuko hiyo. Kwa kufanya hivyo, mifuko hiyo itasaidia vijana katika kujiajiri na itakuwa na manufaa zaidi kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa daraja la Kigamboni, tunaipongeza *NSSF* kwa kuonyesha dhamira ya kujenga daraja hilo ambalo litakuwa mkombozi wa wakazi wa Kigamboni. Aidha, tunashukuru *NSSF* ili kupunguza *Risk,* washirikiane na Makampuni yenye uzoefu wa kuendesha miradi ya *BOT* Jenga, Endesha, Rudisha (Kabidhi). Hata hivyo, tunaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili ikiwezekana utekelezaji uanze katika mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa ni muhimu kwa Taifa letu kutokana na shughuli zake japokuwa lina raslimali-watu isiyozidi wafanyakazi 23. Katika taarifa zilizopo, zinaonyesha kuwa shirika hilo lilikwishatumia kiasi cha Shilingi milioni 213.9 kwa ajili ya kuendeleza kiwanja cha nyumba za wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke wazi nini kimetokea mpaka Wizara ya Ardhi ikakigawa kwa watu wengine kiwanja hicho

ambacho tayari shirika lilishatumia kiasi hicho cha fedha. Aidha, Kambi inataka kujua ni nani walipewa kiwanja hicho na lini Serikali italirejeshea Shirika fedha zake hizo.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maendeleo ya Vijana. Historia inaonyesha kuwa wakati wa mfumo wa Chama kimoja, *UV-CCM* ndiyo kilikuwa chombo cha kutetea maslahi ya vijana nchini. Baada ya mabadiliko ya kisiasa hakuna chombo kinachosimamia, kuwakilisha na kuunganisha vijana nchini. Tangu mwaka 1996, Asasi mbalimbali za vijana kama iliyokuwa *National Youth Forum (NYF)* na baadaye, *Tanzania Youth Vision Association (TYVA)* zimekuwa zikipigania uanzishaji wa Baraza hili na kuambulia ahadi tupu.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka Agosti, 2003 aliyekuwa Waziri mwenye dhamana na vijana aliahidi kuwa Muswada wa Uanzishwaji wa Baraza ungekamilika muda sio mrefu. Majibu ya aina hiyo hiyo yaliyotolewa mapema mwaka huu na Naibu Waziri Mwenye Dhamana na masuala ya ajira, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Mheshimiwa Halima James Mdee kuhusiana na mpango wa Serikali juu ya uanzishwaji wa Baraza la Vijana. Mpaka sasa haijulikani nini kinaendelea, kama ni kweli Serikali ina nia dhabiti ya kuanzisha Baraza husika, ni maneno tu au kama hofu kwamba vijana wakipewa nafasi watatishia nafasi za wazee.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Serikali yanaonyesha kwamba rasimu ya uundwaji wa Baraza la Vijana ambayo ilipitishwa kwenye Mkutano wa kitaifa uliofanyika Iringa mwaka 1998 ilishirikisha wadau. Ukweli ni kwamba vijana hawakushirikishwa ipasavyo katika uandaaji wa rasimu hiyo. Hapakuwa na utaratibu muafaka wa kuwakutanisha vijana kutoka makundi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu ni lini Muswada huo utaletwa Bungeni ili uweze kujadiliwa na ni kwa kiasi gani wadau wa Muswada huo watashirikishwa katika mchakato mzima wa kuanzishwa kwa Baraza husika.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba Idara ya Ajira imeshindwa kufanya kazi yake kikamilifu. Hii inatokana na ukweli kwamba katika kipindi cha Julai, 2005 hadi Machi, 2006 imeweza kuwaunganisha kwa waajiri waombaji kazi 551 tu. Huu ni mchezo wa kuigiza kwa Serikali inayotarajia kutangeneza ajira milioni moja katika kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeahidi kuzalisha ajira milioni moja kwa miaka mitano kama kipimo cha kupambana na tatizo la ajira nchini. Azma hii ina mapungufu ya aina tatu:-

(i) Ilitarajiwa Bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne ifafanue itatengeneza ajira ngapi kwa mwaka huu kama sehemu ya utekelezaji wa ahadi hii, lakini haijafanya hivyo, haijasema itatengeneza ajira ngapi?

(ii) Serikali haijatueleza idadi ya wasio na ajira (*unemployment rate*) ni kiasi gani? Jambo ambalo ni la msingi kuzingatia katika kupambana na tatizo la ajira.

(iii) Uhalisia wa tatizo la ajira nchini. Ajira milioni moja ni kiwango kidogo mno kuwa kigezo cha mafaniko ya utatuzi wa ajira nchini ukilinganisha na ukubwa wa tatizo la ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya utafiti ya *Integrated Labour Force Survey* ya 2004 ambayo imenukuliwa kwenye *Economic Survey Report* ya mwaka 2004/2005 vijana laki 6.5 mpaka laki 7.5 wanaingia kwenye soko la ajira kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa makisio hayo, inaonyesha kuwa hadi kufika mwaka 2010 zaidi ya vijana milioni 3.5 watakuwa wameingia kwenye soko la ajira. Hivyo, kuwa ahadi ya ajira milioni ina maana Serikali imewaacha vijana zaidi ya milioni 2.5 bila ajira kufikia 2010.

Mheshimiwa Spika, hii inamaanisha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya vijana watakaoingia kwenye soko la ajira watakosa ajira. Hivyo, kuna haja kwa Serikali kurejea kigezo chake cha ajira milioni moja ili kiweze kuendana na mahitaji na ukubwa wa tatizo la ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, dondoo za hali ya ajira nchini kwa mujibu wa *Economic Survey Report* ya mwaka 2004/2005 zinaonyesha kuwa asilimia 80 ya watu wenye umri wa kufanya kazi wana uwezo wa kufanya kazi. Kati ya wenye ajira, asilimia 84 wanajishughulisha na kilimo cha asili. Asilimia sita wako katika Sekta isiyo rasmi, asilimia nne wako katika *Formal Private Sector*, asilimia 3.5 Sekta ya Majumbani, asilimia mbili Serikalini na 0.5 Mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinatuonyesha jinsi sekta ya kilimo ilivyo muhimu katika utengenezaji wa ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ingependa Wizara ya Kazi na Ajira ituambie ina mikakati gani ya kushirikiana na Sekta hii ambayo ni mhimili wa Ajira nchini kuhakikisha kwamba inatumia fursa zake kama Wizara kutoa mafunzo na kuwaunganisha na Mashirika ya Kimataifa yanayoshughulika na miradi mbalimbali ya utatuzi wa masuala ya ajira kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani, Benki ya Dunia na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, Ukosefu wa Ajira katika Jiji la Dar es Salaam ni asilimia 46.5, Miji mingine ni asilimia 25.5 na Vijijini ni asilimia 8.4. Vijijini asilimia ni ndogo kwa sababu waliona uwezo wa kufanya kazi ni wachache, kutokana na ukweli kwamba wengi wamekimbilia Mjini. Licha ya kwamba kilimo ni sekta ambayo inatoa ajira kwa wingi, hakilipi kutokana na Serikali kushindwa kuingilia bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Vikao vya Bunge vinavyoendelea Wizara hii iliulizwa swali na Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge Viti Maalum (CHADEMA) kuhusiana na uzoefu katika ajira.

Jibu la Naibu Waziri, lilikuwa la ujumla ambalo bado limeacha maswali. Kwa muhtasari ilisemwa kwamba yapo mashirika ambayo hayatumii kigezo cha uzoefu, hivyo fursa za vijana wahitimu zinaweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, tujiulize na kujadili tukikumbuka matangazo mbalimbali ya ajira. Ni asilimia ngapi hayana kigezo cha uzoefu? Ukweli ni kuwa nafasi nyingi za ajira zina kigezo cha uzoefu. Tena nyingine zinataja miaka mingi mpaka pengine ingeitwa uzoeefu badala ya uzoefu. Hiki ni kikwazo kinachohitaji kujadiliwa. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inatambua na kuthamini mchango wa uzoefu katika utumishi. Hata hivyo, haioni umaana wa uzoefu kutumika kama kigezo cha lazima. Utaratibu wa sasa wa Asasi nyingi za Serikali na Sekta binafsi kutumia uzoefu kama kigezo cha lazima unawazuia vijana wahitimu ambao hawajafanya kazi, bado hata nafasi ya kusailiwa kupimwa uelewa na vipaji vya kuhusiana na kazi husika. Kwani kuna mtu amezaliwa na uzoefu? Watapata lini uzoefu bila kupata fursa ya kupata uzoefu?

Mheshimiwa Spika, kuweka uzoefu kama kigezo cha lazima, ni kama kuweka tangazo la 'Kukopa Kesho', ambalo kila uchao linamzuia mtu kukopa. Serikali ifute utaratibu wa kuweka uzoefu kuwa ni kigezo cha lazima kwenye Taasisi zake, badala yake kiwe kigezo muhimu na hata ikibidi kigezo cha nyongeza. Lakini pia, Wizara iweke utaratibu wa kushawishi sekta binafsi kupenyeza mabadiliko haya katika utaratibu wao.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka ujao wa fedha ni vyema ikatafakari mikakati mingine ya kuvutia sekta binafsi kuajiri wahitimu mathalani kutoa vyeti vya punguzo kidogo la kodi kwa wanaoajiri wahitimu mara baada ya kutoka masomoni *(Graduate Tax Relief Certificate).*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeelezea kwa kirefu agenda ya mikopo kama suluhisho la kuajiri, lakini azma hii tunaiona kuwa ina mapungufu kadhaa. Kwanza mikopo ya Shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa ni pesa kidogo mno kuweza kuwakomboa walalahoi, hasa kama itataka kumpatia kila Mtanzania anayehitaji mkopo huo. Mikopo itakayotolewa itakuwa midogo kuweza kujenga ajira endelevu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ielewe kuwa, sio kila Mtanzania ni mjasiriamali au kila Mtanzania anaweza kuwa mjasiriamali. Kwa kuzingatia hayo, kama Serikali haitakuwa makini, upo uwezekano wa mikopo hii kuwaongezea umaskini Watanzania, kwani watabaki na umaskini kama awali lakini zaidi watakuwa masikini wanaodaiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni bora Serikali itenge fedha nyingi kwa miradi mikubwa ambayo itaajiri Watanzania wengi badala ya kumpa kila mtu anayehitaji mkono wa Sh. 50,000/= mpaka Sh. 80,000/=. Lakini kama Serikali imeamua kutoa *grant* na siyo

mkopo, basi watueleze miradi ya fedha hizo upembuzi yakinifu umeshafanyika katika nchi nzima?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuelekeza fedha hizo kwenye miradi mikubwa, kwani uwezekano wa kurejeshwa kwa fedha hizo ni mkubwa na ajira zitakazopatikana zitakuwa nyingi na endelevu. *(Sustainable)*

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kazi bado inachechemea kiutendaji na ndiyo maana kwa mwaka 2005/2006 ilitoa maamuzi 160 kati ya kesi 292 zilizokuwepo. Pamoja na mabadiliko mengine ya kisheria yaliyoibua *Labour Court* na Kamisheni ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* kama Taasisi zilizo chini ya Mahakama Kuu ya Tanzania, bado wananchi hawajaona umahiri na umakini wa Mahakama ya Wafanyakazi na hasa katika eneo la utatuzi wa kisayansi wa migogoro ya kikazi.

Mabadiliko ya Sheria na majina yanaleta maana kama tu kile kinachosimamiwa na Mahakama ya Kazi kitafanikiwa. Wananchi wanataka ongezeko la ufanisi katika Mahakama ya Kazi ili uzailishaji uendelee kunawiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Watanzania wangependa kujua Wizara yetu ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana imejiandaa na kujipanga kwa namna ipi ili kuhakikisha vijana wa kitanzania wanajipenyeza katika masoko ya ajira ya Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, Lipo wimbi la vijana wa Kenya na hata Uganda wanaopata ajira kirahisi katika Tanzania, huku milango ya msoko ya ajira ya nchi hizo ikiwa migumu kwa Watanzania kujipenyeza. Ni jambo la muhimu kwa Wizara hii kuandaa mkakati wa makusudi wa kuwaandaa vijana wetu kupata ajira ndani ya *East African Community*, iwe ni ndani ya Kenya, Uganda au hata hapa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama Waganda na Wakenya wanavyolikodolea macho soko la ajira la Tanzania kupitia mwamvuli wa *East African Community* Watanzania nao waandaliwe kukamata ajira mbalimbali kule Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inavyo vituo viwili vya mafunzo kwa vijana kule Ilonga na Marangu na zipo juhudi za kuviimarisha. Kwa hali yoyote ile, Vituo hivyo ni vichache sana ikilinganishwa na idadi ya vijana na mtawanyiko wao katika nchi nzima. Vituo hivi viongezwe na visambae maeneo mengi ya Tanzania na viwaandae vijana kujitegemea na Kuwa raia wema kupitia shughuli za uzalishaji katika Sekta za Kilimo na Viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuhitaji uzoefu na hekima za wafanyakazi wazee katika Serikali Kuu, upo umuhimu mkubwa wa kuharakisha zoezi la kutoa ajira kwa vijana wetu wanaohitimu katika Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Juu kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuwa na vijana wengi wanaohitaji ajira isichukuliwe kama tatizo, bali fursa muhimu ya kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Vijana wanatakiwa wachukuliwe kama *asset* na sio tishio. Katika soko la ajira, vijana

wachukuliwe kama tiba ya tatizo na ukosefu wa ajira ndiyo tatizo na sio kinyume chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kizazi cha watumishi wa umma wasiofanana kabisa na matakwa ya karne ya 21 ni lazima sasa kikae kando na kikiruhusu kizazi kipya cha watumishi wa umma, vijana walioelimika vizuri ndani ya dunia ya utandawazi, kichukue nafasi yake stahili. Serikali kupitia Wizara hii na ile ya utumishi iwape ajira Serikalini vijana hawa wenye mtizamo mpya. Tusiendeleze ukosefu wa ajira uliobandia kwa vijana wetu waliosomeshwa kwa gharama kubwa na Watazania ili kuwalinda watu ambao kimsingi wamechoka.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inazo rasilimali nyingi mno za kuwawezesha vijana wetu kujipatia ajira bila ya matatizo. Serikali ni lazima ifanye maamuzi magumu, lakini yenye nia ya kuwawezesha vijana wetu badala ya kuwafurahisha wageni na wakati huo huo kupalilia kuzuka na kukua kwa Jeshi la Vibaka, majambazi na makahaba katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa kuifanya Tanzania ivutie na iwe nzuri kimaisha kwa kila mmoja wetu, upo ndani ya sisi wenyewe. Kupanga ni kuchagua na tukivipanga sawasawa vipaubele vyetu vya kimaendeleo ni lazima tutasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya silaha za kuaminika zaidi ya kupambana na ujambazi nchini mwetu na hata kupambana na maambukizi ya UKIMWI miongoni mwa vijana ni Serikali yetu kukubali kuwekeza zaidi katika maendeleo ya vijana, hasa yale ya kielimu na pia katika eneo zima la uwezo wao wa kiujasiriamali na maendeleo yao katika matumizi ya Sayansi na Teknolojia katika ulimwengu wa karne ya 21.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napenda niwashukuru wale wote ambao waliniwezesha kwa namna moja ama nyingine kuweza kutayarisha hotuba hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa kuwasilisha vizuri taarifa yenu.

Waheshimiwa Wabunge, ingawa nimeendelea kupata maombi ya wachangiaji, lakini orodha hii niliyonayo, ninao Waheshimiwa 12 ambao hata hivyo sio wote watafikiwa hasa wa 11 na 12. Kwa hiyo, nitaisoma sasa.

Wa kwanza, ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Mtakumbuka jana nilimruhusu Mzee Malecela awe wa kwanza, sasa ili kutenda haki leo namruhusu Mama Malecela awe wa kwanza. *(Makofi)*

Halafu namruhusu mdogo wangu Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa ambaye alichangia mara moja tu, nadhani leo ana mambo mazito ya kutuambia, atafuatia Mbunge wa Chalinze - Mheshimiwa Ramadhan Maneno, halafu Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Mhina, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Jackson Makwetta na mwisho Mheshimiwa Balozi Kagasheki.

Kama ikitokea kama jana, kwamba, wazungumzaji wanatumia muda mfupi zaidi, tunaweza tukawafikia wote hawa 11. Kwa hiyo, sasa namuita Mheshimiwa Anne Kilango Kalecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kupata nafasi ya awali ya kuchangia hoja ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara nyeti na kwa kweli ni bahati mbaya kwamba imekuwa ni Wizara ambayo imepewa siku moja.

Mheshimiwa Spika, lakini kwanza ningeomba kwa kuanzia, hebu niseme maana ya kazi ni nini? Naomba ninukuu kutoka kwenye Kamusi ya Kiswahili Sanifu, nini maana ya kazi? "Kazi ni shughuli anayofanya mtu kama vile kulima, kuandika, kufundisha na kadhalika."

Mheshimiwa Spika, neno kazi ni neno pana sana na ndiyo maana nasema Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ni pana. Bila ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, hakuna fedha. Wizara ya Fedha inategemea mapato kutoka kwa watu wanaofanya kazi na kutokana na kodi za wananchi, ndiyo kunakuwa na Wizara ya Fedha ambayo inajitegemea.

Mheshimiwa Spika, bila ya kazi katika nchi yetu hakuna fedha, hakuna afya, hakuna uchumi. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema tunapofika kwenye Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana tujue tunazungumzia Wizara ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kazi, tuanze kwenye kaya. Kaya ambayo baba na mama ni wachapakazi, inakuwa na mapato na inakuwa na maendeleo. Baba na mama wakithamini kazi ndani ya kaya, kaya inakuwa na maendeleo. Jamii inayotuzunguka ikithamini kazi, jamii inakuwa na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu hili la Tanzania iwapo wananchi wote tutathamini kazi, ina maana Taifa hili litapata mapato na litapata maendeleo. Wasiwasi ambao ninao na ninaamini kwamba niko sahihi, ni: Je, ni asilimia ngapi ya Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi wanafanya kazi kikamilifu? Huo ndiyo wasiwasi. Sisi tunaitwa ni Taifa maskini bila ya sababu kabisa. Mimi nina wasiwasi kwamba asilimia ya Watanzania wanaofanya kazi kikamilifu haizidi asilimia 30. Wengi wa wananchi hawafanyi kazi kikamilifu, labda kuna sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, zinaweza zikawepo sababu za msingi. Kwanza, labda sababu za kimalezi zinaweza zikachangia. Pili, sababu za mazingira zinaweza zikachangia wananchi wasifanye kazi vizuri. Tatu, au Serikali haijaweka misingi kamilifu ya kuwafanya wananchi wafanye kazi vizuri. Nne, *may be* vitendea kazi. Tano, labda elimu endelevu kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Watanzania kutothamini kazi ni tatizo kubwa kweli kweli. Sisi akinamama tunapobeba watoto mgongoni, unambeba mtoto wako mgongoni unamfunga kwa kitenge, mtoto anaangalia kisongo cha mama yake. Hawezi kumuangalia mama huku. Sisi wanawake wa Kiafrika tunabeba watoto mgongoni, watoto wanaangalia kisongo chetu.

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye malezi sasa. Kwa hiyo na watoto ndani ya nyumba wanaangalia wazazi wao wanafanyaje kazi, mama anafanya kazi kiasi gani, mama kama anaamka asubuhi anakunywa supu yake halafu anakwenda baa, anarudi usiku kulala, watoto watafuata *trend* hiyo hiyo. Kama baba akiamka asubuhi anakwenda kijiweni kuzungumza, basi watoto wataona maisha ni kukaa wapi, kijiweni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, malezi ya watoto ni muhimu sana. Sasa hivi vijana wengi tunalalamika wanakaa vijiweni. Kwa nini wanakaa vijiweni? Labda wanaangalia wazazi wao wanaishije ambao wazazi ni sisi. Hayo ni malezi ya wazazi. Je, sisi viongozi tunathamini kazi yetu ya uongozi? Hilo nalo ni swali. Je, sisi viongozi ni wachapakazi? Tunafanya kazi ya Taifa inavyotakiwa au tunaomba Ubunge kuja kupendeza pendeza? Hapana. Tusichezee kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kazi katika Wizara hii ambayo ni muhimu kweli kweli. Wizara hii iwapo Serikali na yenyewe itaona iitenge fedha nyingi za kutosha, kwa sababu hii Wizara ndiyo itabeba Wizara nyingine zote. Kwa sababu Waziri wa Fedha analalamika kila wakati anasema Bajeti ndogo, kwa nini? Tuna rasilimali za kutosha, tuna ardhi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Watanzania hatufanyi kazi vizuri. Mimi kwa bahati nzuri, leo kabla ya kuja kuchangia, huwa ni kawaida, naamka mapema sana, nikawa naangalia *ITV* asubuhi. *ITV* mapema imetoa kipindi kirefu sana cha maisha ya Wachina kwa wale ambao mmeangalia *ITV*. Walivyoanza maisha yao ya kupandikiza mpunga, kama sisi watu wa Kiurio tunavyofanya kwa mikono. Lakini *you can see them* kiasi ambacho wako *fast.*

Mheshimiwa Spika, kuna nchi za wenzetu, wananchi wanajua maana ya kazi. Sasa kwa nini Wachina wanathamini kazi asilimia 99, sisi asilimia 40 ndiyo tunaofanya kazi? Hilo ni swali kwa Serikali.

Nafikiri tuna tatizo pia la Sheria ya Kazi. Wananchi wanaona hata wasipofanya kazi, hakuna sheria inayowakamata, ndiyo maana wanaona hata wakishinda kijiweni, hakuna sheria inayowalazimisha kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watu wanaokaa vijiweni ni wengi kweli kweli na ndiyo wanaobaki kuilalamikia Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ooh, hii Serikali, hii Serikali, lakini wanashinda vijiweni na Serikali haina sheria inayowakamata watu ambao wanaishi bila ya kufanya kazi. Serikali ione kuna umuhimu wa kuweka sheria inayowabana watu ambao wanaishi kwenye nchi yetu bila ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimekwenda nikaangalia China. China wana sheria ya kazi. Ni maamuzi magumu, lakini walipoanza walikuwa wameamua kwamba mtu asiyefanya kazi asile na Biblia imesema, asiyefanya kazi asile. Kwa nini sisi turuhusu wananchi wenye uwezo wa kufanya kazi waishi kwenye nchi yetu bila ya kufanya kazi na nchi iendelee kuwa maskini? Naiomba Serikali, sasa ni wakati muafaka, tafadhali sana Mheshimiwa Waziri angalieni ni jinsi gani mnaweza kuleta sheria ya kuwabana Watanzania wote wafanye kazi, tuondokane na huu umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nizungumzie neno wivu. Hakuna kitu kibaya duniani kama wivu. Lakini hakuna kitu kizuri duniani kama wivu wa maendeleo. Ni vizuri Serikali yetu hii ya CCM, Tanzania tuwe na wivu wa maendeleo. Kwa nini Mchina ameendelea, sisi tuko hapa? Huo ndio wivu wa maana.

Ninaiomba Serikali hebu kule ambako tunaweza tukaiga twende tukaige. Serikali nendeni mkaangalia China wametumia njia gani mpaka wameendelea, wametumia njia gani kuhakikisha kwamba wananchi wote wanafanya kazi, wivu unaotakiwa duniani ni wivu wa maendeleo. Kwa nini Anne Kilango anaendelea? Nami ngoja niige ili niendelee kama Anne Kilango. Nafikiri Serikali imenielewa.

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwa vijana, mimi katika kipindi cha uchaguzi kilichopita mwaka 2005, niligombea Jimbo, lakini tukubaliane katika kipindi hicho cha Uchaguzi 2005 vijana wengi sana walipiga kura na vijana wengi sana walijiandikisha. Nilipata uwoga wakati huo, hivi hawa vijana wamejiandikisha kwa nia ya kurudisha CCM tuendelee kutawala au vipi! Kumbe kweli vijana hao walikuwa na nia ya kuhakikisha kwamba Chama cha Mapinduzi kinaendelea kutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye Ilani ya Uchaguzi mwaka 2005 tumezungumza na sisi kuwatendea mambo makubwa vijana. Tumesema vijana tutawawezesha waweze kujiajiri, vijana tutawapatia ajira. Sasa jamani tuzungumzeni ukweli, hawa vijana ni wakati sasa wa kuwawezesha waweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 54 ya *Hansard* ya tarehe 26/6/2006. Alisema: "Aidha, maeneo yenye fursa za kujiajiri ni kilimo, ufugaji na kadhalika, lakini akasema Serikali katika mwaka 2006/2007 imetenga wastani Shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa kupitia Benki husika na akaigusa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwamba ndiyo itakayochukua nafasi kubwa katika milioni 500."

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa kiongozi wa watu, huu ni mwaka wangu wa 16. Nilianza uongozi kwa kuongoza wanawake wenzangu, sasa hivi ninaongoza

wananchi wa Jimbo la Same Mashariki. Ninajua maana ya Shilingi milioni 500 hizi, zitakwenda katika Mkoa wa Kilimanjaro, zitakwenda katika Mkoa wa Dar es Salaam, zitakwenda katika Mkoa wa Mwanza, zinaweza zikaishia pale Mjini, zisifike Vijijini ambako ndiko vijana walipo. Vijana wengi wako Vijijini wamejiunga kwenye vikundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina vijana wana vikundi, wanalima tangawizi, wako Muhigi, Miamba, Lunguru, Mtihi wanalima tangawizi kweli kweli. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapojumuisha, hebu aniambie atakavyozifikishe hizi fedha kule Milimani. Vijana wangu nao wakaongeza mitaji yao, hawataki kwenda Dar es Salaam kuuza soksi, hapana, wanataka kujiajiri kule Same Mashariki Milimani. Hizi Shilingi milioni 500 jamani zifike kote kama ni Mkoa wa Kilimanjaro zifikie mpaka Milimani zisije zikaishia Mjini.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi kina mpangilio mzuri sana na nia yake ni kuleta maendeleo kwa wananchi wake, lakini watekelezaji, fedha hizi Shilingi milioni 500 wanaweza wakawakopesha watu wenye uwezo mkubwa tu, Shilingi milioni 500 zikaishia mikononi mwa watu 10, hapana.

Mheshimiwa Spika, hizi fedha tunaomba Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana mzisimamie vizuri, vijana wetu walioko Vijijini wapate kuongeza mitaji, kwa sababu wamejiweka vizuri sana, wamejiundia vikundi vyao, wana Katiba zao, wana *account* zao Benki, lakini wangependa nao wapate manufaa kutoka kwenye Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba sana Serikali, Shilingi milioni 500 hizi za kila Mkoa ziangaliwe vizuri na zikitumika vizuri zitatuokoa sana hasa kwa vijana wetu waliojiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka kumalizia kwa kuzungumza mambo mawili. Kwanza la msingi, ninaomba sana Serikali ione umuhimu kutunga sheria ya kuwabana Watanzania wote wafanye kazi na waone umuhimu wa kufanya kazi. Kama kuna mapungufu mahali, Serikali ijaribu kuyarekebisha.

Lakini suala la kuwa na asilimia 40 tu ya Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi ndiyo wanaofanya kazi, hii nchi itaendelea kuwa maskini mpaka kiama. Wengine wanashinda vijiweni. *(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nichangie kidogo katika hotuba hii muhimu sana ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kama walivyosema wenzangu, kazi ni uhai.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wenzake wote waliotuletea hotuba. Ni hotuba nzuri na kama utekelezaji

utakuwa na mpangilio kama maandiko yalivyo kwenye kitabu, basi inawezekana tukapiga hatua nzuri. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, mimi nina mambo machache sana, lakini kwa sababu yananikera, nimeamua niyaseme. Kwanza, nianze kwa kupongeza Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii, kama *NSSF* na mingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hii mifuko pamoja na matatizo madogo madogo ambayo labda Mitaani watu wanayazungumza, lakini kimsingi ni mifuko ambayo inasaidia sana katika kutatua matatizo ya wananchi ama mmoja mmoja au kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, jengo hili ni ushahidi mkubwa sana wa msaada tuliopata kwenye Mifuko hiyo. Mimi natumia fursa hii kuwapongeza sana hao watu waliotenga fedha hizi, wakatoa mikopo hii ambayo kwa kweli mwanzo walivyotoa na baadaye baada ya mabadiliko ya bei za vitu na nini, lakini *still* hawakurudi nyuma, wakaamua kufanya *topping up* na leo tunatumia ukumbi huu mzuri ambao mimi nafikiri tutajivunia kwa siku nyingi. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ningependa wafanye zaidi. Mifuko hii ina faida kubwa sana kwa watu, lakini elimu ya umuhimu wa Mifuko hii haijawafikia wananchi. Sisi Waheshimiwa Wabunge hapa tupo zaidi ya 300, mimi sidhani kama tuko Waheshimiwa Wabunge tutimiao 100 tuliojiunga na Mifuko hii na ni kwa sababu hatuelewi umuhimu wake.

Mheshimwia Spika, natumia fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri, awaombe basi watu wa *NSSF* na wengine waje hapa Bungeni wawaelimishe Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge wakielewa wakajiunga minong'ono itaondoka, kwa sababu sisi ndiyo tuko kwa wananchi wenyewe, tutakuwa watetezi. Kwanza, tutajiunga sisi tutafaidika, lakini pia tutakuwa ni Walimu wa Mifuko hii kwa wananchi wenyewe, tutakuwa tumesaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, naomba niondoke hapo, nije kwenye ajira binafsi. Hapa tuna tatizo. Ajira binafsi ndiyo inayohusisha watu wengi, tukate tusitake ama iliyo *formal* au *informal*, lakini inahusisha watu wengi sana. Hapa pana tatizo linalohitaji usimamizi wa karibu wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Waajiri binafsi kwa sisi ambao tunaishi Mitaani, wanawaonea sana wafanyakazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika wakati huu tulionao umlipa mfanyakazi unayemtuma kwa muda wa mwezi mzima Sh. 7,000/= na Serikali ipo na Wizara ipo, lakini hawafuatilii mambo haya. Sasa hawa hawana pa kulalamikia, walalamikia Mitaani tu. Lakini unyonge ni utumwa, analazimika kwenda kufanya kazi katika hoteli, kuanzia pengine alfajiri saa 12.00 mpaka saa 4.00 usiku wanaondoka, *at the end of the month* anapewa Sh.7,000/=. Sasa mtoto analalamika kwa mzazi wake. Mzazi wa mtumishi ni Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana au ni Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri atafute *machinery* ambayo itafanya *survey* kwa ajira binafsi haraka iwezekanavyo. Kama kuna mahali wananchi wanapoteza imani na Serikali ni hapa. Maana yake wanaona hawana mtetezi. Wao wanalazimika kufanya kazi kwa sababu ya unyonge, lakini mapato wanayoyapata ni kidogo na hakuna mtu aliye na habari na ukitafiti ndipo unapojua kosa lako na ndipo unajua kwa nini unahitaji kujirekebisha. Hawa jamaa wa Kiislam wana mfano mmoja wa kiongozi wao mmoja anaitwa Saidina Omar. Huyu alikuwa ni Khalifa wa Waislam. Sasa alikuwa na tabia akitoka usiku, anavaa nguo za ajabu ajabu hivi akitembea Mitaani, anasikiliza wananchi wanasemaje. Siku moja akapita kwenye nyumba mmoja akamsikia mama mmoja analalamika, anasema Khalifa, Khalifa gani huyu? Mimi hapa ninakaa sina chakula, sina chochote nilichonacho, wao wanakaa huko wanatumia fedha zao tu. Akabisha hodi ndani, akibisha hodi akamkuta yule mama, akamwambia mama unasemaje?

Akamwambia ninasema, hivi unavyoniona, nimekoka ule moto nimeweka chungu kichemke ili watoto waone ninapika mpaka wachukuliwe na usingizi. Lakini kwa kweli sina ninachokipiga, ninawadanganya tu na eti tuna Khalifa hapa wa Kiislam anasimamia haki za watu, anapashwa kutusaidia, hatusaidii. Akamwambia mama ujumbe umefika. Akaondoka pale, akaende nyumbani kwake, akachukua unga, akaja ndani ya nyumba ile, akatengeneza mikate kwa mkono wake, akawapa wakala watoto, akala na yule mama na akaagiza katika *Beifilmali a*pelekewe yule mama kila siku fungu la kuweza kuendesha maisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, Maofisa wanakaa Ofisini, hawana habari kinachoendelea, watu wanaendelea kuteseka, watu wanaumia, tunawaambia watu watafute ajira, wanatafuta ajira, lakini ajira isiyowasaidia. Naomba sana jambo hili mlifuatilie. Mtusaidie waajiri binafsi kwa kweli wanaumiza sana. Mimi sisemi ni wote, lakini wengi wao kwa kweli hawaangalii maslahi ya watu, wanaangalia maslahi yao. Ni kweli biashara yoyote lazima upate fedha, lakini sio lazima upate fedha kwa kutoa roho ya wenzio ili upate fedha wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa pili, ni Serikali katika hili ni wajibu wake sasa. Mimi nimejaribu kupita Mitaani hapa Dodoma kwa vijana wale wanaofanya biashara za mkononi. Unawasikia wanasema Waheshimiwa Wabunge wakiwa hapa Dodoma sisi *Alhamdulillah,* tunafanya biashara kwa raha kabisa. Lakini siku watayoondoka, tayari tunakabiliwa na virungu hapa. Sasa Serikali haifai kuwa kama mti wa kifa uongo. Maana mti wa kifa uongo ukiukaribia unabana majani, lakini ukiondoka unaanza kuonyesha majani, Serikali hatakiwi iende hivyo bwana!

Mheshimiwa Spika, inasikitisha vijana hawa wanakopa baadhi ya biashara. Anakwenda dukani anakopa viatu vya watu, anakuja anavipanga anataka kuuza, au anakopa vitambaa vya watu, anapanga anataka kuuza. Ghafla wanatokea Askari wanawafukuza vijana hapa, viatu na vitambaa wanaviacha, huku nyuma maskini vibaka wanachukua. Tunawatia madeni ya bure badala ya kuwasaidia, hatuwasaidii!

Mheshimiwa Spika, kama inapofikia hatua tukaona kwamba hapa labda wamekuwa ni kero kubwa katika eneo maalumu, tuwaambie basi msikae hata siku moja hapa. Lakini siyo leo unawaruhusu wanaona ni mahali halali pa kufanyia biashara, kesho unawafukuzwa, unawapiga, unawafanya waibiwe mali zao, wanakuwa hawawezi kuielewa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri atumie Maafisa wake wajaribu kufuatilia mambo haya ili manung'uniko madogo madogo yaondoke. Serikali inanung'unikiwa kwa vitu vidogo tu mnavyoviona. Watu wanaumia kwa vitu vidogo kama hivi tu, msije mkafikiria kuwa labda watu wanahitaji mambo makubwa, hakuna raia Mtaani anayetegemea kuwa atapelekewe fedha na Serikali akagaiwe atumie, hakuna hiyo. Lakini anategemea Serikali itamlinda katika kufanya mambo ambayo yeye mwenyewe anaweza akajitegemea. Kama vitu hivi havikusimamiwa na Serikali, atasimamia nani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shilingi milioni 500, Mheshimiwa Anne Kilango amesema sasa hivi. Nia ya Serikali kuzipeleka hizi fedha Mikoani ni nzuri. Mimi nina hakika sana ni kwa ajili ya kuwasaidia vijana kupata maendeleo yao. Lakini hii ni fitina kubwa. Kama hamkufanya *vetting machinery* katika kila Mkoa ya kuangalia hawa vijana kweli wamejikusanya, hawa kweli wanahitaji kusaidiwa, watachukua hizi fedha watu wachache na matokeo yake lile lengo la kuwasaidia vijana halitakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima kila Mkoa kuweka *vetting machinery* ndani ya Mkoa ya kuangalia hiki kikundi kweli kipo na kweli kinafanya kazi waweze kupata fedha. Vinginevyo, watajiunga watu kwenye vikundi vikundi walioko Ofisini wachukue fedha watumie na kwa sababu Serikali haina tabia ya kufunga wafanyakazi wake wakitumia fedha za Serikali, mwisho wa siku wamefaidika watu wachache, lakini lengo halikufikiwa. Lazima muwe waangalifu na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro. Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ndiyo mlezi wa Vyama vya Wafanyakazi. Mimi ningeomba labda watusaidie. Hivi mnafanya fanyaje kwa kushirikiana na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi kutatua migogoro inapotokea kama migomo na mambo mengine? Kwa sababu kwa tafsiri yangu mimi, huwa busara haitumiki vya kutosha katika kukabiliana na mambo hayo. Kama ingelikuwa busara inatumika, tusingesikia juzi hapa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii alipolalamika sana kuhusu kufukuzwa kwa Madaktari. Unapomfukuza Daktari uliyemsomesha kwa gharama kubwa, kwa sababu kadai tu nyongeza ya mshahara, mimi nafikiri hawakufanya kitu kizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati umefika basi, Wizara hii kukaa na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi kujadili migogoro hii inapotokea na wakaitatua kwa njia ya busara na hekima kubwa kwa faida ya watu wenyewe na kwa faida ya Taifa. Lakini mpango huu wa kufukuza fukuza, hii ni jazba ambayo hatusaidii, inatuumiza tu, kwa sababu *at the end of the day* mnamfukuza mtaalamu, anaondoka anakwenda nchi nyingine anakwenda anaajiriwa, anapata fedha, anapoteza imani na nchi yake, anaona

nchi yake haimpendi. Ukifanya mahesabu mwisho wa siku, unaona wewe ndiye uliyepoteza. Kwani watoto wetu hawatukeri nyumbani? Kwani ni mtoto gani aliyekukera ukasema wewe ondoka nyumbani kwangu? Au leo sikupi chakula!

Sasa Serikali kwa wananchi ni sawasawa na mtoto na baba yake tu, anaonyesha *concern* ya kuwa analalamika. Dawa sio kumfukuza, dawa ni kuwambia unalalamika hili, hili hatuliwezi, tutakufanya hili na hili, endelee kufanya kazi. Ndiyo watakapopata moyo. Lakini unamfukuza kama unavyomfukuza paka aliyeingia ndani ya nyumba uliyoacha kitoweo! Haifai bwana! Tunabeba mizigo ambayo sio mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi sikutaka kusema sana, kwa sababu ukisema sana unapoteza utamu wa maneno. Nakushukuru kwa kunipa fursa na nawatakia kila la kheri hawa jamaa zangu wapitishiwe Bajeti yao vizuri ili kazi iendelee Mitaani. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mhehsimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wake wawili kwa taarifa yao nzuri yenye kuleta mafanikio kwa mwaka 2006/2007. Hotuba ya Bajeti yao inaonyesha mikakati mizito kabisa ya kuwasaidia wananchi, mikakati mizito ya kuwasaidia vijana hasa kwenye Sekta ya Ajira pamoja na kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ninayapongeza Mashirika ya *NSSF, NIP*, kwa kazi zao kubwa sana wanazozifanya za kuwasaidia wananchi, lakini pia kwa kazi zao wanazozifanya za kuhakikisha Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo na Vijana inatekeleza majukumu yake kwa uaminifu na uadilifu na hatimaye wananchi na wafanyakazi kuwa na imani na vyombo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la wafanyakazi. Nikisema wafanyakazi kwenye Taasisi zetu hizi kama Mashirika na Idara nyingine, kuna Vyama vya Wafanyakazi. Vyama vya Wafanyakazi viko pale kwa ajili ya kuwasaidia wafanyakazi yanapotokea matatizo. Lakini ni ushahidi uliopo kabisa na Wizara inabidi iliangalie suala hili, viongozi walioko pale wa Vyama vya Wafanyakazi wanapofikia hatua ya kuwatetea wafanyakazi yanapotokea matatizo, *managemen*t ina maana uongozi wa juu huwa unawafanya vitendo vya kuonekana kwamba wao hawapo sasa kwa ajili ya kuwatetea wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo ni mengi, inaonekana sasa vile Vyama vya Wafanyakazi havina nguvu, wenye nguvu ni uongozi wa ngazi ya juu.

Mheshimiwa Spika, lakini unakuta wafanyakazi hao wa ngazi ya chini wanapata manyanyaso makubwa, kusimamishwa kazi, aidha, kufukuzwa, utetezi wao ni Vyama vya Wafanyakazi vilivyopo pale. Lakini hatimaye havina nguvu za kutosha za kuamua

nini kinachofanyika au kwa njia gani wapate haki zao. Sasa basi, Wizara hii iangalie vipewe nguvu ya ziada hivi Vyama vya Wafanyakazi, vifanye kazi kwa nguvu kwa kuwatetea wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakuta migogoro inayojitokeza, hatimaye hufikia kuletwa Wizarani. Tunashukuru kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri, rufaa zitapato 265 wameweza kuzishughulikia rufaa 155. Tunawashukuruni sana. Lakini hizi zilizobaki je?

Mheshimiwa Spika, mfanyakazi ni mfanyakazi, amekataa rufaa, huenda amesimamishwa kazi kwa miaka mawili, kwa miaka mitano, basi Wizara iweke mikakati ya ziada na ya makusudi kuhakikisha hizi nyingine zilizobaki nazo zinapatiwa ufumbuzi na huyo mfanyakazi apate uamuzi unaomtakia mafanikio mema.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la ajira za watoto. Wizara ifikie mahali iweke mikakati ya makusudi na sheria kabisa sehemu za kazi au maeneo mbalimbali yanayowaajiri watoto wenye umri chini ya miaka 18. Watoto wenye umri wa chini ya miaka 18 ni wengi, lakini wameajiriwa katika sehemu mbalimbali. Lakini kanuni na utaratibu wa sheria ya nchi yetu, kijana mwenye umri wa chini ya miaka 18 hajafikia kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, Lakini sasa tujiulize, ajira hiyo ambayo alikuwa ameipata hapo ina uhalali? Anapata kipato kile kinachostahili. Hilo nalo Wizara ilifanyie kazi iyaone maeneo kama hayo na ni maeneo mengi ya watu binafsi au Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, wanaajiri watu kwa maana ya kuwapatia kipato kidogo kwa sababu yule ni mdogo, ataridhika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifikie hatua hiyo ya kuona yule ni Mtanzania na yule ana haki na kama ana haki ya kuajiriwa, basi apate kile kipato kinachostahili. Kama hana haki, basi asiajiriwe pale, ila aelekezwe nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, sasa hilo liende sambamba na uanzishaji wa hivyo vikundi ambavyo mmesema mtavianzisha na sisi kama Waheshimiwa Wabunge, pia tutaendelea kuvianzisha kupitia wananchi wetu wa Majimbo na hatimaye kuweza kupata misaada kupitia kwenye Mfuko huu ambao Serikali inakusudia kupeleka Shilingi milioni 500.

Lakini kama walivyosema wenzangu, Shilingi milioni 500 zitakwenda kwenye maeneo hayo, lakini itafika mahali watakaofaidika aidha, ni wasimamizi wa hiyo mifuko kwenye maofisi huko Wilayani na Vijijini hizo fedha hazitafika.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye *ten percent* ambao sasa hivi tunao kwa maana ya asilimia tano ya vijana na asilimia tano ya akina mama, ubadhirifu mkubwa unaofanyika kwa hao mliowapa dhamana ya kugawa hizo fedha. Sasa isitokee tena kwenye hizi Shilingi milioni 500 zilizokwenda Mikoani hatimaye Wilayani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifikie hatua ya kuona ajira za Watanzania zinapata nafasi kubwa kwenye Taasisi ambazo kama uwezekano upo, basi Watanzania wapate ajira. Leo kwenye mahoteli yetu ya kitalii, ni wageni watupu. Lakini utakuta Watanzania wapo wenye sifa hizo. Natumaini hata nyinyi Mikutano mingine mnaweza mkafanya huko kwenye mahoteli hayo na mnaona wageni jinsi walivyojaa kwenye yale mahoteli. Lakini ukiuliza sifa za hao wageni kwenye yale mahoteli kwa kazi wanazozifanya zinalingana na Watanzania. Wizara ifikie mahali sasa imtengenezee utaratibu huyu Mtanzania mwenye sifa za kukaa hapa hotelini apate ajira badala ya kujaza wageni ambao na sisi Watanzania tulistahili kupata kazi maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lingine, vijana ambao wana shughuli mbalimbali za kujitafutia riziki, Wizara iwafuatilie, iweke watumishi wake wa kuwafuatilia hawa vijana kuona ni jinsi gani wanafanya kazi zao na kipato wanachokipata. Tunasema tunataka kuwakomboa vijana, lakini zipo kodi ndogo ndogo kwenye maeneo yetu zinawakatisha tamaa vijana. Anaamua aanzishe biashara kwa kipato cha kupata labda Sh. 5,000/= kwa siku, lakini ataambiwa lipa hiki, lipa hiki hatimaye hiyo Sh. 5,000/= yenyewe itakuwa imekatika na hana tena biashara endelevu kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iangalie wale vijana, isione kwa sababu amepata ajira ya kujiajiri mwenyewe imuache tu. Anateseka na kipato anachokipata, jioni akijumlisha alichokitoa na kilichobaki ni sawa sawa na hakuna. Wizara iwe makini sana kwenye suala hilo ili vijana wapate imani na Wizara hii na nchi hii na vile vile wapate imani na uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, lingine niiombe basi Wizara hao Maafisa Maendeleo ya Vijana walioko huko Wilayani wafanye kazi yao inavyotakiwa ya kuwaelimisha vijana jinsi gani ya kujiendeleza katika kujitafutia kipato. Utakuta baadhi ya Wilaya nyingine hawapo hao Maafisa, lakini kwenye Wilaya ambazo Maafisa wapo, ukimwuliza nitajie Kata au Vijiji vya Wilaya au Jimbo langu mimi nililopo, hajui hata Kata moja, shughuli zote wanamalizia pale Wilayani.

Mheshimiwa Spika, ndio maana hata hivi vikundi nimeona kuna idadi ya vikundi mmeviorodhesha humu kwa mujibu wa kila Wilaya, Mheshimiwa Waziri nataka nikuhakikishie unaweza ukute idadi uliyopelekewa Ofisini kwako ya hivi vikundi huenda huko Vijijini au kwenye Kata zetu, havipo. Ni majina wameyaandika wao na vikundi wameanzisha wao na hatimaye wamekufikishia Ofisini kwako na ndio maana wameviweka humu kwenye ripoti yako ya kuonyesha Bagamoyo ina vikundi 74, huenda sio kweli. Kwa hiyo, wakati umefika, tunaishauri Wizara iwahakikishie Maafisa Maendeleo Vijana walioko Wilayani wafanye kazi ile tunayoitaka ya Awamu ya Nne. Tusingependa turudi huko tulikotoka kwa sababu hawakutekeleza wajibu wao vizuri wakati wa *ten percent*.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, niishauri tu Wizara kutoa ushirikiano wa hali na mali na kuhakikisha vijana mahali popote walipo wanafanya kazi zao kwa uadilifu, lakini pia wajenge imani na Wizara hii. Nalisema hili kwa sababu isifikie mahali sura ya Wizara iwe Dar es Salaam tu. Sura ya Wizara ije Mikoani ionekane. Leo

tunazungumzia Wizara ya Elimu, hata mtoto mdogo wa Kijijini anaelewa, unazungumzia Wizara ya Mambo ya Ndani mtoto mdogo wa Kijijni anaelewa, Wizara ya Usalama wa Raia kwa maana hata Polisi wapo, lakini Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana inaonekana sura iko Makao Makuu, Dar es Salaam, haiko Mikoani. Njooni Mikoani na Wilayani Wizara hii nayo itambulike.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo nakushukuru. Naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri iliyochanganua mambo mengi ambayo ameiweka mbele yetu leo. Lakini pia niwapongeze Waheshimiwa Manaibu Waziri wote wawili, Mheshimiwa Nsanzugwanko na Mheshimiwa Sumari kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri na kuitumikia Serikali yetu. Nianze kwa kusema, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukuza ajira nchini, elimu ni muhimu sana na kimsingi ndiyo mahali pa kuanzia. Kwa sababu, pamoja na ahadi ya ajira milioni moja za aina mbalimbali, hata kama ingekuwa ajira milioni tatu na zinatoka kesho, ukaniambia Mheshimiwa Ndugai *qualification* yetu sisi ni *Form Four* tu nenda kule Jimboni Kongwa katukusanyie *Form Four* wenye *Division Three* tuletee hata kumi tu ambao wapo hawana cha kufanya ni *Form Four Division Three,* huenda nisiwapate. Kwa hiyo, liko tatizo kubwa na pa kuanzia ni hapo tunaposema kwenye Sekondari za Kata nchi nzima. Tuanzie hapo, Serikali iweke fedha kusaidia kila Sekondari ya Kata nchi hii ipate Walimu, vitabu, ili tupate vijana ambao wamevuka kwenye *level* fulani ambayo wakiweza kuwezeshwa, wana uwezo nao kujiwezesha hatua mbili zaidi kwenda mbele. Ndio mnaona Mijini vijana wengi kwenye jamii za wafugaji na maeneo makame Wamasai, Wagogo na makabila mengine yanayofanana na hayo yamejaa huko. Kwa sababu sasa hivi hali ni ngumu, hakuna cha kufanya, ajira zenyewe ni hizo za ulinzi ambazo hazina kitu, sana sana ni ku-*risk* maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pa kuanzia kwa mawazo yangu mimi ni hapo mahali pa elimu. Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Elimu na Wizara nyingine ili kuhakikisha kwamba vijana wanapata ile ya msingi yenyewe kwa maana Elimu ya Msingi na Sekondari na elimu ambayo itawasaidia katika kuendesha maisha yao baada ya hapo.

Serikali kupitia Bajeti hii, wamesema imeahidi Shilingi milioni 500 na mimi kwa kupitia kwa haraka haraka, kwa kila Mkoa. Lakini Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, amesema kwamba utaratibu na kanuni za matumizi za fedha hizi bado zinaandaliwa.

Mimi nasema, hebu tufanye haraka hizi taratibu. Ilikuwa ni vizuri zingelikuja kabla ya Bunge hili kwisha. Moja ya Semina ya hivi karibuni sana, zingekuwa ni kuhusu hizi taratibu za Shilingi milioni 500 ili tunavyoondoka hapa tunaondoka tumeelewana kabisa kwamba hii fedha ni vipi kwa Mkoa wa Dodoma kwa mfano tuna Wilaya tano. Kwa hiyo, ni milioni 100 kila Wilaya na utaratibu wake ukoje?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kwenye hotuba hii, Mheshimiwa Waziri ameeleza jambo moja kwamba walengwa wakuu wa mpango huu ni wajasiriamali ambao kwa kupata mikopo hiyo watapanua shughuli zao za uzalishaji mali na biashara. Ukishasema hivyo, sasa tunaachana njia. Mimi wale wa kwangu kule hata shughuli haiko, hawana kitu.

Mheshimiwa Spika, tunataka sasa tuwawezeshe hawa ambao hawana kitu, tuwatoe huko tuwaingize katika msingi ambao tunautaka. Sasa hizi zikilengwa tena kwa hao wenye shughuli na kupitia Mabenki, inaanza kwenda kule kule kwa Mfuko wa Pembejeo ambao waliolengwa ni wakulima wale wakaishia kuwa watazamaji wa ule mfuko mpaka kesho.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi mwakani tukifika hapa, tutaparurana kweli kweli kuhusu Shilingi milioni 500 kwamba hazijafika. Mimi naomba suala hili mlitazame kwa umakini mkubwa, muone ni namna gani mnaweza kusaidia vijana ambao wana nia ya kufanya kazi waweze kupata mitaji husika hasa zana za kilimo na kule kwetu hata hizi pampu za *money maker* ni muhimu sana. Pampu moja zile za laki moja ukikopesha vijana wengi wakaanzisha bustani zao wakaanza kulima na kumwagilia na kuuza nyanya na vitunguu na kadhalika watajiwezesha vizuri zaidi kuliko huu utaratibu wa mabenki ambao utataka waweke amana na kadhalika, vitu ambavyo hawana.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 35 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, kwa kushirikiana na Wizara yake ikishirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, wana lengo la kuanzisha *SACCOS* moja kwa vijana kwa kila Kata au Tarafa. Lengo zuri sana na mimi nakubaliana nalo. Lakini tatizo langu ni kwamba, ipo sheria ndogo kule Ushirika inasema, kwa kila Kata moja itaanzishwa *SACCOS* moja. Sasa hizi zitakazoongezeka, inakubalika au bado ile hoja ya watu wa Ushirika iko pale pale? Ni vizuri tukawa makini katika jambo hili ili tusije tukawa na nia ambayo haiwezi kutekelezeka kwa sababu ya sheria fulani fulani. Nitaomba ufafanuzi hapo jioni endapo hili la kuanzisha *SACCOS* kadhaa ndani ya Kata moja liko vipi.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi ambao bahati nzuri sasa wamepata *qualifications* zinazotakiwa kutoka kwenye Vyuo vyetu, wanakosa ajira rasmi zilizopo kwa sababu ya kipengele cha uzoefu. Kipengele hiki kimekuwa kikwazo sana. Ukienda kwenye sekta binafsi hawaangalii hiyo, sekta kama ya Mabenki iwe ni *Standard Chartered* iwe ni nini wanachukua vijana *fresh* kutoka *University, bright young people* wanawapa zile *tools* zinazotakiwa ndani ya miaka miwili hawa vijana ni *expertise.*

Serikalini hatuamini vijana kabisa. Kijana anapata *first class Form Four,* anapata *first class Form Six,* anapata Daraja la Kwanza *with hands* lakini bado kwenye ajira una uzoefu wa miaka mingapi? Huyu ni kijana safi kabisa, lakini hawana nafasi kwa sababu

ya kipengele hicho. Ningeomba kiangaliwe sana. Sasa hivi sio kama zamani. Uelewa wa vijana wa sasa ni wa haraka. Imekuwa ni enzi ya kompyuta, hii ni enzi ya televisheni, ni enzi ya utandawazi, vijana wanaelewa mambo mengi kwa muda mfupi ambao miaka ya 1950 na 1960 ilimchukua mtu apate uzoefu wa miaka mitano au kumi kupata hiyo *necessary knowledge,* ilibidi miaka kadhaa. Leo huo muda umekuwa mdogo kabisa.

Yuko tajiri mmoja *South Africa* anaitwa Tokyo Sexwell, alikuwa ni mmoja wa viongozi wa *NC* na alikaa Magereza karibu miaka 15 katika miaka 27 ya Mandela. Walivyotoka, walikubaliana wakagawana wengine wakawa kwenye Chama, wengine wakaenda kwenye *business.* Huyu ni mmoja aliyekwenda kwenye *business.* Ni tajiri mkubwa hivi sasa, ana-*investments* dunia nzima. Kwa nini namtaja hapa? Hata kwenye *exploration* ya mafuta hapa Tanzania nadhani ana *interests* kwenye maeneo haya. Tajiri kabisa! Yeye alichofanya alichukua vijana kabisa, lakini wale *bright youngmen,* wamesoma vizuri akawavuta wale, akatengeneza kikundi cha vijana kama 20 hivi, akaamua kusema hebu mimi nataka tufanye jambo fulani, tufanyeje? Vijana wanaweka vichwa chini leo hii, ndiyo wamemfikisha pale.

Kwa hiyo ninachozungumzia hapa, hizo dharau zetu kwa vijana, hebu tuziache. Tuna vijana wana akili kweli kweli! Matokeo yakitoka yatazameni. Matokeo ya *Form Four, Form Six* yatazameni! Kijana maskini kabisa toka kwenye kona fulani Kigoma huko, Kongwa huko wapi ana-*perform wonders,* anapotoka Chuo Kikuu ana nafasi gani kwenye ajira za nchi yetu? Utakuta ni ngumu sana.

Tulikuwa na maeneo kwa mfano kwenye Halmashauri za Wilaya, kila mwaka tunalia hapa, kwa mfano eneo la Uhasibu. Wahasibu hakuna, Wahasibu hakuna *for the past five years*. Mimi juzi kwenye Halmashauri yangu tumeajiri Wahasibu 12 wiki mbili zilizopita. *Very bright youngmen and women* wazuri kabisa wenye *B.Com* wenye *Accounts* wenye *Advanced Diploma in Certified Accountancy*, wenye *Degree Advanced Level* ya *Auditing,* wenye *Materials Management,* wazuri kabisa, wapo! Fursa hazipo.

Mheshimiwa Spika, tazama Idara ya Maji nchi nzima katika Halmashauri za Wilaya, wapi Idara ya Maji ina watumishi wa maana? Ni wale Mafundi Mchundo wa Vyuma na nini, basi. Ndio wamejaa kila mahali. Lakini Vyuo vyetu vinatoa Wahandisi kwa mamia. Tuna Halmashauri 130 na ngapi tu, lakini hatuwezi kupata Mhandisi mmoja mmoja tu kwa watu mia moja, yaani mia moja wanashindikana na wasaidizi wao. Iko Dar es Salaam *Institute of Technology,* inatoa vijana wangapi kila mwaka. Ni kukosekana kwa ile imani tu kwamba hawa vijana wanaweza tuwape nafasi. Kwa hiyo, tuko tayari twende hivyo hivyo na Halmashauri na Idara ambazo hazina watumishi, lakini vijana tunao. Kwa hiyo, ningeliomba hii hoja tuipunguze, tuwaamini vijana wetu kwamba wanaweza.

Lakini pia vijana wetu niwaase kwenye eneo ameongea kabla yangu ya hoteli za kitalii. Mimi kama nilivyowahi kusema, nimekaa kwenye mambo ya Wanyamapori huko, ndilo eneo ambalo nimekaa muda kidogo. Mambo haya ya Wanyamapori yanataka sana utalii na mahoteli.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo kubwa sana kwa vijana wetu kwa eneo hilo. Ni vizuri tujiweke sawa tuwape mafunzo ya kutosha kwenye eneo hilo la mahoteli. Makaribisho sio mazuri mahali pengi.

Mheshimiwa Spika, unakuta kijana anamkaribisha mgeni na Kiingereza chetu cha kujifunza, cha barabarani hiki, anaanza kumwuliza eeh, *what do you want*? Sasa *what do you want* ametafsiri Kiswahili kinachoulizwa kwenye hoteli ndogo, unataka nini?

Kwa Mzungu ukimwambia *what do you want,* maana yake yuko *out of place*. Maana yake aondoke. Hata sukari mezani, basi ndiyo inapotea hivi. Ukienda vyumbani hoteli chafu. Utakaa mahali unasubiri nusu saa hajaja hata mtu kukuuliza kwamba bwana mbona uko hapa?

Mheshimiwa Spika, sasa mwenye hoteli atachukua watu Kenya au Uganda na hata kama tukiwaambia Waheshimiwa hawa sasa hivi waweke mikingamo sana, jamani si kila siku tunaambiwa hapa *fast trucking* ya Afrika Mashariki suala la ajira ni mojawapo! Katika muda mfupi sana hatutabaguana kwa kusema huyu Mganda, huyu Mkenya katika ajira ndogo ndogo kama hizi za hoteli na kadhalika.

Kwa hiyo, dawa sasa ni kujidhatiti sisi Watanzania tufanane na wengine katika masoko kwa vijana kuchapa kazi. Masoko ya sasa hivi kama huchapi kazi huna nafasi. Hii habari ya kusema ooh, mimi Mtanzania kama ni sifa pekee, haitatusaidia. Tuwawezeshe vijana wetu kupata ajira hapa, tuwawezeshe vijana wetu kupenya masoko ya ajira Kenya, Uganda na kwingineko. Hilo litatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda wangu umekwisha, dogo la mwisho ni tatizo kubwa kwa vijana, tatizo la UKIMWI ambalo linawaua vijana wengi sana. Matumaini ya maisha kwa vijana yamekuwa ni madogo sana. Majuzi hapa nilikuwa nasoma utafiti fulani ambao unadhibitisha kabisa kwamba tohara... *(Hapa kengele ya ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kushukuru sana kwa kupata nafasi ili nami nichangie hoja hii nyeti inayohusu hasa ajira ya vijana. Lakini kabla ya yote naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri Prof. Maghembe kwa hotuba yake nzuri ambayo kimsingi ina mipango yote inayohusu ajira kwa kipindi hiki cha 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nitaanza hasa kuangalia utandawazi v/s ajira . Wakati utandawazi umeleta mambo mengi lakini vile vile yako mambo ambayo hayaendi vizuri katika suala la ajira. Wakati nchi za Ulaya ambako nako pia wana matatizo ya ajira yanayotokana na utandawazi kwa maana kwamba baada ya kupewa uhuru wa kuweza kwenda kuwekeza sehemu nyingine, basi Makampuni hayo yamejikuta yanakwenda kuwekeza katika nchi nyingine kama za Afrika na sisi katika nchi zetu tumekuwa tukiweka mazingira mazuri ya uwekezaji na hivyo kuwavutia hawa

waweze kuja. Katika nchi zao kumekuwa na *gap* na matatizo ya ajira kwa Makampuni yanaondoka yanakuja huku. Lakini kwetu tumekuwa tukifurahia kwa sababu wanawekeza.

Lakini vile vile hao wanapokuja wamekuwa wakija na mitaji mikubwa, wanakuja na vifaa vya kisasa ambapo wakifika kuwekeza katika nchi yetu, basi yale Makampuni madogo ya kwetu yamekuwa yakifa na yanapokufa, basi yanaacha watu wengi bila ajira.

Mheshimiwa Spika, nilichotaka kusema hapa, nilitaka tu kuainisha tu kwamba ni vizuri basi kwa Serikali yetu kupitia Wizara hii kuona umuhimu wa kulinda haya Makampuni ya Watanzania kwa sababu yanakuwa hayana mitaji mikubwa, hayana vifaa vya kisasa, lakini kimsingi haya Makampuni ndiyo yanaweza yakachukua Watanzania wengi kwenye ajira na zikawa ajira za muda mrefu na za kudumu tofauti na hizi ajira za Makampuni ya nje.

Mheshimiwa Spika, nadhani unaweza ukaangalia mwelekeo kama wa *Sheraton* ilibadilika baadaye ikawa *Royal Palm,* sasa hivi tunaambiwa ni *Moven Pick.* Sasa mimi nina wasiwasi ipo siku ukiangalia hasa matokeo yaliyotokea miaka ya 1990 au 1991 wakati mabadiliko ya uchumi yalipotokea nchi za *Eastern Europe* zika-*collapse* kiuchumi, basi tutegemee vile vile mabadiliko ya uchumi kwamba upo uwezekano hawa wawekezaji huko mbele wakapata sehemu nyingine za kuwekeza na wakaondoka na sisi kwa kuwa hatuna Makampuni, basi watu wetu wengi wakakosa kazi. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza, Serikali itoe kipaumbele katika zile taratibu za uwekezaji kwa Makampuni ya Watanzania, iangalie namna ya kupunguzia zile taratibu ikiwa ni pamoja na zile kodi na vitu vingine ili hawa waweze kuajiri Watanzania walio wengi na ambao wanaweza kufanya kazi kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu la pili, ninataka kuongelea suala la maandalizi ya vijana kuingia kwenye soko la ajira huru. Mfumo ambao umekuwa ukitumika huko nyuma hasa miaka 100 iliyopita umekuwa ni ule ambao mtu akihitaji kazi anaandika *CV* yake, anaambatanisha barua ambayo inaelezea sana yeye amefanya nini miaka 20 iliyopita, miaka 10 iliyopita na hizo *application* zinakwenda kwenye Utumishi.

Kwa hiyo, anayeangalia sio yule ambaye yuko kazini na baadaye yule mtu anapangiwa kazi na kusimamiwa na mtu ambaye yeye hakuweza kumchagua. Sasa nataka kusema kwamba, mtazamo wa sasa hivi umebadilika, sasa hivi wanasema kwamba sehemu kubwa ya Makampuni anayefanya *interview* ni mwenye Kampuni mwenyewe, *Businessman* au Meneja mwenyewe. Kwa hiyo, yeye yuko *interested* kwamba wewe unayetaka ile ajira utamfanyia nini na sio kwamba wewe ulifanya nini jana.

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza hapa kwamba, ni vizuri basi maandalizi ya vijana wetu katika soko la ajira yawekwe vizuri na hasa vijana waandaliwe wanapokwenda hizi sehemu kuwa tayari kusema kwamba wao wako tayari kuisaidia ile Kampuni. Kwa hiyo napendekeza mafunzo yazingatie sana vijana hawa kuwa na *skills*

za *problem solving* wawe na *skills* za *innovations, creations, abilities* na kubwa ambalo hata mwenzangu ameliongelea ni *language skills,* wengi wanakuwa na lugha ambayo sio nzuri ambayo wanashindwa kujieleza na baadaye kukosa ajira.

Vile vile, nilikuwa nadhani, basi Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuona kama zile *skills* ambazo zinatolewa kwenye Shule za Sekondari na Vyuo, basi zinakuwa ni *skills* ambazo zinatakiwa kwenye soko hasa ukizingatia kwamba idadi ya vijana wengi ni hawa ambao wako kwenye Shule za Msingi wanaomaliza na Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, nataka kuongezea kwamba ni vizuri tukatumia sana Kituo cha Uwekezaji ambacho kina maandalizi mazuri aliyoyaacha Spika wetu, Mheshimiwa John Samuel Sitta. Ukienda pale utakuta matazamio ya Makampuni mengi yanayoingia Tanzania kwa ajili ya uwekezaji na hivyo utaona mtazamo wa uwekezaji katika viwanda, kilimo, *manufacturing industries* na sehemu nyingine zote. Inaeleza *manufacturing* kwa miaka mingapi itakuwa kwenye soko, kilimo ni kwa miaka mingapi.

Mheshimiwa Spika, nilidhani basi kwa kupitia Wizara hii, kama wanaweza wakapata hizo takwimu na hizo *projections,* basi kwa kushirikiana na Vyuo vya Elimu, viweze ku-*update* mitaala yao kwa kuzingatia hali halisi ya soko inayozingatia uwekezaji nchini mwetu. Hilo ni la msingi. Tulipokuwa tunafanya *review* ya mitaala ya *DIT* tulitembelea kituo hiki na tukakuta kweli kuna vitu vingi ambavyo vinatakiwa vichukuliwe kwa ajili ya kurekebisha mitaala.

Mheshimiwa Spika, nataka nichangie vile vile kuhusu vijana wetu, hiki ni kipengele kingine ambacho nitanukuu kwa lugha nyingine, ni kwamba wanakuwa na *unrealistic expectations* kwenye ajira. Tumejengwa na mfumo wa kupata ajira *permanent full employment*. Lakini mabadiliko ya sasa hivi, kwa sababu Kampuni zetu zina uwezo mdogo, kwa hiyo, haziwezi kutoa vitu kama *security, pension* na vitu vingine kwa kuwa wamejikuta wanaweza kuwa tayari kuajiri vijana ama kwa *contract* ama kwa *part time* au kwa aina nyingine yoyote ambayo inakuwa tu ya muda wa kudumu. Sasa vijana wetu wamekuwa hawapendi ajira za muda wakidhani kwamba hizo sio ajira. Sasa nilidhani hapa suala muhimu ni kupata kazi na nadhani baada ya kupata kazi inawezekana vile vile ukakuta kwamba umefikiriwa kupata *full employment*.

Mheshimiwa Spika, lakini labda niseme kwenye hili, basi naiomba Serikali pamoja na kwamba ajira nyingi sio za *permanent,* lakini takwimu zinaonyesha kwamba njia pekee ya kuweza kujenga uchumi ni pale unapokuwa na *full employment* na hii naomba kwa idhini yako nirejee mkakati wa *ILO* ambao ulikuwa *adapted* mwaka 1964 kama ndiyo njia kuu ya kuweza kujenga uchumi mahali popote na nitasoma: *"Promoting the goal of full employment as basic bioet of economic and social policies and to enabling all men and women to attend secure and sustainable livelihood through freely chosen employment and work"* Sasa hii hata kwenye ule Mkutano wa *World Summit for Social Development* uliofanyika Copenhagen mwaka 1995 uliohudhuriwa na nchi 186 uliona bado hii ni muhimu kwamba *full employment* ni aina moja ambayo ingeweza ikatuletea uchumi, kwani mtu anapokuwa na *security* ya kazi yake, mtu anapokuwa na

pensheni hii ni *incentive* pekee inayomwezesha kuchapa kazi na kigezo cha kuinua uchumi ni pamoja na kuchapa kazi kwa bidii na kwa juhudi zote.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu ajira ya kilimo ambayo nadhani ukiangalia takwimu za mwaka 1999 ambazo zinapatikana kwenye *web* ya Taifa zinaonyesha kwamba vijana milioni 16 nguvu kazi hiyo ndio vijana ambao wanakuwa hawana ajira na wengi wao sehemu kubwa ni kati ya miaka 10 mpaka 19 na asilimia 80 yao wanaishi Vijijini.

Vile vile, inaonekana kwamba, ukiangalia umri wa wale ambao wako tayari kufanya kazi, asilimia 82 wanaishi Vijijini. Sasa nilidhani hapa ndipo kwenye ajira ambapo Serikali inatakiwa iweke mikakati ambayo tumekuwa tukiongelea katika Wizara nyingi hasa masuala ya kuweka miundombinu, masuala ya kuboresha elimu, masuala ya kuboresha ugavi wa bidhaa, kumiliki ardhi na pembejeo na vitu vingine. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Waziri husika aone kwamba kushirikisha Wizara nyingine katika suala la kufanikisha ajira ni suala muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningeomba kwamba wakati *ICT* ilipokuwa inaingia nchini Vyuo vilikazana sana kufundisha kompyuta katika kozi mbalimbali na baadaye *interprenuer.* Nilikuwa nadhani kama maandalizi basi sasa hivi iwezekane kwenye Vyuo ama kwa Semina au kwa namna nyingine, basi watoe mafunzo ya ushirika ili hawa watu wanapomaliza waweze kuwa tayari kuanzisha Vyama vyao vya Ushirika na kuweza kujiajiri baada ya kupewa mikopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba tena nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi na nimshukuru Waziri kwa kutoa hotuba yake hii nzuri ambayo kwa hakika ina mambo mengi ya kukidhi. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa tena nafasi hii ya kuchangia katika Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Awali ya yote ningependa nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu na wataalamu wake kwa kutengeneza hotuba hii nzuri ambayo imeweka wazi dira ya Wizara yake katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi, kuongeza ajira na kuwaendeleza vijana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, ningependa tu niikumbushe Wizara hii kwamba tulitegemea katika hotuba hii kuwepo na tathmini ya mchango wa wanawake katika kuendeleza kazi na kipato cha nchi hii.

Naomba nichukue nafasi hii niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote walioleta wake zao hapa na kuwatambulisha. Sio kwamba waliwaleta hapa kuja kuwaonyesha jinsi walivyo wazuri tu, hapana. Nafikiri wanathamini mchango wao katika kuwasaidia wao kufanya kazi ya kuendeleza majukumu waliyopewa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, wanawake tunafanya kazi nyingi majumbani. Kazi hiyo mpaka leo ninasikitika kwamba Serikali yetu ukilinganisha na Serikali nyingine haijatoa

tathimini ya mchango wa wanawake katika kuchangia pato la Taifa. Tunatunza waume zetu, tunatunza watoto wetu, tunapika maandazi, tunalisha watoto, lakini haya yote tunayoyafanya yamewekwa pembeni. Hii inafanya wanawake tukate tamaa ya kutunza familia zetu na waume zetu. Naomba Wizara hii, basi nafikiri wakati ujao iweke kipaumbele katika kutathmini mchango wa wanawake katika kusaidia maendeleo ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, ningependa pia nizungumzie jambo moja ambalo ni *general*. Jambo hilo ni ile lugha ambayo inaonekana sana katika *Advertisement* za kazi: "Uzoefu usiopungua miaka mitatu." Sasa vijana wetu watapata uzoefu kutoka wapi? Nakumbuka mwaka 2004 nikiwa nachangia Wizara hii, nilizungumzia hilo na nikategemea kwamba Serikali itatoa mwongozo kwamba kama mtu ana *qualification,* basi apewe kazi, ajifunze mle. Huwezi kupata uzoefu kutokana na unavyoishi nyumbani kwa kazi ya Ofisini. Ni lazima uingie Ofisini upate uzoefu. Ninaomba tamko la Serikali la kurekebisha kauli hii kwa sababu limewakatisha tamaa vijana na limetoa mianya kwa wazee wenzetu ambao wamefikia kustaafu kuanza kurudiarudia kufanya kazi kwa mikataba na inaendelea kunyima vijana fursa ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo, ningependa sasa niseme juu ya kukua kwa ajira. Serikali imeonyesha azima yake ya kukuza ajira nchini na imesema kwamba kutakuwepo na kukuza ajira kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta rasmi, mimi sina tatizo nayo, lakini nina tatizo na sekta isiyokuwa rasmi. Katika nchi yetu, mimi nipo hapa na akina mama wengine tunafanya kazi kwa sababu tuna wafanyakazi wa majumbani. Ni wengi na wasichana wetu siku hizi, nafikiri njia pekee ya kuwaajiri waliowengi ambao hawakupata fursa ya kwenda Shule zaidi ni katika majumba yetu, katika Ma-*guest House* na kwenye *Bar*.

Nakumbuka miaka mitatu iliyopita nikichangia katika Bunge hili nilizungumzia hawa wafanyakazi wa majumbani, wafanyakazi wa *Bar* na wafanyakazi wa nyumba za wageni na sehemu nyingine za burudani.

Mheshimiwa Spika, hawa watu ni muhimu sana, lakini mpaka sasa hivi katika sera ya ajira ambayo nafikiri itatoka na katika matamko yote ambayo nimeangalia katika hotuba za Mawaziri wa Wizara hii hawajapewa umuhimu na kipaumbele kinachotakiwa. Mimi ninaomba leo Waziri wa Wizara hii atueleze kwamba, Serikali ina mikakati gani ya kurasimisha ile ajira ya wafanyakazi wa majumbani, wafanyakazi wa kwenye *Bar* na Ma-*guest house* na sehemu nyingine za burudani? Hawa unakuta kwamba mishahara yao inakuwa *dictated* na wale waajiri kwa sababu wanajua kwamba *their desperate*. Hakuna mtu anayengalia kwamba huyu anafanyakazi kama mimi ninayemwacha nyumbani kwangu nakwenda kufanya kazi, anahitaji kuwa na haki na maslahi.

Ningependa leo Mheshimiwa Waziri atueleze, kwenye Shirika la *NSSF* kuna wafanyakazi wangapi wa majumbani wanaolipiwa, wanaowekewa akiba *NSSF*? Kuna wachache wa Ma-*guest house*. Lakini wafanyakazi wa majumbani hakuna anayewawekea

akiba katika shirika letu hili la *NSSF*. Wana haki ya kupata hifadhi, wana watoto, watastaafu, watakwenda wapi, kama atatoka nyumbani kwako wewe amekulimia bustani, amekulishia watoto, amempikia mume wako au amepikia mke wako anaondoka hana maslahi ya kumsaidia yeye na familia yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri leo atamke kwamba atafanya kazi ya kuhakikisha kwamba atatengeneza sera na maelekezo ya kuwasaidia wafanyakazi ya majumbani na wanaofanya kazi kwenye ma-*bar*.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa kwenye ma-*bar* nasikitika kusema kwamba wanatumika kama chambo cha kuvutia wanywaji katika hizo *Bar*. Wengine wanaambiwa kwamba wewe okota vifuniko vyako utalipwa. Wasipokunywa, mtu hajatoka toka nyumbani kwake akaja kufanyakazi? Hao ningeomba na Serikali izungumze kwamba wanalipwa mshahara wa Shilingi ngapi na maslahi yao yaonekane wazi.

Mheshimiwa Spika, lingine ningependa kuzungumzia elimu ya ujasiriamali pamoja na elimu ya biashara na *management* ya shughuli binafsi za vijana. Pale Morogoro kulikuwa na Chuo chetu cha CCM, kiko Kilosa. Kile Chuo kimepewa Idara ya Vijana, lakini mpaka sasa hivi nasikitika kuona kwamba hakuna *activity* yoyote ambayo inaendelea katika lile eneo.

Napenda nitoe ushauri kwamba, kile Chuo na Vyuo vingine ambavyo vipo kwa ajili ya vijana, naomba vitumike kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi ya kufundisha vijana *management* ya *small enterprises* waende kwa wiki moja wiki mbili, wajifunze namna ya kuweka mahesabu yao na wajue kwamba anapofanya biashara yake isiwe tu ni kazi ya kuzunguka duka la barabarani, ajue kwamba ninaondoka asubuhi ninakwenda na bidhaa kiasi hiki, nikirudi nina faida ya Sh.500/=, na hii Sh. 500/= nitumie Sh.250/= kula na Sh.250/= niweke kwenye kopo kama akiba yangu Jumamosi nipeleke Benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wanataabika. Ukimwuliza kama ana chochote ambacho ameweka, anakwambia anatafuta kula. Sasa huyu kijana ambaye anatafuta kula, siku akiamua kuoa na mke atatafuta kula kwa mkewe na watoto barabarani, hataweza. Atafanya mambo mengine ambayo hayafai.

Lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni hizi Shilingi milioni 500 ambazo zitakwenda Benki halafu vijana wakakope. Mheshimwa Waziri hakutueleza kwamba hizi Benki ambazo zitakuwa na wakala wa kutoa hizi pesa watahitaji kuwa na dhamana, riba na kama watachaji riba, tutakuwa tunajaribu kutwanga maji kwenye kinu. Kwa sababu shughuli nyingi watakazozifanya hawa vijana watakuwa na uwezo wa kuweza kutengeneza faida kubwa ya kuweza kulipa riba ya Benki. Sasa tunaomba utuambie sisi Waheshimiwa Wabunge tunapokwenda kuhamasisha kwamba tuwaambie wakakope kwa masharti gani na wanawezaje wakafaidika bila kufanyia kazi ile Benki? Kwa sababu hawatabakiwa na kitu! Naomba hili suala riba liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, kwenye ajira ya vijana, mimi naomba kwa sababu vijana ni suala la mtambuka, nizungumze kidogo kuhusu Halmashauri zetu Idara ya

Ardhi. Katika Manispaa nyingi na *Town Council* nyingi, kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya bustani. Sasa tunashangaa tunasema hawataki kulima. Sasa kijana aliyezaliwa Manzese huwezi kumwambia kwamba aje Morogoro kufanya kazi ya kulima kule? *(Makofi)*

Lakini kuna maeneo ambayo nafikiri yalikuwa yametengwa kwa ajili ya bustani kule Dar es Salaam na hii ni wazi kwa sababu vijana wengine wapo tayari kulima. Ukipita Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Bonde la Jangwani vijana wanalima mchicha. Sasa watasaidiwaje vijana hawa kuweze kupata maeneo makubwa ili na vijana wengine wajiunge nao waweze kulima mchicha ambao nafikiri una faida kwa sababu wanaendelea kulima.

Mheshimiwa Spika, hilo ningependa liangaliwe sana kwamba maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya bustani yasitolewe kwa wafanyabiashara kujenga *Bar*badala ya vijana kwenda kulima mboga waweze kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni lile ambalo lilizungumzwa kwamba hizi *SACCOS* ambazo Wizara imepanga kuanzisha, ikishirikiana na Wizara ya Kilimo, zinakuwa kwenye kila Kata, bado mimi nina wasiwasi. Wizara ya Kilimo na Ushirika haina mtandao mpaka kwenye Kata. Labda kuna *extension officer*.

Kwa kuwa Wizara hii haina mtandao mpaka kwenye Kata, mimi ningeomba ianze ushirikiano na TAMISEMI kwa sababu wao wana mtandao mpaka kwenye ngazi ya Kata ili kuweza kutengeneza mikakati ya kuunda vikundi, kuelimisha pamoja na kuendelea kutoa ushauri wa kudumu endelevu kwa vijana wakiwa wameanzisha ile miradi yao. Kwa sababu kuwapa Semina ya siku moja tu na kuwaachia waanze shughuli, nafikiri hata hizo *SACCOS* zitakufa na mikopo watakayokopa itakufa, watakimbia, watahama, watakwenda kwingine.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nilikuwa natarajia kuona kwamba katika hotuba hii, Wizara yetu ingezungumza au ingetoa mikakati ya kuwawezesha vijana wasihame kutoka Vijijini kwenda Mijini. Vijana wanahama kutoka Vijijini kwenda Mijini kwa sababu hawana burudani, wanakwenda Mijini kwa sababu ndiko kuna kila kitu ambacho ni kizuri. Sasa mimi sidhani kama ina jawabu. Lakini ninaamini kwamba Wizara ikizungumza na vijana kule kule Vijijini watawaeleza kwamba tatizo ni nini linawafanya wanahamia Mijini kwenda kuzunguka kutwa, wakizungusha *pair* mbili za viatu kwenda Mjini.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara kama inawezekana leo au kwa siku za usoni, itueleze kwamba ina mipango gani kabambe ya kuhakikisha kwamba tunawatunza watoto wetu wabakie Vijijini na wasiende kuzunguka Mijini wakitafuta ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, nimeona kuna sera ya vijana, wamesema watapewa vijana na wadau wengine. Mimi naomba kwamba malezi ya vijana yanaanzia kwenye Shule akiwa mtoto. Basi hizi sera nakala zake zipelekwe hata kwenye maktaba zetu, zipekekwe kwenye Shule zetu za *Primary*, *Secondary*, Vyuo na kwenye Taasisi za Dini

na zisizokuwa za kiserikali kwa sababu sisi wote ni wadau wa kuhakikisha kwamba vijana wanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameshukuru mashirika ya kimataifa humu ndani kwa kusaidia Wizara yake. Lakini sijaona popote ambako ameshukuru *NGO's* za kitanzania, ameshukuru Taasisi za Dini ambazo kwa kweli zinatoa mchango mkubwa katika kuwasaidia vijana kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba, atakapofanya majumuisho, atakuwa na ile *courtesy* ya ku-*mention* au kukumbuka kwamba kuna wadau wengine kama mashirika yasiokuwa ya kiserikari yanayoshughulika na vijana, tutashirikiana nao na tutashukuru kwa mchango wao na atatoa tamko kwamba kuna Taasisi za Dini zinazotoa msaada kwa vijana wetu na kuwaomba kwamba waendelee kutoa mchango huo kwa sababu malezi ya vijana ni pamoja na kuambiwa kwamba anawajibika kufanya kazi na misahafu yote inasema kwamba usipofanya kazi na usile.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tukiwaambia hivyo, Mashirika ya Dini na Viongozi wa Dini wakaendelea kugonga nyundo, nafikiri vijana wataona kwamba sasa Mungu anasema tufanye kazi, Taifa linasema tufanye kazi, jamii inasema tufanye kazi, tutafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niitakie Wizara hii kila la kheri katika kutekeleza mipango hii mizuri ya kumtetea mfanyakazi, ya kutekeleza ajira za vijana pamoja na kuwaendeleza vijana wetu. Naomba kuunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwanza kwa kunipa fursa hii niweze kutoa mchango wangu japo kuwa utakuwa mfupi tu. Awali ya yote, napenda kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa. *(Makofi)*

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, kwa hotuba yake nzuri, ambayo maelezo yake kwa kweli yanatia moyo na dalili tumekwishaziona hata sisi pia.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitakuwa mpungufu wa fadhila kama nitaacha kuwapongeza Manaibu Waziri pamoja na Wizara nzima kwa ujumla kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ambayo ametuandalia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika pongeza, napenda niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa makusudi yake ya dhati ya kukabiliana na tatizo la ajira, hususan kwa vijana wanawake na walemavu, kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi zangu hizo pamoja na shukrani, napenda nitoe mchango wangu mfupi kwenye suala la ajira na maendeleo ya vijana, hususan nikizingatia eneo langu la Korogwe Vijijini au maeneo ya Vijijini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kiwango kikubwa cha ajira kwa upande wa Vijijini kinatokana na sehemu mbili hasa au sekta mbili hasa, kwa maana ya kilimo, au rasilimali zilizoko kule. Nikianzia labda na upande wa kilimo, katika kilimo, ajira inaweza ikatokana kule. Aidha na kujiajiri mwenyewe, au kuajiriwa rasmi na wale wenye mashamba makubwa.

Katika suala la kujiajiri mwenyewe, kwa upande wa Mijini, nina imani kabisa kwa wengi wetu, ardhi sio tatizo kwa upande wa sisi wa Vijijini. Bali kikubwa kinachotakiwa ni maandalizi ya jinsi gani ya kutumia kikamilifu ardhi hii.

Mheshimiwa Spika, bila shaka tuweke maanani kwamba wakati sasa umefika wa kutambua kwa vitendo baadhi ya haya machache ambayo nitayataja.

Kwanza Serikali ielewe wazi au itoe thamani kwa ardhi ya mkulima, kwa sababu bila ya kufanya hivyo, kwa kweli mkulima huyu tutakuwa hatukumsaidia sana. Bila kuweka ardhi katika thamani, ina maana hata uwezekano wa kupata mikopo pia utakuwa mdogo sana. *(Makofi)*

La pili, mkulima huyu kwa kweli tumwezeshe kwa kumpatia mikopo, hususan ya pembejeo na zana. Nadhani tukubaliane sote hapa kwamba kilimo tunachokiongolea hapa cha kumwezesha mkulima, kwa kweli wa Vijijini, sio kilimo cha jembe tena, bali ni kilimo cha kutumia zana na pembejeo. Hiki ndicho kitaweza kumwondolea umaskini mkulima wa Vijijini, kitaweza kumwajiri, kitaweza kumpa ajira ya kutegemea.

La tatu, ni lazima mkulima huyu tumhakikishie kwamba tunampatia soko, kwa sababu bila ya kumpatia soko, hata akizalisha hayo mazao ya uhakika, bila ya soko itakuwa bado hatujamwondolea umaskini.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, tumhakikishie miundombinu kwa maana ya barabara, kwa sababu atakapozalisha bila shaka atahitaji barabara za kupelekea mazao yake sokoni.

Mheshimiwa Spika, nimeongelea upande wa kilimo, kama nilivyosema, kumpatia zana mkulima huyu kwa kweli ndiko kutamwondolea umaskini na sio zana tu. Nashukuru sana Serikali yetu imetoa Shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa za kuweza kuendeleza maendeleo mbalimbali katika Mikoa ileile.

Mimi kwa ushauri wangu, kiasi kikubwa cha pesa hizi kwa kweli zingeelekezwa kwa wakulima ili tuwawezeshe. Tuna wakulima wadogo wadogo wengi tu katika maeneo yangu, kwa mfano ya Korogwe Vijijini wakulima wa chai, ambao wako katika Kata za Bugu Dindila, na maeneo mengine. Kama kweli kiasi hiki cha Shilingi milioni 500 kingeweza kikawafikia, nina imani kabisa uzalishaji ungekuwa mkubwa ambao matunda yake wangeweza kuyaona na pia sio wao tu, bali hata uchumi wa nchi ungeweza ukainuka.

Pesa hizi pia sio vibaya kwa kweli zikaelekezwa kwa wakulima wa Kizara, ambao ni wakulima maalum wa zao la Kahawa. Zao la Kahawa linailetea nchi yetu kipato cha

hali ya juu. Kwa hiyo, tutakapowezesha kutokana na hizi Shilingi milioni 500, nina imani kabisa wao wenyewe tutakuwa tumewawezesha na sio wao tu, bali hata nchi pia tutakuwa tumeiwezesha.

Upande wa rasilimali, bahati nzuri katika maeneo ya Vijijini, tuna rasilimali za aina mbalimbali, tunayo machimbo ya madini ya vito mbalimbali, tuna mito ambayo tunaweza tukajiajiri kwenye upande wa uvuvi, tuna maziwa hivyo hivyo, tuna misitu hivyo hivyo. Kwa hiyo, suala la ajira, kwa kutumia rasilimali zetu tulizonazo Vijijini, nina imani kabisa linawezekana. Nitoe mfano mdogo tu kwenye upande wa machimbo, tunazo hazina. Tuna hazina kubwa sana upande wa Korongwe Vijijini, hususan maeneo ya Kalalani, Kigwasi, ambayo yana vito vya madini ya aina mbalimbali. Kama tutaweza kutumia maeneo haya, kwa maana ya kuwatumia vizuri vijana walioko kule, nina imani kabisa suala la ajira, litakuwa tumeliondoa kwa kwa asilimia kubwa tu.

Mheshimiwa Spika, ili wananchi hawa walioko kwenye machimbo waweze kujiajiri wenyewe, nirudi pale pale, mchango ule wa Shilingi milioni 500, ninaishauri Wizara yetu ya Kazi ijaribu kuliangalia kwa makini hili ni kiasi gani kinaweza kikawafikia wananchi wale au wachimbaji wale wadogo wa sehemu hii ya Kalalani na Kigwasi. Kule sio kwamba kuna masuala ya uchimbaji tu, katika kukuza ajira, katika maeneo yale pia tunaweza tukawasaidia hata wale akina mama lishe pia, tukawapatia mikopo midogo midogo, kwa kuitumia Wizara yetu hii ya Kazi ili waweze kuendesha biashara zao, katika njia nzuri na mbadala zaidi.

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa, ni Wizara hii kuweka mikakati madhubuti ya kuwakusanya kwa mfano vijana wale walioko kule kwenye machimbo na kuwawezesha kuwapatia mikopo midogo midogo ya kuweza kuwanunulia mashine, hata kama sio mashine au vyombo vidogo vidogo vya mkono ili wapate kufanya uchimbaji huu katika njia ya umakini zaidi. Pia sio kuwapatia vyombo tu, bali pia naiomba Wizara hii iwapatie elimu kwa sababu, kuwapatia vyombo bila ya elimu itakuwa kidogo hapo tumepunguza ufanisi wa uzalishaji wa kile kinachotoka kwenye machimbo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa tuelewe wazi kwamba umefika wakati tusiwaone vijana wale kwamba ni wavamizi, bali tuwatumie kama wazalishaji, tuwatumie kama watu ambao wanaweza wakajiajiri wenyewe. Maana yake imeshakomaa, zana ya kusema kwamba walio kwenye machimbo kule, ukiachilia mbali wale wachimbaji wakubwa, wale vijana ni wavamizi. Tuiondoe hiyo dhana hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema, mchango wangu utakuwa mfupi tu, labda la mwisho nijaribu kuunganisha Wizara mbalimbali, ambazo zinaweza zikasaidiana na Wizara yetu ya Kazi katika kukomboa au katika kutoa ajira za vijana. Tutakapounganisha Wizara kwa mfano ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Kazi yenyewe, Wizara ya Ulinzi, kwa maana ya Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na TAMISEMI, tunaweza kabisa kuendeleza ajira kwa hususan vijana waliopo kwenye Majimbo ya Vijijini.

Mheshimiwa Spika, hapa ninachokizungumzia kikubwa, kwa mfano tukichukulia Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu, pamoja na hii ya Kazi, ni Wizara ambazo zinaweza kabisa zikafufua ile Sheria ya Elimu *(Education Act)* Na.10 ya mwaka 1995 ambayo ni ya *Local Education Authority Schools* kwa maana ya *trade school*, ambayo pia imeipa jukumu Halmashauri za Wilaya kujenga, kusimamia na kuendesha Shule hizi au Vyuo hivi vya Ufundi, kwa maana ya *trade schools.*

*Trade schools* hizi zitakapojengwa, bila shaka zitawawezesha vijana wetu wengi ambao kwa bahati mbaya hawakuweza kuendelea na masomo ya Darasa la Tisa au na masomo ya *Form One*, kuwapatia sehemu ya kuweza kuendelea na masomo kuwa ya ufundi. Pale wanaweza wakachukua ufundi wa fani mbalimbali wanaweza wakachukua uashi, kilimo, ufundi chuma, na kadhalika. Kwa upande wa wasichana, wanaweza wakachukua cherehani, ushonaji na ususi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza kozi hizi, nina imani kabisa watakuwa kwa njia moja au nyingine, aidha, watajiajiri, wenyewe au kwa kutumia Wizara yetu hii ya kazi, wanaweza wakapatiwa kazi kirahisi. Sio sawa na mtu ambaye hana ujuzi wa fani yoyote. Kwa hiyo, umuhimu wa kurudisha ile Sheria *(Education Act)* Na. 10 ya mwaka 1995, kwa maana ya kujenga Shule ndogo ndogo za ufundi ni muhimu sana. Naomba Wizara pia ilizingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, uhusiano kati ya Wizara yetu hii ya kazi na JKT ninaozungumzia ni pale tunapozungumzia wale vijana ambao wanakaa kwenye makambi miaka miwili. Pale nina imani kabisa watu tunafahamu sio kwamba wanajifundisha bunduki, bali wamejifundisha fani mbalimbali, iwe ni jukumu la Wizara hii tusiachie Wizara ya Ulinzi peke yake, kwamba wakishamaliza kozi zao zile, au muda wao ukishamalizika, basi hilo ni suala la Wizara ya Ulinzi kuwapatia kazi, hapana. Pale pana mafundi vyerehani, mafundi wasusi, mafundi vyuma, mafundi magari, mafundi wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara ijione kwamba au isikie kwamba ni wajibu wake pale panapowezekana kuwapatia kazi vijana wale waliomaliza mafunzo pale, kwa sababu watakuwa ni watu ambao tayari wanaujuzi wao.

Mheshimiwa Spika, nirudie maneno yangu ya awali kwamba mchango wangu utakuwa ni mfupi tu, sasa naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mhina. Mchango haukuwa mfupi, hiyo ilikuwa ni kengele ya pili sasa.

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo. Hapo ndipo tumefikia mwisho wa wazungumzaji kwa asubuhi na muda uliobaki hauruhusu kumwita anayefuata.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumatatu tarehe 7 Septemba, saa tano asubuhi, tutafikiwa na Tume ya Rais, inayotathimini mfumo na viwango vya mishahara ya Watumishi wa Serikali. Kwa hiyo, Wajumbe wote wa Tume ya Huduma za Bunge,

pamoja na wale wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Katiba Sheria na Utawala; Tume na Kamati hizo mbili tutakutana na Tume hii kwa niaba ya Wabunge wote, katika Ukumbi wa Mkutano wa Spika, saa tano asubuhi Jumatatu.

Tume ya Rais inayokusanya maoni na kutathmini mfumo na viwango vya mishahara na marupurupu mengine ya Watumishi wa Serikali. Aidha, siku hiyo hiyo saa 7.30, Tume ya Huduma za Bunge na Kamati ya Uongozi kwa pamoja watakuwa na Kikao na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuzingatia baadhi ya matatizo ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa *APNAC,* yaani Wabunge wanaopambana na tatizo la rushwa, wanachama wa Kamati hiyo Dr. Zainab Gama, Mwenyekiti, anaomba Wajumbe wote wakutane katika Ukumbi wa zamani wa Bunge saa saba mchana leo, Wajumbe wa *APNAC* Tanzania. Waheshimiwa Wabunge kesho saa nne asubuhi, kutakuwa na uzinduzi wa kampeni ya kuongeza kasi ya kutokomeza Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI na uzinduzi huo unafanyika *Jamhuri Stadium,* Mgeni rasmi akiwa ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, kesho saa nne asubuhi.

Mheshimiwa Waziri wa Afya anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wajitahidi kuhudhuria, kutakuwa maonesho pale na hotuba muhimu kuhusu masuala haya. Pamoja na hilo, leo saa 7.00 mchana, kwa madhumuni ya huo uzinduzi, Waheshimiwa Wabunge wanaombwa wapite pale mapokezi, jengo la Utawala kuchukua sare, *T-Shirt* pamoja na kofia, ambazo itakuwa vizuri kuzivaa kesho kwenye uzinduzi huo wa kilele cha kampeni ya kuongeza kasi ya kupambana na magonjwa hayo niliyoyataja.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, leo saa 7.00 ni kuchukua sare, kesho saa 8.00, ni kushiriki. Ile Semina iliyopangwa ya mchakato wa amani katika eneo la Maziwa Makuu *(Great Lakes Region)*, imehairishwa ambayo ilikuwa iwe kesho.

Lakini mkumbuke kwamba Semina kuhusu uwezeshaji wa wananchi wenye kipato kidogo, suala ambalo liko karibu kwa kila Mheshimiwa Mbunge, Semina hiyo ni saa 5.00 siku ya Jumapili tarehe 6 Agosti, 2006, itaendeshwa Taasisi isiyo ya kiserikali, inaitwa *PRIDE*. Mnaombwa kuweza kuhudhuria Semina hiyo, saa 5.00 asubuhi Jumapili, katika Ukumbi wa Bunge wa Zamani.

Mheshimiwa Mohamed Rajab, Mwalimu Msaidizi wa Bunge *Sports Club,* anapenda niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa, timu ya *Bunge Football Club* na *Bunge Netball Club* wafike Bungeni kesho saa 4.00 asubuhi, tayari kwa safari ya Kongwa ambako kuna mechi kali huko. Zote mbili *Football,* yaani soka na *Netball* saa 4.00 asubuhi tayari kwa safari ya kwenda Kongwa. Vifaa vyote vinapatikana jengo la Utawala kwa maandalizi.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwanri, Mbunge wa Siha, ameniomba nitangaze kwa wale wapenzi wa muziki wa injili, kesho Bi. Beatrice Muhone, kutoka nadhani Arusha, atafanya uzinduzi wa *albam* yake ijulikanayo kama “Ingoje Ahadi”, saa

12.00 jioni, Dodoma *Hotel*. Uzinduzi wa *albam* Ingoje Ahadi. Spika amealikwa kama Mgeni Rasmi na amekubali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo jioni saa 11.00, tutaanza na mzungumzaji Mheshimiwa Mwanne, Mchemba Viti Maalum, halafu atazungumza pia Mheshimiwa Jackson Makwetta, saa 11.15. Baada ya hapo, sasa nitamwita Naibu Waziri wa Kwanza, saa 11.30 na Naibu Waziri wa pili saa 11.45. Kwa hiyo, Mtoa hoja ataongea kujibu hoja saa 12.00 hadi saa moja. Kutokana na mjadala ulivyo, Spika, amekwishahisi hakuna matatizo sana kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, tutaingia Kamati ya Matumizi saa 1.00. Natumaini saa 1.45 tutakuwa tumemaliza.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa kuwa muda wa kusitisha shughuli za Bunge umefika, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuwa mchangiaji wa kwanza kwa jioni hii katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri aliyoionyesha kwa kuweka kitengo hiki au kufungua Wizara hii pekee ili iweze kukidhi haja na mahitaji ya vijana.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuiwezesha hotuba hii ikafika siku hii ya leo na ikawa ya uhakika na mahiri. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii ili bila kusahau, kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia hotuba hii, pamoja na uzuri wake, kwa kweli kuna sehemu ambazo zinahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wachangiaji, tangu asubuhi, wamegusia sana suala zima la mikopo. Suala la mikopo tungeliangalia kwa kuzipa kipaumbele huduma zote zinazotolewa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Vijijini kwa huu mkopo ungeweza kusaidia kama wakulima wadogo wadogo wangewza kuwezeshwa kwa kupata pembejeo za kisasa. Ni kweli Serikali imeweza kutoa Mfuko huo wa Shilingi milioni 500. Lakini ukiziangalia hizo

Shilingi milioni 500 kwa mgao wa Mikoa na Wilaya zake, kwa kweli bado zitaleta mkanganyiko mkubwa katika jamii.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali pamoja na kufanya vizuri, ingesaidia kutoa maelekezo mazuri sana ili kusiwe na malumbano kwa sababu mikopo mingi inapelekwa Mijini na mikopo mingi Mijini wengine wameweza kuirudisha na wengine wameshindwa kuirudisha. Lakini ili tuweze kujenga mazingira mazuri na mfano mzuri kwa hawa vijana ambao wako Mijini waweze kurejea Vijijini, ni vyema mikopo hii ikaelekezwa kupelekwa Vijijini, ingesaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikopo hii kama itakuwa na masharti, kama itakuwa na riba kubwa, bado watakaokopa ni wale wenye uwezo tu na wale ambao wenye uelewa. Lakini kwa mtu wa Kijijini akiishaambiwa kuna riba angalau asilimia mbili, ataogopa. Ni vyema hawa watu wakalegezewa masharti kwa kujidhamini na uongozi uliopo kwenye eneo husika. Kwa mfano, Wenyeviti wa Vijiji wanajua hawa vijana wanaishije, wanajua hali zao zikoje na wanajua vijana ambao ni waaminifu. Lakini kama itaelekezwa huko, hawa Viongozi wa Wilaya na Vijiji wakaungana, hatimaye vijana kwa kweli watanufaika sana na huo mkopo kwa sababu, kama tungeweza kuwarithisha vijana ardhi sehemu ambazo wanalima, wakajiajiri wenyewe, kweli wataweza kujidhamini kwa eneo ambalo watakuwa wamekabidhiwa na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niingie sasa katika suala zima la ajira. Tuna tatizo kubwa sana la ajira, hasa baada ya Serikali kujiondoa kwenye masuala mazima ya uzalishaji wa viwanda. Kwa hiyo, tunao Wawekezaji. Wawekezaji wanapokuja hapa nchini, wanakuwa na taratibu zao. Taratibu zao wanapokuja hapa, wanaajiri watu wenye sifa kutoka kwao. Lakini kazi zile ambazo ni za kawaida, wanaajiriwa Watanzania. Lakini hao Watanzania maslahi yao ni duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana, utakapoona kwamba vijana wanalipwa Sh. 30,000/= kwa mwezi. Wanalipwa Sh. 30,000/= kwa mwezi, hawana *facilities* nyingine zozote zinazoweza kuwawezesha ku-*cover* mahitaji yao. Kwa mfano, huyo mwajiriwa anakwenda kazini na daladala au usafiri wowote hata wa miguu, chakula hakuna kwenye maeneo ya kazi. Lakini ukipiga hesabu, inaonekana kwamba huyu mfanyakazi analipwa Sh. 1000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii iangalie kwa makini utaratibu wa kuangalia sheria zetu ili ziweze kuendana na kizazi cha sasa au na ajira za sasa za utandawazi.

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo naliona, sheria ya ajira bado ni tatizo. Wanapokuja wawekezaji, wanapewa sheria ile ile ambayo ilikuwa inatumika wakati wa Chama kimoja. Chama kimoja kilifanya kazi nzuri sana na kilikuwa kinajua mahitaji ya Mtanzania yakoje na ili aweze kuishi, anahitaji nini na ilitosheleza kwa wakati ule.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa hivi, mimi naomba Wizara hii ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kama kweli tunataka kuajiri vijana na kubadilisha maendeleo yao ya vijana, kuondokana na tabia za kuporomoka kwa maadili, ni vyema Serikali ikasimamia kwa ukamilifu suala zima la mishahara na huduma nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la ajira kwa vijana ambao wanafukuzwa hovyo. Migogoro kazini inatokana na ajira ambazo hazina mwelekeo. Ndio zinazosababisha Serikali inawaachia Vyama vya Wafanyakazi, lakini yenyewe haipitishi mkono wake pale. Ingepitisha mkono wake, hata hawa wawekezaji wangeogopa. Wangeogopa sana na wangeheshimu Sheria ya Kazi ambayo inaendeshwa Tanzania.

Kwa mfano, Serikali upande wa utumishi, haina wasiwasi. Yenyewe imeshaweka kima cha chini cha mshahara. Kwa nini Wizara hii isitoe sera au isitoe mwongozo kwa mashirika haya yote ambayo ni ya wawekezaji na watu binafsi kutumia sheria hii ya ajira ya Serikali kwa kuwapa kima cha chini cha mshahara? Ingetengwa kabisa, kwamba, hawa watu wanapoingia, wanapewa kima cha chini cha mshahara ili watu waweze kufaidika na matunda ya ajira kwa miaka mitano ambayo tumeiweka kwenye Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie Mifuko ya Pensheni. Niwapongeze *NSSF* kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu umeingia mpaka viwandani. Unadai asilimia ya mwajiri kumwekea mfanyakazi. Hawa watu lazima wapongezwe sana. Kama sheria hii wakipewa kusimamia mishahara, nadhani wangetekeleza, sina wasiwasi nao.

Mheshimiwa Spika, lakini, kuna Mfuko wa *PPF*. Mfuko huu kwa wafanyakazi ambao wamestaafu na wakachukua fedha kwa mkupuo, mimi ninaomba Wizara hii iangalie pensheni hii kuirudisha angalau kwa wale waliostaafu waliokuwa wanafanya kazi kwenye Mashirika ya Umma.

Serikali imefanya vizuri, imewarudishia wafanyakazi waliokuwa Serikalini angalau waliochukua kwa mkupuo, sasa hivi wanajikuna. Lakini wale watu wengine ambao walikuwa wanafanya kazi kwenye mashirika ya Umma, bado ni tatizo. Naomba Wizara hii pia nayo iangalie jinsi gani ya kusaidia kwenye mifuko hii ili angalau na wao pia waweze kufaidika kwa taratibu ambazo zimewekwa na Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kifuta jasho au nizungumzie suala la Wakala wa Usalama wa Afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kifuta jasho kilichopo pale ambapo mfanyakazi anakuwa ameumia kazini, hakitoshi. Hakitoshi. Analipwa Sh. 85,000/=, akifa analipwa Sh. 85,000/= wale Warithi wanahangaika kuifuatilia Sh. 85,000/=. Ninaomba Mheshimiwa Waziri asaidie hilo tatizo ambalo sheria yake ni ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nizungumzie suala zima la matengenezo ya Ofisi za Idara ya Kazi Mikoani. Mimi naomba, badala ya kutenga kwamba Mikoa fulani watapewa, mimi nafikiri Serikali au Wizara izunguke iangalie hali halisi ya Ofisi za Idara ya Kazi zilivyo mbaya. Hawana vitendea kazi, hawana Ofisi za kuaminika. Mimi naomba Serikali iwakopeshe hata pikipiki kama magari haiwezekani ili waweze kuzunguka na kuangalia maeneo ya kazi yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Mahakama ya Kazi. Naomba Mahakama ya Kazi itoe maelekezo kwenye Mashirika ya Umma au kwenye Idara mbalimbali ili waweze kuwafahamisha wananchi au wafanyakzai ambao wanahitaji kujua sheria za kazi pale wanapopata matatizo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kazi iko Dar es Salaam na kama itakuwepo maeneo mengine, lakini wafanyakazi wengi hawajui haki zao ni nini. Inabidi anapokuwa na tatizo la kazi, lazima amuweke wakili. Sasa kama atajua sheria ambayo inamlinda kazini, ni vizuri, atakuwa ameelewa jinsi gani ya kuanza na kumaliza matatizo yake kwa kutumia Mahakama ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia ucheleweshaji wa maamuzi ya Mahakama ya Kazi. Ucheleweshaji wa kesi zao kwa wafanyakazi na mwajiri huwa kwa kweli zinakatisha tamaa. Mwajiri anakuwa na uwezo wa kufuatilia kesi hiyo, lakini kibaya mfanyakazi hana uwezo wa kufuatilia hiyo kesi. Kwa hiyo, matokeo yake mfanyakazi anakata tamaa, mwajiri anapewa ushindi au anadharau. Lakini, haki ya mfanyakazi inapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sheria zetu tuziangalie kwa msisitizo mkubwa ili haki itendeke kwa wafanyakazi wote na waweze kuridhika na hili suala la ajira kwa Watanzania na hali nzuri ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Bila hivyo, vijana wetu tutawaacha nyuma na bado hawataona kama Serikali yao imewafanyia mema kama sheria zote zinazomlinda mfanyakazi hazitakuwa wazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba pamoja na hayo, nisisitize pia kwamba sheria hii inaonekana inawahusu vijana wa kiume tu. Lakini pia naomba sheria hii pia wajue wanawake nao wamo ni vijana. Kwa hiyo, wanapoanza kulishughulikia hili suala na kukamilisha, wajue kwamba ajira hii iwahusishe asilimia kubwa wanawake ambao wanafanya kazi kubwa sana kupitia vijana hao hao. Sasa hivi tunao mfano mzuri vijana wetu wako humu ndani na wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nafasi hii, nisipoteze muda kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia, lakini pia kwa kufuatilia hoja ambazo ni kama ushauri tuliokuwa tumeutoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sina mengi. Naunga mkono hoja hii tena na tena na tena. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mchangiaji wa mwisho, ninapenda kuwatangazia wageni walioko *Speaker's Gallery*. Walioko hapo ni Wajumbe 14 wa Kamati Kuu ya Chama cha *UDP*, wakiongozwa na Dr. Fortunatus Masha, Makamu Mwenyekiti. Naomba upunge mkono! Kwa wale wasiomfahamu, Dr. Fortunatus ndiye Baba yake na Naibu Waziri wa Nishati na Madini na kwangu mimi ni kaka yangu, *Tabora School* tulikaa naye vizuri sana. *(Makofi)*

Lakini naomba nimtaje Mahsusi Mzee Lameck Bogohe, Mpigania Uhuru maarufu na Muasisi wa Chama cha *TANU* kwenye Kanda ya Ziwa, Magharibi. Pia, mtamwona yupo Mheshimiwa Isaac Cheyo, aliyekuwa Mbunge wa Bariadi Magharibi katika Bunge lililopita, lakini ambaye baada ya mchuano mkali, basi Mheshimiwa Andrew Chenge akafanya vitu vyake. Ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba pia nimtambulishe Mke wa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, Mkewe Miriam yuko pale pamoja na vijana wao wawili. Kijana anaitwa Kisali namwingine Rengalee. Ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Natumaini muda wangu utaongezwa kutokana na *interruption* hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa, tunahesabu unapoanza kuzungumza. Matangazo ya Spika hayahusiani na mchango wako. *(Kicheko)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwisho kwa jioni hii. Nimesimama hapa kuunga mkono hoja ya Wizara ya kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na kumpongeza ndugu na rafiki yangu Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ambayo imetilia maanani maeneo muhimu ya Wizara hii ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, hasa tukiangalia ukurasa wa 16 mpaka 20 ambapo anazungumzia mikakati ya kuendeleza vijana na ule ukurasa wa 35 mpaka 39 wa kitabu hiki cha horuba, kwa kweli hotuba ni nzuri kwa sababu inahangaika kutatua matatizo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu kuhusu Wizara hii ni yale yaliyosemwa na Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya na Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela wakati wakichangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile nimetoa Makala ya Kitabu ambacho nimeandika, "Hatima ya Vijana Tanzania," ambacho nimempatia Mheshimiwa Waziri ambamo napendekeza vile vile mambo ya kufanya kuhusu vijana hasa ukurasa ule wa 14 na wa 16 wa kitabu ambacho nimempatia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, katika hili, ningependa nianze kwa kunukuu maneno ya Mkurugenzi Mkuu wa *ILO*. Kwa idhini yako, naomba ninukuu: "Tunapoteza sehemu muhimu ya nguvukazi na vipaji katika kizazi hiki cha vijana ambacho dunia haijawahi kuwa nacho." *End of quote*. Maana yake ni kwamba, nguvukazi, vipaji vya vijana walioko duniani na hata hapa Tanzania, hatuvitumii vizuri. Kwa hiyo, tunapoteza nguvu hii na vipaji hivi. Kwa Tanzania, karibu asilimia 60 ya watu milioni 35 ni vijana na sehemu kubwa ni vijana ambao aidha wako Shuleni au wanazurura tu hawana kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wengi wanauliza kwa kukata tamaa, Hali yetu ya baadae itakuwaje? Vijana wanauliza! Wanauliza maswali haya kwa sababu ya matatizo ambayo yanawakabili. Vijana, fahari yao ni nguvu yao ya mwili na akili zao. Vijana wako kila mahali, wako Mijini, Vijijini, viwandani, mashambani na maofisini.

Mheshimiwa Spika, vijana wakitumiwa vizuri, vijana ni baraka. Lakini wasipotumiwa vizuri, vijana ni balaa. Kwa wale waliotembelea Magereza ya Tanzania, robo tatu ya wafungwa walioko Magerezani ni vijana. Kwa sababu ya uwingi wao, sehemu kubwa ya majambazi, wezi, wavuta bangi, ni vijana. Vile vile kwa sababu ya umri wao, sehemu kubwa ya wagonjwa wa UKIMWI ni vijana. Wanateketezwa na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, lakini bila ya vijana, hakuna Taifa, kwa sababu hamuwezi mkazaliana, wanaozaliana ni vijana walio na nguvu. Kwa hiyo, vijana ni wa lazima ili muweze kudumu kama Taifa. Hofu yangu ni kwamba, kama hakutapatikana dawa ya UKIMWI kwa mfano,Taifa kama hili huenda likateketea kwa sababu robo tatu ya wanokufa na wanaougua UKIMWI wako katika Bara la Afrika *South of Sahara* pamoja na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vijana ndio hao ninaowazungumza, ni wezi, majambazi, watu wa vijiweni na tunawatazama kama vile ni balaa. Lakini, tunaweza tukaishi bila ya vijana? Haiwezekani! Kwa hiyo, njia siyo kushutumu, bali ni kutafuta majawabu ya matatizo yao na matatizo yao ni mengi na mengine tunaweza tukayatatua, lakini ni lazima tuwe wakweli.

Mheshimiwa Spika, *lip service to youth problems will not pay*, na wengi tunasema maneno tu, vijana wana matatizo na wakati mwingine tunajaribu kutatua matatizo ya vijana kwa *Peripheral Approach* wakati tatizo ni *Concrete*. Kwa mfano katika ukurasa 35 wa kitabu hiki ambacho rafiki yangu amekiandika, amependekeza wazo zuri la kuwa na *SACCOS* kwenye ngazi ya Kata au Tarafa.

Mheshimiwa Spika, wazo ni zuri sana, lakini sio lazima *SACCOS* ziitwe za vijana, maana ukienda na hii *approach*, baadaye tutakuwa na *SACCOS* za wanawake, *SACCOS* za Walemavu, *SACCOS* za Wazee na kadhalika. *Issue* hapa ni kutatua tatizo. Tujenge *SACCOS* katika ngazi hizo, lakini sio lazima ziwe na *label* hiyo. Ila tu- *mobilize* vijana wajiunge na hizo *SACCOS*. Nadhani *spirit* ni hiyo hiyo. Lakini nadhani tukiwa na *label* hizo, baadaye tutawakosa hata wa kuwekeza katika *SACCOS* kwa sababu kila kikundi kitakuwa na *SACCOS* yake kwenye ngazi ya Kata au Tarafa. Jambo la msingi ni ku-*deal* na *concrete problems*.

Mheshimiwa Spika, vijana wanakosa mitaji, vijana wanakosa ajira, vijana wanakosa elimu, vijana hawana mbele na nyuma na vijana wengine wamekata tamaa. Vijana ni wengi kama nilivyosema, ni wengi kuliko rika lolote lile katika nchi hizi za *third world* au nchi maskini kama nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Taifa lolote linalopuuzia matakwa na mahitaji muhimu ya vijana wake, Taifa hilo linajikana lenyewe, haliwezi kudumu. Hali kadhalika Taifa lolote linalopuuzia matakwa ya walio wengi (kwa Tazania ni vijana) Taifa hilo litashindwa kulinda hata matakwa ya wale wachache ambao inadhania ndio wanaochangia kwa kiwango kikubwa katika maendeleo yake. Kile kikundi kidogo mwisho hakitaweza kudumu kama Jeshi la wasio na kitu, litazidi kuongezeka na kuwa kubwa zaidi kuliko Jeshi la walionacho.

Mheshimiwa Spika, suala la vijana kwa maoni yangu, ni suala la kufa na kupona. Mheshimiwa Mama Anna K. Malecela, asubuhi alijaribu kupendekeza wazo moja zuri kuhusu vijana. Hawa watu wako wapi? Wako vijiweni, wamejaa Mijini, hawafanyi kazi ila kupiga soga tu toka asubuhi mpaka jioni, lakini wanataka kula. Akapendekeza kwamba kwa nini Serikali isitumie nguvu ili kuwafanya watu hawa wafanye kazi za uzalishaji mali?

Mheshimiwa Spika, kwa mazingira ya dunia tunayoishi sasa, kwa kweli, tumechelewa kwa sababu ile sheria ya nguvu kazi ilipigwa marufuku kwa sababu ya dhana ya uhuru wa binaadamu kufanya kazi. Hata kumwondoa mtu anayezurura Mjini Dar es Salaam, hatakiwi kufanya hivyo kwa sababu sheria zinakataza. Kwa hiyo, ile sheria ya nguvu kazi kwa Tanzania hatuwezi kuitumia kwa sababu inakwenda kinyume cha sheria za *ILO*. Lakini ukiangalia mazingira ya dunia, nchi kama Ujerumani, Urusi, Uingereza, nchi zote zilizoendelea, wakati walipokuwa katika mazingira kama yetu, walikuwa wanatumia *a bit of force*. Sizungumzii kiboko, nazungumzia sheria, kulazimisha watu kufanya kazi.

Sasa mkazo uko katika utawala bora, demokrasia, wakati watu wanatembea uchi, hawana elimu, ni wagonjwa na hawana chakula. *How can democracy flourish in a hungry stomach or in an empty head*? Haya ni baadhi ya matatizo ambayo ni magumu sana, kwamba mtu hana kitu, mradi anakwenda uchi kupiga kura au hana kitu tumboni, mgonjwa, haya ni baadhi ya mambo magumu sana kwa mazingira ambayo tunaishi hivi sasa. Wakubwa watakuja hapa na kusema, usitumie nguvu. Acha mtu awe huru kuchagua. Atachaguaje hana elimu kichwani? Hata uwezo wa kuchagua, unahitaji mtu kujua kusoma na kuandika. Lakini, watu wengine tusipowalazimisha kusoma, watabaki wajinga milele. Sasa ni hiari kwenda kusoma au ni lazima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengi tuliyoyapata kabla ya kufuta sheria hii, sehemu kubwa ilikuwa ni ya nguvu kwa maana ya kutumia sheria, kwa mfano, Kisomo cha Watu Wazima, kwa mfano baadhi ya shughuli inasemekana hata walipoleta zao kama la Kahawa kule Moshi, walitumia nguvu kidogo. Kilimo cha Tumbaku kule Songea, walitumia nguvu kidogo, inasemekana hata kilimo cha Korosho. Hebu chambua maajabu ya dunia kama Mapiramidi ya Misri, yamejengwa nadhani siyo kwa hiari. Tazama *The Hanging Garden of Babilons*, *The Great Wall of China*, haya yote yamefanywa na watu chini ya mazingira ya nguvu nguvu.

Mheshimiwa Spika, demokrasi haijawahi kutengeneza maajabu katika dunia hii. Kwa hiyo, kwa sisi tunaotaka maajabu kwa njia hii ya lele mama, kwa kweli kwa mazingira haya tutabaki pale pale.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujibu hoja kwamba tunaishi kwenye mazingira ambapo wakubwa sasa ndio wanao-*determine* au kutoa maelekezo na kutoa miongozo ya utawala bora na nini kifanyike na usipotii watakunyima hata misaada. Kwa hiyo, tuko kwenye tatizo.

Mheshimiwa Spika, hakuna demokrasia katika hali ya mazingira haya tuliyonayo. *Are we democratic* kwa sababu tunachagua au hatuchagui Viongozi wetu? Kwame Nkrumah aliwahi kusema kwamba:

*Democracy is the Freedom of a Free People to Manage or mis-manage their own Affairs."* So *we are free to mis-manage our own affairs* kwa sababu ya demokrasia. Lakini ningependa kusema kwamba katika mazingira fulani, aina fulani ya nguvu ni ya lazima. Lenin aliwahi kusema kwamba: *"Force is a midwifery of any Society preginant of a new one."*

Mheshimiwa Spika, kama mama anakuwa mjamzito na siku za kujifungua zimefika na hajifungui, kwa mtu mwenye busara, atampeleka huyu mama hospitali na Dokta mwenye busara, atatumia kisu kumpasua mama huyu ili kumwokoa yeye, pamoja na mtoto aliye ndani ya tumbo lake, vinginevyo atakufa yeye na mtoto. *This is the type of force I am talking about, noble force. Force* ambayo ni ya ukombozi. Kutumia kisu katika mazingira ya kawaida au bunduki ni makosa, lakini kwenye vita si makosa.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeshiriki kwenye vita ya ukombozi tukiwa na Museveni, *the late* Shija, tulitumia bunduki, lakini kutumia bunduki katika mazingira gani, nguvu katika mazingira gani. Sisi hapa *we are oppressed* na *poverty*. Ili *democracy* istawi vizuri ni lazima kuwe na mazingira fulani yanayofanya istawi. Hata hii *manipulation* ya kurushwarushwa ni kwa sababu ya *poverty, we are poor.* Unaweza kuwa *manipulated* na shilingi mia mia tu, unatupiwa chini kama kuku unaokota. Nashindwa kuelewa hii dhana ya wakubwa, lakini nasema wakazanie kutu-*liberate* kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Azimio la Arusha ambalo tulilitunga mwaka 1967, tulisema kwamba: "Sehemu kubwa ya akina baba waishio vijijini na nusu ya akina mama waishio mijini, wako *leave* nusu ya maisha yao." Kama tungeandika leo, nadhani tungeongeza vijana kwa vile nusu ya maisha yao wako *leave*. Hakuna mtaji, hakuna kazi, kwa hiyo, wanatumia nguvu zao katika mambo ambayo siyo ya kujenga. Sasa katika hili, siyo lazima tukubaliane na ninyi wenzangu, tunaruhusiwa kutofautiana, lakini tukubaliane kwamba, hizi nchi za Ulaya, sehemu kubwa ya hayo maajabu tunayoangalia ni matokeo ya matumizi ya nguvu kidogo. Nguvu ninayotumia mimi hapa ni sheria, kwa mfano, kulazimisha watu kwenda kusoma, kulazimisha watu waelewe uhuru wao, ndiyo aina hiyo ya nguvu, siyo nguvu ya risasi wala nguvu ya namna nyingine. Nguvu inayofanana na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nimalizie kwa kusema kwamba, tafuteni kwanza maendeleo ya vijana na mengine yote yatafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kitabu hiki ambacho nimeandika, nimeandika mengi na ninadhani kwamba, dhana ya vijana itatatuliwa tu kama kila Wilaya, kila Mkoa, kwa mazingira yao, watajaribu kufuata mwongozo kama alivyopendekeza Mheshimiwa Waziri, kusudi kufanya vijana hawa wajenge maadili ya kazi. Hata kufanya kazi nayo ni kazi, ni lazima tujenge maadili, maana mtu anazaliwa Dar es Salaam, hajui kulima wala kufanya kazi yoyote, kwa hiyo, huyu unaposema aende akalime Njombe, anashangaa!

Anataabika, hawezi kushika jembe, anaona tabu kuona udongo unashika miguu yake. Kwa hiyo, nasema tuna kazi kubwa na kufanya kazi hii siyo lelemama. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MOHAMED ALI SAIDI:** Mheshimiwa Spika, tunajua kuwa vijana ndio nguvukazi ya Taifa, lakini vijana wetu wengi sasa hivi hawana kazi na hii ndiyo maana vijana wetu wengi wamejiingiza katika vitendo viovu. Kwa hiyo, napendekeza kuwa, vijana wote wasiokuwa na kazi nchini, waorodheshwe na wagawanywe kwenye vikundi mbalimbali baadaye waelekezwe nini wafanye na wawezeshwe kwa kupewa mikopo na hatimaye watafutiwe masoko ya uhakika kwa mauzo ya watakacho kizalisha.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nielezee kuhusu ajira binafsi. Kwa kweli ajira hizi zinawadhalilisha vijana wetu kwanza, kwa kuwafanyisha kazi kubwa na kuwapa malipo madogo sana na kuwanyanyasa hasa hawa vijana wa kike wanaofanya kazi majumbani.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwa, Serikali itunge sheria itakayowatetea vijana wanaoajiriwa na watu binafsi, itakayoondosha unyanyasji na maslahi duni kwa wafanyakazi hawa.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima. Aidha, nawashukuru wanawake wote wa Mkoa wa Manyara, kwa imani yao kwangu hata kuniwezesha kuingia katika Bunge hili Tukufu na niweze kuwasilisha mawazo yao pamoja na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nikipongeze Chama changu cha Mapinduzi katika mchakato wa kumpata Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, pamoja na safu nzima ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, inataka kuwe na ongezeko la ajira milioni moja ifikapo mwaka 2010. Naomba nitumie fursa hii, kukipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa kuona umuhimu wa kuongeza ajira kiasi hicho.

Naomba Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, iandae mkakati madhubuti kwa ajili ya Ilani hii. Katika kukabiliana na tatizo la ajira, Serikali haina budi kuanza kutekeleza mipango mbalimbali ya kiuchumi, ambayo inaendana na kupanua wigo wa ajira.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la mwezi Februari, 2006, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria ya Kuweka Utaratibu Utakaosimamia Uanzishaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji Rasilimali *(Special Economic Zone).* Kwa kuwa moja ya faida ya kuanzishwa kwa maeneo haya maalum mathalani *Mererani Special Economic Zone,* ni kupanua ajira na kuongeza wastani wa kipato cha Mtanzania, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ihakikishe kuwa inatoa kipaumbele na kuwezesha ajira nyingi zishikwe na Watanzania. Nashauri kwamba, sheria zetu za kazi zifanyiwe marekebisho ili ziendane na wakati huu wa utandawazi hususan tunapoingia katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. La sivyo, tutajikuta nafasi zote nzuri za kazi zimechukuliwa na wenzetu.

Mheshimiwa Spika, eneo linalonikera ni kwamba, wakati Serikali yetu inahangaika kubuni mbinu na mikakati ya kuongeza ajira kwa vijana wetu, inasikitisha kuona baadhi ya kazi ambazo zingeweza kufanywa na Watanzania, sasa zinafanywa na wageni, mathalani biashara ndogo ndogo zinazofanywa na wageni katika maeneo ya Kariakoo Dar es Salaam. Naomba nipatiwe maelezo ya kina, ni nani anayehusika katika kutoa vibali *(working permit),* vya kufanya kazi hapa nchini? Nafikiri utaratibu unaotumika sio sahihi hata kidogo, kwa sababu hakuna Mtanzania anayeweza kwenda nchi nyingine na kuweza kufungua *saloon* au biashara nyingine mfano kuuza maua. Kama ni utandawazi, kwa nini wasilete bidhaa zao wauze kwa bei ya jumla ili kusiwe na haja ya kwenda nje kununua bidhaa hizo? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, Shamba la Ngano la Mbarali Mkoani Manyara lina ukubwa wa ekari 13,000 za mraba. Shamba hili lina wafanyakazi takribani mia sita. Shamba hilo limeuzwa na sasa watu wamesimamishwa kazi. Je, baada ya wafanyakazi hao kusimamishwa kazi, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gain, ukizingatia bado hawajalipwa malimbikizo ya mishahara yao? Je, Serikali haioni kwamba, wafanyakazi mia sita kusimamishwa kazi, inapunguza zile ajira 1,000,000 zilizoahidiwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi? Naomba maelezo kuhusu wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kupeleka shilingi milioni mia tano kwa kila Mkoa. Pia kuhusu Mfuko wa Mikopo kwa Vijana wachache sana hususan wa mijini, unaonesha ndio utawanufaisha. Katika Mkoa wa Manyara Wilaya ya Simanjiro, sijui kama mikopo hiyo imewahi kufika sijui. Tatizo lingine la mikopo hiyo ni urejeshaji, nafikiri urejeshaji wa mikopo hiyo si mzuri. Napendekeza Serikali ichukue hatua za makusudi, kwa kuitumia Banki ya *NMB* itumike kutoa mikopo hiyo ili iweze kudhibiti urejeshaji wake.

Mheshimiwa Spika, ajira ya watoto miaka 13 – 18, kukomesha utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari. Nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha

Mapinduzi, kwa kutambua tatizo hili la utumikishwaji wa watoto na kuweza kutafuta mashirika mbalimbali Duniani kama *ILO*. Awamu ya kwanza ya mpango huu, ilifanikiwa sana kwani watoto wengi wameondolewa katika Wilaya 11 na kupatiwa elimu na mafunzo mbadala, kama stadi za kazi na mafunzo haya yanachukua miezi mitatu tu. Naomba waongezewe muda angalau miezi mine au mitano, ndipo wapatiwe vyeti. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, ikiwa mpango huu wa awamu ya pili utatekelezwa vizuri, tuna uhakika wa vijana wengi kuachana na utumikishwaji na kuweza kujiajiri wenyewe. Lakini la msingi sana, naomba Wizara yako iangalie pale watoto hawa wanapomaliza mafunzo ya ufundi, wapatiwe vifaa vya kujiendeleza au wapewe mitaji. Naomba pia wapatiwe semina mbalimbali, hasa semina ya biashara ili waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ni imani yangu Mwenyezi Mungu, ataniwezesha kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa walengwa wakuu wa Wizara hii ni vijana, ambao Serikali ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete imewaangalia na kuona ipo haja iwaajiri vijana wasiopungua milioni moja, kwani ndio waathirika wakuu kiajira. Naishukuru Serikali kwa kuliona hili na naitakia kufanikisha azma yake kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu waajiri binafsi, Serikali ipo, lakini haijui ni kiasi gani wanawaajiri vijana wa Kitanzania. La kusitikitisha sana, ni jinsi waajiri binafsi wanavyowatesa vijana wetu. Kijana kwa shida aliyonayo ya kimaisha, amepata ajira kwa mtu binafsi, hupata ajira isiyo na mkataba, hivyo mwajiri huitumia nafasi hii kumfanyisha kazi kijana huyo kiutumwa, hasa wale wanaofanya kazi majumbani. Mfanyakazi huyu ni mtumwa kabisa, kwani hufanya kazi bila mapumziko na hatimaye hukemewa kwa maneno machafu. Ukiangalia hili zaidi utaona malipo yake, mshahara mkubwa ni Sh.10,000/= kwa mwezi, Serikali ipo, lakini imekaa kimya.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina vijana mahiri, wamesoma na ni waaminifu, inakuwaje haya mahoteli ya kitalii yawe na wafanyakazi wa kigeni? Hii ni haki yetu, lakini Serikali imeshindwa kuwaambia wawekezaji kutoka nje wawe na mikataba ya wafanyakazi. Ni vyema vijana wetu wawe ndio waajiriwa katika maeneo kama hayo. Kijana anapoandaliwa anaweza kujiajiri binafsi kwa kazi ya kilimo, mifugo na kadhalika, lakini Serikali imekaa kimya. Sasa wakati umefika wa Serikali kuwawezesha vijana wetu ili waweze kujiajiri binafsi.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia kuwa na afya njema na kuweza kuchangia Wizara hii. Nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote

wawili, kwa kuweza kutuongoza katika Bunge hili kwa ufanisi na umahiri mkubwa na kuweza kutuunganisha sote na kuwa ndugu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii, pamoja na wale wote waliotoa ushirikiano kwa kuchambua hotuba hii. Nampongeza Mwenyekiti wa Kamati hii na Wajumbe wote waliomo ndani ya Kamati, kwa ushirikiano wao kwa kutoa mchango ndani Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichangie Wizara hii ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwanza, naipongeza Wizara kwa kuanzisha Kituo cha Ajira, Jijini Dar es Salaam na kufanya kazi yao nzuri kwa kuwatafuta waajiri kwa kutoa ushauri juu ya kituo cha ajira. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alitoa ahadi ya kuwaajiri vijana milioni moja katika kipindi cha miaka mitano. Hivi sasa ni miezi minane, je; Wizara hii imewaajiri vijana wangapi?

Mheshimiwa Spika, tunasikitika kuwa vijana wengi wanapofika kwenye Wizara, hufanyiwa usaili, halafu baadaye ni wachache tu wanaoajiriwa hata kama wana uwezo kielimu. Kwa hiyo, wanaohusika waache kuwaajiri vijana wasiokuwa na uwezo kwa ajili ya uhusiano au rushwa. Hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa watoto, Wizara hii ifanye kila hali kusimamia tatizo hilo ili watoto wetu wasipoteze masomo na kuajiriwa kazi nzito kama kwenye mashamba ya chai, migodini au biashara ya ukahaba na kazi nyingine nyingi wanazofanyishwa. Kwa hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Wizara hii, ituambie ina utaratibu gani kukomesha kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Usalama wa Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* Serikali inaajiri watu wengi na wanafanya kazi mahali ambapo pengine hakuna usalama, kwa mfano, wale wanaofanya kazi migodini na wale wanaofanya kazi Manispaa, wote wanafanya kazi katika mazingira magumu. Kwanza, wanahitaji kuchunguzwa afya zao mara kwa mara angalau kila baada ya miezi miwili, kwani wanasafisha makaro na mahali pote penye uchafu. Inatakiwa kila baada ya mwezi mmoja, wapewe vifaa vya kutendea kazi ili waweze kuwa na afya bora. Pia, wale wanaofanya kazi kwenye mashirika yasiyokuwa ya Serikali, wapewe elimu juu ya waajiri wao na Serikali iwaangalie wafanyakazi wanapopata ajali wapewe mafao ili wapate msaada kwenye maisha yao na wamiliki pia waelimishwe hayo.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama tujuavyo, vijana ndio nguvukazi ya Taifa letu. Vijana hawa tunahitaji tuwapatie shughuli zitakazowafanya wajipatie vipato vyao halali. Vijana wanasoma, wanamaliza shule na kubaki kuzurura kwa ukosefu wa ajira. Ajira sio lazima za kuajiriwa ofisini, hata kujiajiri binafsi pia ni ajira.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara iwapatie vijana mafunzo ya ujasiriamali ili waweze kujitegemea wenyewe katika kujiajiri. Tatizo la kukosekana kwa ajira kwa vijana ndio chanzo cha wimbi la ujambazi, ubakaji, ulaji unga na kadhalika. Kijana anapokosa shughuli ya kufanya, ndipo anapojiingiza katika tabia mbaya.

Mheshimiwa Spika, pia tatizo lingine linalowapata vijana ni pale wanapohangaika kutafuta kazi. Wanapotafuta kazi, wakati mwingine huwajibika kutoa rushwa. Rushwa hii iko ya aina nyingi, aidha inaweza kuwa rushwa ya fedha, lakini sana sana rushwa ya ngono. Vijana ndio waathirika wakuu wa janga hili la UKIMWI kutokana na rushwa hii ya ngono. Ninaiomba Serikali iweke mikakati mahsusi ya kukomesha utoaji rushwa katika nchi yetu kupitia ajira. Uandaliwe mkakati kabambe wa utoaji ajira kwa vijana bila kutumika rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuna vijana ambao wanajiajiri wenyewe, mfano vijana wanajijengea vibanda vyao, aidha vya kuuzia maziwa, juisi, kadi za simu au chipsi. Cha kushangaza, baadhi ya Halmashauri kwa makusudi, huamua kuwabomolea vibanda vyao hivyo na bila ya kuwaandalia sehemu nyingine watakazokwenda kufanyia kazi. Hii inasababisha ukataji tamaa kwa vijana na kuwasababishia vitendo viovu. Naiomba Serikali ihakikishe inapoamua kuwahamisha vijana sehemu fulani, basi ni bora watafutiwe sehemu ambayo wataweza kuendeleza biashara zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naiomba Serikali ielekeze zaidi mikopo kwa vikundi vya vijana baada ya kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali. Tukumbuke vijana ni nguvukazi ya Taifa, kuwaacha wakizurura ni sawa na kuliandaa taifa liwe na omba omba waliokithiri kila sehemu. Vijana kuanzia vijijini wapatiwe elimu ya ujasiriamali, waondokane na dhana potofu ya kukimbilia mijini kwa dhana kuwa ndiko kuliko na kazi, kumbe kazi ni popote pale.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nchi nyingi zinazoendelea zimeruhusu wageni wawekeze katika nchi zao kwa kuingia ubia na wazawa, lengo likiwa ni kudhibiti ajira kwa wageni, kupata uzoefu wa kazi ili mwekezaji anapoondoka utaalam wake uendelezwe na mzawa. Kwa kweli nchi yetu haina sheria hii, wawekezaji wanawaajiri wageni watakavyo wao na kuwalipa mishahara watakavyo wao. Naiomba Serikali, iangalie upya suala la wawekezaji wageni kuingia ubia na wazawa ili kulinda ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie kwa karibu suala la ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi na hasa katika Sekta Binafsi. Wafanyakazi wengi wananyanyaswa katika Sekta Binafsi na maeneo mengine, hawaruhusiwi kuunda Vyama vya Wafanyakazi. Migomo katika Sekta Binafsi, zisizo na ushirikishaji wa wafanyakazi haiishi. Ili kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi mahali pa kazi, naiomba Wizara kushauriana na Sekta zote za binafsi, TAMISEMI na Serikali Kuu, kudumisha ushirikishwaji wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itoe viwanja kila Mkoa kwa Shirika la *NSSF* ili Shirika hili liendeleze ujenzi wa nyumba za bei nafuu kila Mkoa na kukopesha kwa wanachama wake, kama ilivyo kwa nyumba za Kinyerezi.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza Shirila la *NSSF* kwa kutoa huduma nzuri kwa wateja wake na kushiriki katika kuleta maendeleo kwa Watanzania kwa kujenga majumba za kifahari katika Jiji la Dar es Salaam na pia uamuzi wa kujenga daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali na Chuo Kikuu kikubwa kinategemewa kujengwa Dodoma, naliomba Shirika hili lione umuhimu wa kujenga sehemu za biashara ndogo ndogo katika Mkoa wa Dodoma. Ujenzi huo utawasaidia wanawake na vijana, kupata maeneo ya kuendeleza biashara zao kwa kuzingatia kuwa, chuo hicho kitakuwa na wafanyakazi wengi na wanafunzi elfu arobaini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuwajengea uwezo vijana kwa kuwapa mikopo ya riba nafuu. Mikopo hiyo itakuwa ya manufaa iwapo itawanufaisha walengwa. Walengwa (vijana) watanufaika iwapo mikopo hiyo itatolewa baada ya wao kupata mafunzo ya kuridhisha/kutosha. Nashauri kwamba, mabenki yatakayotoa mikopo yaandae *program* maalum za kuwafundisha vijana kabla ya kuwakopesha.

Mheshimiwa Spika, Serikali ieleze ni utaratibu gani uliowekwa ili vijana wengi waweze kunufaika na mikopo hiyo, kwani mabenki yetu hayatoi mikopo bila mkopaji kuwa na dhamana.

Mheshimiwa Spika, taarifa/takwimu za kujua idadi ya vijana, mahali walipo na wanafanya nini, iendelee kwa kasi kubwa ili kubaini uwezo wao wa kufanya biashara/kujiajiri. Naishauri Wizara hii kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili kazi hii ikamilike kwa muda muafaka na ili vijana washirikishwe katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, maoni/mapendekezo ni kwamba:-

- Wizara iangalie na kusimamia maeneo yaliyosahaulika hasa ajira na maslahi kwa wahudumu katika baa *(barmaids),* kwani mishahara yao ni kati ya Sh.15,000/= na Sh.25,000/= kwa mwezi, hutumika kufanya kazi kwa saa 16 hadi 20 kwa siku. Hii husababisha wasichana wengi kuingia katika tabia ya ukahaba kwa sababu ya ujira mdogo.

- Wizara ikutane na Chama cha Wahudumu wa Baa na Mahoteli, kutafuta ufumbuzi wa kutatua tatizo hili ambalo ni unyanyasaji wa wanawake kijinsia.

- Wizara ifuatilie kero za wafanyakazi katika viwanda vinavyomilikiwa na wageni, pia vinavyomilikiwa na wazawa.

- Kuwepo na *program* katika kila Taasisi binafsi kuelimisha wafanyakazi wao kuhusu janga la UKIMWI.

- Wizara ijielekeze katika kuelimisha vijana hasa kuhusu ujasiriamali na mafunzo mengine yatakayosaidia vijana kujiajiri.

- Wizara ishirikiane na Wizara ya Usalama wa Raia kuwapiga marufuku vijana kukaa vijiweni bila kazi na badala yake kujihusisha na kuvuta bangi na madawa ya kulevya.

- Wizara itoe takwimu sahihi za vijana wote wasio na kazi maalum kwa kuhusisha kila Kata au Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchangia naomba nichukue nafasi hii kwanza, kumpongeza mtoa hoja, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, kwa hotuba yake makini inayolenga katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM kwa mwaka 2005 mpaka 2010.

Mheshimiwa Spika, nina mambo kama manne hivi ya kuchangia katika hoja hii. Kwanza, napenda nigusie kuhusu suala la uanzishwaji wa *Youth Development Centres* au Vituo vya Maendeleo ya Vijana. Kimsingi vijana wengi hawana dira ya wapi waende ama nini wafanye wanapomaliza masomo yao, kuanzia wale wanaomaliza darasa la saba mpaka hata Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, vituo hivi vikianzishwa vitakuwa na faida zifuatazo:-

(a) Vitatoa fursa ya tathmini ya vijana wangapi, wenye ujuzi gani au kama hawana kabisa na wasaidiwe vipi ili waweze kuandaliwa kuwa na sifa za ajira.

(b) Vituo hivi vitaweza kuandaa elimu au mafunzo ya ziada ambayo yataweza kusaidia kufanya wawe *more employable.*

(c) Vituo hivi vitatumia wataalam wa kisaikolojia, vitaweza kujenga ari ndani ya fikra za vijana na hatimaye mitazamo chanya kuhusu ajira.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni umuhimu wa kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Vijana *(Youth Development Bank)*. Benki hii itasaidia sana katika kuongeza ajira kwa vijana. Ikumbukwe kwamba, Serikali katika uchumi wa soko huria, sio tena mwajiri mkuu kama ilivyokuwa zamani Njia ya haraka ya kupata kwao ajira, inataka kujikita katika sekta binafsi *(private sector),* lakini nia itawezekana tu kama watakuwa na mitaji. Tatizo la mitaji kwa kupitia mabenki ya kawaida ni gumu. Vijana wengi hawana mali *(collaterals)* kama vile nyumba ambazo ni hitaji la muhimu katika kupata mkopo wa benki. Ikianzishwa benki itakayoelekeza msisitizo katika kuhakikisha wanakopesheka kwa kuwawekea riba za chini na masharti nafuu, sambamba na udhamini wa Serikali, vijana wengi watakomboka kwa kupata mitaji na hivyo kujipatia ajira.

Mheshimiwa Spika, lakini mikopo hii lazima iende sambamba na elimu maalumu ya udhibiti na matumizi ya fedha za mkopo. Bila ya elimu hii, itakuwa ni sawa na kutwanga maji kwenye kinu, hela hizi zinaweza zisiwanufaishe.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii. Naanza kwa kumpongeza Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa hotuba yake makini na nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inabeba majukumu muhimu sana katika ujenzi wa uchumi wetu, kwa sababu kazi ndio msingi wa maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huu, ni lazima Wizara ya Kazi ichukue hatua za makusudi za kuwa wahubiri wa dhana ya umuhimu na ulazima wa kufanya kazi, hasa kwa vijana vijijijni.

Mheshimiwa Spika, *publicity* za wazi na za ana kwa ana, katika vipindi vya *Television,* vyombo vya habari na michezo ya kuigiza, ziongezwe kwa bidii kubwa na iwe ya kudumu ili kuwa-*sensitize* watu wapende kazi na wachukie uvivu au kukaa bila kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mawazo haya, ni muhimu zaidi, Wizara ikawa na kitengo maalum cha wataalam cha kutembelea nchi nzima katika sehemu mbalimbali ili kufanya *job innovation* katika mazingira mbalimbali vijijini.

Kwa mfano, vijana wanaweza kushauriwa kuunda kikundi cha wapaliliaji na uvunaji wa mazao mashambani au kikundi cha wafukia mashimo katika barabara vijijini, ambao wanaweza kuwekewa utaratibu wa kutambuliwa na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu wananchi wanapokuwa katika maeneo yao kwa muda mrefu, inakuwa vigumu kwao kutambua *opportunities* za kazi za

kujiajiri, zinazoweza kuwepo na kufanywa. Ni rahisi zaidi kwa mtu wa nje kutambua *opportunities* hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalomshauri Waziri wa Kazi ni kutafuta namna ya kuwadhibiti Menejimenti za Kampuni binafsi katika masuala yafuatayo: Makampuni binafsi wanachelewa sana kutekeleza malipo ya mishahara kwa wafanyakazi ya *minimum wage,* punde Serikali inapotangaza tarehe ya kuanza kulipa mishahara hiyo. Ili kuwabana waajiri binafsi, napendekeza Serikali itunge Sheria inayotoa *deadline,* ambapo kila kampuni inapaswa kutimiza malipo ya *minimum wage* ili atakayechelewa awe amevunja sheria na aadhibiwe inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ufuatiliaji wa migogoro baina ya wafanyakazi na menejimenti ni ndogo mno, kiasi inawafanya wafanya kazi kukata tamaa na kuamua kuchukua hatua kupeleka malalamiko yao ngazi za juu sana Serikalini. Wiki iliyopita, nikiwa katika mkutano wa hadhara katika Kata ya Kidodi, Kijiji cha Ruaha jimboni mwangu, nilipokea malalamiko yafuatayo kutoka kwa wapiga kura shupavu, ambao ni wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero: Walikwishapeleka malalamiko mengi kimaandishi Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, dhidi ya unyanyasaji wa Menejimenti ya Kampuni ya Sukari Kilombero.

Pia wamepeleka barua kama hiyo Ofisi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini mpaka sasa hawajaona mwelekeo wa kuwa matatizo yao yanashughulikiwa, ikiwa ni pamoja na kulipwa mishahara kiubaguzi.

Wamedai kuwa kutokana na unyanyasaji uliopo na woga waliokumbwa nao, wameniomba nikuone na nikuombe umwombe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, awatembelee kikazi huko ili waeleze kwa uwazi na ukweli, madhara nyeti yanayofanywa na wawekezaji wa Ishoro na kuathiri mapato na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, achukue hatua za haraka kulifuatilia suala la malalamiko ya wafanyakazi wa Kilombero, kwa sababu eneo hilo la makazi lina historia ya *cycle* ya fujo na mvurugano baina ya wafanyakazi na menejimenti.

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Waziri atazingatia ushauri huu. Naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa katika mpango mzima wa Taifa wa kukuza ajira, naupongeza mpango wa kuanzisha vituo vya ajira lakini ni vyema mpango huo ungekuwa kwenye ngazi ya kila Mkoa na siyo vituo vitatu tu vya Mwanza, Arusha na Mbeya tu. Ni vema pia katika mfumo wa Serikali za Mitaa, ukawepo mpango wa ajenda ya ajira na uundaji wa vikundi kwenye ngazi ya Kata ambapo ipo Kamati ya Maendeleo

ya Kata chini ya Diwani wa Kata. Katika upatikanaji wa Mitaji, ngazi hii ya Kata ni muhimu.

Kuhusu utaratibu na kanuni za namna shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa zitakavyowafikia walengwa ni muhimu kuweka wazi jinsi fedha zitakavyotumika kama dhamana ya mikopo ya masharti nafuu. Nashauri kuwa, ingekuwa vyema kama vigezo vya masharti nafuu vitatangazwa sasa kwa sababu tayari Wizara imeamua kuwa mikopo itatolewa mapema katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa 2006/2007, muda ambao tayari theluthi moja umewadia.

Kuhusu kurasimisha mali na biashara (MKURABITA) ni lini sasa utaratibu huo utaanza kwa sababu jambo hili limesemwa sana kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2005 na hili litahusu sana eneo la masharti nafuu ya mikopo itakayotolewa?

Mhesihimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri kazi njema na Wasaidizi wake.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, napendekeza JKT ihamishiwe Wizara hii ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ili kama jina linavyosimama, iwe na kazi ya kujenga taifa kwa kuwawezesha vijana wengi zaidi wajiajiri baada ya *Vocational Training.*

Wizara ya Elimu na Ufundi Stadi watoe *(provide) inputs* kwa Wizara ya Kazi kama vile waalimu, wataalamu mbalimbali na washauri. Pia Wizara ya Ulinzi itoe *inputs* kufundisha nidhamu, ukakamavu na uzalendo katika makambi hayo ya vijana.

Mahakama za Kazi zipunguze urasimu, zinafanya kazi kama Mahakama za Sheria na hivyo kuvuta mlolongo wa urasimu usiokuwa na sababu na hivyo, kuashiria mazingira ya rushwa. Wafanyakazi wanasubiri muda mrefu hata miaka. Wizara ije na kuharakisha maamuzi ya Mahakama za Kazi ili wafanyakazi watendewe haki mapema na kuwadhibiti waajiri wakorofi na wasiofuata mikataba ya ajira.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kumteua Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, kuongoza Wizara hii akisaidiwa na Naibu wake, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko. Pia uteuzi wa Katibu Mkuu Dr. Ladislaus Komba na Naibu wake, Ndugu Edris Mavura, umeifanya Wizara ipate wataalam katika fani zote zinazohitajika ndani ya Wizara, ninayo imani kuwa kazi sasa zitasimamiwa vizuri zaidi. Naunga mkono hoja ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha utandawazi ni budi jitihada zikafanyika kutoa elimu kwa wafanyakazi na kuandaa semina ambazo zitakwenda na wakati wa sasa, ili kupunguza migogoro ambayo inaweza kudhoofisha mahusiano kati ya waajiri na waajirwa na kuzorotesha uchumi. Tume ya kusuluhisha na utatuzi wa migogoro ya kikazi, isiwe inasubiri migogoro ianze bali wajitahidi kuizuia ili isiwepo.

Matumizi ya Sheria ya Utatu nayo yapewe msukumo ili kudumisha mahusiano mema mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Taifa wa kukuza ajira nchini, lazima upewe umuhimu wa pekee, kwa sababu sekta rasmi haiwezi kubeba uzito wa majukumu haya. Sekta isiyo rasmi ndiyo mkombozi wetu. Matumizi mazuri ya Sh.500 milioni kwa kila mkoa iwe ni kichocheo cha kuanzia nia hiyo. Vijijini wanahitaji pembejeo na zana ndogo za kilimo wakati mijini wanahitaji biashara ndogo ndogo. Nashauri fedha hizo zitolewe mwongozo na ikiwezekana zikae kwenye taasisi zisizo za Kiserikali kama *SACCOS.* Vyombo vya fedha vihamasishwe ili navyo vitoe mikopo kwa riba nafuu.

Mipango ya kuwawezesha vijana ya kuingia kwa hiari katika shughuli za kilimo, iangaliwe. Mwaka 1998 wakati nikiwa Wizarani, nilijaribu kuona kama vijana wa Jiji la Dar es Salaam wanaweza kupenda kilimo. Nilishangazwa kwa jinsi vijana hawa walivyo tayari, zaidi ya vijana 10,000 walionekana kutaka kujiunga na kilimo katika Wilaya ya Kisarawe sehemu za Kidunda na Kitongoji cha Nyani. Taasisi za Kimataifa za *FAO* na *ILO*, walianza kuunga mpango huu ambao baadaye ukaungwa mkono na wataalam mbalimbali wa vyuo Vikuu vya *SUA* na Muhimbili. Ni vizuri kuendeleza juhudi hizi bila kuwapa ahadi za kuwapa fedha bali kwa kusaidia tu, huduma muhimu kwa mfano maji, afya na barabara.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii, liweke mkakati wa kuendeleza mipango ya kuwajengea nyumba za bei nafuu na kuwakopesha wanachama wake.

Shirika la Tija la Taifa *(NIP),* halijulikani sana nchini. Napendekeza litekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi, kwa kusambaa nchi nzima ili wananchi wengi watambue kuwa *NIP* ni kwa ajili ya wote na gharama zao ni nafuu kuliko baadhi ya taasisi.

Ajira ya akina mama vijijini inaweza kukuzwa kwa kuwatumia kwenye ujenzi wa barabara kama mpango wa *Intensive Labour Utilization* wa *ILO*, ulivyokuwa unasaidia sana kwa kuwahusisha kwenye barabara za Wilaya katika maeneo yao, wanafyeka majani, wanapalilia na kuweka mifereji. Makandarasi waagizwe, watumie wananchi katika maeneo wanamopitia kuliko kuwaleta kutoka mijini.

Mheshimiwa Spika, ajira ya wageni kwa kazi ambazo zinaweza kufanywa na wananchi ni budi zichunguzwe vizuri ili kupunguza malalamiko yasiyokuwa ya lazima. Tusingependa kuona wageni wanaanza kutupiana madongo mitaani, jambo ambalo tusingependa litokee kama tutakuwa makini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa viwango vya juu.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Magogoni na kwa niaba yangu, naomba kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ajira kwa vijana imekuwa tatizo kubwa ndani ya nchi yetu, kwenye hotuba ilielezwa na kweli bado kuna ufinyu wa nafasi za ajira. Je, Serikali ina mipango zaidi kupitia Wizara hii, vijana waweze kuajiriwa wengi zaidi na kupunguza kero za mitaani kuzingatia vijana ndio viongozi wa kesho?

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wanaofanya kazi katika makampuni, mahoteli na sekta nyingine, hawana uhakika wa usalama wa afya zao, kuna upungufu huduma za afya sehemu zao za kufanyia kazi. Naiomba Wizara ifuatilie kuwe na usalama wa afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunao vijana wengi wenye uwezo wa kazi na wakielimishwa huelimika. Lakini vijana hawa wengi hawana kazi wala hawaelimishwi na pale inapotokea kazi katika makampuni, mahoteli na pengine basi huingizwa wageni kutoka nje ya nchi, waliokuwa hawana hata uhalali wa uingiaji na makazi. Je, Serikali haioni hilo na kama suala hilo lipo halikeri; kwa nini lisichukuliwe hatua nafasi hizo zitumike kwa vijana wetu? Naomba majibu ya kuridhisha, kwa manufaa ya wananchi jimbo langu na Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Pamoja na pongezi, napenda kufahamu au kupata ufafanuzi wa mambo yafuatayo: Kwanza, yapo makampuni/viwanda vya wawekezaji toka nje na wawekezaji wa ndani, ambavyo vimewaajiri vijana wetu kwa miezi mingi sana lakini bado wanawalipa kama vibarua hadi sasa, tena wengine wanalipwa shilingi 900/= mpaka 1,200/= kwa siku tangu saa moja asubuhi hadi 12 jioni. Naomba ufafanuzi kama ni haki au sheria kuwa kibarua kwa miezi kadhaa au zaidi ya mwaka. Lakini lingine ni wawekezaji hao kuajiri wafanyakazi toka nje ya nchi hata kama kazi hiyo Watanzania wengi wanaiweza.

Pili, naipongeza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa jinsi inavyofanya vizuri katika kuwapatia mafao wanachama wao. Nawapongeza kwa kuwekeza katika majengo/majumba, uwekezaji ambao unawapatia faida kubwa sana. Sambamba na kupata faida kubwa katika uwekezaji, iendane na kuboresha mafano ya wanachama wao.

Naomba nifahamu Wizara inaisaidiaje Mifuko hii ili iweze kuwekeza zaidi katika majengo, maghala, *real estate* na barabara ili watumiaji wawe wanalipia.

Wizara iangalie zile shilingi milioni 500 kwa kila mkoa. Mkoa wa Dar es Salaam ni mkubwa sana, fedha hizo ni kidogo, tunaomba Wizara/Serikali iangalie uwezekano wa kuipa kila Wilaya ya Dar es Salaam shilingi milioni 500 ili kukidhi haja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GODGREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri ya mwaka 2006/2007, ni hotuba nzuri inayotoa matumaini. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Sasanda – Mbozi, lenye ukubwa wa hekta 335 (ekari 828), lilianzishwa zaidi ya miaka 20 iliyopita na lilifanywa kuwa kituo cha maendeleo ya vijana. Jambo la kusikitisha ni kwamba, eneo hilo limebaki bila kuendelezwa kwa kipindi chote hicho. Naomba Serikali/Wizara, itoe maelezo ya kuridhisha kwa nini inaendelea kuhodhi eneo hilo bila kuliendeleza wakati ikijua fika kwamba, wananchi wana shida ya mashamba. Je Serikali haioni kwamba, muda umefika wa kuliendeleza eneo/shamba hilo ili litumike kwa madhumuni ya kuanzishwa kwake? Kama Serikali haiko tayari kuyaendeleza mashamba hayo; je, isingekuwa busara kutoa eneo/shamba hilo kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, mimi sitaunga mkono hoja ya Waziri, kama sitapatiwa majibu ya kuniridhisha mimi na wananchi wangu wanaoishi jirani na shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, uendeshaji wa Mabaraza ya Usuluhishi *(Concilliation Boards),* siyo mzuri sana, kwa maana ya kwamba, uendeshaji wa Mabaraza hayo hugubikwa na mazingira ya rushwa. Aidha, ofisi zinazotumika na maafisa wa kazi *(Labour Officers),* ziko kwenye hali mbaya sana, hazina samani, makaratasi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia ni kweli kwamba, *Labour Officers* hawana sifa za kuendesha Mabaraza hayo, kwani kiwango chao cha elimu ni kidogo sana, wengi wana *diploma* badala ya kiwango cha digirii kinachotakiwa. Hali hii husababisha uendeshaji usiyoridhisha wa mashauri mengi. Aidha, waajiri wengi hupoteza kesi dhidi ya wafanyakazi kwa sababu maafisa walio wengi, kama nilivyobainisha hapo juu, hupokea rushwa sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iyaangalie masuala hayo yote, ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya utendaji wa maafisa wa kazi, kuwaongezea maslahi (posho, mshahara na kuwapatia usafiri). Pia nashauri Wizara ihakikishe kwamba, *labour officers* wana sifa ambazo afisa wa aina hiyo anapaswa kuwa nazo. Nashauri pia kila wilaya iwe na Baraza la Usuluhishi ili kuharakisha uendeshaji wa mashauri, hali hii itawapunguzia waajiri na wafanyakazi kusafiri mwendo mrefu takriban kilomita 100 kufuata Mabaraza hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Kazini *(Security Employment Act, 1964)* imekuwa ikitumika kwa muda mrefu sana. Hata hivyo, sheria hiyo ilibainika kuwa na upungufu mwingi na hivyo kufanya Serikali ilete Muswada Bungeni. Najua Muswada wa Sheria mpya ulishaletwa hapa Bungeni na kupitishwa. Najua pia kwamba, sheria hiyo ilishasainiwa na Mheshimiwa Rais. Ninachotaka kujua hapa ni kwamba, Sheria hiyo mpya itaanza kutumika rasmi lini na hivi ni sahihi kuendelea kutumia sheria ya zamani wakati sheria mpya ilishapata kibali cha Rais? Je, hatukujiandaa kuanza kutumia sheria hiyo?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuja na mpango huo wa uanzishwaji wa *SACCOS* kwenye ngazi ya Kata/Tarafa. Ninachotaka kuishauri Wizara ni kuweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa mikopo yenyewe, kwani kuanzisha *SACCOS* ni jambo moja na uendeshaji na upatikanaji wa mikopo ni suala lingine. Naomba pia Wizara itoe tamko ni lini mikopo hiyo itaanza kutolewa ili kuwaondolea Watanzania, maswali mengi juu ya ni lini mikopo itaanza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* na suala ununuzi wa Maghala ya Ubungo na *Quality Plaza Nyerere Road,* naomba Wizara ilitolee suala hili ufafanuzi ili Wabunge na Watanzania wengi walielewe vizuri. Kuna habari kwamba, *NSSF* ilimkopesha mfanyabiashara mmoja aitwaye Yussuf Manji, kiasi kinachokadiriwa kufikia shilingi bilioni tisa, kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo mawili. Lakini katika mazingira yasiyojulikana, Manji aliyauza majengo hayo mawili kwa taasisi ya *NSSF.* Maghala ya Ubungo na Taasisi ya *PSPF*, Jengo la *Quality Plaza,* kwa gharama zinazokadiriwa kufikia zaidi ya shilingi bilioni 83. Majengo yajengwe kwa kiasi kisichozidi shilingi bilioni tisa, lakini mwenye nayo anamwuzia aliyempa mkopo kwa takriban shilingi bilioni 83! Naomba ufafanuzi wa kutosha. Ahsante sana.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii muhimu katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Baada ya utangulizi huu, naona nichangie hoja katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuwa wazi na kukiri kuwa, kuna tatizo juu ya ajira kwa wageni. Ukweli huu wa Serikali unatia moyo kwa wananchi na daima kuunga mkono maelekezo ya Serikali, kutokana imani kwa Serikali yao. Hata hivyo, naunga mkono maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba, kazi zote ambazo Watanzania wanaziweza, basi ziwe kwa Watanzania tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, Serikali ilipitisha Sheria ya Kazi Na. 6 ya Mwaka 2004 na Sheria ya Mahusiano Kazini Na. 7 ya Mwaka 2004, bado sheria hizi hazijatoa ufafanuzi kuhusu ajira na mahusiano kazini, kwa wafanyakazi wenye ulemavu. Hata ukizichambua sheria hizi kwa undani, bado hakuna maelezo kuhusu wafanyakazi wenye ulemavu, ambao wana mahitaji maalum na ajira kwao wakati huu wa ushindani ni ngumu kupatikana hata kama wametimiza vigezo vya usaili vinavyotolewa na waajiri mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa, sheria hizo zipitiwe upya kwa ajili ya marekebisho ili walemavu wasomi nao wafaidike na ajira mbalimbali na katika mchakato huo, wadau wenye ulemavu washiriki kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, mikopo ni njia mjawapo ya uwezeshaji wa wananchi na Wizara hutoa mikopo kwa vijana wanawake na wanaume, hasa wale waliojiunga kwenye vikundi vya uzalishaji. Hata hivyo, nasikitika kuona kwamba, vijana wanawake kwa wanaume, wenye ulemavu, hawafaidiki na mikopo (fursa hii), kwa sababu Halmashauri

za Wilaya ambazo ndizo zenye dhamana ya kusimamia utoaji na urejeshwaji, haziwahamasishi walemavu kujiunga kwenye vikundi au *SACCOS*. Kwa msingi huo, naishauri Wizara ambayo ndiyo msimamizi wa Sera, itoe maelekezo kwa Wizara nyingine kama Wizara ya TAMISEMI ili iweze kuzingatia maelekezo hayo katika utendaji kwenye Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, hotuba iliyowasilishwa inatoa mwanga mzuri kwa vijana na wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kuhusu fedha zitakazopelekwa mikoani za maendeleo kwa wananchi pamoja na vijana. Shilingi milioni 500 za kila mkoa ni ukombozi wa wanyonge hasa wanawake na vijana. Naomba kufahamishwa, je, Zanzibar zitapelekwa pia, maana nako kuna umaskini mkubwa sana kwa vijana na wananchi kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, ajira ni tatizo sugu kwa vijana wetu. Kwa hiyo, napendekeza Serikali ifuatilie zaidi ajira binafsi kwa vijana na kufanya hivyo kwa kuwapa mikopo na kuwaanzishia miradi tofauti hasa vijijini ili miradi hiyo iweze kuwakwamua na wao waweze kuajiri vijana wengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikiamua kufanya hivyo, basi viajana wengi watakuwa wana ajira binafsi na tatizo la ajira litapungua.

Mheshimiwa Spika, baada ya michango hii, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia moja. Ahsante.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kufika leo hii kujadili bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana katika kipindi cha mwaka 2006/2006.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu Vijana, katika nchi yetu ya Tanzania wapo vijana wengi ambao wanazurura ovyo bila kuwa na msingi wowote wa kujipatia riziki. Hii imetokana na umaskini uliokithiri nchini, lakini zaidi ni kutokana na vijana wengi kuachwa katika kuendelea na masomo ya sekondari na pia wapo vijana ambao hujitolea kuanzisha vigenge kwa madhumuni ya kupata riziki angalau kuwasaidia wazazi wao ambao ni maskini zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba, Baraza la Manispaa hupita mitaani na kuvunja maeneo hayo kwa suala la mipango miji.

Mheshimiwa Spika, pia wapo vijana wanaojitokeza kuanzisha vikundi vya ushirika angalau kujikwamua kiuchumi. Jambo la kusikitisha ni kuwa, Serikali hutenga fungu maalum kwa ajili ya vikundi vya ushirika, lakini wanakuwa wanapata shida sana katika kupata mikopo hiyo, mwisho vikundi hivyo vinakuwa haviendelei.

Mheshimiwa Spika, vijana hao hujiingiza katika masuala mbalimbali yakiwemo kujihusisha na uvutaji unga, ulevi, wizi na mengineyo kutoakana na kuvunjika moyo kwa mambo fulani.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aweze kuliona jambo hili na kuwaeleimisha vijana nchini, kwa kuandaa semina mbalimbali vijijini na mijini ili vijana wetu wasiendelee kuvunjika moyo.

Mheshimiwa Spika, pale zinapotokea ajira katika sehemu ambazo hazina vikwazo vikubwa kielimu, basi tuwachukue, tusiangalie jamaa wa karibu tu. Tukaweza kushauriwa Wabunge kuweza kuorodhesha vijana ambao wamejitokeza katika vikundi vya ushirika katika mikoa yetu na kuweza kuangalia katika kupatiwa mikopo nafuu nchini.

Mheshimiwa Spika, vile vile wapo vijana waliomaliza sekondari na Vyuo Vikuu, lakini hawana ajira na wamekwisha hangaika sana. Je, Serikali ina mkakati gani katika suala hilo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, kadhalika maoni ya Kamati na maoni mazuri ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, mimi napenda kuchangia eneo moja tu na nitapenda kupata ufafanuzi toka kwa Waziri katika hili, ambalo mimi linanifedhehesha sana. Nchi yetu imeridhia Mkataba wa Kimataifa juu ya ajira mbaya kwa watoto.

Watoto wanaingizwa katika ajira hizo pamoja na sababu nyingi na mojawapo ni umaskini. Umaskini huu upo katika familia za watoto hawa. Mapambano sahihi juu ya ajira za watoto hawa ni kuondoa umaskini katika familia zao.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha unapoona Watanzania wamegeuza madampo na kufanya kazi katika mazingira magumu bila kinga au katika vinu vya kusaga nafaka makundi kwa makundi. Hawana njia mbadala ya kubadilisha maisha yao. Serikali hii inayojali watu wake na kusema maisha bora kwa kila Mtanzania, hawa Watanzania tuwaondoe hapo, wanahitaji maisha bora.

Mheshimiwa Spika, hofu yangu, fedha hiyo itakayotolewa na Serikali, shilingi milioni 500 kila mkoa, itaelekezwa katika vikundi vya sanaa vya CCM na vikundi vya UWT na si kwa wanachi. Basi agalau fedha hizo zielekezwe katika kundi la familia maskini, kuboresaha maisha yao na kufundishwa stadi za kazi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. SEVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na Mheshimiwa Waziri, kuhusu ajira kwa vijana imekuwa danganya toto. Vijana kila siku wamechoka kudanganywa. Kwa masikitiko makubwa, vijana huwa wanajitahidi sana kujianzishia ajira zao binafsi, lakini wanasumbuliwa sana na kunyanyaswa. Kwanza, hawa tunaowawekeza hapa nchini, unakuta wanawafanyisha kazi hawawalipi pesa zao na wale ambao wanawalipa ni pesa kidogo sana wanazowapa. Kwa mfano, kuna vijana wengi wanajitahidi, lakini wanasumbuliwa sana.

Mheshimiwa Spika, unakuta kwenye viwanda mbali mbali, kama mimi nilishaleta malalamiko ya vijana wa Kiwanda cha Sukari cha Kagera, wanawafanyisha kazi, wanawaacha wameadhirika. Vijana wanavunjiaka moyo. Kama vijana wanaanzisha miradi mingine, Wamachinga wanapanga vitu vyao wanafukuzwa. Kwa nini Serikali isiandae sehemu kuwaweka wakafanyia huko biashara zao ambazo ni ajira mojawapo?

Mheshimiwa Spika, naomba nieleweshwe mambo yafuatayo: Hawa wanaofanyishwa kazi bila kulipwa na wanaolipwa pesa kidogo kwa watu binafsi, pamoja na vijana wanaojianzishia miradi yao, Serikali inawafikiria nini; kwa nini isiwawekee mikakati angalau kuwapangia maeneo ya kufanyia shughuli zao?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hawa tunaowawekeza, Serikali iwaeleze kabisa wasiwe wanawanyanyasa wafanyakazi. Kwa mfano, tabia hiyo nimeiona sehemu nyigi Mererani, Kagera na Geita kwenye machimbo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii iwasaidie vijana. Nashukuru sana kwa sasa vijana kupewa mikopo. Ninaomba Serikali ifuatilie kama inawafikia vijana hao, pamoja na vijana wavuvi wafikiriwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, natamka kuunga mkono hoja nikitaraji kuwa yale ambayo Wizara imekusudia kusimamia, yatakuwa na tija na manufaa.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kuelezea kuwa, Serikali inategemea kujiendesha kwa kukusanya kodi na maduhuri toka vyanzo mbalimbali. Moja ya vyanzo hivyo muhimu ni kodi toka kwa wafanyakazi wa Serikalini, Viwandani na Sekta binafsi. Hawa ndio wanaowezesha kodi kukusanywa kwa uhakika, maana inakuwa moja kwa moja toka kwenye mishahara yao .

Mheshimiwa Spika, ili kodi hii ipatikane kwa uhakika na ya kutosha, inabidi mazingira ya kazi yapewe ubora stahili. K wa maana hiyo, inafaa Wizara isimamie watumishi wapate maslahi stahili. Lakini maslahi hayo, yatakuwa ya maana kama elimu kulingana na fani za wafanyakazi itatolewa ili waongeze tija.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema kuwa, itatoa ajira milioni moja katika kipindi cha miaka mitano ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itambue kuwa ajira nyingi kati ya hizo milioni moja, zinapatikana vijijini. Ni vizuri basi Wizara ikashirikiana na Wizara ya Kilimo na Mifugo, ili kuhakikisha vijana wengi wanapatiwa ardhi ili waweze kuendeleza kilimo na hivyo kujiajiri. Ili ajira hiyo iwe makini, TAMISEMI ihusike, wana mtandao wa Uongozi hadi chini.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Jimbo la Kigoma Kusini nikiainisha na shilingi milioni 500. Nashauri pesa hizi zitumike kama za Mfuko wa Pembejeo wakati ulipoanzishwa, walijikopesha watu ambao hawakupeleka fedha hizo kwenye kilimo. Hofu yangu ni kwamba, shilingi milioni 500 zinaweza kupewa wasiohusika. Kwa hali hiyo, naiomba Wizara ihakikishe kuwa kwa upande wa Kigoma Kusini zinasimamiwa ili Wavuvi na Wakulima, hususan vijanaa wafikiwe na hizi fedha. Ajira kubwa Kigoma Kusini ni uvuvi na kilimo. Kwa hali hiyo ni vyema Wizara ikasimamia fedha hizi ili vijana wafaidike na pesa hizi ili wajenge ajira yao na hivyo, kuanza kuchangia Pato la Taifa. Kwa kufanya hivyo, wanaweza kufanya Mfuko huu uwe endelevu na kwa mana hiyo kufanya ajira kwa vijana kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia kuwazuia *(retain)* vijana vijijini ambako watakuwa wamejiajiri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, narudia kusema naunga mkono hoja .

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuzungumzia kazi. Kazi ni kitu muhimu kwa maisha ya binadamu na kuna neno linalosema, asiyetoka jasho asile, kwa hiyo, lazima tukubali kwamba kazi ni uhai.

Mheshimiwa Spika, tumekosea sana tangu zamani, tulipowaacha wananchi wakabweteka bila ya shughuli muhimu, kwa hiyo, kama tunataka watu wafanye kazi, lazima tufunge kibwebwe, kazi si lazima za ujira, Mwenyezi Mungu ametupenda ametupa ardhi.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu kwanza, tuangalie maeneo yetu ya ardhi, kilimo gani kinastawi wapi, tuanze kuweka vijana wetu kwenye makundi tuwape elimu kwamba, kilimo sio mateso, tuwaeleweshe hivyo, tuwasimamie tuwape walimu/wakulima wawafundishe mwaka mmoja watakuwa wamepata akili na watajikuta wananufaika na Serikali inanufaika.

Mheshimiwa Spika, siku hizi tuna vipindi vya TV zinaonesha wananchi wetu wanavyotumia mikono yao kutengeneza vitu vizuri. Hapo nje ya Bunge, kuna akinamama wameshikilia majagi ya maua, wanayatengeneza kwa mikono yao. Hao akina mama tayari wao wameshaweza, kilichokosekana ni masoko, wangekusanywa wakapewa mtaji, wakapewa vijana wakawafundisha na hapo hapo Serikali ikafanya njia ya kuwapatia masoko, Serikali ingepata na wananchi wangepata ajira.

Mheshimiwa Spika, hii ni mifano michache tu, hatujakosa kazi ila hatuna wasimamizi wa kutuongoza.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* na Mashirika kadhaa, ambayo yanaweka fedha za wananchi, yanasaidia sana katika hilo, lakini kwa nini Mashirika haya yanatumia fedha za wananchi wanazochangia kwenye Mifuko yao na kuzifanyia kazi bila kuwashauri? Je, hiyo faida inayopatikana mbona haiwasaidii hao wahusika; kwa nini faida inayopatikana wasipewe wenyewe?

Mheshimiwa Spika, wahusika wanapotaka fedha zao iwe rahisi kuzipata, kwani unapomwambia mhusika arudi kwenye Mashirika alikofanya kazi, eti akajaziwe hizo fomu, anapofika kwenye Shirika husika ni usumbufu wa hali ya juu ili ajaziwe fomu hizo, kwani kama kitambulisho anacho, jina lake wanaliona, kwa nini *NSSF* wasitafute kwenye makabrasha yao wakapata hizo fehda na wakamlipa mwenyewe, kwa nini arudi alikoajiriwa wakati *NSSF* walipokea fedha zake vizuri wakati wa kumlipa ndiyo iwe balaa?

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya vijana na ajira kwa wageni, vijana wetu hapa hawana pakwenda, kwa nini tunashindwa kabisa kuwaendeleza? Wizara ambayo imekubali kubeba jukumu hilo zito, basi wakae chini ili waelewe nini la kufanya.

Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 500 zilizotengwa eti kuondoa umaskini, mimi sioni kama ni kweli. Fedha hizi zingechukuliwa wakaendelezwa vijana kwa kupewa elimu ya kilimo na kazi za mikono kama nilivyoelezea hapo juu na baadae kukawa na viwanda vidogo vidogo, kilimo chao kama mboga au matunda wakasindika na kupatiwa masoko. Fedha hiyo ingezunguka, ajira ingepatikana na kilimo kingekua, sherehe baada ya kuwa mateso. Lakini fedha hiyo eti wakopeshwe, mnunuzi nani, baada ya kuwaondoa kwenye umaskini walipo hapo mnataka kuwafilisi hata vitanda wanavyolalia na magodoro, eti wameshindwa kurudisha mikopo.

Mheshimiwa Spika, wageni wamejaa ndani ya nchi hii, kazi wanazofanya vijana wetu wangeweza kuzifanya, lakini ukiuliza unapewa jibu kwamba, waume zao au wake zao ni wawekezaji. Hebu Wizara irudi tena kwenye Sheria ya Uhamiaji, iangalie taratibu za wageni kufanya kazi kwenye nchi hii, naomba Wizara inipe jibu kwenye suala langu hili moja tu.

Mheshimiwa Spika, wale Wapakistani waliompiga Mtanzania kwenye kiwanda cha nguo, hivi kazi walizokuwa wakifanya Watanzania wanashindwa kuzifanya? Kama mwenye Shirika hataki kuajiri wananchi, basi asipewe ruhusa kufanya biashara hapa nchini. Kuna Mashirika mengi tu ambayo yameajiri wageni kufanya kazi za ajabu. Maoni yangu, Wizara ifanye kazi ya kuchunguza hayo Mashirika na ifanyike kazi hii kwa uangalifu sana, kwani hao vijana mnaowatuma kuchunguza wakienda kule wakikuta wageni, wanapewa visenti wanasema sawa, mradi wageni wanaofanya kazi nchini kuanzia maombi ya kwanza ya mgeni kuingia nchini mpaka akiwa hapa ni rushwa tupu.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wote kuanzia Waziri, Naibu Mawaziri, Wakurugenzi na wafanya kazi wote wa Wizara, nawaomba wafanye kazi kwa utulivu ili mavuno yaonekane. Ahsante.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kushauri kuwa, Wizara zisisahau kutafuta mikakati ya kuhakikisha nguvu kazi kubwa iliyoko vijijini, wanasaidiwa pesa hizi na wao wanufaike, isiwe kama fedha nyingi zilizotolewa na Serikali kupitia Benki na Taasisi nyingine ziliishia kwa wakubwa. Vijana wanajiajiri kwa mfano, vijana wa stendi wanauza magazeti na biashara ndogondogo, kwanza hawafikiwi na hawajulishwi, ukiuliza wanasema watendaji ni vigumu kuwaweka pamoja. Naomba iandaliwe mikakati ya kuhakikisha vijana hawa wanakusanywa, wanaelimishwa na wanasimamiwa kuendesha biashara za ujuzi wao. Mkiwaacha ahadi ya CCM, ajira za vijana za kujiajiri haitotekelezwa, kwani vijana wengi ambao ni wapiga kura ndiyo wenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira za watoto, ninazungumzia vijana wanaoajiriwa majumbani. Kuna vijana wengi waliomaliza darasa la saba na wengine ni wadogo, ambao hawaendi shule wameajiriwa kama wafanyakazi za nyumbani na kuchunga ng'ombe. Naomba kuwe na utaratibu wa kuwafitilia majumbani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira za nje ya nchi, hivi sasa kuna ajira za vijana Arabuni, kuna makampuni yanatafuta ajira Arabuni na kuja Tanzania kuwatafuta watu wafanye kazi Arabuni. Naomba Makampni haya myatazame. Wanawatapeli watu, wanachukua fedha za watu kisha wanawapiga danadana. Naomba Wizara, vijana wanaotafuta kazi nje ya nchi wajiandikishe Wizarani na Makampuni haya yaje Wizarani kupata majina ya vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushuru wa Halmashauri unawanyanyasa watu wanaojiajiri. Kuna kodi zinazokera, zinazowafanya wanaojiajiri waendelee kunufaisha Halmashauri na *TRA* na wao wanabakia maskini. Wakurugenzi kutotafuta njia mbalimbali za kupata mapato, wanawanyanyasa vijana wetu wanaojitahidi kupata kipato mfano, Kibaha na madreva taxi wanatakiwa kila siku walipe Halmashauri shilingi 600, kwa mwezi ni shilingi 18,000/= na kwa mwaka ni shilingi 216,000/=. *TRA* inawataka vijana hawa walipe kodi zaidi ya shilingi laki mbili kwa mwaka. Mwenye taxi kwa kodi hizi na mshahara wa dreva, mwisho wa mwaka anabakia na nini? Wakurugenzi wanawashawishi Madiwani kiasi kwamba, Mbunge ukiwashauri wapunguze, unaonekana ni mkorofi. Naomba Wizara hii wakisaidiana na TAMISEMI, wafikirie utaratibu wa kuwapunguzia mzigo wa kodi.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimwombe Mwenyezi Mungu, aniwezeshe kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba niende kunako mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema niishukuru Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, kwa kukiri kwake kuwa, sehemu kubwa ya jamii ya Watanzania ni vijana na kundi hilo ndilo linaloathirika zaidi na ukosefu wa ajira. Serikali ya Awamu ya Nne, inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, imeahidi kutengeneza ajira milioni moja katika kipindi cha miaka mitano ijayo, yaani 2006 - 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ni Rais wa Muungano, ambaye ndiye aliyetoa tamko hili, ambalo ni tamko jema kwa vijana wetu, hali hii itawapelekea vijana kupatiwa ajira. Ni vyema sasa utekelezaji wake ufikie kule kote waliko vijana wa Kitanzania, wenye elimu tofauti na sio vijana maalum. Maumbile ya Watanzania yametofautiana kijinsia, kielimu na kimaisha. Serikali inapaswa ielewe walowezi katika vijana wetu nchini ni maskini, ambao elimu yao ni ya chini. Hii inaeleweka kwamba, maskini mara nyingi hukwama njiani katika masomo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira ya watoto, kuna watoto wengi mitaani ambao ni waajiriwa majumbani, hali ya kuwa ni watoto wadogo sana. Kuna watoto ambao wanawalea watoto majumbani kiajira. Kuna watoto ambao ni wafanyakazi katika majumba kiajira. Watoto hawa ni lazima wataathirika kielimu, jambo ambalo ni hasara kubwa kwa mtoto huyu, pia kwa Taifa kiujumla. Wizara imechukua hatua gani za kunusuru watoto hawa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa wageni, kijana wa Kitanzania anayo haki katika nchi yake. Waajiri wa nje ama wa ndani, mara nyingi huwanyanyasa vijana wetu katika kazi zao. Mara nyingi waajiri huwageuza waajiriwa ni watumwa. Dosari hizi zipo na zinaendelea kuwepo. Ni juzi tu ambapo waajiri wa kigeni katika hoteli fulani nchini, iliwapiga wafanyakazi wa Kitanzania na mmoja wao alipigwa hadi kulazwa hospitalini. Jambo hili ni udhalilishaji kwa Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haikulikemea hili kwa nguvu zote, litaleta madhara kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kijana sio lazima apatiwe ajira na Serikali ama kampuni au kwa tajiri fulani. Kijana anapoandaliwa anaweza kujiajiri binafsi na matokeo yake kijana huyu atampatia kijana mwenzake ajira. Serikali sasa ni wakati muafaka wa kumwandaa kijana ili aweze kujitegemea.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuamua kuweka Wizara hii mahsusi kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari na Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo, nashauri kwamba, fedha hizi za mikopo wapewe wakulima wadogo wadogo, ambao tayari wameonesha njia ya kujiajiri kwa kulima mboga mboga, kwani asilimia kubwa ya kilimo hicho hufanyika wakati wa

kiangazi. Nashauri wapewe pembejeo za kisasa kama vile majembe ya kukokotwa na ng'ombe, kilimo bora kinachotumia pembejeo za kisasa. Vijana wahamasishwe kulima mazao ya biashara, ambayo yanaweza kulimwa katika kila Mkoa. Sheria za Kazi zibadilishwe na kurekebishwa. Pia Ofisi za Idara za Kazi Mikoani ziangaliwe na kukarabatiwa, hususan jengo la Tabora halifai. Wapewe vitendea kazi vya kisasa. Elimu itolewe kwa wafanyakazi ili wajue sheria za kazi na haki za Mahakama ya Kazi.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kumpongeza Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Naibu Mawaziri wa Wizara hii na Katibu Mkuu wa Wizara. Hongera sana kwa kuweka mikakati kadhaa ya kuendeleza vijana, ikiwa ni pamoja na kuwajua vijana kuwa wako wapi na wanafanya nini katika vikundi vyao. Hongera sana.

Baada ya kusema hayo, kabla sijaendelea, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa kwanza kabisa, ninapenda kuuliza suala lifuatalo: Sheria inasema nini kuhusu Sheria ya Kazi kwa mtu anayelipwa shilingi 200,000/= *gross;* je, mtu huyu anastahili vilevile kulipwa *overtime* au hastahili? Mheshimiwa Waziri naomba jibu la swali hili, nijue kwani kuna utata juu ya suala hilo kwa waajiriwa katika makampuni ya watu binafsi.

Pili, je, Serikali ina mpango gani juu ya kufuatilia waajiri wa Taasisi, Mashirika mbalimbali ya binafsi, kama Toyota na kadhalika, kuona wanatendewa haki wafanyakazi katika malipo ya ajira. Ni bora kuona mashirika ya umma, viwanda, mashirika binafsi na taasisi mbalimbali, zinaangaliwa vilevile katika viwango vyao vya mishahara. Nina wasiwasi kwamba, baadhi ya Mashirika ya watu binafsi na viwanda kama wanawalipa kihalali au sawasawa watumishi wao. Naomba hili lichunguzwe. Serikali inapoongeza mishahara na wao waangalie pia uhalali wa kuongeza.

Tatu, kuhusu vikundi vya vijana vya kuzalisha mali nchini, vilivyofanyiwa utambuzi *(Youth Mapping).*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu, ninamwomba Mheshimiwa Waziri uendelee katika Wilaya nyingine ambazo bado kufanywa. Katika Mkoa wa Lindi, Wilaya za Ruangwa, Nachingwea, Liwale na Kilwa bado kufanyiwa uchambuzi wa vikundi vya vijana vya kuzalisha mali *(Youth mapping).* Tunaomba sana tufanyiwe.

Nne, suala la *SACCOS,* hii elimu ya *SACCOS* bado haijatiliwa mkazo kwa vijana. Jitihada za makusudi zifanywe kwa kila Wilaya, kuwaelekeza vijana kuhusu suala la kuwa na *SACCOS* kwa vijana, wanawake na wanaume ili washiriki kikamilifu.

Tano, Mradi wa *NSSF* wa ujenzi wa majumba, uje pia Mkoa wa Lindi na Wilaya zake zote.

Sita, ajira ya watoto wadogo, bado inaendelea majumbani. Jitihada ziendelee kufanywa ili kuwaokoa watoto hawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, basi ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nyongeza ya hoja yangu, kuhusu ajira na maendeleo ya vijana, viwanda na mashamba ya Mashirika ya Umma Tanzania kutolipa wafanyakazi wake. Kuna mashamba na viwanda vilivyokuwa vimebinafsishwa, ambayo yameacha wafanyakazi wake wa siku za nyuma bila malipo hadi leo. Kwa mfano, mashamba ya Mbarali, watu 170 na *Hanang W. Complex* watu 400 hadi leo bado hawajalipwa haki zao za kisheria. Si hao tu, kuna kiwanda cha *Mhata Saw Mill* Mkoa wa Tanga, Kiwanda cha Chuma Tanga na Mashamba ya Mpira Muheza. Ninataka kujua hawa watalipwa lini? Naomba kupata ufafanuzi.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wa wote wa Wizara hii, kwa mchango wao mkubwa na kazi nzuri waliyoifanya katika kuandaa hotuba hii ya Bajeti, ambayo kwa kiasi kikubwa, inatoa tegemeo kwa vijana wetu, ambao kwa namna moja au nyingine, macho yao wameyaelekeza sana kwenye Wizara hii katika mustakabali wa maisha na maendeleo yao.

Katika mchango wangu wa kwanza kwa Wizara hii, napenda kwa moyo mkunjufu, kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha shilingi 500,000,000/= kwa kila Mkoa ili ziwasaidie vijana wa Tanzania kujiendaleza kimradi, jambo ambalo litatoa ajira kwa vijana wetu. Napenda kuelewa juu ya suala hili la kupatiwa shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa ni Mikoa ya Tanzania Bara tu au na Tanzania Visiwani? Nachukua fursa hii kumpongeza Waziri, kwa kuandaa mpango mzuri wa ukusanyaji wa taarifa za vijana katika Wilaya za Tanzania. Jambo hili litaleta faraja kubwa, kwani litawezesha vijana wote kujulikana walipo na shughuli wanazozifanya Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake alieleza kwamba, ana ushirikiano mkubwa na Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hivyo, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, ni vyema wakashirikiana pia katika suala hili ili na vijana wa Tanzania Visiwani, zipatikane taarifa zao na shughuli wanazozifanya kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kujua kuhusu hizi nafasi 1,000,000 za ajira, zitatolewa namna gani na vijana wenyewe wanaeleweshwa vipi? Nasema hivi kwa sababu vijana wengi sana, wanaelewa ama wanategemea ajira ni ile inayotolewa na Serikali tu. Hivyo, ni vyema suala hili likawekwa/kuelezwa vizuri ili vijana waelewe nini ajira na ili Serikali yetu ya Awamu ya Nne, ijieleze kwa nafasi jinsi ilivyotekelezwa

Ilani ya Uchaguzi juu ya suala la ajira, basi ni vyema liwekwe wazi jambo hili la ajira na vijana wafahamu jinsi wanavyopata ajira hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nasema kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Chaani, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Nashukuru na mimi kuchangia kwa maandishi, maana mjadala wa Wizara kwa siku moja sio rahisi kupata nafasi ya kuchangia kwa mazungumzo. Katika ukurasa 8 – 10 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kaorodhesha kazi zilizofanywa na Wizara yake. Moja kati ya kazi hizo ni Mkataba wa *ILO* wa kuwatumikisha watoto katika kazi za hatari.

Mheshimiwa Spika, kusaini Mkabata wa Kimataifa haitoshi bila ya kuitungia sheria ili itumike kuwabana wale wanaotesa watoto. Pia kuna haja ya kuweka mkakati wa kuweka kitengo maalum cha kufuatilia wale wanaoajiri watoto ili wachukuliwe hatua za kisheria na watangaze hatua hizo ili wengine wanaofanya kosa kama hilo waogope.

Mheshimiwa Spika, jana nilipigiwa simu mbili kuhusu machango wa mwenge. Mchango wa mwenge sehemu nyingine za nchi hii sio la hiari. Sehemu nyingi hasa vijijini, wananchi hasa wafanyabiashara, wanalazimishwa kuchangia fedha za mwenge.

Wafanyabiashara wanatishwa kufutiwa leseni zao za biashara, kama hawakulipa mafuta ya mwenge. Mkoa wa Shinyanga wafanyabiashara wamelazimishwa kulipa shilingi 50,000/=. Kama Wizara hiana mafuta ya kutembezea mwenge Tanzania nzima, basi ni bora Wizara iachane na mbio za mwenge, inaweze kwenda kuomba mchango wa mwenge lakini sio kuwalazimisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FELEX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Wizara hii katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inao wajibu mkubwa wa kuwapo ajira vijana kwa sababu imekuwa kero kubwa kuwaona vijana wakihangaika. Wakati mgombea Urais akijinadi katika Mikoa yote, alitoa matumaini makubwa ya ajira kwa vijana. Baada ya uchaguzi kukamilika, ni budi sasa Wizara hii ijikite kutoa ajira, kwa kusimamia vikundi vya vijana na kutoa mikopo kwao ili waweze kujiajiri katika nyanja kadhaa za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuwatetea wafanyakazi wa sehemu mbalimbali ni la Wizara hii. Mara nyingi kumekuwa kukijitokeza matatizo ya kunyanyaswa kwa wafanyakazi, kunakofanywa na waajiri. Watu hawa wamekuwa wakikosa utetezi. Kwa makusudi mazima, Wizara ni lazima ijiimarishe katika kuhakikisha kuwa, Mahakama ya Kazi yanakuwepo kwa ajili ya kuwatetea watumishi wa aina hiyo, wanaonyanyaswa. Kwa usimamizi wa namna hii, waajiri ambao wamekuwa na tabia ya kuwaonea watumishi, watajikuta wakichukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia ya watu kutoka nje ya nchi kushikilia nafasi za kazi, ambazo zingefanywa na Wizara. Hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na wageni hawa kuja kufanya kazi bila vibali. Usimamizi wa vibali hivi vinavyotolewa kienyeji ni kutokana na kutokuwa na usimamizi wa kutosha, kwa watoa vibali ambao wanatoa vibali kwa watu wasiohusika kwa kuhongwa fedha. Sambamba na hali hii, imesababisha kuwa na wageni haramu, ambao wanaipatia kazi ya kuwasaka na kuwarudisha kwao Wizara ya Mambo ya Ndani na hasa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, unapotembezwa mwenge katika Wilaya mbalimbali, ikiwemo Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba, wafanyabiashara huchangishwa fedha ili kuhudumia mwenge. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akanieleza michango hiyo ni hiari au si ya hiari?

Vilevile Mheshimiwa Waziri kwa kupitia Wizara yake, wanaratibu vipi matumizi bora ya fedha hizo ambazo licha ya wafanyabiashara na wafanyakazi pia wanachangishwa?

Mheshimiwa Spika, ajira ni mtambuka kwa maana kila Wizara inaajiri na hutoa nafasi ya ajira kwa wananchi au wageni. Ninachoshauri hapa Wizara hii isitoe vibali vya wageni kupata ajira hapa wakati wapo wananchi wanaomudu kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, ajira siyo ya Serikali tu, je, Wizara inasemaje kuhusiana na wageni wanaoitwa wawekezaji, matokeo yake wanafanyabiashara za kawaida? Je, Serikali haioni suala hilo linapunguza ajira kwa vijana?

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa majukumu ya Wizara hii ni kufanya ukaguzi katika maeneo ya kazi, kama inavyodhihirishwa katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa 14, hufanya ukaguzi katika viwanda na makampuni. Kwa mifano iliyotolwa na viwanda vilivyokaguliwa, mpaka sasa inaonekana ukaguzi huo unafanywa kwa kasi ndogo. Je, Wizara iansemaje kuhusu hilo, haioni ukaguzi wa aina hiyo utafanya zile sehemu ambazo hazijakaguliwa, wananchi waendelee kudhalilishwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshsimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Waheshimiwa Naibu Maaziri na watendaji wote, waliosaidia kuwezesha kutolewa kwa hotuba hii nzuri mwaka huu wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, migogoro kati ya wafanyakazi na wawekezaji. Kumeanza kuzuka na kuendelea kwa migogoro ya unyanyasaji kati ya wafanyakazi na wawekezaji. Migogoro ya aina hii, inatishia sana juhudi za uwekezaji nchini hasa viwandani. Mambo makubwa yanayosababisha ni kama yafuatayo:-

Wawekezaji kudhamiria kutowapa mafao mazuri na hata kinga kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo ya hatari au mazingira magumu.

Wawekezaji kutojali kuheshimu kanuni na sheria za kazi.

Wafanyakazi kutojali uzalishaji wenye tija ila mapato na matumizi yaweze kukidhi haja ya faida kwa wawekezaji.

Wizi unaokithiri ndani ya viwanda kwa bidhaa zinazozalishwa hivyo, kuingiza hasara badala ya faida.

Mapungufu ya Elimu ya Sheria na Kanuni za kazi kwa pande zote mbili; wafanyakazi na wawekezaji.

Wajibu wa Wizara ni kuona njia bora za kuondoa dosari zinazojitokeza ili kutoa motisha kwa wawekezaji na wafanyakazi kwa maendeleo ya viwanda. Kuratibu na kuwa na orodha ya idadi ya vijana wasiokuwa na kazi Kitaifa. Wizara iharakishe kujenga takwimu za uhakika Kitaifa juu ya idadi ya vijana wasiokuwa na kazi. Orodha ielekeze idadi kwa Miji, Wilaya na Mikoa na pia kwa maeneo ya vijijini. Hii ndiyo njia pekee ya kisayansi, itakayowezesha kutafsiri kauli mbali mbali za viongozi wa Taifa kuhusu hali ya ajira kwa vijana nchini. Kwa mfano, Mheshimiwa Rais akisema atahakikisha kutoa ajira kwa vijana milioni moja; je, takwimu hiyo itatafsiri vipi kwa kiwango cha asilimia iwapo Wizara inayohusika na ajira haina takwimu kuu ya kigezo *(Base Figure)?*

Ni wajibu sasa wa Wizara, kujenga mafumo wa tafsiri za kisayansi juu ya hali ya ajira hapa nchini. Mwelekeo wa Kitaifa ulenge kujenga uchumi utakaowezesha hapo baadaye kama ilivyo katika nchi zilizoendelea, kuwalipa wasio na kazi, kiwango cha fedha kuwawezesha kukidhi mahitaji yao muhimu.

Wilaya ya Muheza ilikaa kwa muda mrefu bila kuwa na Afisa wa Kazi wa Wilaya. Hali hii ilisababisha kesi za wafanyakazi kufanyika Mkoani Tanga. Kutokana na umbali na gharama za nauli, wafanyakazi waliokuwa wakilalamika, walishindwa kuhudhuria kesi zao na hivyo kukosa haki zao.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara sasa iepuke kuchelewesha kupeleka Maofisa muhimu Wilayani, mara inapotokea vifo au uhamisho wa Maofisa waliokuwepo kama ilivyokuwa Wilaya ya Muheza.

Iwapo eneo la kiwanja ilipo Ofisi ya Kazi, barabara ya Bibi Titi Mohamed Dar es Salaam, kama mali ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, basi nashauri Wizara itumie fursa ya uwezo wa *NSSF*, Taasisi iliyopo chini ya Wizara hii, kujenga

jengo kubwa la kisasa katika kiwanja hicho badala ya jengo dogo lililopo katika eneo muhimu la uwekezaji katika barabara kuu kama ile ya Bibi Titi Mohamed.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha pamoja na kazi nzuri wanazofanya, nawapongeza sana.

Kwanza, naishauri Wizara pesa zitakazotolewa kwa akina mama na vijana kujiajiri, zipelekwe katika *SACCOS* za kata ili ziweze kuwafikia walengwa. Kata ambazo hazina *SACCOS,* zishauriwe kuunda *SACCOS* za Kata.

Pili, shilingi milioni 500, mgao wa Mkoa wa Dar es Salaam wa kuwawezesha vijana na akina mama kujiajiri hazitatosha kutokana na wingi wa vijana na akina mama wa Mkoa huu. Tunaomba tufikiriwe kuongezwa japo tupewe shilingi 1,500,000,000/=.

Nashauri kuvibadilisha vikundi vya vijana na akina mama kama *camps*. Vijana mbalimbali wa muziki vijiweni, vilabu vya mipira vya aina zote na vikundi vyote vya vijana vya burudani, Wizara itafute namna ya kuvifanya kuwa vikundi vya uzalishaji mali.

Wananchi wa Temeke wanampongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Shirika lake la *NSSF*, kwa kupewa jukumu la kusimamia ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Wananchi wa Temeke na Dar es Salaam, wanatarajia kupata ajira ujenzi utakapoanza na utakapokamilika utapunguza sana msongamano wa Barabara ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Wananchi wa Dar es Salaam, daraja litajengwa kwa wakati na litaisha kwa wakati uliopangwa. Nawatakia kila la heri katika kazi zenu za ujenzi wa Taifa.

Naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi kwa mpango wa Wizara kuanzisha Miradi ya *Millenium Complex Ubungo.* Kwenye ziara ya Rais Mkoa wa Dar es Salaam alipongeza sana kwa maana sasa mpango wa *Export Driver Products* utafanikiwa kwa viwanda hivyo vilivyojengwa na *NSSF*, ajira zitapatikana na Serikali itapata kodi. Naomba mpango huu uendelee Mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa mingine.

Nashauri sasa Wizara iwe na *Job Centre* ili iweze kupata au kuwa na *pool* ya vijana wenye taaluma mbalimbali, kuanika uwezo wao na hatimaye kupata ajira. Suala la ajira kwenye nchi nyingine, hutumia mpango wa *community enforcer,* huangalia mazingira na ulinzi. Malipo yao hutokana na *fine* za makosa. Mkazo sasa utolewe kwenye masoko ya usiku, *seed money* zitolewe kwa vijana kama mtaji na Wabunge

washirikishwe kwenye zoezi zima. Wabunge wapate fursa ya kutembelea China, kujifunza mikakati iliyofanikiwa kwenye nchi hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wamekuwa wakifanya kazi kwa mazingira magumu sana(hasa Idara ya Kazi). Vituo 32; wilayani vituo 12, ofisi za mkoa 20, Afisa Kazi anatakiwa kushughulikia mkoa mzima. Je, Wizara ina mikakati gani katika kulitatua hili? Ni ofisi ngapi za Idara za Kazi, ambazo zitatengenezwa/kukarabatiwa katika mwaka huu wa fedha?

Bajeti ya Waziri wa Viwanda na Biashara mwaka 2004/2005, aliliarifu Bunge kwamba, ingelinunua jengo la *Millenium Tower* kwa ajili ya *EPZ.* Kwa nini Wizara iliamua kununua *Hifadhi House* kwa bei ya kutupwa wakati miundombinu yake ni sio bora kama ya *Millenium* T*ower (LAPF)?*

Ni lini Mabaraza ya Wafanyakazi yataanzishwa ili kusaidia utatuzi wa migogoro makazini?

Ni lini *Regulations* za *CMA* na jengo la *CMA* zitakuwa tayari kwa kuzingatia ahadi Mheshimiwa Waziri aliyotoa kwenye Mei Mosi mbele ya Mheshimiwa Rais?

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha, naomba nichukue fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina, ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Ninaamini kuwa, hotuba hii ikitumika vizuri, itakuwa ni dira ambayo itasaidia sana katika kusukuma mbele maendeleo ya jamii.

Tatizo la ajira kwa vijana wetu ni tatizo ambalo kwa maoni yangu, linaweza kupunguzwa kwa sekta binafsi na Serikali kuanzisha miradi mbalimbali na mikubwa ambayo itatoa ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ALI HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na viongozi wengine wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Baada ya mfumo wa uchumi na siasa kubadilika, soko huria na mfumo wa vyma vingi vya siasa, panahitajika kuwepo vya wafanyakazi wenye uwezo na nguvu za kutetea wafanyakazi hasa pale sekta binafsi itakapoongoza kwa kuwa na wafanyakazi wengi nchini. Hivi sasa waajiri binafsi karibu wote, hawathamini sheria na taratibu za kazi nchini. Wanalipa mishahara watakayo, nje ya kima cha mshahara kwa mujibu wa sheria nchini. Kwa vile kuna uhaba wa kazi, wanalazimika kukubali kulipwa na waajiri kama watakavyo. Ombi langu, Serikali iimarishe vyama vya wafanyakazi ili viweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Vinginevyo wajanja wachache wataendelea kutajirika na kundi la walala hoi litakua.

Wizara izidishe kasi na ielimishe jamii ili ielewe faida za *SACCOS,* kuliko *NGOs* nyingine zenye mwelekeo wa utegemezi wa ufadhili toka nje ya nchi yetu, ambazo madhumuni yake wakati mwingine ya kisiasa, kuingilia uhuru wa nchi zetu na utamaduni, mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe. *SACCOS* zitasaidia kupatikana mikopo toka vyombo vya fedha, ni mbinu mojawapo ya kutokomeza umaskini nchini.

Usalama na Afya Mahali pa Kazi, kwa maoni yangu Muswada wa Afya na Usalama kazini ni muhimu sana ingawa umechelewa Bungeni. Hata hivyo, naipongeza Wizara kwa kuandaa, uletwe Bungeni mwaka huu, unusuru afya za wafanyakazi na kudhibiti maafa na hata vifo vya wafanyakazi.

Kwa sasa mahali pa kazi pachafu, nyumba mbovu, ukosefu wa vifaa vya usalama kazini, Wizara inachukua hatua gani kurekebisha hali hii mbali na kwamba sheria bado inaandaliwa?

Mashirikiano kati ya *NSSF* na *ZSSF,* Tanzania ni Nchi moja yenye Serikali mbili, kama vile zilivyo nchi nyingine zenye mjumliko wa nchi nyingi kama vile *(USA),* naomba kufahamu mahusiano yaliyopo katika vyombo hivi na yamesaidia kwa kiasi gani kukuza mahusiano, tija, ujuzi na mafanikio?

Waziri katika hotuba yake ukurasa 31, mbali na maelezo mengine, ameeleza ifuatavyo: Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi inatambua kuwa sehemu kubwa ya jamii ya Watanzania ni vijana, kundi ambalo linaathirika zaidi na ukosefu wa ajira. Kwa kuwa upatikanaji wa mitaji ni moja ya kichocheo cha ajira, naomba kufahamu tu wastani wa shilingi milioni 500 kwa kila mkoa, vijana toka Zanzibar watafaidika vipi na maamuzi haya ya Waziri Mkuu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, pmoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nitachangia machache tu, ambayo nitahitaji majibu na ufafanuzi wa kina. Naomba Waziri atueleze ni ajira zipi zinazohitajika kufanywa na wataalam kutoka nchi za nje? Kwa sasa hivi kumekuwa na wafanyakazi wengi sana nchini, ambao wanafanya kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya kwa mfano, wafanyakazi wa mahotelini, Wachina wananyoosha magari yaliyogongwa na kadhalika. Mimi sipingi wataalam kuja Tanzania, kuwafundisha Watanzania, hatimaye kazi hizo zifanywe na Watanzania baada ya kupata ujuzi kutoka kwa wataalam. Hawa wageni wanapewa kibali kwa muda gani? Lazima muda wa ku-*train* uwepo, la sivyo wageni hawa watahamia kabisa hapa na Watanzania hawawezi kupata kazi.

Idara ya Kazi ishirikiane na Uhamiaji waangalie ni jinsi gani ya kudhibiti watu wanaokuja nchini kama watalii na baadaye wanafanya kazi. Mfano *arrival form* za wageni kwa kipengele kinachouliza ni *seeking employment*, kama mtaalam anakuja Tanzania si unakuta ameshapewa kibali cha kazi toka huko alikotoka? Hii inawapa mwanya wa kupata kibali cha kufanya kazi kwa urahisi. Je, Serikali ina takwimu ni Wakenya na Waganda wangapi wanafanya kazi bila vibali? Wanapita tu mipakani na kufanya kazi nchini lakini kwa Mtanzania kufanya kazi kwenye nchi hizo ni kitendawili. Kuna mikakati gani iliyopo ya kuwadhibiti na kuwarudisha kwao?

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naomba majibu. Nashukuru naomba kuwasilisha.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kuipongeza Serikali, kwa mpango wake wa kuwapatia mitaji wananchi, kuchochea ajira kwa kutumia mgao wa fedha wa shilingi milioni 500 kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Waziri Mkuu. Naiomba Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa Mkoa wa Dar es Salaam kufikiria mambo yafuatayo:-

(a) Kuiomba Serikali kuongeza kiwango cha fedha katika mpango huo kwa kuwa kiwango kilichopangwa cha shilingi milioni 500 ni kidogo ukilinganisha na wingi wa watu katika Mkoa wa Dar es Salaam, pamoja na uhamiaji wa watu kila siku katika Mkoa huo.

(b) Fedha za mpango huo napendekeza itumiwe Benki ya Watu wa Dar es Salaam, ambayo nayo iliazishwa kwa misingi hiyo hiyo.

(c) Wizara iwe tayari kushirikiana na Ofisi za Wabunge, kuanzisha *SACCOS* katika kila Kata ndani ya Majimbo (*SACCOS* za Kata)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* ijitahidi kufungua Ofisi yake katika kila mkoa kwa kuzingatia umuhimu wa kazi zake.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa ajira nchini ni moja ya kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Nne hivyo, naiomba Wizara ya Kazi, kukitangaza zaidi kwenye vyombo vya habari, Kituo cha Ajira *(Labour Exchange Centre)*, wananchi wengi wakielewe na hatimaye kuwatumia katika harakati za ajira.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara hii, kwa jinsi ilivyosimama kidete kutetea na kuhalakisha kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) katika ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Hatua hiyo itaiweka Chama Tawala katika nafasi nzuri kwa wananchi, hasa wa Kigamboni, pia kuimarisha uchumi wa nchi yetu na sekta ya utalii. Pongezi pia ziwaendee Shirika la Hifadhi ya Jamii la Taifa *(NSSF)*, kwa huduma bora wanazotoa kwa Watanzania pia katika kuisaidia Serikali, kupiga vita umaskini kwa kujenga nyumba na kukopesha kwa bei nafuu

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri. Nachangia kuhusu Shirika la Hifadhi la Jamii *(NSSF).*

Shirika linakusanya michango toka kwa wanachama na kuwekeza, lengo la kuwekeza ni kupata fadia, kwa kuwa fedha ni za wananchama, wanachama wanayo haki ya kupata gawio la faida inayopatikana. Je, Shirika limepatia faida kiasi gani, tangu lianzishwe na wanachama wamegawiwa kiasi gani?

Pili, uwekezaji katika majengo unahitaji umakini wa hali ya juu, ni hatari kununua majumba kutoka kwa wawekezaji maana yanauzwa kwa bei ya juu. Mfano majengo yaliyonunuliwa ya *Ubungo Plaza* na *Quality Plaza,* ukitaka kuyauza sasa baada ya mwaka mmoja, huwezi kupata hata nusu ya bei uliyonunulia. Hivi nani kasema biashara ya ujenzi wa majumba na maofisi ya kupangisha, itakuwa biashara nzuri kwa miaka ijayo?

Naomba pia ufafanuzi, wananchama watafaidika je na ujenzi wa daraja la Kigamboni? Fedha yao itarudishwa kwa njia gani na kwa faida?

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, kwa kuja na hotuba nzuri sana, iliyojaa mikakati sahihi ya kuendeleza majukumu ya Wizara.

Ombi langu kubwa ni kwa Wizara kujipanga vizuri kabisa ili yaliyoelezwa kwenye hotuba hii, yaweze kutekelezwa kikamilifu. Wananchi wanasubiri kwa hamu, *outputs* za hotuba hii. Ahadi ya CCM kwa Watanzania kubwa iko humu. Wasiwasi wangu tu ni iwapo Wizara itatekeleza inayoyaeleza, kwa kiwango gani; kwa asilimia 40, asilimia 60 au kwa asilimia 80? Nitafurahi sana iwapo utekelezaji utafikia asilimia 80. Hii ni changamoto iliyoko mbele yenu.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la heri na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari na Mheshimiwa na Daniel N. Nsanzugwanko, Naibu Mawaziri wa Wizara hii, kwa kazi nzuri waliyoonesha katika utekelezaji wa majukumu ambayo Wizara hii imepewa katika Serikali ya Awamu ya Nne.

Kwa ufupi naomba niseme yafuatayo: Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* ni kitengo muhimu sana, kama kitaandaliwa kukabili majukumu yake kwa ufanisi na kwa upana unaolingana na malengo yaliyowekwa na Serikali. Malengo ya sasa ni finyu, madogo sana na kwa kweli sioni namna gani watachangia kwa kiwango kinachotakiwa na malengo ya Awamu hii ya Nne. Mafunzo ya uongozi 80, tafiti nane katika maeneo ya kuondoa umaskini, ni malengo finyu mno. Naomba maelezo ya Serikali.

Mahakama ya Kazi ina majukumu azimu, lakini inalalamikiwa sana na watu wengi, ambao kwa namna moja au nyingine, wamehitaji huduma ya Mahakama hiyo. Imelelamikiwa kwamba, maamzui yanachelewa na mara nyingi wafanyakazi wa kipato kidogo, wana nafasi ndogo ya kupata haki inayostahili. Ni chombo gani ambacho kina jukumu la kusimamia utekelezaji kwa ukamilifu wa kazi za Mahakama ya Kazi? Naomba maelezo.

Katika ukurasa wa 41 mpaka 42 wa kitabu cha hotuba ya Waziri, amesema Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* litakusanya shilingi 208.7 kutoka vyanzo vyake na itawekeza katika sehemu mbalimbali za kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na JWTZ, Polisi, *TRA*, ujenzi wa nyumba nyingine na sekta binafsi. Hata hivyo, Kamati ya Maendeleo ya Jamii katika Taarifa yake inasema, kuna matatizo katika utoaji wa mikopo na hivyo kuishauri Serikali, iangalie upya Mikataba ya Mikopo ya *NSSF.* Naomba maelezo, matatizo hayo ni yepi? Je, kwa nini Serikali hakizungumzia matatizo ya utoaji wa mikopo katika hotuba ya Waziri?

Naomba Waziri, anipe maelezo ya kina ya mafanikio au hasara ya sera za uwekezaji unaofanywa na *NSSF?*

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. CASTOR R S. LIGALLAMA:** Awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, Manaibu wake na Katibu Mkuu, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, asilimia 60 ya wananchi wetu ni vijana. Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu cha CCM, imeahidi kuibua ajira milioni moja katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kwa kiwango kikubwa, mwajiri mkubwa wa nchi hii ni kilimo. Kama Serikali itaweka mkakati mzuri wa kupata maeneo kwa ngazi ya vijiji au kata na kuweka kila tarafa matrekta mawili, *harrows* mbili na *planters* mbili, kwa ajili ya kuhudumia maeneo hayo ya vijana, kwa kiwango kikubwa tutakuwa tumewaajiri vijana. Kwa mfano wa Wilaya yangu yenye tarafa tano, tutahitaji *tractors* kumi, *harrows* kumi na *planters* kumi. Makao Makuu ya Wilaya, pajengwe *Farm Service Centre,* ambako matrekta hayo yatakuwa yanafanyiwa *service* na *repair*. Kila kijana angalau alimiwe hekta moja (ekari mbili na nusu). Kwa kufanya hivi, tutakuwa tumewaajiri wananchi kwa maana ya vijana wengi kwa wakati mmoja. Napendekeza zoezi hili, lifanyike kwa kutegemea mazao yanayostawi katika maeneo husika. Kwa mfano, Mikoa ya katikati ya nchi, ilime mtama wenye kustawi kwa mvua chache.

Mheshimiwa Spika, vyama vya kuweka na kukopa, ni vichocheo vikubwa vya uchumi katika vijiji vyetu. Serikali inaweza kuwasaidia vijana kwa kuwaongezea mtaji juu ya mtaji wao wenyewe. Ni vyema vyama hivi vikaanzishwa na vijana wenyewe, kuondoa fikra kwamba, Serikali imewapa ruzuku. Serikali iwaongezee fedha kwa njia ya mkopo ili kuwajengea vijana dhana ya uwajibikaji. Benki pia zinaweza kusaidia vyama

hivi kwa kuongeza mkopo zaidi. Katika Wilaya yangu, *SACCOS* zilizo kwenye mashamba ya miwa zimefanikiwa sana, kwani hukopa fedha toka kwenye Benki na wao huwakopesha wakulima wadogo wa miwa *(outgrowers),* kwa ajili ya kuendeleza zao la miwa.

Mheshimiwa Spika, biashara ndogo ndogo ni sehemu pia ambayo inaweza kuajiri vijana wengi, ambao hivi sasa wanazunguka mitaani wakiuza biashara mbalimbali (Machinga). Wale wenye maeneo (vioski), wawezeshwe ili waweze kukuza biashara zao.

Mpango huu wa Kuondoa Umaskini na Kukuza Uchumi ni ukombozi kwa vijana, kama wataibua miradi mbalimbali huko vijijini. Mkazo mkubwa katika utekelezaji wa MKUKUTA iwe ni kutilia mkazo vijana wengi kubaki vijijini. Serikali ijielekeze katika kuweka miundombinu muafaka, kama vile umeme kupitia Mpango wa *Energization Rural Transformation (ERT)*, maji, barabara na kadhalika.

Kwa kuweka miundombinu hiyo, kutachochea viwanda vidogo vidogo katika vijiji hivi na kutazuia ile hali ya sasa ya vijana kukimbilia mijini kutafuta ajira.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, pamoja na Naibu Mawaziri wake; Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari na Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, pamoja na Katibu Mkuu Dr. Ladislaus Komba, Naibu Katibu Mkuu na watalaam wote, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri katika maeneo machache, utaratibu wa mfuko wa uwezeshaji wajasiliamali wa wastani wa shilingi milioni 500 kila Mkoa. Katika hotuba ya Waziri, sikusikia nafasi ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Je, tulisahaulika au hatupaswi kuwa wajumbe kwenye Kamati hiyo?

Usalama na afya mahali pa kazi *(OSHA)* katika kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Afya na Usalama mahala pa kazi ni vizuri yafuatayo yazingatiwe:-

Umuhimu wa kuweka maeneo mazuri na salama kwa ajili ya wafanyakazi kupata mapumziko na chakula cha mchana. Kuvitaka viwanda/makampuni, kuweka vituo vya watoto wadogo *(crèche)* ili wanawake wanaofanya kazi katika kiwanda/makampuni wafanye kazi zao bila wasiwasi wa usalama wa watoto wadogo hasa umri sifuri mpaka miaka sita, umri sifuri mpaka miaka mitatu na/au miaka mitatu mpaka sita. Vituo hivi vitasaidia kuendeleza malezi, makazi na maendeleo ya awali ya mtoto, kusaidia akina mama kunyonyesha watoto wao. Mfano mzuri ni kiwanda cha *A to Z* ambapo asilimia 92 ya wafanyakazi wote ni wanawake.

Kuvitaka viwanda/makampuni kutenga maeneo au kuwa na mkataba na *centres* zinazotoa huduma ya mazoezi/*gymnasium* kwa ajili ya afya zao, kuendelea kutoa ushauri nasaha na misaada kwa wafanyakazi waathirika wa Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia tena kwa maandishi bajeti hii ya Wizara ya Kazi Ajira na Maendeleo ya Vijana. Nampongeza Waziri na Naibu Mawaziri na watalaamu, kwa matayarisho ya hotuba hii ya mwelekeo wa maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu vijana ni wengi sana na ndio nguvu kazi ya nchi yetu. Lakini jambo la kusikitisha, vijana wengi hawana ajira, pamoja na Wizara kusaidia ajira sekta hii, lakini tatizo bado lipo.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inatafuta mipango ya kusaidia vijana, kuna wimbi kubwa la Wachina, wanafanya kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya mfano, kuuza viatu, mapazia, maua na kuitana wenyewe kufanya kazi hizo na vijana wachache ndio wanawaajiri kuwa walinzi au kubeba mizigo. Je, hawa ndio wawekezaji tunaohitaji na pia usalama na afya zao mahali pa kazi wakala *(OSHA)*, amewafanyia ukaguzi na uchunguzi wa afya Wachina hawa ili kunusuru taifa na janga la maradhi?

Mheshimiwa Spika, vijana wapewe elimu mara kwa mara ya ujasiriamali ili kukidhi haya ya matumizi ya fedha wanazopewa ili kuondoa hatari ya kupoteza fedha hizo, ikizingatiwa hawa ni vijana, matumizi yao makubwa.

Mheshimiwa Spika, Machinga vijana hawa hawa wa Kitanzania wanayumba sana. Je, Wizara ya Vijana ina mikakati gain, kuhakikisha vijana hawa wanapata maeneo ya kudumu ili kuondoa unyanyasaji wa mara kwa mara na hata kuhatarisha usalama na kunyang'anywa mali zao? Vijana wa vijijini, waandaliwe mazingira mazuri ili wasishawishike kuja mijini.

Napenda kupendekeza kuwa Serikali itenge maeneo ya mashamba makubwa na kusaidia matrekta ya kisasa na watalaamu sambamba na vitendea kazi na elimu, vijana hawa wanaweza kupunguza kuelekea mijini na wakapewa masoko ya kuuzia bidhaa zao. Madawa ya kulevya na Ukimwi yamewaathiri sana vijana. Wameadhirika na majanga haya pamoja na jitihada kubwa za Serikali, lakini tukiri tatizo hili ni kubwa na Serikali itoe elimu zaidi mijini na vijijini na kwenye mashule. Napenda kutoa pendekezo, wanafunzi wapimwe wakiwa mashuleni itawafanya watoto waogope na kuwa waangalifu, kwa kuhofia aibu ya kujulikana ugonjwa huu na madawa ya kulevya. Wawekewe kambi ambayo itakuwa inawahudumia wale waathirika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuwa mmojawapo wa kuchangia kwa maandishi kwenye hoja hii ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwanza, naipongeza hotuba hii ya Waziri kwa maelezo ya uwiano kwenye kitabu hiki.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia kwanza, kwa niaba yangu na wananchi wangu wa Jimbo la Mwakwerekwe, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Wizara hii ina kazi kubwa sana na hasa kwa kuwa inashughulikia ajira pamoja na maendeleo ya vijana. Kwa sababu vijana wote hivi sasa wanaitegemea Wizara hii, kwa ajira na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Wizara hii hivi sasa, kujipanga vizuri sana kwa kuwawezesha vijana kiajira na maendeleo. Ukurasa wa 35 wa kitabu cha Hotuba ya Waziri, unaelezea kuhusu maendeleo ya vijana. Pia unaelezea kukuza ajira, kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)*, mpango huu ni lazima usimamiwe vizuri sana hasa ilivyokuwa ni jambo la mkopo. Yatolewe mafunzo ya uhakika kwenye vikundi hivyo ili visije kufilisika.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Wizara hii, aangalie wananchi wanaoajiriwa na wafanyabiashara binafsi madukani, migahawani, mahotelini na kadhalika. Matajiri hao huwa wanawanyanyasa vijana wanao waajiri kwa kuwapa kazi kubwa na malipo huwa madogo sana. Pia waajiri hao huwafukuza vijana hao makazini bila ya mpango wowote. Kwa hiyo, kuwe na sheria ya kuwalinda wafanyakazi wanaoajiriwa na matajiri.

Mheshimiwa Spika, nategemea kuwa Wizara hii itafanikisha vizuri sana ili kuitekeleza Ilani ya uchaguzi 2005 – 2010 na utekelezaji wa Sera ya Chama cha Mapinduzi. Pia nategemea kuwa Wizara hii itawalinda vijana wetu wanaoajiriwa na matajiri sehemu mbalimbali wasinyanyasike ovyo. Ule mpango wa kuwafanyisha kazi vijana au wananchi kwa muda mrefu, baadaye kuwafukuza ghafla na bila malipo waondoke mara moja ili wafanye kama hao matajiri wao wawalipe mafao yao ya muda waliofanya kazi. Lazima haki itendeke. Ahsante.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze sana kwa hotuba zenu nzuri na za ufasaha, nampongeza Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe. kwa hotuba nzuri. Pia namshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, kwa kuitembelea Wilaya yetu ya Njombe na kutusaidia *Ubena SACCOS* kusajiliwa.

Sambamba na hilo, ningeshauri sana utusaidie kuanzisha na kusajili *SACCOS* kila kata za jimbo langu; yaani Usuka, Mdandu, Imalinyi, Saja, Ilembula, Luduga, Wangame, Wanging’ombe, Mdandu. Tukifanikiwa hilo, vijana wataondokana na tatizo la ajira kupata kipato. Tatizo kubwa liko kwa Afisa Ushirika, Ndugu Konjumu, yeye ni kikwazo wa ushirika kwenye jimbo langu, amejikita kwenye siasa za makundi. Hivyo, ningeshauri ahamishwe na amekaa muda mrefu sana. Vijana wako mstari wa mbele kupenda ushirika. Mimi kama Mbunge wa Njombe Magharibi, nitajitahidi kuhamasisha vijana kwenye michezo ili vikundi hivyo viwe kwenye vikundi vya uzalishaji mali.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii. Kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Wizara hii, pamoja na Naibu Mawaziri wake, kwa kazi kubwa ambayo wanayo.

Kwanza kabisa, niko upande wa ajira. Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alitamka ajira kwa vijana na vijana wengi waliamua kujiajiri kwa sababu ya kujiondolea umaskini.

Sasa baada ya kujiajiri, Halmashauri za Miji, zimekuwa vikwazo kwa vijana hawa. Hivyo, naiomba Wizara hii ifanye kazi kwa uangalizi wa karibu na Halmashauri hizo, kwani ni kikwazo kikubwa. Mfano pale ambapo vijana wa kike, wanapoamua kujiajiri kwa kufungua *saloon* ili kupunguza ukali wa maisha, Halmashauri hufika na kubomoa vibanda hivyo. Matokeo yake ni wasichana hawa kujiunga na biashara ya ukahaba, angalieni hili ni mojawapo ya ongezeko la gonjwa la Ukimwi.

Naomba Wizara hii iangalie sana, isije ikawa badala ya ajira, ikawa ongezeko la Ukimwi. Hili naliona katika Jiji la Mwanza, kutokana na manyanyaso ambayo vijana hao hupata, wengi huamua kula unga, kuvuta bangi na hata wengine kuwa vibaka na kuwanyang'anya akina mama mikoba yao.

Hivi karibuni nimesikia redioni vijana wa pikipiki katika Mji wa Mwanza na Bukoba wakipigwa marufuku biashara hiyo. Je, hawa vijana waende wapi au wafanye kazi gani, ambapo pikipiki hizo wamenunua kwa mikopo toka *PRIDE* na *FINCAR*, je, watarudishaje mikopo hiyo? Hawa watakuwa ni ongezeko la waharifu. Tunaiomba Wizara, itupe msimamo na nini wamekiandaa kuhusu vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo la rushwa kwa wanaoomba kazi, mtu anaweza kukidhi vigezo vyote na akakosa pesa za rushwa, kijana huyu hatopata kazi na akija kijana ambaye hakidhi vigezo kama ana pesa tu na akaamua kutoa rushwa, basi anapata ajira. Kumekuwepo pia na rushwa ya ngono kwa watoto wa kike. Kama hawezi kutoa ngono hata kama ana vigezo vya kukidhi hapati kazi, matokeo yake kama kuna binti anayeweza kutoa rushwa ya ngono basi atapata kazi, hata kama hana vigezo vya kukidhi. Tunakuwa na vijana wanaofanya kazi katika ubabaishaji na kushindwa kumudu kazi zao. Wizara ilione hilo kwa mapana yake. Wapo vijana ambao wamemaliza kidato cha sita lakini wamo mijini tu wanazagaa, wamo waliomaliza hata kwa *division one* ya *point nine,* lakini hawana la kufanya na hata wengine kuwa makondakta wa daladala. Tunaiomba Wizara, iweze kutoa elimu kwa vijana ili waweze kujua nini cha kufanya baada ya elimu yao.

Mheshimiwa Spika, nawatakieni kazi njema katika Wizara hii ngumu, kwani hata katika viwanda vya samaki vilivyoko katika Jiji la Mwanza, vijana hufanya kazi ngumu na kiwango cha malipo ni kidogo sana. Wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo Mwanza, wengi hulalamikia ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi, kama wale wanaofanya kazi katika mashine za kuchambua pamba, hawana vifaa vya kuvaa puani kuzuia vumbi la pamba na mapato yao ni madogo.

Tunaomba Wizara ifuatilie suala hilo na kubaini kama ni kweli. Kama ni kweli, Wizara ichukue mkondo wake wa kufanya kazi vijana hao bila vifaa vya kinga.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MADGALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Wizara hii ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Manaibu wake, pamoja na wataalam wao, kwa kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, suala la kukosekana kwa ajira kwa vijana wa Tanzania ni tatizo kubwa. Cha kusikitisha kila mwaka vijana wanaongezeka na mpango kabambe wa kuwatafutia ajira bado.

Mheshimiwa Spika, tunao vijana waliohitimu elimu kwa fani mbalimbali kutoka vijijini. Wameweka vyeti vyao pembeni wapo vijijini, wanavuta bhangi na madawa ya kulevya. Nguvu tunayoipoteza ni kubwa sana ambayo ingesaidia maendeleo ya Taifa hili changa. Serikali iweke mikakati, itambue vyema ni vizuri kutumia ujuzi, ufahamu, uelewa na utaalam wa vijana hawa, wanaosomeshwa kwa fedha nyingi za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaoshinda vijiweni wakipiga zogo, kuvutia bhangi na madawa ya kulevya, wanahitaji kula, kulala na kuvaa; huduma hii waipate wapi, sio kwamba usiku ndio wanaovunja nyumba za raia na kuvamia watu?

Mheshimiwa Spika, ni muda muafaka Wizara ikae na kusaidia kuondoa tatizo hili kubwa.

Mheshimiwa Spika, kituo cha kutafuta ajira kwa vijana kilichopo Dar es Salaam, kinasaidia sana vijana wengi. Naishauri Serikali kuweka kituo kama hiki huko mikoani pia, kwani si vijana wote wenye uwezo wa kusafiri hadi Dar es Salaam. Pia kituo hiki kiboreshwe kwa kupatiwa vitendea kazi ili kurahisisha utendaji wake. Wakati mwingine inachukua miaka hadi mitatu tangu kujiandikisha, ndipo wanakujulisha kuhusu *progress* yoyote kuhusiana na ombi lako.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* inasaidia wafanyakazi kujiwekea akiba ya maisha ya baadae pale anapopumzika kazi au kupata tatizo kazini. Fedha inayoachwa *NSSF* ni sehemu ya mshahara wa mfanyakazi na sehemu aliyowekwa na mwajiri wake.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pale fedha ya Mfuko huo inapotumwa kuwekeza mahali popote, wenye mali wafahamishwe na wafaidike na uwekezaji huo. Fedha hizo ni haki yao, kuweka mambo wazi kuona itasaidia kujenga imani na Shirika hili muhimu na pia itaondoa taswira ya kuonekana kwamba, Mfuko huu ni wa kikundi cha watu fulani.

Mheshimiwa Spika, wapo wafanyakazi wa Sekta Binafsi, ambao hawapo kwenye Mfuko huu, hawalipwi *NSSF* kwa miaka mingi. Matokeo yake wanawanyima haki hii ya msingi na wafanyakazi wengine hawajui suala hili na wengine wanaogopa kutoa siri kwa kuhofia ajira zao. Naomba Wizara ifuatilie Mashirika haya na Sekta Binafsi, watoe haki kwa wafanyakazi wao. Pia mishahara wanayopewa hawa *Staff* wa *Private Sectors* hailingani na kazi wanazozifanya. Wapo wanaolipwa shilingi 20,000/=, kima cha chini cha mishahara kwa mwezi. Tunaomba Serikali ifuatilie wafanyakazi hawa ambao ni wengi sana.

Mheshimiwa Spika, suala la kustaafu kwa wafanyakazi Serikalini nalo ni tatizo. Watu hawataki kuacha nafasi hizo. Serikali imeweka kiwango cha miaka ya kustaafu kwa watumishi wake. Ningependa kujua Wizara/Serikali, inafahamu kama wapo watu wamefoji *(backdate)* miaka yao ili waendelee kuwepo kwenye ajira kwa muda zaidi? Ikiwa hili halitafutiwi dawa ni kwa namna gani vijana wanaohitimu masomo watapata kazi?

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kabisa, ninaomba nitoe pongezi zangu za dhati kabisa, kwa kazi nzuri na mikakati ambayo kwa muda mfupi Wizara imeweza kupanga na mingine kuwepo kwenye hatua za utekelezaji, nikianza na Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote.

Baada ya pongezi zangu nzito, ninaomba kwa kuwa ndio kwanza hii timu ya wachapakazi imeanza kazi na kuweka mikakati kabambe ya utekelezaji, nitoe ushauri wangu wa jumla kwa Wizara kuwa ili yaliyokusaidiwa yatimie na kuonekana, Wizara iwashirikishe Waheshimiwa Wabunge wote, hasa wa Majimbo, kwenye mikakati yote ili Waheshimiwa Wabunge nao waweze kuwashirikisha Waheshimiwa Madiwani kwenye Halmashauri zao, kwani ndio wanaofahamu maeneo ya kipaumbele kwenye Kata zao.

Pia ninashauri Wizara iwe inajitangaza na kuelezea kwa umma, yale yanayofanywa na Wizara hii, kwani kuna mengi mnayoyafanya na kupanga, ambayo yana *impact* kubwa sana kwa jamii ili yafahamike na kueleweka vizuri kwa jamii yote ya Watanzania. Hongereni kwa kitabu cha hotuba ya bajeti, ambacho kimesheheni mipango mizuri.

Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya na Jimbo la Hai, ninawakaribisheni Hai na kuwaahidini ushirikiano wetu daima.
Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri na Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki. Ahsanteni sana.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Wizara hii.

Napenda kujua Wizara ina mkakati gani kuhakikisha kuwa, vijana wanakukuza kipato chao na upatikanaji wa ajira kama Rais alivyoahidi, atatoa ajira milioni tano, kila mwaka ajira milioni moja. Kwa kipindi cha miezi saba ni vijana wangapi wameajiriwa? Napendekeza vijana wakusanywe ili waundiwe ushirika na kupewa mkopo mkubwa ili waweze kujiendeleza.

Ajira isichague chama, vijana wote waajiriwe kwa mujibu wa uwezo wao. Pia tunapendekeza ianzishwe Benki ya Vijana ili vijana waweze kupata mikopo ya riba nafuu.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru *Allah Subuhanahu-wataalah,* kutujalia tukiwa wazima na salama.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili la Hifadhi ya Jamii, ninalipongeza sana kwa kazi nzuri linazozifanya kwa kukusanya fedha za wafanyakazi. Lakini mimi ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri katika michango hiyo ya Wafanyakazi hao wanayoitoa, ni kiasi gani wanavyofaidika nayo au faida yao ni pale wanapokoma kuwa wafanyakazi na kupewa pensheni zao tu? Ikiwa ni hivyo, basi naomba kwa kuwa michango yao inatumiwa kwa kufanyia kazi nyingine na inapata faida, Shirika liangalie faida hiyo na ikiwa kubwa wapatiwe gawio.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ajira, napenda kuchangia kuhusu namna watu wanavyoajiriwa hasa hasa katika Sekta binafsi. Bahati nzuri mimi ninakaa *guest* na ninakula chakula kwenye migahawa na huwa napenda kudadisi baadhi ya wafanyakazi na kuona malipo wanayolipwa. Inasikitisha mtu anaingia kazini saa 12 asubuhi mpaka usiku saa sita, analipwa shillingi elfu moja, wengine wanalipwa shilingi mia saba na wengine mia nane. Walinzi wa magesti nao wanalipwa shilingi 24,000/= kwa mwezi, yaani mia nane kwa siku, usiku kucha na baridi.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali haiwezi kuweka kima maalum kwa wafanyakazi hawa wa Sekta Binafsi nilizozitaja . Mheshimiwa Waziri naomba maelezo kwa hili. Ahsante.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii kwa kutoa ushauri ufuatao:-

- Wizara iweke mikakati madhubuti ya kuweka kipaumbele katika kuwawezesha vijana wengi walioko Vijiji zaidi ili kupunguza wingi wa mrundikano wa vijana wasio na ajira rasmi mijini. Mfano, kupeleka vitendea kazi kama vya kilimo, viwanda na kadhalika kama matrekta na kuwawezesha kimasoko. Pia Wizara ihakikishe miundombinu inapatikana kwa nguvu zote vijijini, kama barabara, umeme, simu na kadhalika.

- Serikali iweke Sikukuu Maalum ya Vijana Kitaifa na kila Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata zishirikishe vijana kuonesha shughuli wanazofanya na mafanikio yao. Kuwe na ushindani na zawadi zitolewe. Iwe kama ilivyo Maonesho ya Sabasaba au Nane Nane. Hii itawafanya vijana wengi kujituma kufanya kazi. Hii ijumuishe na vijana wote walioajiriwa katika fani ya biashara, wakulima, wafugaji, ufundi, sanaa mbalimbali na kadhalika kuwe na motisha.

- Maafisa Ushirika watoke maofisini waende kwenye Kata na Vijiji kufanya Mikutano ya Vijana ili kutoa Semina mbalimbali kwa kuwaelewesha nini cha kufanya katika kujikwamua toka hali ngumu ya uchumi kwa kutumia fursa hii ya ongezeko la kujiajiri.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Waziri wa Wizara hii, Manaibu wawili; Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri na Manaibu wake ni dhahiri kabisa Rais katika uteuzi wake amepatia kabisa kuwapa wazalendo, ili kusimamia Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni tegemeo kubwa kwa Watanzania, hususan kundi kubwa la Vijana wanaosubiri ari, nguvu na kasi, wataletewa Mipango na Mikakati ya Kuwawezesha wajiajiri wenyewe; wasimamiwe katika Elimu ya Kujitegemea; wasimamiwe ajira; wasimamiwe katika masomo yao; Shule za Msingi; Shule za Sekondari na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, Waziri katika hotuba yake, ametoa majukumu ya Wizara yake
kama ifuatavyo:-

- Jukumu la Maendeleo ya Vijana ni Kubuni na Kusimamia Sera na Taratibu zinazojenga mazingira endelevu.

- Jukumu la Idara ya Utawala na Utumishi ni kuajiri, kusimamia utendaji kazi, masuala ya jinsia, kutoa mafunzo ya utendaji kazi; kupambana na rushwa na ugonjwa wa Ukimwi.

- Jukumu la Msajili ni kusimama na kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri na kadhalika

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara zinazotegemewa huduma zake kwa jamii kubwa, ambao ni jamii, wanawake na vijana. Naomba Wizara hizi, zilete Mikakati na Mipango Endelevu kwa mambo yafuatayo ili mwaka 2007/2008 tusije kuwahoji tena:-

- Baada ya ubinafsishaji, watasimamiaje kulinda ajira za Watanzania kwa Viwandani Migodini na Ofisini ili vijana wetu wasomi waajiriwe.

- Migogoro katika maofisi sasa iangaliwe kwa kulinda Utaifa wetu, si kupendelea watu wa nje na kubeza vijana wetu.

- Vyama vya Wafanyakazi vipewe meno katika kuhoji sheria zilizotungwa, zilindwe na ziheshimiwe wakati wanatetea haki za wafanyakazi.

- Mahakama za Kazi, zitumie muda mwingi katika kuona haki za waajiriwa si kuegemea tu kwa waajiri

- Wafanyakazi Waheshimiwe kwa jinsia elimu ukizingatia tuna vijana wetu wengi wanahitimu Vyuo Vikuu, Serikali haiwatumii, matokeo yake wameenda nje ya nchi.
- Wizara ilete Mpango wa kuwaweka sawa vijana au maandilizi mazuri mara wanapohitimu masomo yao vyuoni, Serikali inawatumiaje?

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri atumie muda mwingi, kutoa elimu kwa vijana kuwa ajira si kuajiriwa tu na Serikali. Elimu hii itasaidia kuwaandaa toka Shule za Msingi hadi Vyuo Vikuu hivyo, watakuwa tayari wamejiandaa wao wenyewe badala ya kusubiri ajira toka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, lakini bado ni jukumu la Wizara kuhakikisha ajira zote ziwe chini yao na wahakikishe nafasi zote zinagawanywa sawa hadi vijana wanatoka mikoani (vijijini), ukizingatia kuwa vijana wengi wanafikiri ajira ziko Dar es Salaam tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii bado inajipanga vizuri, naomba niishie hapa lakini mwaka ujao wa 2007/2008, nitataka walete utekelezaji, ni jinsi gani vijana wamewatoa katika hali ya kucheza kamali, bao saa za asubuhi limekomeshwa, vijana wawe wameandaliwa katika kuwekwa katika vikundi ili wakopesheke na maandalizi ya ajira kwa vijana wanapomaliza Vyuo Vikuu na Vyuo vya Taaluma na Ufundi wanalindwaji katika kutumia taaluma zao Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, wapewe fedha hizi zote, ili waokoe vijana wetu. Nawatakia kazi njema.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza sana kwa hotuba yako nzuri, yenye ufafanuzi mzuri wa Wizara yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo: Bajeti iliyotengwa ni kidogo sana kwa Wizara hii, ambayo ina majukumu makubwa na muhimu.

Naiomba Serikali ipeleke Maafisa wa Kazi kila Wilaya na kuwapatia vitendea kazi vya kutosha, ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa ambayo haina Afisa wa Kazi wa Wilaya. Afisa wa Kazi atasaidia sana kutatua migogoro ya kikazi katika Wilaya zetu.

Vile vile naiomba Serikali ihakikishe ajira ya mtoto inakomeshwa ili watoto hao wapate elimu itakayowasaidia kujiajiri.

Serikali ihakikishe waajiri wote hasa wa Sekta Binafsi, wanawalipa wafanyakazi wao ujira/mshahara unaolingana na kazi wanazofanya. Pia ihakikishe kuwa wafanyakazi hawanyanyaswi katika maeneo ya kazi Serikalini na katika Sekta Binafsi.

Kwa kuwa migomo hutokea katika maeneo ya kazi, je, migomo hii husababishwa na nini, uongozi mbovu au maslahi duni? Serikali imeweka mikakati gani kumaliza migogoro hiyo kwa kushirikiana na Vyama vya Wafanyakazi?

Hivi karibuni Julai, 2006, Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, aliitembelea Wilaya ya Mpwapwa na kuzungumzia vikundi mbalimbali vya uzalishaji, tunamshukuru sana kwa ziara hiyo. Ushauri wangu ni kwamba, shilingi milioni 500 zilizotengwa kila mkoa, ziwafikie walengwa na vijana, wazee na walamevu ambao wameunda vikundi vya uzalishaji ambao na hata mtu mmoja atakayetimiza masharti ya mkopo. Mfuko huu ni *Revolving Fund,* wanakopa na kurejesha mikopo. Mpwapwa Mjini, Ving'hawe na Mwanakyanga, kuna vikundi mbalimbali vya uzalishaji, useremala, wauza mboga, wenye migahawa, *saloon* na watengeneza baiskeli, wapewe mikopo ili kuendeleza biashara zao na kuondokana na umaskini. Katika shilingi milioni 500 zilizotengwa, asilimia ngapi kwa vikundi vya vijana?

Mfuko wa Vijana katika Halmashauri za Wilaya, je, Serikali itaendelea kuchangia mfuko huo?

Ajira za Vijana 1,000,000; je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha kuwa ajira hizo zinapatikana Serikalini, kilimo, wawekezaji na wataajiri asilimia ngapi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, asilimia 70 ya wananchi wa Tanzania ni vijana, lakini *nataasaf* kusema kwamba, bado Serikali haijawaandalia vijana mazingira bora ya kufanya kazi/kujiajiri. Kundi kubwa hili la vijana mara nyingi huwa tunalihitaji katika nyakati maalum na hasa wakati wa uchaguzi. Serikali huwakusnya vijana wengi wakati huo na kuwaahidi ajira na baada tu ya shughuli ya uchaguzi, vijana hao tunawaacha bila ajira na pia kutowajali. Hii hupelekea vijana wetu kujiingiza katika mambo ya uzururaji, ubakaji na ufuska wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Miji nazo huwa chanzo kuwafanya vijana waendelee kuwa wazururaji na kubaki na umaskini, kutokana na kwamba vijana huwa wamejiajiri kwa kufanya biashara zao ndogondogo, kama vile mamantilie kujenga vibanda vya biashara, lakini Halmashauri huvunja vibanda hivyo, kumwaga biashara za, kuwapiga na kuwadhalilisha bila kuwaandalia mazingira mahsusi ya kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, tusiondoe kabla kuweka, tuwatayarishe vijana kabla hatujawaathiri.

Mheshimiwa Spika, hiki ndiyo chanzo cha ukahaba, wizi, uporaji na mengine, kujiingiza katika madanguro na kupelekea kuathirika na janga la Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, vijana ambao wamekopa kwenye mashirika yanayotoa mikopo na kujinunulia pikipiki kwa ajili ya biashara, tumesikia redioni kwamba, kule

Mwanza biashara hizo zimepigwa marufuku. Nia ya vijana hao ni kujiongezea kipato na kujiondoa katika umaskini. Je, vijana hao tunategemea waende wapi na wafanye nini wakati Serikali inawarudisha nyuma. Hatuoni kwamba, vijana hao wanaweza kujiingiza katika biashara nyingine za ajabu ajabu na wengine kulazimika kuondoka nchini, jambo ambalo ni hatari kwa Taifa letu, kwani Taifa bila vijana, ambayo ndiyo nguvu kazi ya Taifa, si Taifa imara.

Mheshimiwa Spika, Taifa liendelee kuimarisha ujenzi wa vyuo vya ufundi kwa ajili ya vijana na nafasi zitolewe kwa wote ili tuwadhibiti vijana wetu wasijiingize katika vitendo viovu na pia wapewe nyenzo za kujiajiri wanapomaliza mafunzo yao.

Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu gani wa kusajili hivi vikundi, kwani kuna baadhi ya maeneno kuna idadi tu lakini hawaonekani washiriki (wanawake/wanaume) haukufanywa utafiti wa kina?

Mheshimiwa Spika, uzinduzi wa miradi wakati wa mbio za mwenye 2005, je Wilaya ya Wete hakuna mchango wowote?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuipongeza Wizara hii, hasa Waziri wa Kazi na Naibu Mawaziri wake wote wawili, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi ya CCM inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kuwa na mkakati maalum kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, kuweka msukumo na kipaumbele kuhusu elimu ya umuhimu wa kufanya kazi katika jamii.

Mheshimiwa Spika, walimu wana nafasi kubwa ya kuweza kuwafundisha watoto hawa, kwani wanaweza wakaamua kutumia utaratibu wa kuweka siku moja kwa wiki na kutumia magazeti au mtaalam yeyote, anayeweza kufika katika shule na kutoa mada kuhusu masuala ya ajira au kujiajiri mwenyewe ili iwe chachu kwa vijana ambao wataamua kujiajiri wenyewe baada ya masomo. Suala hili linaweza kutekelezwa katika ngazi zote za utoaji wa elimu kuanzia shule ya msingi darasa la tano hadi sekondari. Litawasaidia kuwapa mbinu na uzoefu mbalimbali wa jinsi ya kujikwamua na hali mbalimbali katika kukabiliana na umaskini katika ngazi zote.

Elimu hii ya vitendo pia itasidia kujenga imani kwa vijana kuwa, wanaweza kujiajiri wenyewe, kwani hali halisi iliyopo hivi sasa, inaonesha kuwa vijana wengi wanaogopa *risk* ya kuamua kuanza kufanya kazi yoyote ya uzalishaji bila kuwa na uhakika wa soko la bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii. Napenda kumpongeza Waziri, kwa hotuba ya Wizara yake aliyoitoa hapa Bungeni. Pia nawapongeza Naibu Mawaziri wake na Wataalam wa Wizara, kwa ushirikiano wao ambao umewezesha na kufanikisha hotuba hii ya Bajeti kusomwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nianze naa tatizo la ajira kwa vijana, ambalo ni kero kubwa sana kwa nchi yetu hii. Tatizo hili la ajira linatusumbua sana sisi Wabunge vijana, tunapokutana na hawa vijana katika maeneo tunayotoka, malalamiko ni mengi sana na wanaona kama sisi tumeridhika na hatuwajali.

Mheshimiwa Spika, hata wale ambao wana elimu nzuri na wana uwezo wa kufanya kazi ambazo zinakuwa zimetangazwa katika vyombo vyetu vya Habari kama Magazeti, bado wanashindwa kuzipata kutokana na kigezo cha uzoefu katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kigezo hicho ni kumnyima haki kijana huyu wa Kitanzania, ambaye alisoma kwa bidii akiwa na mategemeo ya kupata ajira. Mimi bado najiuliza hivi vigezo vitatoka wapi bila vijana kupata ajira ili waweze kuonesha uwezo wao? Naomba hili litazamwe.

Ajira kwa Wageni bado ni tatizo. Zipo kazi ambazo Mtanzania wa kawaida, anaweza kufanya mfano katika mahoteli ya kitalii, utakuta kuna wafanyakazi kutoka nje ya nchi, ambao wameletwa kwa ajili ya kuosha vyombo na kutandika vitanda. Hivi kweli kazi hizi Mtanzania anashindwa kuzifanya na wapo Watanzania wenye fani hizo lakini wakienda kwenye hoteli hizo, hawapewi kazi. Hilo nalo tunaomba litazamwe kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nami napenda kuipongeza Serikali kwa hutoa shilingi milioni 500 kwenda katika kila Mkoa, ila nina waiwasi na haya yafuatayo: Utaratibu wa mgao wa fedha hizo utakavyokuwa, maana tumeona ile ya wananchi ilivyokuwa inatolewa kwa ubaguzi wa itikadi za vyama na wengine ambao ni viongozi, walitumia vibaya nafasi zao kwa kuwapa wake zao, ndugu zao na hata marafiki na kuwakosesha walengwa mikopo hiyo. Hivyo, tunaomba Wizara itoe taratibu hizo mapema ili Wabunge waelewe na waweze kuhakikisha taratibu hizo zinafuatwa na wale watakao kiuka, wachukuliwe hatua kali za kinidhamu ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kufanya *Youth Mapping* katika Wilaya ya Ludewa, shughuli hiyo inaelekea kutokukamilika. Je, ni nini kinatakiwa kufanywa na kwa utaratibu gani na lini?

Katika juhudi za kukuza ajira kwa vijana duniani, ratiba ya warsha hizo za Kitaifa ikoje na lini itafanywa Wilayani Ludewa?

Mara nyingi katika maeneo ya kazi, wafanyakazi licha ya kupewa vifaa vya kujikinga na athari za mazingira ya kazi kwenye afya zao, wafanyakazi hao huwa hawatumii vifaa hivyo na hivyo kuhatarisha afya zao. Je, Wizara inaweka mpango gani kuweka sawa suala hili?

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha vijana nchini kujiunga katika vikundi na kuanzisha miradi ya kiuchumi; je, Wizara inatumia mbinu zipi na ni mikakati gani imewekewa kuhakikisha kila Wilaya vijana wanachangamkia *opportunity* hii?

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba yako hata kabla hujaiweka kwenye waya. Kwanza, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pili, kilichobaki ni kumwomba Mheshimiwa Waziri au Msaidizi wake, aje kuiona Ruangwa. Kwa kweli mtajionea wenyewe matatizo yote pale pale hata bila kuambiwa na mtu yeyote yule. Chonde chonde karibuni.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuwateua Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake, ambao wanaiongoza Wizara hii, ambao leo hii wameiwasilisha hotuba yao, iliyojaa matumani katika maendeleo ya jamii ya Tanzania.

Napenda kuchukua nafasi hii, kutoa mchango wangu katika Wizara hii, ambapo nitaomba nipatiwe majibu ya hoja zangu.

Mheshimiwa Spika, ni lini vijana ambao wako nje ya mijini, (wanaoishi vijijini), wataendelezwa katika misingi ya uzalishaji mali, kwa maana ya kilimo/ufugaji na uvuvi, ukizingatia kwamba, wengi wa vijana wamepoteza matumaini ya kuishi vijijini kwa kuwa hawana njia ya kuwapatia kipato cha uhakika na kuamua kukimbilia mjini, kujitafutia ajira. Matokeo yake, baadhi yao hujiingiza katika shughuli za kufanya maovu au kufanya biashara ambazo kipato chake ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, nimepokea taarifa ya ujenzi wa Daraja la Kigamboni kwa furaha kubwa sana. Napenda niipogneze Serikali kwa uamuzi huo, kwani ujenzi wa Daraja hilo utaleta maendeleo makubwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam na pia litakuwa kiungo kwa Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara. Hivi sasa Barabara ya Kilwa imekuwa ni adha kubwa sana kwa wananchi wa mikoa hiyo, kutokana na kucheleweshwa kwa wananchi wanaotumia Barabara hiyo nyakati za saa za kazi *(pick hours)*. Vile vile ujenzi wa Daraja hilo, utasaidia kuongeza kipato cha Halmashauri za Mikoa niliyoitaja.

Naomba nipatiwe majibu yatakayoleta matumaini katika ujenzi wa Daraja hilo, ni lini ujenzi utaanza badala ya kila mwaka kusuasua?

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa sana la kutokuwepo kwa vijana, suala hili lisiposhughulikiwa kwa juhudi ipasavyo, litakuwa na athari mbaya kwa vijana wanaohusika na Taifa kwa ujumla.

Juhudi zimeanza kufanywa, kuwapatia vijana ajira. Juhudi hizo zinakabiliwa na matatizo mengi lakini mawili ni mazito zaidi. Tatizo la kwanza la vijana wengi ni ukosefu wa stadi za kazi. Mfumo wetu wa elimu, hauwapatii vijana stadi hizo na mara nyingi inachukuliwa tu kwamba, watu wanaweza kufanya shughuli ambazo hawajawahi kuzisomea. Tunahitaji kuandaa utaratibu, utakaowapatia vijana mafunzo kwa wingi katika fani mbalimbali. Katika hili, vyuo vya ufundi kama *VETA* na vingine ni muhimu sana. Wizara ishikiane na JKT ili vijana wanaopitia kwenye Jeshi hilo, wawe wanapitia mafunzo ya aina hiyo. Aidha, kabla vijana hawajapatiwa mikopo na kuanzisha miradi mipya, wapewe mafunzo yanayohusika na wasimamiwe kwa karibu wakati wa utekelezaji, kwa lengo la kuwapatia mafunzo kazini na kuhakikisha kwamba, shughuli wanazoanzisha zinafanikiwa.

Tatizo la pili ni mitaji. Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Serikali imetenga shilingi 500 milioni kwa kila Mkoa, kwa ajili ya kukopesha wananchi. Tunaipongeza sana Serikali kwa hatua hii. Jambo muhimu sasa ni utaratibu wa kutoa mikopo hiyo na kusimamia matumizi yake ili malengo yaliyokusudiwa yapatikane.

Hapa nchini na nje ya nchi, kuna mifano mingi ya mikopo iliyofanikiwa sana. Mafunzo yanayotokana na mifano hiyo yatumike katika kuwapatia vijana mikopo. Lengo la kuwapatia vijana mikopo ni ili kuwawezesha wajiajiri. Kama nilivyotangulia kueleza hapo juu, ni lazima vijana waandaliwe na kupatiwa mafunzo kabla ya kukopeshwa na baada ya mikopo kutolewa ni lazima uwepo utaratibu wa ufuatiliaji na usimamizi wa karibu sana ili kuhakikisha kwamba, utekelezaji unafanikiwa.

Baadhi ya vyombo vya fedha vimeanza kuonesha nia ya kukopesha vijana na makundi mengine ya jamii, kwa ajili ya shughuli zao. *CRDB Bank* wamepata mafanikio makubwa katika kushirikiana na *SACCOS* na *SACCAS*. Mafanikio hayo yametokana na usimamizi wa karibu unaofanywa na Watumishi wa Benki hiyo. Kwa kuwa mikopo mingi itakayoombwa na vijana ni midogomidogo sana, gharama zinakuwa kubwa sana. Vijana wanapoungana katika vikundi, ukubwa wa mikopo huwa mikubwa zaidi, usimamizi unafanywa na vikundi na marejesho ya mikopo huwa ya uhakika zaidi.

Serikali ina Watumishi wengi, ambao wako katika ngazi zote na hawana kazi za manufaa wanazofanya. Wakati umefika wa kuwatumia Watumishi hawa ili washiriki katika kuandaa miradi ya vijana na kusimamia utekelezaji wake. Inawezekana tujipange vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Sasa tumefunga mjadala hapo, ila imebakia sasa upande wa Serikali kuanza kujibu hizo hoja. Nitamwita Naibu Waziri wa kwanza, ambaye ni Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, atafuatiwa na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, kila mmoja kwa robo saa, halafu mtoa hoja ataingia saa 12.00. Natumaini atajitahidi amalize kwa dakika 50 hivi ili tuingie katika Kamati ya Matumizi.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nami naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu, naungana nanyi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu wote, kuwapongeza Viongozi Wakuu wa nchi yetu, ambao ni Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na pia tumpe pole kwa safari ya kurudi toka katika matibabu Uingereza na tunamshukuru Mwenyezi Mungum amemrejesha salama. *(Makofi)*

Pia, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa na wewe Mheshimiwa Spika, kwa ushindi mkubwa ulioupata katika uchaguzi wa mwaka 2005. Aidha, nawapa hongera Wabunge wote, kwa ushindi wenu mlioupata, tutakiane heri katika miaka hii mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kasulu Mashariki, kwa kunipa heshima ya kunichagua kuwa Mbunge wao, kwa kishindo na kwa namna ya pekee. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua mimi kuwa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na hususan nashughulikia ajira. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa heshima kubwa, nizishukuru Jumuiya za Wanawake wa Tanzania (UWT) na Jumuiya ya Vijana Wilaya ya Kasulu, kwa kazi kubwa na nzuri, waliyoifanya wakati wa kampeni. Pia, naomba kwa njia ya pekee kabisa, nimshukuru kwa dhati kabisa, mke wangu, Midlasta, aliyelazimika kuchukua likizo ndefu toka kazini kwake ili anisaidie kampeni kule Kasulu. Mchango wake wa kampeni ulikuwa mkubwa kiasi hata mimi ulinishangaza. Kwa hakika akina mama, wana uwezo mkubwa sana. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Vile vile, napenda kumshukuru Waziri wangu, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, kwa maelekezo yake na ushauri na pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara, kwa ushirikiano mkubwa ambao wananipa hadi sasa. Mwisho kabisa, lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru marafiki zangu wote na wapenzi wa CCM, kwa dua zao na sala zao ambazo zilinisaidia katika kampeni. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nipitie baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwa haraka haraka kama ifuatavyo: Nianze na Mheshimiwa Yono S. Kevela, rafiki yangu Mbunge wa Njombe Magharibi. Ananishukuru kwa kufanya ziara kule kwao na ananipongeza kwa kuwezesha usajili wa *Ubena SACCOS* na kwamba sasa yule Afisa Ushirika tuliyemkemea akasajili *Ubena SACCOS* sasa tumhamishe kwa sababu hana adabu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, mambo yanakwenda hatua kwa hatua. Lakini nimpe pongezi kwamba, *SACCOS* yake ya Ubena sasa imesajiliwa, hongera sana. Hili suala la kumhamisha yule Afisa wa Ushirika, liko

chini ya mamlaka nyingine, lakini akiendelea kusisitiza hivyo, basi tutashauri liende kwenye mamlaka husika, kwa wenzetu wa TAMISEMI ili kulishughulikia.

Pili, naomba nipitie hoja ya Mheshimiwa Adam K. Malima, Mbunge wa Mkuranga. Yeye amezungumzia Shirika la Tija la Taifa na kwamba, malengo yake ni finyu na kwamba haoni watachangia kwa kiwango gani kutekeleza malengo ya Awamu ya Nne.

Naomba niseme tu kwamba, *NIP* au *National Institute for Productivity,* inatoa huduma zake kwanza kibiashara, hilo ni la mwanzo. *NIP* hii imeandaa mpango wake wa kazi *(strategic plan),* wa miaka mitano ili iweze kujipanua zaidi kutoa huduma zake. Lengo kuu la mpango huu ni kulijengea shirika uwezo ili liweze kuwafikia walengwa wengi zaidi. Lakini zaidi ya hayo, nikuthibitishe tu kwamba, Wizara yangu pia inalipa ushirikiano wa hali ya juu, Shirika la *NIP* ili liweze kutoa huduma zake kwa kiwango cha hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ilizungumzia juu ya fidia ya Sh.213,900,000/= kwa kiwanda cha *NIP* kilichonyang'anywa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kupewa shirika lingine. Ni kweli kiwanda cha *NIP* kilinyang'anywa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, wakapewa *Medical and Technological University* ya India.

Lakini Wizara yangu tunaendelea kufuatilia kwa karibu na wenzetu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili *National Institute,* walipwe fidia yao hiyo. Taarifa tulizonazo ni kwamba, mazungumzo yanaendelea vizuri na katika muda si mrefu, wataweza kurejeshewa fedha zao hizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul P. Kimiti naye alizungumzia suala la ufanisi wa Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* na kusema kwamba, shirika hili halifahamiki vizuri na halijajisambazwa nchini. Naomba niseme tu kwamba, *NIP* imeanza kujitangaza vilivyo kupitia Vyombo vya Habari kufika nchi nzima na hakika imeanza kutoa mafunzo yake hata kwa Wizara nyingine. Kwa mfano, ni hivi majuzi tu Shirika la *NIP* liliwakutanisha Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Mameya 53 katika mafunzo maalum yaliyofanyika pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ulitoka kwa Mheshimiwa Sigfrid S. Ng'itu, Mbunge wa Ruangwa. Yeye ametupongeza kwa kazi nzuri na kutualika twende Ruangwa. Mheshimiwa Bunge nikuhakikishie tu kwamba, huo mwaliko tumeupokea na sisi tuna mpango wa kuja huko Ruangwa na tutakuarifu ili tukukute katika maeneo yako tuweze kufanya kazi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ulitoka kwa Mheshimiwa Anna K. Malecela, Mbunge wa Same Magharibi, ambaye amezungumzia kwa uchungu mkubwa, tatizo la watu kutopenda kufanya kazi na akashauri itungwe sheria ya kulazimisha watu kufanya kazi. Kwanza, niseme wazi kabisa kwamba, tunashukuru kwa mchango wake na hamasa hiyo ya kwamba, watu lazima wapende kazi. Lakini niseme tu kwamba,

Serikali kupitia Bunge hili, ilifuta Sheria ya Nguvu Kazi na ninashukuru Mheshimiwa Jackson M. Makwetta amelizungumzia hili.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Nguvu Kazi Na. 6 ya mwaka 1983, ilifutwa na badala yake ikatungwa Sheria ya Ajira Na. 9 ya mwaka 1999. Pia, tumeridhia sisi kama nchi, Mkataba wa Kimataifa wa Kazi Na. 29 na Na. 105. Mikataba hii inakataza kazi za shuruti *(force labour)* na Mkataba huu umezingatiwa katika Sheria Na. 6 ya mwaka 2004. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, sisi na wananchi kwa ujumla, tuendelee kuihamasisha jamii ili watu wapende kazi na kuchukia uvivu. Kwa kweli suala la kukuta vijana kijiweni tu hawana shughuli ya kufanya, haipendezi hata kidogo. Hata mkakati wetu huu wa ajira milioni moja na hizi shilingi milioni 500, ambazo Waziri atazungumzia, zinalenga katika kuwashika mkono wale vijana, ambao tayari wameanza kuhangaika na shughuli zao mbalimbali katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa amesema, Wizara ifanye *survey* kubaini mishahara midogo inayolipwa kwa watumishi, hususan watumishi wa ndani na Wizara itembelee maeneo na Sekta Binafsi ili kujionea hali halisi. Napenda kumhakikishia kwamba, ushauri wake tumeupokea, ni ushauri mzuri na kaguzi zitaimarishwa mara kwa mara ili kujionea hali halisi. Lakini niseme tu kuhusu mishahara hii, Wizara imeunda sasa Bodi za Mishahara za Kisekta, ikiwa ni pamoja na Sekta Binafsi na Bodi hizi zitakapoanza kufanya kazi, ni matarajio yetu kwamba, tatizo la mishahara midogo midogo inayolipwa kwa wafanyakazi, hasa wafanyakazi wa majumbani, litapungua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, ametoa hoja, Serikali iandae sheria zinazoendana na wakati na kupunguza migogoro inayodhoofisha mahusiano kati ya waajiri na waajiriwa. Napenda kusema tu kwamba, ni kweli, kama kuna mambo ambayo yanatusumbua Wizarani pale ni suala zima la migogoro sehemu za kazi. Lakini Sheria yetu ya Mahusiano Kazini, *Employment Act* na *Labour Relation Act* Na. 6 ya mwaka 2004, imelenga kuboresha mahusiano hayo kati ya waajiri na wafanyakazi. Wizara inadumisha utatu ili kudumisha mahusiano sehemu za kazi, yaani waajiri, wafanyakazi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, ushauri wake tumeuzingatia. Pia, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, amezungumzia kuhusu Mabaraza ya Usuluhishi, ushauri huu tumeuzingatia.

Mheshimiwa Spika, sasa niangalie mchango wa Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini. Yeye anasema kuna makampuni yanayotafuta watu kufanya kazi katika nchi za Uarabuni na anashauri makampuni haya yaangaliwe kwa sababu mengi ni ya matapeli. Kwanza, niseme kwamba, ni kweli makampuni haya yapo, lakini kwa sababu tunafanya kazi kwa ushirikiano, kama kuna shirika lolote ambalo Mheshimiwa Mbunge analifahamu linaendesha utapeli, basi atunong'oneze ili mkondo wa sheria uweze kufanya kazi yake. Lakini hata hivyo, ushauri huu tumeupokea na niseme tu kwamba, Sheria yetu ya Kazi Na. 6 ya mwaka 2004, inayorekebishwa sasa, itatilia mkazo vipengele vya hayo makampuni binafsi, yanayokuja ku-*recruit* watu kwa

ajili ya kufanya kazi nje ya nchi yetu. Lakini niseme tena kwamba, kama kuna mawakala wanaofahamika, basi tunong'oneze ili tuweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kamati na Wabunge wengi kadha wamezungumzia hili Shirika letu la Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA).* Napenda kusema kwamba, hili ni shirika ambalo limefanya kazi kubwa kweli kweli kwa mwaka uliopita. Kwa mwaka uliopita 2005/2006 peke yake, shirika hili limeweza kufanya kaguzi 3,400 sehemu za kazi na bado wanaendelea kufanya kazi zao. Lakini kweli uwezo wa kifedha ni mdogo na ni shabaha ya Serikali kuongeza uwezeshaji katika shirika letu hili la *OSHA*. Lakini kwa hakika, wanafanya kazi nzuri na wameanza kujitangaza vizuri. Mimi mwenyewe mwezi wa nne mwaka huu, nilikuwa mgeni wa heshima, nilimwakilisha Mheshimiwa Waziri kule Arusha, kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi na tuliweza kutoa vyeti kwa watu ambao wanatekeleza Sheria za Usalama Mahali pa Kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mbunge wa Msalala, ushauri wake na maoni yake tumeyazingatia ni mazuri tu. Amezungumzia ajira za wageni, kwa kweli ni kero na sisi suala hili tunalitazama kwa macho mawili na tumeanza kufanya *surprise visits* katika baadhi ya maeneo, kukagua na kujiridhisha kwamba; je, hawa wanaofanya kazi wana sifa zinazostahili na je, wanachukua ajira za Watanzania Wazalendo? Yote haya tunayafanyia kazi na ushauri huu ni mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, ametukumbusha hapa juu ya wachimbaji wadogo wadogo takriban elfu kumi katika maeneo ya Bulyanhulu, Busalwangili, Mwazimba, Nyangh'wale na Sagehe. Yote haya ni ushauri mzuri na hatuwezi kuacha, maana hawa sisi kwetu ni wateja. Vijana elfu kumi katika eneo moja, hakika nikuhakikishie tutafanya kila lililo ndani ya uwezo wetu, kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini kama nilivyoshauri hapa kwenye hoja yako, kuhakikisha juu ya mikopo, juu ya mafunzo ya usonara na kadhalika. Hilo tumelizingatia. Pia, amezungumzia suala la Shirika la *OSHA,* napenda kusema kwamba, tunaliimarisha zaidi na mwaka huu wa fedha, tumepanga kuongeza wakaguzi wa viwandani takriban 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, mawazo yake kuhusu Sera ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi tumeyazingatia, ni ya msingi. Kuna umuhimu wa kuweka maeneo mazuri na salama kwa ajili ya wafanyakazi wanawake wenye watoto katika viwanda na akatoa mfano wa kiwanda kama *A to Z*, ambapo kuna wafanyakazi wanawake wengi. Yote hayo tumeyazingatia.

Mheshimiwa Spika, yako mengi, lakini mengine Mheshimiwa Waziri, atayapitia hapa. Niseme tu kwamba, naunga mkono hoja na kazi iliyoko mbele yetu ni kubwa na hatuwezi kujiruhusu kushindwa kupata kazi milioni moja tulizoahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi. Nawashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mungu, kwa kunijalia kusimama mbele ya Waheshimiwa Wabunge na mbele ya Bunge lako Tukufu na nimshukuru vile vile kwa kutupa sote afya njema, kwa muda huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru vile vile sana kwa kunipa nafasi hii ili nifafanue baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, zinazotokana na maombi ya bajeti ya Wizara yetu. Naomba niunge hoja mkono kwa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia kwa mara ya kwanza, nafasi hii maalum kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa nchi yetu. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu Maalum wa CCM, kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama chetu cha Mapinduzi. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa imani na heshima hii kubwa sana ya kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Ninaomba kurudia ahadi yangu kwake Mheshimiwa Rais, ya utii kwake na uadilifu katika nafasi aliyonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza vile vile Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais. Ninaomba kumpongeza sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kisha kuthibitishwa na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu Tukufu na pia nimpongeze Mheshimiwa Mama Anne S. Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na nirudie maneno yangu ya wakati ule wa uchaguzi kwa kusema kwamba, inapendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kukabidhiwa dhamana hii kubwa ya uwakilishi. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kushika nafasi hizi za juu za utumishi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitume shukrani za pekee kwa wananchi wa Arumeru Mashariki, kwa kukichagua Chama cha Mapinduzi kwa kishindo kwenye Uchaguzi Mkuu Desemba, 2005 na kumchagua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Rais na mimi kuwa Mbunge wao na kwa kuwachagua Waheshimiwa Madiwani wa Chama cha Mapinduzi kwenye Kata zetu zote za Jimbo letu la Arumeru Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, kwa kunishirikisha kikamilifu kwenye uendeshaji wa Wizara yetu. Lakini pia namshukuru sana Naibu mwenzangu, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, kwa ushirikiano wake mkubwa. Ninawashukuru

sana Katibu Mkuu, Dr. Ladislaus Komba na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Idrisa Mavura. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara na pia wafanyakazi wengine wote wa Wizara, kwa ushirikiano wao na misaada mbalimbali ya kikazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sasa katika hizi shukrani, naomba nimshukuru sana mke wangu Miriam, kwa kuja kunipa joto hapa Dodoma na siku hizi kuna baridi kweli kweli hapa na nyie mnajua. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini namshukuru vile vile mwanetu Kisali, kwa kuja na pia Lengaree kwa kuja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa maswali yao mazuri sana, hoja nzito na muhimu na pia kwa wingi wa ushauri mliotupatia. Ninawahakikishia kuwa, mliyoyasema yatazingatiwa na yatakuwa sehemu ya kutimiza wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nijibu na kufafanua baadhi ya ushauri wenu na maswali yenu. Mengi katika hayo, yatafafanuliwa na Mheshimiwa Waziri na mengine Mheshimiwa Naibu ameshafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, anasema mpaka sasa haijulikani ni kitu gani kinachoendelea na kama Serikali ina nia thabiti ya kuanzishwa kwa Baraza la Vijana au ni maneno tu au kuna hofu kwamba, vijana wakipewa nafasi watatishia nafasi za wazee. Eeeh, sasa nafasi za wazee ni za wazee na nafasi za vijana ni za vijana!

Mheshimiwa Spika, napenda niwaambie Waheshimiwa Wabunge kuwa, Baraza la Vijana linahusisha wadau mbalimbali na siyo tu *National Youth Forum,* ambayo ilitajwa na *Tanzania Youth Vision Association* pekee. Serikali haijatoa ahadi kwa asasi hizi peke yake, isipokuwa ina nia ya kuunda Baraza hili.

Baraza hili litaundwa kisheria na ni nia ya Serikali kwamba, kwa sababu ni Baraza la Vijana, basi lihusishe vijana wote wa nchi hii bila kujali dini, bila kujali itikadi na bila kujali tofauti zozote, ambazo zinaweza kuwemo ndani ya kundi la vijana wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke kwamba, vijana tunaozungumzia hapa ni vijana ambao wanakaribia takriban 12,500,000. Kwa hiyo, ni wengi kidogo, ni theluthi moja ya idadi ya wananchi wa Tanzania. Wizara ilianza mchakato wa kuunda, ni kweli siku zimepita, ilikuwa ni mwaka 1998 katika mkutano kule Iringa.

Kwa kutambua dhana ya ushirikishwaji na nchi yetu, tukumbuke ni kubwa na vijana ni wengi, ambayo pia inabeba gharama kubwa. Wizara ilibidi itafute fedha na kwa bahati nzuri, Shirika la *UNICEF* likakubali kusaidia na kwa hiyo, ukaendeshwa mkutano ambao ulijumuisha mikoa yote ya nchi yetu.

Katika mkutano ule, walihudhuria vijana 1,200, hii ilifanyika mwaka 2003/2004 na sasa tumefika mahali pazuri. Mpaka sasa Waraka wa Sera ya Vijana ambao unaagiza kuundwa Baraza uko tayari, utarejeshwa kwenye Baraza la Makatibu Wakuu wa *Inter-Ministerial Technical Committee* na baada ya hapo utarejeshwa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, lakini ucheleweshaji mwingine wa kuunda hili Baraza ulitokana na Uchaguzi Mkuu kwamba, wakati ule isingewezekana kufanya hivyo.

Sasa ni matarajio ya Wizara kuwa, mchakato wa kuunda Baraza hili, utatengemaa baada ya kuleta Muswada hapa Bungeni kupitishwa na kwamba, Baraza hili litaundwa Mungu akitujalia katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, maana yake ni mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, lakini tunashukuru vile vile kwamba, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, anatambua kwamba, kuna Vyuo vya Vijana vya Mafunzo. Tunakiri kwamba, ni vichache, kwani tuna vyuo vitatu; kimoja kiko Ilonga, kingine kiko kule Sasanda Mbozi na kingine kiko kule Marangu.

Lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliainisha kuwa, lengo la Wizara ni kwamba, ndani ya muda mfupi na wa kati, kila Wilaya na ndiyo lengo letu, tuwe na Kituo cha Vijana na hapo ndipo tutakapoweza kutimiza kweli lengo letu la kuwahusisha vijana katika ujenzi wa nchi. Kwa hiyo, naomba tuvute subira, wale ambao wanakwazika kidogo na kucheleweshwa kwa kuunda Baraza hili, niwahakikishie kwamba, lengo la Serikali ni kuona kwamba hili Baraza la Vijana linaundwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia, anasema na anaomba Wizara ikamilishe haraka zoezi la ukusanyaji takwimu za vijana. Hilo ndilo lengo letu. Idara ya Vijana inafanya kazi hii.

Katika maswali mbalimbali, ambayo yameulizwa hapa Bungeni kuhusu suala hili, tumejibu kuwa mpaka sasa hivi tumeweza kufikia Wilaya 76. Tunazo Wilaya 119, zimesalia Wilaya 44 na lengo ni kujua vijana wako wapi.

Lakini pamoja na Mradi huo, kuna mwingine wa kuainisha vijiwe viko wapi. Mpaka sasa hivi tumeshamaliza kuainisha Dar es Salaam na kama Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka, tulitaja hapa ndani kwenye Bunge Tukufu kwamba, tulibaini kuna vituo 509 pale Dar es Salaam peke yake, kwa hiyo tutaongeza jitihada.

Hili zoezi kwa mara nyingine nirudie ni ghali vile vile, lakini tutakwenda kwa jinsi ambavyo tutaweza kugharamia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuratibu utoaji wa urejeshwaji wa mikopo, hapa anazungumzia nafikiri Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Tumeainisha taratibu nyingine ambazo zinatilia sana mkazo kwenye urejeshwaji wa mikopo hii na tunaamini kwamba, itakapoanza kutolewa tena kwa vijana, Wizara itakuwa na uwezo wa kufuatilia na kuhakikisha kwamba, inarejeshwa ili iweze kurudi tena kwa vijana wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubaguzi katika kazi, jambo hili limeulizwa na Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum na anasema kwamba, sheria mpya hazijatoa ufafanuzi kuhusu ajira na mahusiano kazini, kuhusu wafanyakazi wenye ulemavu.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Margreth Mkanga, kwamba sheria namba sita ya mwaka 2004 ambayo tunatarajia itaanza kufanya kazi mwaka huu. Chini ya kifungu cha saba na kifungu kidogo cha nne cha sheria ile imekataza ubaguzi wa aina yoyote katika kazi ama mahali popote pa ajira na sheria hii inahusu wafanyakazi wote wa jinsia zote na hata wale ambao kwa bahati mbaya Mungu hawakuwajalia uzima kama wengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mama Margreth Mkanga, nakuomba ukae ukijua kwamba sheria hii punde itakapoanza kazi utalindwa kikamilifu.

Lakini kwa sababu kengele imelia nihusishe na somo moja linalohusu Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana na hoja hii ilijitokeza kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ambayo inasema kwamba sera hii imechelewa sana kuanza kutumika kwa kuwa ndiyo dira ya maendeleo ya vijana kutokuwepo kwake nini mbadala wake? Niseme kuwa Serikali inayo Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ambayo ilipitishwa mwaka 1999 wakati wa utekelezaji wa sera hii hoja mbalimbali ziliibuka na wadau na vijana wenyewe ambapo ilionekana kuwa kuna haja ya kufanya mapitio ya sera hii kwa sababu ya mabadiliko.

Kwa mfano sera ya 99 ilisema kwamba kijana wa Tanzania ni Mtanzania yeyote mwenye umri kati ya miaka 15 na 24. Lakini ikabainika kwamba hapana tukifanya hivyo tunawaacha walio vijana wengi nje ya hilo kundi. Kwa hiyo, Serikali ikaamua kwamba kijana wa Tanzania awe Mtanzania aliye na umri kati ya miaka 15 na 35. Halafu kuna mabadiliko mengi ya kiuchumi, ya kijamii, ya kisiasa ambayo yametokea toka mwaka 1999 na kwa hiyo, kumekuwa na umuhimu wa kufanya mapitio kwenye sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, moja ya hoja nyingine ambazo zilijitokeza ni kuwa vijana hawakushirikishwa katika maandalizi ya sera ya mwaka 1996 na hivyo tumefanya sasa. Kwa kutambua umuhimu wa ushirikishwaji wa vijana katika mchakato wa kuboresha sera hii, Wizara ilianza mchakato wa kuwashirikisha vijana. Kazi hii imefanyika mwaka 2003/2004 ambapo mikutano ya vijana ilifanyika katika kanda sita na kuhusisha ushiriki wa vijana kutoka mikoa yote kwa njia ya uwakilishi. Rasimu ya sera iliwasilishwa kwenye Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na kujadiliwa hadi kufika ngazi ya *IMTC.* Kutokana na harakati za uchaguzi baadhi ya nyaraka hazikuweza kupelekwa kwenye Baraza la Mawaziri. Baada ya uchaguzi nyaraka zilizokuwa *IMTC* zimerejeshwa Wizarani ili viongozi wapya ambao ndiyo sisi wa Serikali wazipitie na kuona kama zinakidhi hali ya sasa. Waraka wa sera hivi sasa uko tayari kujadiliwa tena na *IMTC* lakini haya yote yakiendelea sera ya mwaka 1996 inabidi bado iwe ndiyo inafuatwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuwa ni mikakati gani ambayo Wizara imeandaa kuwasaidia vijana, tayari mkakati huo wa maendeleo ya vijana umeshakamilika, unazingatia sana mambo kadhaa, mojawapo ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005/2010 ni dira ya maendeleo ya Milenia ya mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuhitimisha hoja yangu ambayo niliitoe leo asubuhi. Napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa hoja zao ambazo wamezitoa katika hoja ya Wizara yangu. Waheshimiwa Wabunge 65 wametoa hoja zao kwa maandishi na Wabunge 13 wametoa hoja zao kwa kuzungumza hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hao kuna Wabunge 12 ambao walitoa hoja zao wakati wa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Aidha, kwa sababu ya hoja nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, haitawezekana kuzijibu hoja zote katika kipindi hiki cha saa moja na nusu ambacho mimi na wenzangu wawili tumepewa kuzijibu hoja hizo.

Hata hivyo tumedhamiria kabisa kwamba tutazijibu hoja zote ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaondoka hapa Dodoma katika kikao hiki cha Bunge. Hata hivyo, tutajaribu kuzijibu hoja nyingi iwezekanavyo na kengele yako ndiyo hiyo tu itatusimamisha katika kutoa hoja hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa sababu ya idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja basi wakati ninawashukuru na kuwataja majina yao naomba muda huo utupatie kama ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ambao walichangia hoja hii kwa maandishi ni Mheshimiwa Ali Haji Ali, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Omar Kwaangw’, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji na Mheshimiwa Adam Malima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Sigifrid Ng’itu, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

Wengine ni Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Fatma Mikadadi, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na Mheshimiwa Said Amour Arfi.

Wengine ni Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Ali Said Salum, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ni Mheshimiwa Amina Mpakanjia, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifan, Mheshimiwa Anna Malecela, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Laus Mhina, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ridhaa yako kama kuna wengine sikuwataja majina yao basi nisaidiwe na nitaendelea kuwatambua jinsi tunavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingi zimetolewa, moja ya hoja kubwa ni hoja ya shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa. Napenda niongezee maelezo zaidi kidogo pale nilipokuwa nimeachia asubuhi halafu nitoe *rational* kidogo kwa nini tumechukua muda kidogo kulifikiria suala hili. Suala hili ni kubwa na tunataka tukianza kazi ya kupeleka fedha hizi kwenye Mikoa ziweze kuleta mabadiliko katika uchumi wa nchi yetu. Tunataka iwe *operation* kubwa na tunataka ilete msisimko na iongeze ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, hivyo tuliangalia shilingi milioni 500 kama mbegu nzuri ambayo ingeweza kupandikizwa katika uchumi wetu na kuleta mabadiliko. Tukifiria kwa ndani kama mbegu tuliangalia kwa mfano kama shilingi milioni 500 zinapelekwa kwenye Mkoa wa Tanga, ambao una Halmashauri kumi, utaona kwamba fedha zitakazokwenda kwenye Halmashauri ni kama shilingi milioni 50 na kama Mkoa una Halmashauri sita au saba basi kiwango ni kati ya milioni 50 mpaka milioni 70, milioni 80.

Sasa fedha kiasi hiki kikienda kwa hali ambayo ilivyo kule kwenye Mikoa yetu, vijiji vyetu na Wilaya zetu haitaleta *impact* ya kutosha, haitaleta msisimko wa kutosha. Kwa hiyo, tukawa tumeanza majadiliano na Mabenki ya Biashara ili kutumia fedha hizi kama dhamana. Fedha hizi zikae kwenye benki kama *deposit* na benki ambazo zina fedha zitoe fedha zake zikijua kwamba kwa utaratibu wa kutoa fedha kama *SACCOS* kiwango cha urejeshwaji wa *SACCOS* ni kuanzia asilimia 90 mpaka 100 kwa hiyo, benki zinaweza kuchukua jukumu ikatoa fedha hizi mara mbili mpaka mara tatu ya fedha ambazo tumeweka katika benki zao kuwakopesha wananchi katika kila Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, bado tunashughulikia suala hili na siku ya Jumatatu ndiyo tutakuwa na kikao cha mwisho na ninategemea kwamba tutakuwa na utaratibu ambao tutauleta hapa na kuwaeleza ili mjue mtu aliyeko kijijini fedha hizi zitamfikia namna gani.

Mheshimiwa Spika, nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na hasa alipokuwa anazungumza Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, alikuwa anaeleza kwamba fedha zitatokaje Moshi zifike Kisiwani, zipande kule juu Kighale Mlimani na kwa sababu ya uzoefu wa huko nyuma watu wanakuwa na mashaka, fedha zitatokaje Tabora ziende zifike Uyui halafu zitoke Uyui ziende kule Kijijini? Sasa mambo haya watu wana wasiwasi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachosema Waheshimiwa Wabunge, tusaidieni katika majimbo yenu waunganisheni vijana, waunganisheni akinamama, waunganisheni wananchi ambao hawana kazi katika *SACCOS* na *SACCOS* hizi ndiyo zitakuwa za dhamana. Hakutakuwa na dhamana inayotakiwa. *SACCOS* zitapewa mkopo, halafu *SACCOS* zitawapa mkopo wanachama wake na kusimamia wanachama wake warudishe mkopo kwenye *SACCOS* ipeleke mkopo benki. Huo ndiyo utaratibu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunachofikiria ni kitu ambacho kinawezekana kwa sababu *SACCOS* hizi zitakuwa na akaunti sasa kwenye Wilaya au kwenye mji ambapo kuna benki. *SACCOS* ndiyo zitachukua jukumu ya kuondoa fedha kijijini kupeleka kwenye benki kule mjini, siyo mkopaji mmoja mmoja. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limeulizwa sana hapa na watu wamelisemea kwa nguvu kabisa ni suala la vibali kwa wageni wanaofanyakazi hapa nchini. Kwanza tuwe na *best line* kwamba tuko katika dunia ya utandawazi kwa hiyo, sisi kama Watanzania hatuwezi kuwa kisiwa ambapo wageni hawatakuja nchini kwetu. Lakini wageni wanapokuja kwenye nchi yetu basi waje wakiwa na mchango wa kuendeleza nchi yetu.

Kwa hiyo, vibali vinavyotolewa pale Wizarani kwangu *basically* viko vya aina mbili. Kibali cha aina ya kwanza ni kibali wageni *grade A* wale ambao wanakuja kuwekeza. Mtu ana kiwanda chake, mtu anataka kuanzisha shughuli ya uwekezaji hapa nchini anapitia kituo chetu cha uwekezaji anapewa *certificate* ya uwekezaji. Ile *certificate* kwa sheria yetu ile ya kituo cha uwekezaji ana ruhusa ya kuwa nafasi tano za watu anaowaajiri kutoka popote anapotaka. Wengine atawaajiri hapa nchini kwa sababu ni muhimu kuajiri hapa ili ajue mazingira hapa yakoje. Lakini anaruhusiwa kuajiri watu watano kwa sheria ile.

Mheshimiwa Spika, sasa kama atahitaji wafanyakazi wengine lazima aombe kibali cha kuajiri mgeni *grade B* ambacho kinaombwa kupitia Wizara ya Kazi. Kibali hicho sasa ili akipata lazima kazi anayohitaji mtu itangazwe hapa nchini. Labda nirudi nyuma kidogo niseme kwa sababu hiyo ya kibali kupitia *TIC* na kibali kupitia Idara ya Ajira, tulikuwa na kamati mbili za kutoa vibali ili kuharakisha utoaji wa vibali

wawekezaji wasingoje vibali vikatolewa kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, tulikuwa na kamati inatoa vibali vya aina ya ‘A’ kupitia kwa Kamishina wa Kazi na vibali vya *grade ‘B’* kupitia kwenye Idara ya Ajira. Tulipoangalia malalamiko juu ya vibali hapa ni mengi sana. Nikachukua uamuzi kuunganisha Kamati hizi mbili na kuzipa utaratibu wa kukutana mara tatu kwa mwezi mmoja kwa hiyo, hakuna kibali ambacho kitaombwa pale Wizarani kina viambatanisho vyote kichelewe zaidi ya siku kumi ama kitaambiwa umepata au hujapata ndani ya siku kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kibali cha *grade ‘B’* lazima kazi hiyo itangazwe hapa nchini na tuwe na ushahidi na kwamba mtu atakayepewa kibali hicho ana utalaam ambao wakati huo kinatolewa hakuna Mtanzania aliyenacho au aliyeomba kazi hiyo. Halafu mtu huyu kweli ana sifa za kufanyakazi inayosemekana. Sasa kamati inafanya kazi nzuri sana na mimi nitatoa mfano mmoja tu, wiki mbili zilizopita kamati iliombwa ku-*renew* vibali vya wageni wanne wanaofanyakazi katika moja ya mabenki makubwa hapa nchini. Wafanyakazi wale walipewa vibali huko nyuma miaka miwili iliyopita kwa masharti kwamba watafanyakazi miaka miwili tu na vibali hivyo havitaongezewa muda. Lakini wamekaa, wamependa kukaa kwetu, baadaye wanaomba tena. Sasa tukaangalia kwa vigezo hivi nilivyovisema kwamba kazi imetangazwa wanazo sifa na hakuna Watanzania wengine ambao wana kazi hizo tukakuta kwanza kazi haikutangazwa, pili hawana sifa ambazo zinahitajika na tatu kuna Watanzania wengi ambao wana sifa ya kupata kazi hizo. Kwa hiyo, wakanyimwa kibali.

Kwa hiyo, kamati inafanyakazi nzuri sana, hata hivyo ni muhimu sana kwa kamati hii kuwa na tahadhari ya kufanya kazi yake ikijua kwamba kazi yake kwanza ni kukuza ajira kwa ajili ya Watanzania, lakini pia iweze ku-*balance* hoja hii pamoja na hoja ya kuendeleza uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, kamati inafanya kazi kubwa pamoja na Wizara kukagua maeneo mbalimbali ya kazi, kuangalia wageni wanaofanya kazi kwenye mashirika hayo, wana vibali ambavyo ni halali kama vibali vyao bado viko *valid* na kama hakuajiriwa mtu ambaye hastahili. Kazi hii imefanyika katika mahoteli ya Dar es Salaam, katika mahoteli ya Mkoa wa Tanga, katika Mahoteli ya Mkoa wa Kilimanjaro, katika Mahoteli ya Mkoa wa Arusha na Mahoteli ya Mkoa wa Manyara na kazi inaendelea. Katika utaratibu huo kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Mambo ya Ndani, tunachukulia hatua papo kwa papo wale ambao wanavunja sheria. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mtupe muda wakati tunashughulikia suala hili kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limejitokeza pia hapa suala la uzoefu kazini kwamba hicho ndicho kigezo cha kuajiri watu. Ningependa nitoe rai kwamba mtu yeyote anayetaka mfanyakazi ana sifa maalum anazotaka kwa mtu huyo ili amfanyie kazi yake. Sasa kama hospitali inatafuta daktari inasema natafuta *GP,* natafuta daktari ambaye ametoka shuleni au daktari ambaye hajafanya masomo ya uzamili au inasema nataka daktari bingwa wa watoto. Sasa kama anataka daktari bingwa wa watoto lazima aseme hivyo maana huyo ndiyo anayemtaka. Lakini nakubaliana kabisa na Waheshimiwa Wabunge na Serikali inakubaliana kabisa na ina-*practice* hili kwamba pale ambapo siyo lazima hiki kisiwe

kikwazo cha kuajiri vijana na kwa sababu ndiyo maana Serikali imeamua kwamba walimu wote waajiriwe kutoka moja kwa moja na wapangiwe kazi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kwamba wote wanaojifunza katika vyuo vya afya, waganga, manesi, madaktari wapangwe moja kwa moja kutoka vyuoni kwenye vituo vya kazi na Serikali itaendelea kwenda kwa njia hii ili kuhakikisha kwanza kwamba vijana wanapata kazi, lakini pia kwamba hakuna urasimu wa kuajiri watu ili huduma kwa wananchi ipatikane kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo maswali aina nyingi kidogo kuhusu Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* na kuna yale ambayo nitayajibu moja kwa moja na yale ambayo ningependa nitoe angalizo kidogo. Nchi yetu ni mfano mzuri wa kutolewa mfano wa utawala bora. Tunatolewa mfano kwa sababu tunakubali, tunafanya kwa vitendo na tunaamini juu ya mihimili mitatu ya utawala kwamba tunayo Serikali kwa maana ya *Executive,* tunalo Bunge kwa maana ya *Legislative* na tunayo Mahakama.

Sasa kama suala liko Mahakamani ni kweli kwamba kuna vyombo vya habari ambavyo vinaendelea kuzungumza juu ya suala hili, lakini kama suala liko Mahakamani na sisi ni Waheshimiwa Wabunge ambao tunataka mtu asiingilie *legislative* na tunaamini kabisa kama mahakama ni chombo ambacho lazima tukiheshimu na tunangoje mpaka kitoe uamuzi wake ni vizuri maswali yale ambayo mahakamani tusiyajadili kwenye Bunge, kwa sababu tayari ushahidi wa aina mbalimbali unatolewa ndani ya Mahakamani na sisi tutakuwa tunafanya makosa kuingilia utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nitajibu maswali mengi yale ambayo yameulizwa na Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Suala la kwanza limetolewa na Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ni kwamba *NSSF* itoe mikopo kwa wanachama wake. *NSSF* ni tofauti na uwekezaji katika mabenki. Uchangiaji katika *NSSF* ni kwa ajili ya mafao ya uzeeni na mengineyo kama yalivyoainishwa katika sheria ya *NSSF*. Hata hivyo *NSSF* imebuni mradi wa kujenga nyumba za kuisha wanachama wake za bei rahisi na inawakopesha wanachama wake kama ambavyo inafanya katika eneo la nyumba 194 kule Kinyerezi na waliokopeshwa nyumba hizi wanalipa kidogo kidogo kwa muda wa miaka 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa kujenga nyumba na kuuza umeanzia Dar es Salaam na baadaye itatawanywa katika Mikoa mingine kwa jinsi uwezo na wawekezaji wa shirika wanaofanya maamuzi watakavyoona inafaa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Kigamboni niliusema kidogo mtakumbuka kwamba Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambayo inasimamia Wizara yangu na Kamati ya Miundombinu, zilikutana kwa pamoja ili kujadili suala hili na ikatoa maagizo ambayo yalikuwa *specific* kabisa, Wizara yangu na Wizara ya Miundombinu tumekuwa tunafanyakazi bega kwa bega kuhakikisha kwamba tunatatua matatizo ambayo yalikuwa yanalikabili suala hili.

Mheshimiwa Spika, tumefika mahali ambapo sasa tumekubaliana eneo la kujenga daraja kwenye eneo la Kurasini badala ya kule kwenye bandari, mantiki yake ni kwamba ukijenga upande wa Kurasini unaweza kuingilia Bandari kwa eneo moja tu ambazo meli zinaweza kujiegesha. Lakini tukijengea kule *dockyard* tutaathiri maeneo kama hayo mara nne.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumekubaliana daraja lijengwe kutoka Kurasini. Pia tumekubaliana kwamba sasa *NSSF* itoe mapendekezo rasmi ya kujenga daraja hili pamoja na *timetable* ya kujenga daraja hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha kazi itakayofanywa ni kufanya usanifu kamili wa daraja hili na kuchukua hatua za kumpata mkandarasi atakayejenga daraja hilo na kwamba mwaka kesho wa 2007/2008 ndiyo daraja hilo litaanza kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa mapendekezo kwamba wafanyakazi wa *NSSF* wachangie katika *PPF*. Ni kweli wafanyakazi wengi hasa *Senior Officers* wa *NSSF* michango yao inakwenda *PPF* kisheria na hii inatokana na Sheria zilizoanzisha mifuko hii. Hata hivyo, asilimia 99 ya wafanyakazi wa *NSSF* ni wanachama wa hiari katika mfuko wa *NSSF*.

Pili, hivi ninavyoongea Sheria Mpya ya Hifadhi ya Jamii ambayo itaweka uzuri na itaunganisha Sheria zote za mashirika haya manne ambayo tunayo zitaunganishwa na tunategemea kwamba italetwa Bungeni mwezi Oktoba, 2006. Katika Sheria Mpya ya Hifadhi ya Jamii, itatoa mwongozo wa jinsi ya kuhamisha michango au mafao kutoka mfuko mmoja kwenda mfuko mwingine.

Mheshimiwa Spika, itakapofika hapo basi wafanyakazi wa *NSSF* wataamua wao wenyewe ni mfuko gani waweke mafao yao. Kumekuwa na wasi wasi kwamba labda wafanyakazi hawawakilishwi katika Bodi na vyombo vya maamuzi vya *NSSF*. Napenda niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba Bodi ya *NSSF* ni Bodi ya utatu, ina wanachama tisa na Mwenyekiti ni wa kumi. Oh, niseme Bodi ya *NSSF* ina Wajumbe tisa na Mwenyekiti, ni wa kumi. Wajumbe watatu wanachaguliwa na Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)*. *(Makofi)*

Wajumbe watatu wanachaguliwa na Shirikisho la Waajiri Tanzania na wajumbe watatu wanachaguliwa na Waziri kuiwakilisha Serikali na mjumbe mmoja ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwa hivi, Mwenyekiti wa Bodi hii anateuliwa na Rais. Kwa hiyo, hakuna uwezekano kwamba wafanyakazi hawawakilishwi au waajiri ambao wanapeleka michango kule hawawakilishwi, wote wamewakilishwa tena kwa usawa. *(Makofi)*

Sasa kumekuwa na mawazo kutoka kwenye Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge kwamba mafao ya *NSSF* yaboreshwe na mimi nakubaliana kabisa na Kamati kwamba *NSSF* itafanya kila juhudi chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne kuboresha kila wakati mafao ya wanachama.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* ijihusishe na ujenzi wa miondombinu ya kilimo. *NSSF* iendeleze mradi wa hosteli kwa kujenga hosteli kwa ajili ya shule za sekondari. Serikali iko katika hatua ya juu ya mazungumzo na Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* na Chuo Kikuu kikishirikisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu ya Chang'ombe kuhusu ujenzi wa hosteli za wanafunzi za chuo hicho. Aidha, *NSSF* inaendelea na mazungumzo na Vyuo vya *SUA,* Mzumbe na Chuo Kikuu sehemu ya Muhimbili kwa ajili ya kujenga hosteli katika maeneo hayo. Kwa wakati huu hapo ndipo tulipo na tunajua kwamba mahitaji ni makubwa lakini tutapanua huduma hii kutokana na uwezo lakini pia kutokana na kuangalia kwamba uwekezaji huo utakuwa unaongeza mafao kwa ajili ya wanachama.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* inachangia katika maendeleo ya kilimo kwa kuwekeza katika mikopo kama ile ya *Kagera Suger, Katani Limited* na uwekezaji huo unatoa ajira moja kwa moja na pia kupitia wakulima wadogo wadogo wanaouza bidhaa zao katika viwanda hivyo. Kwa hiyo, *NSSF* itoe elimu kwa wananchi na pia ifanye semina kwa Wabunge. *NSSF* inatoa semina kwa wanachama wake katika sehemu zao za kazi. Kwa mfano, mwaka 2005/2006 *NSSF* ilitumia shilingi 66,700,000 kwa ajili hiyo. Mwaka 2006/2007 *NSSF* itatumia shilingi milioni 99 kwa ajili hiyo. Ushauri wa kufanya semina umepokelewa na utafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na maswali hapa kutoka kwa Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, juu ya *NSSF* imepata faida kiasi gani tokea ianzishwe na wanachama wamegawiwa kiasi gani tokea ianzishwe na wanachama wamegawiwa kiasi gani na *NSSF* iwe makini katika uwekezaji wa majengo.

Mheshimiwa Spika, *NSSF* inaendeshwa kwa mfumo wa hifadhi ya jamii. Uwekezaji unaofanywa ni kwa ajili ya kuboresha mafao. Katika kipindi cha uhai wake michango pamoja na mapato ya wawekezaji yamekuwa na kufikia shilingi bilioni 398. *Not worth* bilioni karibu bilioni 400 (*four hundred million dollars)*.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni, 2005 baada ya kutoa malipo ya mafao na gharama za uendeshaji. Kama ilivyo duniani kote *NSSF* haina utaratibu wa kutoa gawio kwa wanachama kwani hii ni kinyume cha msingi wa hifadhi ya jamii kama inavyoainishwa kwenye mikataba ya Shirika la Kazi Duniani Na. 102 ya mwaka 1952.

Mheshimiwa Spika, mwisho tuliulizwa swali hapa na Mheshimiwa Halima Mdee, kuhusu *tower* ya hifadhi kwamba inakuwaje *tower* ya hifadhi inanunuliwa kwa bei chee halafu kuna *tour* na kuna *millenium tower*. Nilikuwa nataka niseme tu kwamba katika Shirika hili *Hifadhi Tower* ni Ofisi za Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na sina taarifa ya kwamba *Hifadhi Tower* inauzwa. Nategemea kwamba *Hifadhi Tower* itaendelea kuwa nyumbani kwa Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Millenium Tower* ninayojua ni *tower* ya Shirika la *LAPF* ambayo iko Kijitonyama Mjini Dar es Salaam nayo sina taarifa kama na lenyewe linauzwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba pia niseme kidogo juu ya maswali yaliyoulizwa kwa nguvu sana juu ya kazi na ajira kwa mtoto. Ndugu yangu Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waziri Kivuli ameeleza kwa masikitiko makubwa juu ya ajira mbaya kwa vijana katika mashamba, katika uchimbaji madini na katika maeneo mengine. Serikali inaliona suala la ajira mbaya kwa watoto kwamba ni suala muhimu sana la kukabiliana nalo mpaka tatizo hili liondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu hiyo, katika Sheria Na. 6 ya Mahusiano Kazini na Taasisi za Kazi ya mwaka 2004. Suala la kuajiri watoto chini ya miaka 15 ni suala la jinai.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Tanzania iko mbele zaidi ya nchi zote duniani katika kupambana na suala hili na katika mkutano wa *ILO* uliofanyika mwezi Juni, 2006 Tanzania ni nchi iliyopigiwa mfano kwa kupambana na suala hili kwa dhati kabisa kwa kutunga Sheria kupinga ajira mbaya kwa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili mwaka 2004 tulipitisha katika Bunge hili marekebisho ya Sheria ya Elimu inayomlazimisha kila mzazi ampeleke mtoto wake shuleni anapofika miaka saba na kufanya kwamba hili ni kosa kwa mzazi yeyote ambaye hampeleki mtoto shuleni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nchi yetu inapambana kweli kweli na suala hili na halijakamilika na matatizo tuliyonayo ni pamoja na ugonjwa wa UKIMWI ambao unaongeza yatima kila siku na kwamba suala hili la watoto kwenda kufanya kazi ni kwa sababu ya matatizo katika familia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala hili tunalishughulikia kwa nguvu zote na wenzetu duniani wanatupigia sisi ndiyo mfano wa dunia wa kupambana na suala hili. Na tunategemea kwamba katika muda mfupi chini ya miaka 10, 15 tutaweza kulitokomeza kabisa tatizo hili.

Suala la vibali tumeshalijibu. Suala lingine ambalo limeulizwa hapa kwa nguvu ni suala la Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria ya Taasisi za Kazi kwamba Sheria hizi zitaanza kutekelezwa lini. Sheria hizi mbili ni sheria ambazo kwa kweli uendeshaji wake na utekelezaji wake unahusisha wadau wengi sana. Unahusisha wafanyakazi, waajiri, Serikali na katika Serikali unahusisha zaidi ya Wizara tatu. Wizara yangu ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Rais, Utumishi.

Mheshimiwa Spika, mahali tulipofika, tayari zile taratibu za uendeshaji na sheria za kuendesha Mahakama ya Kazi ili Mahakama ile iondoke kutoka *Industrial Court* iwe Idara ya Mahakama Kuu katika Mahakamu Kuu ya Tanzania zile Sheria, utaratibu ziko tayari na Kamati ambayo imeundwa na Jaji Mkuu itatoa taarifa yake ya kukamilisha kazi ya kuzipitia hizo tarehe 11 Agosti, 2006.

Mheshimiwa Spika, sheria za uanzishwaji wa Sheria ya Ajira Na. 6 taratibu zake ziko tayari na ziko kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali zinangojea kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Sambamba na hilo wafanyakazi na *scheme of service* ya kazi ya wafanyakazi wa Kamisheni ya Usuluhishi na Majadiliano au *Commission for Mediation and Abitration* utaratibu wake wa kufanya kazi, maofisa watakaohusika na kamisheni yenyewe yaani ile Bodi yenyewe itakayoendesha kamisheni hiyo tayari imeundwaa katika Mamlaka zinazohusika ili wale ambao wanapaswa kuwa katika kamisheni hizo waweze kuteuliwa rasmi. Kwa hiyo, naweza kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba Sheria zile zote mbili zitaanza kutumika katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ziko hoja nyingi sana hapa. Ningependa nizungumzie kidogo kuhusu hoja ya Mwenge. Shughuli za Mwenge wa Uhuru ni moja ya majukumu ya Idara ya Maendeleo ya Vijana. Majukumu hayo yalihamishiwa katika Idara ya Maendeleo ya Vijana baada ya Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa kuanza mwaka 1992. Malengo yake yalikuwa nini? Kuhamasisha wananchi kujitolea katika michango ya hali na mali kwa ajili ya miradi yao wenyewe ya maendeleo. Kuelimisha jamii juu sera, programu na mikopo mbalimbali ya maendeleo kama ambavyo ujumbe wa mwaka huu wa Mwenge ulivyo. Kuhamasisha Muungano wetu wa Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania na hivyo vijana kutoka Tanzania Zanzibar na vijana kutoka Tanzania Bara kila mwaka wanakimbiza Mwenge nchi nzima kufika katika kila Wilaya ya nchi yetu na ujumbe mmoja wa Mwenge. Ni kuwa kiungo kati ya wananchi na Serikali na kuongeza ushindani wa maendeleo. Kama nilivyoeleza leo asubuhi kwa mwaka 2005 peke yake, Mwenge ulizindua au kuweka jiwe la msingi la kufungua miradi ya wananchi yenye thamani ya shilingi bilioni 54.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilipokuwa nawasilisha mapendekezo ya matumizi ya Wizara yangu kulikuwa na vitu muhimu ambavyo nilikumbushwa na wachangiaji. Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, alitueleza kwamba hawa watu ambao tuliwashukuru hapa sio wenyewe tu ambao wanashirikiana na sisi katika kuleta maendeleo ya vijana katika kujenga ajira na kujenga mahusiano mazuri ya kazi na sisi tunakubali na kwa sababu hiyo ningependa niisome sehemu hii ya shukrani ya hotuba yangu ili kukidhi mahitaji yale ambayo yaliombwa na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya.

Kwa hiyo, napenda nitoe shukrani zangu kwa viongozi wenzangu hasa kwenye Wizara na Taasisi ambazo zinaongozwa na Wizara yangu kwa mchango mkubwa ambao wametoa na kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenionyesha wakati na mimi ninajifunza fani hii ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, Naibu Waziri na Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki, Naibu Waziri. Napenda nimshukuru Katibu Mkuu Dr. Ladislaus Komba, napenda nimshukuru Naibu Katibu Mkuu, Edris Mavura, Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara yangu. Napenda pia

niwashukuru Wenyeviti wote na Wajumbe wa Bodi zote za Mashirika ambayo yako kwenye Wizara yangu.

Aidha, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru washiriki wetu wa karibu ambao kwa namna mbalimbali wametuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu tuliyopewa na Taifa na kwa njia ya pekee naomba niitaje Bodi ya Ushauri wa Kazi, Uchumi na Masuala ya Kijamii *(LESCO),* Shirikisho la Waajiri Tanzania *(ATE),* Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi *(TUCTA)* na vyama vyote huru 19 vya Tanzania. Wote mmetupatia mchango na ushauri mzuri uliosaidia sana katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kutambua michango mbalimbali ya wahisani ambayo imesaidia kwa kiwango kikubwa katika kutekeleza majukumu yetu. Shukrani za dhati ziende kwa Serikali za nchi na Mashirika ya Kimataifa ya Denmark, Marekani, Ujerumani, Benki ya Dunia, *Global Fund, ILO, UNDP, UNICEF, TACAIDS, Kahama Gold Mine, Kagera Sugar Limited* na Mashirika yote ya Dini, *NGO's* ambayo hatuna majina yao moja moja, lakini ambayo yamelenga sana katika kuwakuza vijana kwa maadili mema, kuwapatia ajira na kuwaunganisha wananchi ambao hawana kazi katika *SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hoja bado ni nyingi na tunaahidi kwamba tutazijibu hoja zote hizi kwa maandishi kabla hatujaondoka hapa Dodoma kwa kikao hiki cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 60 – Mahakama ya Kazi**

Kifungu 1001 - *Administration and General... ... ... ... ... ... ..* 626,264,900/=
Kifungu 2001 - *Arusha Zone... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...* 65,749,000/=
Kifungu 2002 - *Dar es Salaam Zone... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...* 39,740,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 - Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana**

Kifungu 1001 - *Administration and General ... ... ... ... ...* 2,183,951,800/=

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Ni hiyo hiyo *Vote 65,* Programu 10, Fungu dogo 250100 Mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Sina tatizo na mshahara wake lakini wakati nachangia hapa nilizungumzia pamoja na Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia suala la ile shilingi milioni 500 itakayokwenda kwa kila mkoa. Ningependa ufafanuzi japo amesema kwamba mbele ya safari ndiyo atafafanua vizuri zaidi. Lakini katika hatua hii ili tunapotoka hapa tunapoenda kwa wananchi wakituuliza kuhusu suala hili tuwe na maelezo ambayo yanaeleweka. *(Makofi)*

Katika ukurasa wa 32 wa kitabu chake amesema kwamba fedha hizo zitaenda kwa walengwa kwa kupitia Benki Kuu na Benki ya Biashara nikidhani ikimaanisha na *NBC* na *BOT* kitu cha namna hiyo. Lakini akasema walengwa wakuu wa mpango huu ni wajasiriamali ambao kwa kupata mikopo hiyo watapanua shughuli zao za uzalishaji mali na biashara. Lakini ikumbukwe kwamba picha ambayo tumeipata sisi Waheshimiwa Wabunge ni kwamba fedha hizi zinalenga kuwawezesha kiuchumi *disadvantage groups* za vijana, akinamama na wasio na ajira kitu ambacho amekizungumza kwenye ukurasa wa 33 pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi ninaoutaka ni wa kupitishia fedha hizi benki, ili ziwafikie walengwa. Benki tumeshawahi kuwaambia mara kadhaa wana fedha ambazo hazikopesheki kwa sababu ambazo ziko wazi. Wana masharti ya ajabu ajabu, wana taratibu za ajabu ajabu, sasa sababu yake ameelezea kwamba ile shilingi milioni 500 kwa baadhi ya mikoa ambayo ina Halmashauri nyingi ambayo ukiigawanya itakuwa ndogo na kwa hiyo, inatoa fursa kwa benki waongeze hela zao ili kwa hiyo wakopeshe, je, haoni kwa kufanya hivyo sasa ndiyo itakuwa ita-*complicate* suala zima la nia njema ya hii shilingi milioni 500? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Waziri atakubali kwamba ni vizuri kwamba kabla hatujamaliza Bunge tukapata muda wa kujadili vizuri hili suala la shilingi milioni 500 ili tuondoke hapa tukiwa tunaelewana? Ni ufafanuzi tu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kwamba kama nilivyosema hatujakamilisha kabisa ule utaratibu wa jinsi fedha hizi zitakavyoshughulikia kukamilisha kabisa ule utaratibu wake, kama nilivyosema jana tulikuwa na kikao na kikao cha mwisho wataalam wakishakamilisha utaratibu ambao utakuwa siku ya Jumatatu na nimesema kwamba baada ya utaratibu huo tutauleta hapa Bungeni tuwaeleze Waheshimiwa Wabunge jinsi gani utakavyokuwa kabla kikao hiki cha Bunge hakijamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kidogo baada ya Jumatatu kutakuwa na utaratibu wa kueleza suala hili. Suala la benki, nilikuwa niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba huu ni utaratibu maalum ambao utaangalia namna ya kuhakikisha tunaondoa urasimu ule wa kibenki ambao unawafanya watu wengi wasipate fedha mle. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasisitiza kwamba tuanzishe vyama vya Ushirika wa akiba na mikopo na vile ndiyo vitakuwa dhamana. Siyo nyumba ambayo anayo, *SACCOS* inayo au dhamana aina nyingine na hili likifanikiwa litakuwa ukombozi mkubwa sana kwa sababu litawahusisha Watanzania wengi katika mfumo rasmi wa fedha. Hii itabadilisha uchumi wetu kabisa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani niseme tu lilivyoeleweka ni kwamba Benki yoyote ile ya biashara itakayofanya shughuli hii itakuwa na dirisha la hao walengwa siyo kwamba wanapitishwa katika utaratibu wa kila mtu. Nadhani ndivyo ilivyokuwa kuna dirisha lao hawa. Kwa hiyo, namawita Mheshimiwa John Lwanji. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi ningeomba kupata ufafanuzi kuhusu sera ya Wizara kuhusu mikataba ya wafanyakazi, wanapoacha kazi *Vote 56,* Programu 10, *sub-vote 1001.*

**MWENYEKITI:** Ni *Vote 65* Mheshimiwa.

**MHE. JONH P. LWANJI:** *Vote 65,* halafu *sub-vote 1001, item* 250100. Ningependa kupata ufafanuzi kuhusu mikataba ya wafanyakazi. Sera ya Wizara hii inasemaje hasa pale ambapo wafanyakazi wanaachishwa. Tumeona katika zoezi la ubinafsishaji, jinsi kwa kweli Serikali ilivyopuuzia kuhusu masuala ya mikataba ya wafanyakazi inapokuja kwenye suala la mafao kwa kisingizio cha kusema kwamba wanalipa mafao ya msingi tu. Nikitoa mfano mwaka 2001 Shirika la *Tanzania Motor Services* lilibinafsishwa, sasa hili shirika ni la umma lilikuwa la umma chini *State Motor Cooperation* na mwaka 1985 hili shirika liliundwa kutokana na makampuni ya Lonrho, kwa hiyo, likawekwa chini ya Serikali lakini likachukua wafanyakazi, waliokuwa makampuni ya *Riddoch Motors* kwa mfano *Tanzania Motor Cooperation* na makampuni mengine ya Lonrho, sasa walipochukua *on board* wao wakapewa nafasi ya kwamba mikataba yao ile ya mwajiri wao wa zamani inakuwa *carried of* na mwajiri mpya.

Lakini sasa mwaka 2001 ilipofika shirika hili kubinafsishwa, mikataba ile ikapuuzwa, basi wafanyakazi sasa wako barabarani mpaka leo zaidi ya wafanyakazi 200 wanasota, kwa sababu ya uamuzi huo, wenzao wale walioachwa walilipwa na kati ya kipengele kimoja wapo wanachosema malipo ya *ex-gratia*, asilimia 25 ya mshahara wa mtu kwa miaka yote aliyofanya kazi na waliwekeana sahihi, hiyo ikawa *put aside* wakasema bwana ni masuala ya msingi, nauli, notisi, mshahara wa mwezi mmoja, badala ya notisi, halafu na mizigo.

Sasa mimi ningeomba kwa sababu hili shirika halikuwa maskini, hili shirika halikuwa mufilisi, hili shirika wakati linabinafsishwa lilikuwa na majengo ya biashara 19 yakiwa *valued* kwa shilingi bilioni 11, halafu likawa na majengo ya kuishi 18, yakiwa *valued* kwa bilioni 1.2, jumla bilioni 12.3. Mafao ya wafanyakazi kwa kuzingatia *ex-grassier* yalikuwa yawe 1.6 bilioni, sasa unaweza kuona ndio maana nilikuwa nasema tulijali zaidi rasilimali fedha kwa rasilimali majengo, lakini inapokuja kwenye suala la rasilimali watu linawekwa kando.

Mimi ningependa kupata ufafanuzi juu ya sera ya Serikali kuhusu suala hili na tunaye mzee mmoja pale, Mzee Salum alianza kazi mwaka 1953 pale *Riddoch Motors, specialist* wa *engine* wale mnaofahamu *Riddoch Motors* ndio ilikuwa inashughulikia masuala ya magari ya *bedford*, matrekta ya *ford,* huyu mzee amekaa kuanzia mwaka 1953 mpaka 2001 bahati mbaya yeye anakaa karibu na Dar es Salaam anatoka Rufiji, amepewa hundi shilingi 200,000, mtu amefanya kazi miaka 48 na akaachwa kufuatia mafao madogo ya *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali alilouliza ufafanuzi Mheshimiwa Mbunge mwenzetu, halianguki katika kazi ya Kamati ya Matumizi, ni jambo mahususi linatarakimu nyingi, linaleta kitu kipya kabisa. *(Makofi)*

Sasa mimi napendekeza kwamba Mheshimiwa John Lwanji, aliandike kama swali na nitahakikisha nalifikisha kwa kipaumbele ili lijibiwe kabla hatujaondoka. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 396,481,400/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 – *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 548,959,000/=

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kumhakikishia Waziri ya kwamba maelezo yake yalikuwa ni fasaha, lakini katika kuangalia *sub-vote* 1003, kifungu cha 260800 *Training Expenses* na kifungu cha 310400 nilikuwa nahitaji ufafanuzi, kwa sababu kwa mantiki ya kujenga ajira na kuwaimarisha vijana nilifikiria kwamba kuna umuhimu sana wa *training* ya kuwapa mafunzo vijana na mafunzo wale watakao wafunza vijana na pia mkakati wa *transfer* ya teknoloji kwa vijana, kwa sababu wakati tulionao, sasa tunaweza kuendelea kugawana mapesa lakini hao watu kupata teknoloji ya kufanyia kazi wakashindwa hata kuzitumia hizo pesa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, kwa mfano vijana wa Wilaya ya Ukerewe ambao ni wavuvi ili waweze kupata nyenzo za kuvulia anahitaji *minimum* ya shilingi milioni nne apate mtumbwi, apate na mashine ya kuendeshea mtumbwi, nyavu, karabai, lakini akishapewa hizo nyezo ana uwezo wa kuzirudisha hizo pesa shilingi milioni nne katika miezi kama hali ya hewa inakuwa nzuri na asipopata hizo katika *SACCOS,* wanaweza wakatumia mtumbwi wa makasia, wasiweze kupata faida hiyo. Sasa huo nimetoa tu ni mfano mdogo, lakini vijana wengine Tanzania wanahitaji pesa, wanahitaji *training* na wanahitaji pia teknolojia ili tuweze kuwapeleka hatua moja mbele. *(Makofi)*

Sasa katika vifungu hivi badala yake naona vinazidi kupungua kwa mfano katika mwaka uliopita katika *training expenses* kulikuwa na shilingi 41,257,600 na sasa imepungua mpaka shilingi 13,032,200 na ukienda pia katika kifungu cha *acquisition of technical equipment and tools,* utakuta ya kwamba pia zimepungua kutoka shilingi milioni 18 kwenda shilingi milioni 9.5.

Kwa hiyo, mimi nilitaka ufafanuzi, je, Wizara itawezaje kujenga hizi ajira milioni moja na kuweza kuhakikisha kwamba zile pesa ambazo tutawagawia katika *SACCOS* zinaweza kutumiwa kwa ufanisi kama hawakuwa teknolojia na mafunzo ya kutosha?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, kwa swali lake na jinsi alivyoona hali halisi ilivyo. Ni kweli kwamba vijana ili waweze kumudu mikopo hii ambayo watapewa watahitaji mafunzo na jinsi tulivyolenga katika mwaka huu wa fedha kwanza ni kutumia shilingi milioni 500 ambazo tumepewa kwenye mfuko wa vijana na katika mfuko ule kufikia mwezi Mei, 2006 tulikuwa pia na albaki ya shilingi bilioni moja, kwa hiyo, fedha hizo zitatumika kwa kuanzia katika utaratibu huu, aidha, katika idara mbalimbali kuna fedha kidogo kidogo tunategemea kwamba jinsi tunavyokwenda na katika bajeti ya miaka inayofuata, fedha hizi za kutoa mafunzo zitaongezeka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001- *Labour*.. ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...2,246,163,000/=
Kifungu 2002 - *Employment* . ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 1,299,466,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Youth Development*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... . 1,382,631,700/=

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 65,* Programu 50, *Sub-vote 5001,* kifungu kidogo 261100. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa 51, kielelezo namba (a) kuna vikundi ambavyo vilitambua au utambuzi wa vikundi *(Youth Mapping)* katika Wilaya ya Mpwapwa kuna vikundi zaidi ya 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, alitembelea hivi karibu mwezi wa saba na kuona baadhi ya vikundi Wilaya ya Mpwapwa, lakini nimeona Wilaya nyingine kuna vikundi ambavyo vimefanyiwa *Youth Mapping,* lakini kwa Wilaya ya Mpwapwa, hakuna hata kikundi kimoja, sasa naomba maelezo kwa nini hawakufanya *Youth Mapping? (Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hakuna vikundi ambavyo vimefanyiwa *mapping* katika

Wilaya ya Mpwapwa, kama tulivyotoa maelezo kazi hii imekamilika katika Wilaya 76 na bado Wilaya 43, kazi bado inaendelea, ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Mpwapwa. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 65 - Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana**

Kifungu 1001- *Administration and General* ... ... ... ... ... ... ...437,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 2,663,000,000/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ili niweze pengine kupata ufafanuzi zaidi juu ya suala la shamba au kituo cha vijana...

**MWENYEKITI:** Kifungu Mheshimiwa, kifungu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani *Vote 65,* kifungu kidogo cha 1003, kifungu kidogo zaidi 6388 *Rehabilitation of Labour Office and Youth Centres.*

Kwa hiyo nilikuwa nasema, wiki iliyopita niliuliza swali likihusu kutaka kujua matumizi zaidi ya eneo la Sasanda. Shamba hili nilisema kwamba lina ukubwa wa ekari 828 na limekuwa hivyo karibu miaka 25 sasa halijaendelezwa. Waziri alipojibu swali hili alisema kwamba wana mkakati wa kuliendeleza, sasa nilipoangalia kwenye mafungu ya maendeleo nimeona kama kuna shilingi karibu bilioni mbili lakini kwenye hotuba ya Waziri ametaja maeneo karibu matano ambayo yako hapa. Sasa nilitaka kujua na kwa sababu wananchi wa Mbozi na hususan wale wanaozunguka eneo lile kwa kweli wamekuwa wanaiomba sana Serikali iwagawie walau eneo kidogo, ili waweze kujenga hata shule.

Lakini Serikali bado ilisema mwaka huu iko *serious,* inataka kulitumia eneo hilo, sasa nataka Waziri anifafanulie *how serious is the government* na wame-*commit* kiasi gani katika hizi shilingi bilioni mbili ambazo ngapi zinaenda Sasanda, ili kweli wananchi waone kwamba Serikali inataka kabisa kuliendeleza hilo eneo na ili wasione kwamba wananyimwa tu pasipo sababu za msingi kama vile ambavyo wamekuwa wananyimwa huko nyuma.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa hili ni shamba la vijana au ni shamba tu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kituo, wanaita kituo, kwa ajili ya maendeleo ya vijana, ni *centre*.

**MWENYEKIT:** Hiyo Sasanda?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Ndiyo.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na namshukuru sana Mheshimiwa Godfrey Zambi, kwa kutaka ufafanuzi. Tulipojibu swali lake juzi kuhusu Sasanda nilisema kwamba ni kweli lile shamba lina hekta 335, kule nyuma lilikuwa linatumika na mkoa wa Mbeya. Mkoa wa Mbeya ukalitoa kwa Serikali wakati ule ilikuwa kambi. Pana nyumba mbili pale, *plot* mbili, sasa Wizara ikageuza ile kambi kuwa kituo cha maendeleo ya vijana. Tulikiri vile vile kwamba ni kweli kwa muda uliopita, Serikali ilikuwa inaonekana kana kwamba imelitelekeza, lakini sivyo, hoja ilikuwa Serikali iwape wananchi wa Mbozi ili walitumie kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu letu lilikuwa hapana, kile kitabaki kuwa kituo cha maendeleo ya vijana, katika hizi fedha tulizoomba shilingi 2,900,000,000 zinatarajiwa zitatumika kwa ajili ya kuboresha vituo vitatu vya Wizara, Sasanda ikiwa mojawapo. Sasa kiasi kitakachotumika, itategemea sana ni kitu gani kinachohitajika, kwa matengenezo ya kile kituo yataendana na masharti ya kutoa zabuni na makisio mengine. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndio Serikali itakitengeneza kile kituo ili vijana waweze kukitumia. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nilikuwa nataka niombe Serikali kwa sababu eneo hili ni kubwa, kama alivyosema mwenyewe na kama ambavyo pia nimekuwa naeleza hekta 335 ambazo nina hakika Serikali haiwezi kuzitumia zote. Sasa wakati Serikali inaendelea na taratibu za kutumia eneo lote je, haioni kwamba itakuwa vizuri eneo litakalobaki basi wawape wananchi wawe wanalima na pale ambapo watakuwa tayari kulitumia lote, basi wawaambie wananchi kwamba wanahitaji kulitumia sasa?

**MWENYEKITI:** Kama ni ushauri, lakini sidhani kama itasaidia sana, kwa sababu itakuwa ni yale yale ya kuwapoza wananchi kwa kitu ambacho si endelevu, hili nadhani halina msingi kabisa. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, *vote 65, sub vote 1003,* kifungu kidogo 6380, *Rehabilitation of Labour Office and Youth Centres*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu *clarification* kutoka kwa Waziri kwa kuzingatia kwamba ofisi za kazi ni kati ya ofisi ambazo zinaongoza kwa hali mbaya sana Tanzania. Sasa katika hizi shilingi bilioni mbili, ni ofisi ngapi ambazo zitafanyiwa marekebisho na vile vile kama hizi pesa zina jumuiya msaada ambao *DANIDA* walitoa

wakisema kwamba watajenga ofisi tano na vile vile, ningeomba Mheshimiwa Waziri anipe *clarification* kwa sababu wamesema tunaanza kutumia hizi sheria hivi karibu, lakini taarifa ambazo mimi ninazo, ni kwamba bado jengo halijapatikana, sasa kama jengo limepatikana atanijibu, lakini kama halijapatikana, mbona hapa hakuna kitu chochote kinachohusiana na jengo? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ofisi za kazi nchi nzima zimechoka kweli kweli na mwaka huu Serikali imechukua hatua ya kuanza kuziweka katika kiwango kizuri na kuzipatia vifaa na itafanya kazi hii mpaka ofisi za mikoa yote zitakapokuwa zimekarabatiwa na kutengenezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 Serikali imepanga kukarabati ofisi ya kazi ya Morogoro na itatumia shilingi 180 milioni, ofisi za kazi Dodoma na itatumia shilingi 450 milioni, ofisi za Mtwara nayo itatumia shilingi 165 milioni, ofisi za Arusha, Dar es Salaam na Arusha zimeshughulikiwa katika mwaka wa fedha uliopita, ofisi ya Dar es Salaam, ile *Mazdo House* itashughulikiwa kwa kutumia shilingi 177 milioni, ofisi ya Moshi shilingi 198 milioni na ofisi ya Kigoma shilingi 175 milioni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuna jengo aliulizia Mheshimiwa Halima Mdee, sijui ni jengo lipi nadhani ndio hilo swali la pili, Mheshimiwa Halima Mdee, unaweza kufafanua lile jengo lingine.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama angefafanua ingetusaidia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni kwamba wakati Mheshimiwa Waziri anajibu kuhusiana na hizi sheria mpya, alisema kwamba zitaanza ku-*take effect* mwaka huu na kwa ufahamu wangu najua kwamba lazima kuwe na jengo maalumu kwa ajili ya ile *Commission for Mediation* na *arbitration* na ninavyofahamu mimi *still* jengo lilikuwa halijapatikana, sasa nilikuwa naomba aniambie kama limeshapatikana na ndio maana halipo na kama halipo kwa nini hapa hamna wakati tumeambiwa *plan* inaanza robo ya mwisho ya mwaka huu?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDLEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima Mdee, ni mfanyakazi wa Wizara ya Kazi aliyeko kwenye likizo bila malipo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni kweli anajua mambo ya ndani kule ndani ya Wizara, nilikuwa napenda nilieleze Bunge Tukufu kwamba tumechukua nyumba moja ya zile *Tower* za Nyerere katika Mtaa wa Bibi Titi kwa ajili ya kuzi-*house* au ili ziwe ofisi za *CMA* na ofisi za Mahakama ya Kazi na kwa sababu hiyo nilikuwa nawashukuru Shirika la Maendeleo la Denmark kwa kukubali kulipia kodi ya ukodishaji wa majengo hayo ili taasisi hizo za kazi ziweze kufanya kazi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Labour* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 100,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Youth Development*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 200,000,000/=

**MHE. RUTHI B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *Vote 65, sub vote* 5001, kifungu 5492 *HIV/AIDS.* Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utaratibu au ni suala linaloeleweka kwamba matatizo ya UKIMWI ama maambukizi ya virusi vya UKIMWI, ni suala mtambuka ambalo liko katika Wizara na kwa kweli kila Wizara inatakiwa kutenga fungu kwa ajili ya kusimamia jambo ama kuendelea kuona kwamba mambukizi yanazidi kupungua na wagonjwa wanahudumiwa vizuri.

Lakini ninapotaka kulizungumza hapa chini ya Wizara hii ninalenga kwamba waathirika wakubwa wa ugonjwa wa UKIMWI ni wale wenye umri ambao naamini kwamba uko chini ya Wizara hii ambayo ni miaka 15 mpaka 49 ndio walio wengi walioambukizwa. Sasa kwa kipindi kilichotangulia tumeona elimu inatolewa sana kwa vijana wanaokaa mijini na hasa wa maofisini ambapo nimeona fungu tumemaliza kulipitisha sasa hivi limelenga wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili kwa sababu liko wazi nasema *youth development,* basi napenda nimuulize Mheshimiwa Waziri kama upo utaratibu ambao umewekwa sasa ambao umeandaliwa katika Wilaya za mikoa ya Mipakani ikiwemo mikoa ya Kagera, ambapo ndipo ugonjwa hasa ulikosemekana kuanzia jambo kuwa maambukizo yanateremka, Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Mara, Mwanza, Tabora, Lindi, Mtwara, mikoa ambayo iko mbali na makao makuu na kusudia kusema mikoa iliyo mbali na makao makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utaratibu gani ambao umewekwa wa kuhakikisha kwamba vijana wa maeneo hayo wanapata elimu ya kujikinga na UKIMWI ambayo tutaiona hasa na kwa msingi huo ukiitoa kwa msingi wa Wilaya katika Wilaya zile ambazo zina majimbo zaidi ya jimbo moja, mara nyingi lile jimbo ambalo vijana wake wanakaa makao makuu ya wilaya ndio upata elimu, sasa itolewe kwa msingi wa majimbo ili wahakikisha kwamba katika majimbo 232 ya Tanzania, ambayo yale yaliyokaa pembeni katika mikoa ya mipakani, basi yote yanaweza yakapata elimu. Je, Serikali imeandaa utaratibu kuwa vijana wote wa maeneo yale niliyoyataja watafikiwa, ni utaratibu upi huo ambao Serikali inao? Ningependa maelezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naelewa suala litakuwa ni pana zaidi, kwa sababu Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu wengi wanashiriki katika kusaidia katika kupambana na gonjwa hili zito, lakini sehemu inayohusu Wizara ya kazi hebu Waziri utusaidie, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ahsante sana Mheshimiwa Ruth Msafiri, kwa swali lako zuri, kwanza ni kweli kwamba waathirika wakubwa wa UKIMWI ni vijana wa kati ya miaka 15 mpaka 49. Lakini na ni kweli pia kwamba suala hili ni mtambuka na kama umeona karibu katika kila Wizara kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya UKIMWI ku-*address* suala hili la UKIMWI. Sasa hivi shilingi milioni 200 ni kwa Wizara na ni kuhudumia vituo vyetu vya vijana si kwamba ni kwa vijana nchi nzima, lakini niseme kwa sisi mikoa ya pembezoni hasa Kigoma na Kagera ambao najua vizuri na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani wewe ni shahidi hapa sisi huwa tuna mkakati wetu wa maeneo yaliyoathirika na wakimbizi na tunapata fedha kupitia *other sources* za *donor community* na usisahau pia kuna *TACAIDS* nao wana-*support initiative,* kuna Wizara ya Afya wana mkakati huo na kwa mfano mkoa wa Kigoma mwaka huu unaoanzia 2006/2007 tuna fedha nyingi kwa ajili ya kupambana na maambukizi ya UKIMWI hali kadhalika na Mkoa wa Kagera hasa Wilaya ya Ngara na Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hizi ni fedha mahsusi kwa ajili ya Wizara na Vituo vya Vijana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nilidhani utanisahau. Hii *Vote 65,* Kifungu 5001 Kifungu kidogo 5492, nimechukulia kwamba ni *Youth Development* maana yake na kwa vile katika kitabu chetu ukurasa wa 38 kuna *bullet* ya mwisho pale inayozungumzia kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa Vituo vya Maendeleo ya Vijana katika ngazi za Wilaya, ndiyo hizo *Youth Development Centres.* Nilitaka tu ufafanuzi, sisi Ludewa tunapenda kuanzisha vitu kama hivi lakini hatujui utaratibu wake, *how to go about* kuanzisha *a Youth Development Centres*, tungependa sana na sisi tuanzishe. Ningependa ufafanuzi, *how to go about doing it,* ningeshukuru sana.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kueleza suala hili.Fungu hili ni kwa ajili ya mafunzo ya kupambana na virusi vya UKIMWI na UKIMWI katika Wizara, Idara ya Vijana na kuwafundisha vijana ambao wanakuja kufundishwa Stadi za Kazi katika Vituo vya Vijana vya Marangu, Ilonga na Sasanda na siyo *Youth Development* kama kwa mapana yake, hilo ndiyo lengo lake. Kama Wilaya ya Ludewa ina nia ya kuanziasha kituo cha vijana basi ni vema tuzungumze ili tuone ni jinsi gani tutawasaidia au tusaidiane kuhakikisha kwamba kuna Kituo cha namna hiyo katika Wilaya ya Ludewa.

**MWENYEKITI:** Kwa maana nyingine kwa jibu hilo Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, ndiyo mazungumzo yameanza hivyo kwa hiyo uchangamke muendelee. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa Fedha 2006/2007 Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nafurahi kutangaza kwamba Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2006/2007 yamekubaliwa na Bunge na kupitishwa leo. *(Makofi)*

Ninayo matangazo machache, la kwanza, asubuhi nadhani nilikosea kidogo tangazo halikueleweka siku ya Jumatatu, tarehe 07 Agosti, 2006 saa 05.00 asubuhi Tume ya Rais inayosikiliza maoni kuhusu mishahara na marupurupu ya watumishi Serikalini itatutembelea hapa Bungeni na kwa niaba ya Bunge itakutana na Tume ya Huduma za Bunge, Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa hiyo, Kamati hizi mbili pamoja na Tume ndiyo watakaozungumza na hii Tume ya Rais ni saa 05.00 asubuhi na kwa ajili ya nafasi badala ya kuwa ni kwenye Ukumbi wa Spika, itakuwa ni kwenye Ukumbi wetu wa Bunge wa zamani ili ipate nafasi ya kutosha kwa sababu ni Kamati mbili pamoja na Tume, kwa hiyo saa 05.00 asubuhi siku ya Jumatatu. Baada ya hapo saa 07:30 mchana kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Spika, Jengo la Utawala Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge itakutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuzungumzia mambo ambayo ni muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge. Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, anaomba kesho saa 04.00 asubuhi kwenye chumba cha Kamati namba 231 Wajumbe wa Kamati hiyo yaani ya Kilimo na Ardhi muweze kukutana ni kikao kifupi tu. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu Msaidizi wa Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi anatangaza kwamba leo jioni hii saa 02:00 usiku au mara baada ya kutoka hapa kutakuwa na Mkutano wa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, katika ukumbi wa zamani wa Bunge. *(Makofi)*

Naomba nikumbushe ratiba ya wiki ijayo kwa uchangiaji Wizara, Tarehe 07 Agosti, 2006 yaani Jumatatu ni Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, tarehe 08 Agosti, 2006 ni sikukuu yaani ni sikukuu kwa hiyo, hakuna lolote litakalofanyika, watakaopenda kwenda Morogoro kwa ajili ya Nanenane utaratibu unaweza kufanywa waweze kwenda asubuhi na kuweza kurudi, watakaopenda hivyo wanaweza kupewa usafiri. Kuna Maonyesho ya Kilimo kwenye Sikukuu ya Nanenane. Siku ya Jumatano ni Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Siku ya Alhamisi ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ijumaa ni Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Hii ndiyo ratiba kwa maana ya kujiandaa wale ambao mngependa kuchangia. Huwa napenda kugawana nanyi baadhi ya hisia ninazozipata, nimegundua kwamba Waheshimiwa Mawaziri wanaume wana tabia hii njema ya kuwaleta wake zao hapa Bungeni ili siku wanapotoa hotuba tuweze kuwafahamu na wao kina mama hao wasikilize shughuli za Bunge. Lakini Mawaziri wanawake hata Naibu Mawaziri wanawake hawana tabia hiyo sijui wenzangu basi nawaachia tu, ni la … *(Kicheko/Makofi)*

Basi nawatakia *weekend* njema na kwa kuwa hakuna tena shughuli nyingine naahirisha Bunge hadi Jumatatu saa 03.00 asubuhi.

*(Saa 01.39 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 07 Agosti, 2006 Saa 03.00 asubuhi)*